**16 JUNI, 2022**

# BUNGE LA TANZANIA

___

## MAJADILIANO YA BUNGE

___

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Arobaini na Tano – Tarehe 16 Juni, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. ZAYTUN S. SWAI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2022/2023 na Tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu!

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali, Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki sasa aulize swali lake.

Na. 396

### Matengenezo ya Barabara ya Malula Kibaoni – Ngarenanyuki kwa Kiwango cha Changarawe

**MHE. DOROTHY G. KILAVE K.n.y MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa kiasi cha fedha ilizoahidi kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Malula Kibaoni hadi Ngerenanyuki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini imetenga kiasi cha Shilingi Bilioni Moja kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Malula - King'ori – Leguluki - Ngarenanyuki yenye urefu wa kilomita 33.7 kwa kiwango cha changarawe. Ujenzi wa Barabara hiyo umefikia asilimia 70 ambapo kazi zilizotekelezwa hadi sasa ni uchongaji wa barabara kilomita 33.7, karavati 16 na uwekaji wa tabaka la changarawe kilomita Tisa umekamilika na ujenzi unaendelea. Ujenzi huu unatarajiwa kukamilika Tarehe 28 Juni, 2022.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Danielson Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, lakini kwa kuweka rekodi sawasawa majina yangu ni John Danielson Pallangyo.

**SPIKA:** Kwani ulitamkwaje mwanzoni Mheshimiwa? Maana ndivyo inavyosoma hapa karatasi yangu Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki.

**MHE. DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Ulikuwa unarekebisha nini?

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Ulisoma Danielson Pallangyo bila John.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tuwe tunaelewana vizuri, tuwe tunaelewana vizuri. Uliza swali lako moja la

nyongeza maana yake aliyekuuliza swali ni mtu mwingine.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali la nyongeza. Nashukuru pia Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kutupa fedha Shilingi Bilioni Moja mwaka jana ambazo ndizo zimetumika kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, swali, barabara hii ni moja ya ahadi ya Mheshimiwa Rais ili ijengwe kwa kiwango cha lami. Je, Serikali inasemaje kuhusu hilo, ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hatua ya awali ni hii ambayo tunarekebisha hii barabara ili walau iweze kupitika kipindi chote wakati ambapo tunatafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza hiyo ahadi ya kujenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan itatekeleza ahadi yake kwa vitendo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwita Kembaki Michael, Mbunge wa Tarime Mjini sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

Na. 397

**Changamoto ya Michango Shule za Sekondari**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE K.n.y. MHE. MICHAEL M. KEMBAKI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza michango kwa Wanafunzi wanaojiunga Kidato cha Kwanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Kembaki Michael, Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Waraka wa Elimu Namba 5 wa mwaka 2015 iliamua kutoa Elimu Msingi kuanzia Elimu ya Awali hadi Kidato cha Nne bila malipo. Azma hii ya Serikali ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 ambayo ina lengo la kuhakikisha kwamba watoto wote wa Kitanzania wenye rika lengwa la Elimu Msingi wanapata elimu bila kikwazo chochote ikiwemo ada au michango.

Mheshimiwa Spika, michango inayoendelea shuleni kwa sasa ni michango ya lishe ambayo imepata kibali cha Mkuu wa Wilaya baada ya kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Wazazi. Michango hii ni kwa wanafunzi wote wa Kidato cha Kwanza hadi Kidato cha Nne.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninamshukuru Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza:

Mheshimiwa Spika, kwanza; kwa kuwa sasa tuna elimu bure ya sekondari na mpaka Kidato cha Sita. Ninashukuru kwa hilo kwa Serikali, nimshukuru Mama Samia kwa kutoa elimu bure kwa Kidato cha Tano na cha Sita. Sasa lipi Serikali itafanya kusamehe michango ya sekondari 20,000? Kusamehe michango ya Kidato cha Sita na cha Tano ya 70,000 au kutoa michango ya sekondari ambayo inafikia Shilingi Laki Tano au michango ya Kidato cha Sita ambayo inafikia Shilingi Milioni Moja, kipi kifanyike sasa?*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere hayo ni maswali manne katika swali moja. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwita Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa swali lake lilikuwa ni la jumla na nimwambie tu kwamba baada ya elimu bila

ada maana yake wanafunzi wale hawalipi ile ada ambayo walikuwa wanalipa ya Shilingi 20,000 kwa Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne. Maana yake na hivi tunavyokwenda kwa Kidato cha Tano na Kidato cha Sita ambapo ada kwa miaka yote imekuwa ni Shilingi 70,000 maana yake sasa hivi wazazi hawatalipa hiyo ada ya Shilingi 70,000. Kwa hiyo, huo ndiyo msimamo wa Serikali kuhakikisha kwamba tunawasaidia wananchi wote wa Tanzania ili waweze kupata elimu bila malipo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hiyo michango mingine tunaendelea kuiangalia ili kuhakikisha kwamba haiathiri masomo ya wanafunzi na wazazi kuhakikisha watoto hawa wanapata elimu bora. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Monni swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Kumekuwa na michango mingi sana hasa kwa hawa wanafunzi wanaojiunga na Kidato cha Tano. Nina mwanafunzi ambaye hana wazazi hana familia, alikuwa anaenda Bwiru Sekondari, nimelazimika kutoa fedha nyingi mara nne zaidi ya ile fedha ya ada.

Nini sasa tamko la Serikali leo juu ya shule hizo ambazo michango ni mikubwa mara Nne zaidi ya fedha ambazo unatozwa za ada?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa

Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Monnie Mbunge wa Jimbo la Chemba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kwamba yote lazima iwe imepitishwa kwa kuzingatia mazingira yaliyopo. Kama kuna shule ama kuna eneo lolote lina michango mikubwa tunaomba taarifa hizo ofisi ya Rais TAMISEMI ili tuweze kuchukua hatua katika hayo maeneo ambayo wamezidisha michango.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, michango ambayo imezidi kiwango ni michango ambayo haikubaliki na Serikali tulishatoa kauli yetu.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri kumekuwa na lugha ya *pre-form one* ambayo inatumika sana kwenye shule binafsi na ina michango mingi sana kwa wazazi wanaopeleka watoto kwa masomo hayo. Mnatoa tamko gani kama Serikali kuondoa hili neno la *pre-form one* kwa sababu inaongeza gharama kwa familia na wazazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, masuala yote yanayohusu shule binafsi yanashughuliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, nasi kama wadau tunatambua mchango mzuri ambao unatolewa na shule binafsi katika kukuza elimu bora nchini. Kwa hiyo, nimuelekeze Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tumelipokea na tutalifikisha Wizara ya Elimu ili waweze kuchukua hatua ambazo zinastahili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Migilla, swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kutoa elimu bure kwa wanafunzi wetu lakini bado kuna michango mingi sana ambayo inakera kwa wazazi. Mfano katika shule za kwetu huko vijijini, shule inaambiwa iwe ya bweni, mzazi anahitajika atoe mpaka kitanda, na kuna baadhi mpaka hela ya chakula. Sasa inapotokea mzazi ameshindwa kutoa hizo huduma ambazo anatakiwa achangie mtoto anaadhibiwa.

Je, Serikali ina kauli gani kuhusu hizi shule ambazo zinatoa adhabu kwa wanafunzi, badala ya kwa mzazi ambaye ameshindwa kuhudumia hiyo michango?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza

ninampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake fasaha.

Mheshimiwa Spika, pia niipongeze sana *Young Africans* kwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na sera ya elimu bila malipo, ambayo Serikali tunaendelea kuitekeleza, katika hili nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuendeleza sera ya elimu bila malipo na kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha alivyosoma hoja yake ya Bajeti Kuu, na sasa hivi tunaenda mpaka Form Five na Form Six tunamshukuru na kumpongeza sana Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa michango ya wazazi, kwenye masuala ya uendeshaji wa shule za sekondari, upo mwongozo ambapo Bodi au Kamati za Shule zinashirikisha wazazi au walezi. Kwa hiyo, ningependa kutoa maelekezo kwa Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu kushirikisha wazazi au walezi kupitia mwongozo ambao Serikali imeutoa namna tunavyoshikirikisha wazazi au walezi kwenye ile michango tunahitaji kushirikisha wazazi au walezi kuendesha shule zetu.

Mheshimiwa Spika, mwongozo upo bayana kwa hivyo maelekezo yangu kwa Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu, ni kuwashirikisha wazazi kupitia vikao ambavyo vimepangwa kwa taratibu zilizopo, bodi za Shule na Kamati za Shule, hayo ndiyo maelekezo yangu. Ninashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa George Mwenisongole swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza lakini nimeridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo sitakuwa na swali la nyongeza. Ahsante.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Michael Mwakamo swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kutokana na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini kwa kuwa Wabunge wote katika swali hili linaonesha ni namna gani wananchi wanakerwa pamoja na kuwa na huo mwongozo.

Je, Serikali haioni ipo haja sasa ya kuwaelekeza Walimu na hizo Bodi wasitumie mwongozo huo kama uchochoro wa kuwapatia wazazi mzigo mzito?*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Michael Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumepokea wazo la Mheshimiwa Mbunge na tunatoa maelekezo kuwakumbusha shule zote nchini juu ya utekelezaji wa mwongozo huo. Ahsante sana

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako, kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 398

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi – Dunga**

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia ujenzi wa Kituo cha Polisi Dunga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tathmini iliyofanyika imebaini kuwa kiasi cha Shilingi 43,000,000 kinahitajika ili kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Dunga kilichoko Wilaya ya Kati, Mkoa Kusini Unguja. Serikali kupitia Jeshi la Polisi inatafuta fedha hizo ili kumalizia ujenzi huo, kama njia ya kuunga mkono juhudi za wananchi na wadau, hususani katika mwaka wa fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza napenda kushukuru Serikali yangu sikivu kwa jitihada zake inazozifanya kuibua miradi ya vituo vya Polisi nchini.

Mheshimiwa Spika, kituo cha Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja, kilianza kujengwa toka mwaka 2016, hadi hii leo 2022 kituo hicho bado hakijamalizwa. Kilijengwa kikapigwa plasta baadhi ya vyumba, chooni bado, nje hakijapigwa *plasta* hadi hii leo Polisi wapo Wilaya ya Kati wameazimwa eneo la vitambulisho ndiko wanakofanyia kazi zao. Je, Serikali itamaliza lini Kituo hiki cha Polisi cha Dunga, ili Polisi waweze kufanya kazi kama kawaida?*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake makini juu ya kituo hiki na juhudi zilizofanywa na wananchi katika kujenga kituo hiki mpaka hatua iliyofikiwa, ulituelekeza siku moja hapa na mimi nikajibu kwamba Wizara inaandaa mpango wa kumalizia vituo na kujenga maeneo ambayo hayana vituo kabisa. Kipaumbele kitawekwa kwenye maeneo ambayo tayari wameshajenga vituo kama hawa wa Dunga. Kwa hiyo, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika

mwaka ujao tutafanya kila liwezekanalo ili ukamilishaji wa kituo hicho uweze kuanza.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Ushetu wamejichanga wakafanikiwa kujenga msingi wa Kituo cha Polisi lakini mpaka leo ni zaidi ya miaka mitatu Serikali haijafanya chochote. Sasa, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi kwa wananchi wa Jimbo la Ushetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cherehani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunafahamu Ushetu ni moja ya Wilaya mpya ambazo hazijawa na Vituo vya Polisi ngazi ya Wilaya na kwenye Kata mbalimbali. Pia tunatambua juhudi ambazo zimefanywa na wananchi kuanza ujenzi wa vituo hivi na Serikali inao wajibu wa kusaidia kukamilisha. Ninapenda kumuahidi Mheshimiwa Mbunge kama nilivyokwishasema kwenye jibu la msingi kwamba kipaumbele kitawekwa kwenye maeneo ambayo wananchi na wadau wameanza kujenga vituo hivyo ili kuvisaidia ujenzi huo uweze kukamilika. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ghati Chomete swali la nyongeza.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Wilaya ya Butiama haina Kituo cha Polisi chenye hadhi ya Wilaya. Je, ni lini Serikali itajenga kituo hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ghati Chomete, Mbunge Viti Maalum Mkoa wa Mara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Wilaya ya Butiama ni moja ya Wilaya mpya ambazo hazina Vituo vya Polisi ngazi ya Wilaya na Kata zake mbalimbali hazina vituo hivyo. Kama nilivyokwishasema kwenye jibu langu la msingi, kipaumbele katika ujenzi wa Vituo vya Polisi utazingatia Mikoa, Wilaya na Kata ambazo hazina kabisa vituo lakini msisitizo utawekwa kwa wale ambao tayari wana maeneo na wameanza kujitolea. Kwa hiyo, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba Wilaya ya Butiama ni moja ya eneo litakalozingatiwa katika bajeti ijayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri inabidi Butiama uipe kipaumbele cha ziada. Mheshimiwa Livingstone Lusinde swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza lakini nami niwapongeze Yanga kwa kupata Ubingwa baada ya kusota kwa miaka minne ndiyo leo wanapumua hapa unawasikia, ubingwa ulikuwa

mikononi mwa Simba. Baada ya kuwapongeza naomba niulize swali moja la nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Waziri, utakubali kuongozana nami kufika Mvumi kujionea hali ilivyo kwa askari wa pale Mvumi Misheni ili tuweze kujenga kituo pamoja? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lusinde kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hakuna shida kabisa, baada ya Bunge hili tutazingatia ratiba ili tuweze kuongozana tukatizame changamoto zinazowakabili wananchi wa Kata zako ambako hakuna Vituo vya Polisi ili tuweze kushirikiana kuvikamilisha. Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Malima swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, vitendo vya uhalifu vimekithiri sana katika Kata ya Berege iliyopo Jimbo ya Mpwapwa. Je, Serikali itajenga lini Kituo cha Polisi ili kukabiliana na wimbi hili la uhalifu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George Malima, Mbunge wa Mpwapwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba baadhi ya maeneo hasa Miji inayokua na kuchipua ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa kuna kuongezeka kwa vitendo vya uhalifu. Kama nilivyowahi kusema hapa, uhalifu ni zao la jamii lakini si jambo jema kufanywa na vijana wetu ambao wanazo fursa mbalimbali wakizitumia wanaweza kupata riziki zao bila kulazimika kuleta uhalifu katika jamii. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kulitaka Jeshi la Polisi ngazi ya Mikoa, Wilaya na Kata kuimarisha shughuli za usimamizi wa usalama wa raia na mali zao lakini kuchukua hatua thabiti dhidi ya vijana au watu wanaojihusisha na matendo ya uhalifu. Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii yakuuliza swali la nyongeza. Wananchi wa Jimbo la Kishapu, wadau wa maendeleo pamoja na Mfuko wa Jimbo tumechangia zaidi ya Milioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuambatana na mimi kwenda kuona jitihada za wananchi na kuweka mchango wa Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la

Mheshimiwa Boniphace Butondo, Mbunge wa Kishapu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubali kuongozana na Mheshimiwa Butondo ili kwanza kutambua juhudi zilizofanywa na wananchi, wadau pamoja na yeye mwenyewe kupitia Mfuko wake wa Jimbo. Pili ni kuona namna ambavyo Serikali inaweza kuchangia kukamilisha kituo hiki cha ngazi ya Wilaya. Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi. Ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa Kituo cha Polisi Mbande Kata ya Chamazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdallah Chaurembo Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tunatambua juhudi za Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo lake Mbagala kwa juhudi wanazofanya katika kuimarisha usalama wa raia na mali zao. Kwa kutambua juhudi hizo, nasi kama Serikali kupitia Jeshi la Polisi tutatembelea Kituo cha Mbande kutathmini kiasi gani kinahitajika ili kuweza kumalizia na hivyo kutoa mchango wetu ili kukamilisha kituo hicho kama sehemu ya kuunga mkono juhudi za wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bube Mwakang'ata swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kituo cha Polisi cha Sumbawanga Mjini Mkoani Rukwa ni cha toka enzi za mkoloni, ni kidogo hakina hewa. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa kituo hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua *wilaya* za zamani ikiwemo Wilaya ya Sumbawanga ina Vituo vya Polisi ambavyo moja vimejengwa muda mrefu baadhi vimeanza kuwa chakavu lakini vingine havikidhi haja ya viwango vya Vituo vya Polisi vinavyotakiwa kuwepo sasa hivi ngazi ya Wilaya. Kwa hiyo, ninachukua dhima kumuahidi Mbunge kwamba katika kazi tunayoifanya ya kuimarisha maeneo ambayo hayana kabisa vituo, jambo jingine ni kukarabati na kuboresha vituo vya kizamani ili kuweza kukidhi mahitaji ya sasa. Kwa hiyo, Sumbawanga itakuwa ni eneo litakalozingatiwa.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Jenejelly Ntate swali la nyongeza.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Tuangoma ni Kata yenye mkusanyiko wa watu wengi sana na kata hiyo haina Kituo cha Polisi. Je, ni lini

Mambo ya Ndani mtajenga Kituo cha Polisi pale Kata ya Tuangoma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Janejelly Ntate Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Dar es Salaam kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Tuangoma ni moja ya Kata za Jiji la Dar es Salaam ambao haina Kituo cha Polisi, nimuombe Mheshimiwa Mbunge na especially Mbunge wa Jimbo achangie kidogo na kuhamasisha wadau kushiriki ili Serikali ije isaidiane nanyi kukamilisha, kama ambavyo maeneo mengine wamefanyakazi hiyo. Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Eric Shigongo swali la nyongeza.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, Jimbo la Buchosa lina takriban idadi ya watu wasiopungua 400,000 lakini na kituo cha Polisi katika Mji Mdogo wa Nyehunge ambacho hadhi yake ni ndogo sana. Je, ni lini Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kutembelea kituo hiki ili aweze kukiona na hatimaye kufikia maamuzi ya kujenga kituo kingine?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza

Mheshimiwa Eric Shigongo Mbunge wa Buchosha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni bahati njema kwamba nimepanga kufanya ziara katika Mkoa wa Mwanza na Wilaya hii ni sehemu ya Mkoa wa Mwanza. namuahidi Mheshimiwa Mbunge, nitakapofanya ziara eneo hilo nitatembelea eneo ya Nyehunge ili kuona ni nini tushirikiane na Mbunge kufanya kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi kama njia ya kuimarisha usalama wa raia kwenye maeneo hayo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jerry Silaa swali la nyongeza.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kauli yake kwamba Serikali itaunga mkono jitihada za wananchi. Pale Mzinga Injinia Cyprian Romeja na wananchi wenzake wamechanga Milioni 108 na Mbunge amechangia Milioni 8.7 kwa ujenzi wa Kituo cha Polisi. Je, ni lini Serikali itakamilisha Kituo kile cha Polisi kwa kutuchangia fedha za ujenzi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jerry Silaa Mbunge wa Ukonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nafahamu juhudi za Mheshimiwa Silaa na mara kadhaa amenishirikisha juhudi wanazozifanya ikiwemo kuchangia ujenzi wa vituo hivi, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika mpango

wetu wa uboreshaji, ukamilishaji na uendelezaji wa Vituo vya Polisi eneo la Mzinga ni moja ya Kata itakayozingatiwa katika ukamilishaji huo. Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Wananchi wa Kiharata katika Kata ya Mapinga wamepambana wamepata kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi. Je, Serikali ipo tayari kutusaidia ili tuweze kukamilisha Kituo hicho mapema?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shabani Mbunge wa Bagamoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunafahamu juhudi za Mbunge na wananchi wa Jimbo lake katika kutunza usalama raia na mali zao na uwepo wa Vituo vya Polisi ni moja ya mahitaji ya kukamilisha jambo hilo. Ninamuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutashirikiana nae mwenyewe, wadau wa Wilaya ya Bagamoyo pamoja na wananchi ili kujenga kwenye kiwanja hiki cha Mapinga ambacho wananchi wamejitolea kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho. Ni moja ya eneo tutakaloingia kwenye mipango yetu ya uendelezaji wa Vituo vya Polisi. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ussi Pondeza swali la nyongeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami ningependa nimuulize swali moja dogo la nyongeza Mheshimiwa Waziri. Je, Jimbo langu la Chumbuni tumekuwa na matatizo sana ya hivi vituo na tumekuwa hatuna kituo zaidi ya mwaka wa nne, tumekuwa tukisema sana lakini tumekuwa tukiahidiwa na Wizara kuwa itakuja kushughulikia. Mheshimiwa Waziri upo tayari nasi tukijenge kile kituo kwa nguvu zetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ussi Pondeza Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, natambua juhudi za Mheshimiwa Mbunge, wamefanya mambo mengi katika Jimbo lake ikiwemo kuanza ujenzi wa vituo hivi, nilitembelea huko na nikaona. Ninamuahidi katika maeneo tutakayozingatia na kuyapa kipaumbele katika utekelezaji wa mpango wetu wa ukamilishaji na ujenzi wa vituo, Jimbo la Chumbuni litapewa kipaumbele. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tunakwenda Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe, sasa aulize swali lake.

Na. 399

**Kujenga Mahakama ya Wilaya ya Buhigwe**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya ya Buhigwe ili wananchi waweze kupata huduma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Pinda majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Buhigwe ni moja kati ya miradi ya Mahakama inayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2021/2022. Kupitia programu ya maboresho ya Mahakama, Mkandarasi wa ujenzi wa Mahakama hii amepatikana ambaye ni Lucas *Construction* na kukabidhiwa eneo la ujenzi mwezi Oktoba, 2021. Kazi za ujenzi zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika ifikapo Julai, 2022.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kavejuru Felix swali la nyongeza.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kutujengea mahakama ya Mwanzo katika Tarafa ya Manyovu na Muyama?

Pili, kwa kuwa Tarafa ya Manyovu ina Kata 14 ambazo kijiografia zimesambaa umbali mrefu, Kata Saba zina umbali kwenda Makao Makuu ya Tarafa kati ya kilometa 50 – 84. Je, Serikali inaweza kutusaidia Mahakama mbili za mwanzo katika Tarafa moja ya Manyovu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu ujenzi wa Mahakama hizi mbili alizoziomba katika Tarafa ya Manyovu na Muyama hizi zipo katika mpango ambao tulikwishaueleza huko nyuma kwamba tunakwenda kujenga Mahakama katika Tarafa zote nchini na *program* hii itakwisha 2025 ambapo tuna uhakika Tarafa zote zitakuwa zimepata Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kata ambazo zipo mbali na Makao Makuu ya Tarafa, ofisi yangu imeweka utaratibu wa kufanya *assessment* kutoka kwenye Makao Makuu ya Tarafa na itatoa upendeleo kwa Kata zile ambazo ziko mbali. Kwa hiyo, nina uhakika kabisa kwa sababu baada ya Bunge hili ziara yangu ya kwanza ni Kigoma, tutakwenda kuangalia hiyo na kuipa umuhimu unaostahiki.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Mahakama za Mwanzo hasa zilizopo Vijijini ambazo miundombinu yake imechakaa sana, ikiwepo Mahakama ya Gonja Maore, Jimbo la Same Mashariki katika Mkoa wa Kilimanjaro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuena kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mahakama nyingi za mwanzo zilijengwa katika mfumo ambao ni wa kizamani sana, na kwa sasa tunaendelea kuziondoa zingine katika sura kabisa ya Mahakama ulivyo sasa ili tujenge Mahakama nyingine nzuri zaidi. Kuhusu ukarabati kwa zile ambazo tunaziangalia kama zinaweza zikarekebika hizo ndizo tunaziwekea mpango wa kwenda kuzifanyia ukarabati na zoezi hilo linaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Gonja, Mahakama za Mwanzo kama nilivyoeleza kwamba tutazipitia nazo kuangalia namna ambavyo tunaweza tukazifanyia kazi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwenye bajeti iliyopita tulitengewa fedha kwa ajili ya kujenga Mahakama ya Wilaya ya Kyerwa lakini mpaka sasa Mahakama hiyo haijaanza kujengwa. Ni lini Serikali itaanza ujenzi ili kuondoa adha wanayoipata wananchi wa Wilaya ya Kyerwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; nipende kujibu swali la Mheshimiwa Bilakwate Mbunge wa Kyerwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika mpangokazi wa Wizara yangu tulipanga kuanzisha ujenzi wa Mahakama hii, iko kwenye mpango wa 2021/2022. Ninapenda tu kumuahidi kwanza Mheshimiwa Mbunge kwamba baada kikao hiki tutawasiliana kuona kama kuna uhakika wowote mradi huo haujaanza kwa sababu ofisi yangu haijapokea taarifa za kutoanza kwa mradi huu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amandus Chinguile swali la nyongeza.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Jengo la Mahakama ya Wilaya ya Nachingwea ni chakavu na limejengwa tangu enzi za wakoloni. Je, nini mpango wa Serikali wa kujenga jengo jipya litakaloendana na hadhi ya Wilaya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Nachingwea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwamba ni kweli kama nilivyoeleza kwenye swali ambalo nimetoka kulijibu muda siyo mrafu, tunayo majengo ambayo yamechakaa lakini tunayo majengo ambayo yamekosa hadhi, kwa maana ya uhalisia wa miradi tuliyonayo kwa mwaka huu ambao unakwenda kumalizika tulikuwa tulikuwa na miradi 22, mwaka ujao tutakuwa na miradi 13 na inawezekana kabisa katika mwaka ujao ukawa umeingia kwenye mpango wa kuangalia uwezekano wa kujengewa Mahakama nyingine. Kwa hiyo, naomba tu Mbunge awe na utulivu katika kipindi hiki kwa sababu miradi yote mpaka kufikia 2025 tutakuwa tumekamilisha majengo yote ya ngazi ya Wilaya asante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdallah Juma swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, asante sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali kupitia Mahakama zake imejenga Mahakama za Wilaya kwa kiwango safi kabisa. Je, ni lini Serikali itakamilisha kujenga Mahakama za Wilaya zote Tanzania kwa kiwango kama kile ambacho wameshajenga? ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma (Mshua) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza sehemu zote zenye Mahakama, zenye majengo ambayo yanaendelea kutumika hatuna mpango wa kwenda kuvunja na kuanza upya. Tuna mpango wa kujenga mahakama katika maeneo ambayo hayana mahakama kabisa lakini tutakarabati kwa kiwango bora zaidi kwenye yale majengo ambayo sasa yameendelea kutumika asante.

**SPIKA:** Eh naona Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesimama, karibu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria ameendelea kuyatoa kuhusiana na miundombinu ya Mahakama. Ningependa kuongeza taarifa ya uhakika kwamba Mahakama ya Tanzania ilishafanya utafiti wa hali ya miundombinu ya Mahakama nchi nzima kwa ngazi ya Mahakama za Wilaya, Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama Kuu. Kwa hiyo, upo mpango wa miaka mitano unaohusu ujenzi wa miundombinu ya Mahakama. Mpango ambao unaendana na mpango mkakati wa Mahakama ambao unaendana na kiasi cha fedha kilichotengwa kwa mahala ambako hakuna jengo la Mahakama kabisa, vilevile fedha iliyotengwa kwa Mahakama zinazohitaji ukarabati.

Mheshimiwa Spika, nitaomba labda Wizara ya Katiba na Sheria inachoweza kufanya ni kuwasilisha ule mpango ofisini kwako ili baadae mpango huo uweze

kufikika kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Pia tutaangalia uwezekano vilevile nakala kwa njia laini kama itawezekana ukaweza kuwa *accessible* na kila Mbunge. Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa baada ya majibu hayo naona bado mmesimama Mheshimiwa Josephine Genzabuke swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali iliahidi kujenga jengo la Mahakama katika Tarafa ya Heru, tarafa maalum ambayo alikuwa akiishi Mwami Theresa Ntare. Je, ni lini sasa Serikali itajenga jengo kumuenzi Mwami Theresa Ntare? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, samahani hilo jina la Tarafa sijalisikia vizuri ili niliweke kwenye kumbukumbu sahihi.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Heru aliyokuwa akiishi Mwami Theresa Ntale.

**SPIKA:** Haya karibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba tunapopeleka miradi kwenye maeneo mbalimbali tunapeleka kwa ajili ya mahitaji ya watu, sina uhakika sana kama tutakuwa tukipeleka kwa majina ya watu. Mimi ninapenda tu kumhakikishia kwamba eneo hilo kwa mahitaji yake tutakwenda kulipitia na kuona umuhimu wa kuweka hilo jengo lakini siyo kwa sababu aliishi mtu Fulani. Ahsate.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Jengo linalotumika katika Mahakama ya Wilaya katika Wilaya ya Meatu halikidhi hadhi kwa sababu lilikuwa ni Mahakama ya Mwanzo tukiwa Wilaya ya Maswa. Je, Serikali iko tayari kutujengea jengo jingine kwa kuwa eneo la kujenga Mahakama ya Wilaya tunalo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Leah Komanya Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari kujenga jengo la Wilaya kama tu wanaendelea kutumia majengo ambayo hayakuwa mahsusi kwa ajili ya Mahakama za Wilaya. Kama tulivyoeleza hapo mwanzo tayari wako kwenye mpango na tutakapowasilisha ofisini kwako na kuwatumia wao wataona kila mtu kwenye *position* yake Mahakama yake inajengwa lini. Asante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Josephat Kandege swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kalambo ni miongoni mwa Wilaya ambazo hazina Mahakama za Wilaya na tayari kiwanja kilishapatikana kwa ajili ya ujenzi wa ujenzi wa Mahakama ya Wilaya. Je, Serikali ina kauli gani kwa ajili ya kujenga Mahakama katika Wilaya ya Kalambo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Josephati Kandege Mbunge wa Kalambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya utangulizi ni kwamba Serikali iko kwenye mkakati wa kujenga Mahakama za Wilaya na mradi huu utachukua kama alivyouleza *AG* unaishia 2025/2026. Kwa hiyo napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba anakwenda kujengewa Mahakama ndani ya kipindi hiki nilichokitaja na nitawasiliana nae kumpa uhalisia wa mwaka ambapo tunapeleka mradi wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome Makamba swali la nyongeza.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi. Kwanza kabisa niwapongeze Serikali kwa kutujengea Mahakama Kuu nzuri na ya kisasa katika Jimbo la Shinyanga Mjini. Swali langu Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Mwanzo na Mahakama ya Hakimu Mkazi imechakaa sana, *actually* ilijengwa tangu kipindi cha ukoloni. Nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba Mahakama hizo zinakarabatiwa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Makamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoeleza katika mpango wetu kwamba tumetenga fedha za kukarabati majengo yote chakavu nchini na kujenga mapya katika maeneo yale ambayo yana uhitaji huo. Ninakuahidi tu Mheshimiwa Mbunge uvute subira kidogo utaona kazi inaendelea kule kwa ajili ya ukarabati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Almasi Maige swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kweli kuniruhusu na mimi niulize swali la nyongeza. Mahakama ya Wilaya ya Uyui inafanyakazi katika chumba kidogo kilichoazimwa kutoka kwa *DC*. Je, lini Serikali itajenga jengo la Mahakama ya Uyui?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maige Mbunge wa Uyuwi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kule tuna mradi tayari unaendelea na tutafuatilia kuona unakamilika lini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDUMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Itilima ni Wilaya mpya haina jengo la Mahakama.

Je, ni lini Serikali itajenga jengo hilo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Kwimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Kwimba ni Wilaya mpya na katika maelezo yangu ya utangulizi nimeeleza uhalisia wa mpango kazi ambao tunakwenda nao. Mimi nitapenda tu kuwasiliana nae baada ya kipindi hiki leo hii ili nimpe kalenda ya ujenzi utakavyoanza katika eneo lake la Kwimba. Ingawa katika mazingira ya kawaida Kwimba ipo katika mpango wa 2021/2022 *program* ambayo nina uhakika kabisa Kwimba kuna jengo linaendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa kule nyuma sijui ni Mbunge wa Jimbo gani, Mheshimiwa Shekilindi swali la nyongeza.

**MHE. SHABAN O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mahakama ya Wilaya ya Lushoto ni ya zamani tangia mkoloni. Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati au kujenga Mahakama mpya Wilayani Lushoto?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shekilindi Mbunge wa Lushoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Lushoto nilifanya ziara hivi karibuni na tayari wataalam walishafanya *assessment* juu ya ukarabati ule. Kwa hiyo, muda wowote jengo lile la Wilaya linaweza likaanza ukarabati. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza nishukuru Serikali kwa kujenga Mahakama ya Hydom imekamilika kabisa. Je, ni lini sasa Mheshimiwa Waziri mnafungua Mahakama ile ya Hydom ili ipate kutumika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hydom tayari jengo limeshakamilika na utaratibu wa matumizi unaweza ukaanza wakati wowote. Lini tutakwenda kuzindua rasmi ni mpango wa Mahakama ambao huwa wana utaratibu ambao wanautumia katika kwenda kuzindua na uanzishwaji wa matumizi ya Mahakama. Juzi Waziri wangu alikuwa pale Hydom kuangalia hilo jengo na nina

uhakika kabisa Mheshimiwa Mbunge alikubaliana jambo na Mheshimiwa Waziri. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge ahsante sana. Waheshimiwa tunaenda Wizara ya Afya Mheshimiwa Santiel Erick Kirumba Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 400

**Kitengo cha Watoto Njiti - Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga**

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaboresha Kitengo cha Watoto Njiti katika Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Santiel Erick Kirumba Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga kwa sasa ina sehemu maalum yenye uwezo wa kulaza Watoto Njiti 18 kwa wakati mmoja. Hata hivyo, ujenzi unaendelea wa Bilioni 1.2 utakaowezesha hospitali kuwa na vitanda 42. Kwenye bajeti ya mwaka 2022/2023 zimetengwa Shilingi Bilioni Sita kwa ajili ya ujenzi.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Santiel Erick Kirumba swali la nyongeza.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Je, Mheshimiwa Waziri uko tayari kuambatana na mimi ili ukaweze kunidhibitishia mradi huu utakamilika mwaka huu wa fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili kutokana na changamoto nyingi wanawake wanazozipitia kipindi wanachokuwa wajawazito; Je, Serikali haioni haja kushusha huduma hii Wilayani ili tuweze kupata huduma hii kwa Mkoa wa Shinyanga kwa Watoto Njiti? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Santiel Erick Kirumba Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja niko tayari kuandamana naye kwenda Shinyanga na nitafurahi tukiwa wawili tu peke yetu. Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni kwamba Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kupeleka kwenye hospitali za Wilaya huduma hizi. Kwenye bajeti yetu Mheshimiwa Waziri wa Afya Ummy Mwalimu alisema kwamba, kwa mwaka huu unaokuja wa fedha tunaenda kujenga sehemu za Watoto Njiti 100 na siyo tu kwenye hospitali za Wilaya na kwenye Vituo vya Afya. Kwa hiyo, fedha zimeshapatikana sasa imebaki kuwasiliana na Waziri wa TAMISEMI ili kupanga sehemu za vipaumbele vya kuanza na kwa jiografia ya Mkoa wa Shinyanga ni mojawapo ya maeneo yataenda kufaidika na huu ujenzi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye jibu lako la mwanzo hiyo ziara aliyoiomba Mheshimiwa Mbunge ni ziara ya kikazi kwa hiyo lazima uambatane na *DMO,* sijui Mganga Mkuu wa kufanyaje, uambatane nao usiende wewe peke yako na Mbunge. Waheshimiwa Wabunge nawaona wengi mmesimama niwakumbushe tu swali la msingi linahusu kitengo cha Watoto Njiti niwakumbushe.

Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Hospitali ya Mkoa ya Tumbwi siyo kwamba inahudumia watu wa Pwani tu na wale wapita njia. Kitengo cha Watoto Njiti kweli kipo lakini uboreshaji ni pamoja na vifaa tiba. Watoto wanazaliwa pale lakini inabidi wakimbizwe.

Je, ni lini Serikali pamoja na kuboresha kitengo cha Watoto Njiti na vifaa tiba vitaboreshwa lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dokta Kaijage kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwamba Hospitali ya Tumbwi ni mojawapo kweli kuna eneo la Watoto Njiti lakini hospitali inazidiwa. Katika Bilioni 59.3 ambazo zimetengwa kwa ajili ya uboreshaji, Hospitali ya Mkoa wa Tumbi ipo mojawapo na eneo ambalo limetengewa hela kwa ajili ya kulipanua na kuongezea vitanda ni eneo hilo la Watoto Njiti. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zainab Katimba swali la nyongeza.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, Serikali haioni haja ya kumjumuisha mtoto njiti kwenye Bima ya Mama yake ili pindi anapozaliwa aweze kupata huduma hiyo na kumwondolea Mama mwenye mtoto njiti adha ya kuanza kufanya usajili wa mtoto kwenye Bima ya Afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, swali aliloliuliza Mbunge ni swali muhimu sana na nitumie fursa hii kumwagiza Mkurugenzi Mkuu wa Bima ya Afya kwamba suala la kuhudumia mtoto njiti ambaye mama yake ana bima yake ya afya lisiwe mjadala. Mtoto njiti akizaliwa na huduma yake inakuwa ni *automatic*. Vilevile kwa sababu tunakwenda kwenye suala la bima ya afya kwa watu wote Wabunge wote tukumbuke hayo mambo tuhakikishe sasa tutaweka kwenye sheria ijayo iweze kufanyika vizuri zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Katika Hospitali yetu ya Mkoa wa Iringa tuna kitengo cha Watoto Njiti na tuna upungufu mkubwa wa mashine na dawa inaitwa *Lung surfactant* ambayo dozi moja inauzwa Shilingi Laki Tano na mtoto ili a-*survive* anahitaji dozi tatu. Serikali ina mpango gani kuangalia kwamba dawa hizi angalau zinawekewa ruzuku ili kupunguza gharama hiyo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, moja kwanza sioy dawa kuwekewa ruzuku kwa taratibu na sheria na taratibu za Wizara ya Afya ni kwamba huduma ya mtoto chini ya miaka Mitano *including* hawo Watoto Njiti na Mama na Mtoto ni bure. Kwa maana kwamba tunaposema mlitupitishia bilioni 200 kwa ajili ya kununua dawa na vifaatiba. Hilo eneo tutakwenda kulielekeza nguvu nyingi kuhakikisha kwamba Watoto njiti hawawezi kukutana na matatizo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dokta Christina Mnzava swali la nyongeza.

**MHE. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, Hospitali ya Kahama inahudumia watu kutoka pembezoni kwa maana ya Mikoa ya Tabora pamoja na Geita. Je, ni lini Serikali itaboresha kituo cha Watoto njiti pale Hospitali ya Kahama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nijibu swali la Mheshimiwa hapa, ukisikia Serikali inasema inajenga vituo vya afya kwa kila Tarafa na kazi ile imeendelea kufanyika kupitia TAMISEMI ni kwenda kupunguza wagonjwa ambao sasa wanaenda kurundikana kwenye hospitali moja kama ilivyo Kahama.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri Mbunge ni muhimu tukatembelea hospitali hiyo inawezekana tukikaa mle ndani tutaona tu maeneo ambayo tunaweza tukaweka

sehemu ya Watoto njiti, ibaki kazi ya kuleta vifaa na kuvipachika na Watoto waweze kupata huduma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Serikali imetueleza kwamba wana mpango wa kujenga vituo 100 vya Watoto Njiti hapa nchini; Je, sisi ni miongoni mwa watu tutakaofaidika Jimbo letu la Mchinga kwa kituo hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wao ni wafaidika na Wilaya yake ni sehemu ambayo inafaidika, kuna utaratibu ambao unatumika hata ndani ya miezi miwili ijayo kuna vifaa vinapelekwa kwenye Jimbo lake kwa ajili ya huduma ya Watoto Njiti.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Lugangila swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Ni dhahiri kwamba viko visababishi ambavyo vinapelekea mama kujifungua mtoto njiti ikiwemo mahitaji ya lishe. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inaimarisha huduma za lishe kwa akina mama wajawazito ili waweze kufikisha *full term* yaani mtoto azaliwe ndani ya umri anaotakiwa kuzaliwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy Mwalimu ameshaelekeza, kumekuwepo na makongamano mengi, kumekuwepo na semina nyingi ambazo zinazungumzia suala zima la lishe. Sasa badala ya kufanya makongamano na semina fedha hizo zitaelekezwa kununua vitamini ambazo zina *multiple vitamin* na akina mama wajawazito wote wanapewa hizo *vitamin*. Lakini niendelee kuwaomba Wabunge wa kike na wa kiume mojawapo ya sababu za Watoto Njiti ni *stress.* Sisi wote tunapofika mahali kina mama wajawazito wanakuwepo tuhakikishe mazingira yao ya kufanya kazi lakini sisi wanaume tuwe karibu nao ili kuondokana na mambo mengine yanayoweza kuzuilika yanayosababisha uwepo wa Watoto Njiti.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dokta Charles Kimei swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Swali langu nilikaa nikafikiri kwamba *ultrasound machine* pamoja na x-rays ni muhimu sana kwenye suala zima la Watoto Njiti. Kwa hiyo nilitaka nimuulize Waziri kwamba ni lini watepeleka *ultrasound machine* na *x-ray* katika kituo cha Afya Himo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, labda nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mimi na yeye nikimaliza haya maswali kama kituo chake hakina *ultrasound* tukae chini ili tuweze kuelekeza *MSD* wapeleke mara moja *ultrasound* kwenye eneo lake. Pia suala la *x-ray* kuna fedha zile ambazo Waziri wa Afya amesema zimeokolewa tumefanikiwa vilevile kupata *x-ray* 33 za ziada, kwa hiyo katika hiyo ziada tutaona tunaelekeza

maeneo gani baada ya watalaam kuchakata na kuona vipaumbele.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Tunayo changamoto kubwa sana katika Hospitali ya Rufaa ya Kitete iliyopo Mkoani Tabora ya chumba ama kitengo maalum kwa ajili ya Watoto Njiti. Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha kitengo hiki ili kuweza kukidhi mahitaji yaliyopo hivi sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Katika hospitali ambazo zimetengewa fedha kwa mwaka huu wa fedha Bilioni 59.3 mojawapo ni hospitali ya Kitete. Kwa maana hiyo eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge unalisema tutaenda kulingalia kwa umakini zaidi. Pia maeneo ya kutembelea inawezekana tatizo siyo sehemu ya kuweka Watoto Njiti lakini maamuzi katika kupanga vyumba inawezekana tunahitaji tu vifaa. Tutaenda kuangalia kwa pamoja Mheshimiwa Mbunge halafu tuone tunafanya nini kama ni uhitaji wa vifaa tutaweka vifaa mapema. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar swali la nyongeza.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa ni ahadi ya CCM ya kuimarisha ushirikiano baina ya Wizara hizi ambazo siyo za Muungano. Je, Wizara ya Afya inashirikianaje na Wizara ya Afya ya

Zanzibar kwenye kutatua changamoto hizi za Watoto Njiti? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, anachokisema Mbunge ni kweli na nimejaribu kutembelea baadhi ya maeneo upande wa Taifa letu upande wa Visiwani ni kweli kunahitajika maboresho makubwa sana kwenye huduma za afya. Jana Mheshimiwa Waziri wa Afya Ummy Mwalimu alikuwa anajadiliana na baadhi ya wadau ili kuona ni namna gani hawa wadau ambao wanatoa huduma huku upande wa Bara waweze kwenda upande wa pili wa visiwani na kuweza kuboresha miundombinu ya afya badala ya kupeleka fedha kwenye maeneo hayo. Tayari *AMREF* wamekubali kuelekea upande huo wa pili kwa ajili ya kuboresha maeneo unayosema Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kabula Enock Shitobelo swali la nyongeza.

**MHE. KABULA E. SHITOBELO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mkoa wa Mwanza una hospitali na vituo ambavyo bado havijapata huduma hii ya chumba cha mtoto njiti.

Je, Serikali lini itakamilisha kutuwekea vyumba maalum kwa mtoto njiti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli anavyosema lakini kwenye hospitali ya Sekou-Toure ya Mkoa wa Mwanza ujenzi mkubwa sana unaendelea,

suala ni kwenda kuamua na kuweka vifaa kwenye eneo hilo ili watoto waweze kupata huduma. Nafikiri anazungumzia Mkoa mzima kwa ujumla na hasa maeneo ya visiwani. Kwa mfano, Ukerewe ambako ni Visiwani sasa hospitali ya Wilaya ile inaenda kujengwa kwa *level* ya hospitali ya Mkoa ili mambo yote ya Rufaa ya Mkoa yaweze kutolewa huko huko Visiwani. Kwa hiyo, tutaendelea kufanya ziara na kugundua matatizo mbalimbali kwenye maeneo na kuelekeza fedha kadri ya mahitaji ya maeneo husika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Katibu!

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI**

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika,

KWA KUWA, timu yetu ya Taifa ya Soka ya Watu wenye Ulemavu *(Tembo Warriors)* imefuzu kushiriki fainali za Kombe la Dunia kwa watu wenye Ulemavu zitakazofanyika Uturuki mwezi Oktoba mwaka 2022;

NA KWA KUWA, Tarehe 07 Juni, 2022 siku Timu ya *Serengeti Girls* ilipokaribishwa Bungeni kwa ajili ya kupongezwa kwa kufuzu fainali za kombe la Dunia Mheshimiwa Spika alitoa maelekezo kwamba Timu ya Tembo *Warriors* iletwe Bungeni kwa ajili ya kupongezwa

kwa sababu ushindi walioupata ni jambo la kupongezwa na wananchi wote ikiwepo sisi Wabunge kwani inaipa Taifa letu sifa kubwa;

NA KWA KUWA, Bunge la Jamhuri ya Tanzania lina utaratibu wa kupongeza timu zetu zinapofanya vizuri, jambo ambalo huongeza morali kwa wachezaji katika kufanya vizuri zaidi;

NA KWA KUWA, timu ya Tembo *Warriors* ipo hapa Bungeni mahsusi kwa ajili ya kupongezwa na Bunge na itapendeza endapo pongezi hizi watazipata vizuri wakiingia ndani ya Bunge;

NA KWA KUWA, Kanuni ya 160(1) inaelekeza kwamba wageni wanaoruhusiwa kuingia Bungeni watakaa maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili yao pasipo kuingia ndani ya Ukumbi wa Bunge;

HIVYO BASI, kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kuweza kutoa pongezi zake kwa Timu ya Tembo *Warriors* kwa utaratibu wa Kibunge, Kanuni ya 160(1) itenguliwe ili kuwezesha Timu ya Tembo *Warriors* pamoja na Viongozi wake waingine ndani ya Bunge na kupongezwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, nitawahoji kuhusu *Tembo Warriors* kuingia Bungeni.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Kutengua Kanuni iliafikiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa kabla Tembo *Warriors* hawajaingia humu ndani nitangaze wageni tulionao. Wakati nikitangaza wageni kwa sababu Wabunge hamruhusiwi kusimama wakati mimi nikiwa nimesimama ama kutembea nitawaruhusu waliopo upande wangu wa kulia watafute sehemu za kukaa ili wawaachie hiyo sehemu Tembo *Warriors* wakati natangaza matangazo ya wageni.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na wageni waliopo Jukwaa la Spika, kwanza ni wageni 142 wa Bunge ambao ni wajumbe….

Waheshimiwa Wabunge nimetoa nafasi ya kuhama na siyo kuzungumza ili muwe mnasikiliza matangazo.

Tunao wageni 142 wa Bunge ambao ni Wajumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania wa Chama cha Mapinduzi (UWT) kwa mwaka 2018-2022. Karibu sana Viongozi wetu wa Wanawake wa nchi hii, karibu sana Bungeni. Kwa uwakilishi wameambatana ama wameongozwa na Ndugu Gaudensia Mugosi Kabaka, ambaye ni Mwenyekiti wa *UWT,* pia yupo Ndugu Thuwaybah Edington Kissasi, ambaye ni Makamu Mwenyekiti, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Dkt. Philis Misheck Nyimbi, ambaye ni Katibu Mkuu, karibuni sana Viongozi wetu wa Wanawake wa Chama cha Mapinduzi. Katika Wajumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania wapo pia Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji ambao ni sehemu ya Wajumbe hao, karibu sana. Wabunge Wanawake wa Chama cha Mapinduzi na Wabunge Wanaume wa Chama cha Mapinduzi watakaohitaji kuwasalimia Wajumbe wa Baraza watakuwepo Msekwa baada ya muda wa kusitisha shughuli za Bunge mchana. Kwa hiyo, mnakaribishwa sana kuja kuzungumza nao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 41 wa Bunge ambao ni Viongozi Kamati ya Amani na Jumuiya ya Maridhiano Tanzania wakiongozwa na Sheikh Alhad Mussa Salum, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Amani na Jumuiya ya Maridhiano Tanzania, karibuni sana Viongozi wetu, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwataje alioambatana nao kwa uwakilishi yupo Mchungaji Elias Silayo ambaye ni Makamu Mweyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano Tanzania. Yupo pia Askofu Daktari Israel Maasa, ambaye ni Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Maridhiano Tanzania. Yupo pia Mheshimiwa Ole Kisongo, ambaye ni Kiongozi wa Masai na Mjumbe wa Jumuiya ya Maridhiano Tanzania, sasa hapa ameitwa Mheshimiwa Ole Kisongo lakini huyu ni *Chief* wa Wamasai pia. Yupo pia Mheshimiwa Mohamed Waseem, Mdhamini Jumuiya ya Maridhiano. Yupo pia Azim Dewji ambaye ni Mdhamini Jumuiya ya Maridhiano, karibu sana. Yupo pia Mchungaji Ilikupitye Pannasekara, ambaye ni Kiongozi wa Bundha Afrika. Yupo pia Mheshimiwa Philemon Molel, ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Maadili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Mheshimiwa Asha Nasoro, Mhazini wa Jumuiya ya Maridhiano Tanzania. Yupo pia Askofu Laurent Kameta, ambaye ni Mjumbe Kamati za Amani, karibu sana. Yupo pia Mheshimiwa Balozi Mohamed Badawy, Kiongozi wa Mabalozi Tanzania, karibu sana. Yupo pia Sheikh Nurdin Mangochi, ambaye ni Mshauri Kamati za Amani, karibu sana. Yupo pia Mheshimiwa Riyaadh Mohamed Husein, ambaye ni Mjumbe Kamati za Amani. Yupo pia Mheshimiwa Altaf Mansuurali, ambaye ni Mshauri kamati za Amani Tanzania. Yupo pia Profesa Emmanuel Shija, Katibu Kamati za Maadili. Yupo na Mheshimiwa Amran Batenga, ambaye ni Mjumbe Halmashauri Kuu Mwanza. Tunawashukuru sana Viongozi wetu kwa kuendelea kudumisha amani yetu hapa nchini na karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni wengine wa Bunge ambaye ni Mchungaji Boniface Mwamposa na Wachungaji wengine wawili ambao ameambatana nao, karibu sana. Hapa yupo Mchungaji Mwamposa, yupo Mchungaji John Ssekalala na Askofu Jonathan Shemhambo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni Sita wa Bunge ambao ni Watendaji wa Kampuni ya *Silent Ocean Limited* wakiongozwa na Mohamed Kamilag, ambaye ni Mkurugenzi wa Mauzo na Masoko na Ndugu Rachel Sindbad, Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Abdallah Ulega ambaye ni Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi na hawa ni familia yake, ikiongozwa

na Mke wake Bi. Mariam, karibu sana. Sasa katika hii familia yake huyu mgeni mmoja inabidi atajwe mahsusi kwa sababu ana jina kama langu naye anaitwa Tulia Abdallah Ulega, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, jina hili kama mnakumbuka lilitolewa hapa Bungeni Juni, 2016 kwa hivyo leo ni siku yake ya kuzaliwa jamani Binti Tulia. Haya ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wa Waheshimiwa Wabunge ambao tunao hapa ndani. Tunaomba Waheshimiwa wageni hawa wa Waheshimiwa Wabunge wasimame kwa pamoja tuwatambue, karibu sana wageni wetu, nadhani mmewaona Wabunge wenu wakiwawakilisha vizuri humu ndani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni pia waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wapo wanafunzi 11 kutoka Chuo Kikuu Huria Tanzania, wanafunzi 11 karibuni sana Bungeni. Tunao pia Viongozi 23 wa Tawi la Chama cha Mapinduzi Mji Mpya kutoka Jijini Mbeya, sijui wamekaa upande gani hawa, haya pengine hawajapata nafasi ya kuingia, lakini hapa nimeletewa taarifa kwamba kuna Askofu Eliud Isangya, ambaye ni Mjumbe Kamati za Maadili, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sababu tumeshaafiki hoja ya kutengua Kanuni na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu wakati ule walipokuja hapa Serengeti *Girls* kwa kuwa walikuwa wamefuzu na sisi tukawapongeza na nikaaelekeza waletwe Tembo *Warriors* kwa sababu na wao wamefuzu kwenda kucheza Kombe la Dunia kwa Kombe la Watu wenye Ulemavu. Lakini sasa kabla hawajaingia hapa Mheshimiwa Waziri amenipa taarifa

ambayo nadhani itatolewa hapa sasa maalum, siku ile mtakumbuka nilisema wale watu waletwe kama kesho yake hivi halafu tukaambiwa wako Poland ama wanasafiri kwenda Poland. Kwa hiyo tukasema wataletwa siku nyingine wakisharejea. Sasa huko Poland nimeletewa taarifa hapa kwamba wamefanya mambo mazuri. Tembo *warriors* wameshinda tuzo ya timu bora nchini Poland kwenye mashindano yaliyojumuisha timu za nchi nne. Kwa hiyo wamefanya vizuri huko Poland lakini pia, mchezaji wa Tanzania ndiyo amekuwa mfungaji bora wa mashindano hayo nchini Poland. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, sasa kwa heshima kubwa kabisa niwakaribishe *Tembo Warriors* waingie humu ndani ili wapate fursa ya kupongezwa kwa kufuzu kwenda kushiriki Kombe la Dunia. Karibuni sana, *Sergeant At Arms* tuletee Tembo *Warriors. (Makofi)*

*(Hapa Timu ya Taifa ya Watu Wenye Ulemavu Tembo Warriors Iliingia Ukumbini)*

**SPIKA:** *Sergeant-At-Arms* ahsanteni sana. Wakati wanamalizia kuketi, nimuite Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, aje aseme machache kuhusu timu yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri nimeshakuruhusu kusema machache.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujalia afya njema sote na kwa kukutana hapa siku ya leo na kutuwezesha kufanikisha shughuli hii muhimu ya Kitaifa. Kwa namna ya kipekee kabisa nitumie fursa hii

kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuliongoza vyema Taifa hili kwa misingi ya haki na usawa. Hakika fikra na maono yake yanazidi kuliimarisha na kulishamirisha Taifa letu ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, aidha nikushukuru wewe binafsi kwa namna unavyoendelea kuliongoza Bunge hili Tukufu sambamba na maelekezo yako mbalimbali unayotupatia kwa ajili ya utekelezaji katika Wizara ikiwa ni pamoja na agizo hili la kuileta Bungeni Timu yetu ya Taifa ya *Soccer* la Walemavu *(*Tembo *Warriors)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwapa heshima hapa Bungeni mashujaa wetu, Timu ya Taifa ya *Soccer* ya Vijana Wanawake wenye umri chini ya miaka 17 *(Serengeti Girls)* kwa mara nyingine tena leo hii nimesimama hapa mbele naomba idhini yako kuwatambulisha mashujaa wetu wengine hawa, Timu ya Taifa ya *Soccer* la Walemavu *(Tembo Warriors)* ambayo imealikwa hapa Bungeni na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, mahsusi kwa ajili ya kupongezwa pamoja na kusalimiana ana kwa ana na Waheshimiwa Wabunge na Viongozi mbalimbali wa Serikali kwa ujumla. Timu yetu ya Taifa ya Soka la Walemavu *(Tembo Warriors)* nayo imetutoa kimasomaso baada ya kufuzu kwenda kucheza Kombe la Dunia nchini Uturuki katika mashindano yatakayofanyika mwezi Oktoba, 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa mashindano yaliyoshirikisha zaidi ya nchi 13 za Afrika na kufanyika Jijini Dar es Salaam, Tanzania. Itakumbukwa kuwa, juhudi za ushindi huo zilichagizwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, alipomtuma Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenda kambini kuwaongezea ari na hamasa wachezaji pamoja na kutoa kiasi cha Shilingi Milioni 150 zilizosaidia kuitunza Timu yetu ya Taifa pamoja na maandalizi mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakika ilikuwa ni wakati wa jasho na damu, kufa ama kupona kwa ajili ya kupambania maslahi ya Taifa kwa Tembo *Warriors,* ili kupata nafasi hiyo walifanikiwa kufanya yafuatayo:-

Moja, waliikong'ota timu ya Morocco mabao mawili kwa moja; waliipiku timu ya Sierra Leone bao moja kwa bila; na tatu, waliichakaza timu ya Cameroon kwa mabao matano kwa bila. Timu hii kwa sasa ipo kambini tangu mwezi Februari, 2022 kwa maandalizi ya mashindano ya Kombe la Dunia yatakayofanyika nchini Uturuki kwa Mwezi Septemba na Oktoba, 2022 ambapo Serikali ndiyo inagharamia kambi hiyo kwa matumizi yote ikiwemo malazi, chakula, ufundi, usafiri wa ndani na nje, pamoja na posho za wachezaji na *bench* lao la ufundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha maandalizi ya timu hii tarehe 09/06/2022 mpaka tarehe 13/06/2022 timu yetu hii ilishiriki michezo mitatu ya kimataifa ya majaribio nchini Poland ambayo ilijumuisha pia nchi ya Morocco, Italia, Uingereza na Poland ambapo tulishinda mechi moja katika mashindano hayo. Pamoja na kwamba, *Tembo Warriors* haikuchukua ubingwa, lakini mchezaji wetu Alfan Athumani Kyanga aliibuka mfungaji bora kwa kuweka kapuni magoli Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Alfan Athumani Kyanga ndiye alikuwa mfungaji bora kwa kuweka nyavuni magoli sita na kutunukiwa tuzo ya mfungaji bora. Sambamba na hilo pia timu yetu imepewa tuzo ya kuwa timu bora na yenye nidhamu katika michuano hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizo ni jitihada za kuiimarisha timu ili iweze kufanya vizuri katika mashindano ya dunia. Aidha, Serikali ndio imefanikisha safari hiyo kwa ajili ya kushiriki mechi hizo maalum za maandalizi ya Kombe la Dunia kwa Watu Wenye Ulemavu. Ni matumaini yangu kuwa mazoezi hayo waliyoyapata yatawasaidia kujirekebisha na kujiimarisha zaidi kwani watakuwa wameona taswira ya mashindano ya Kombe la Dunia. *(Makofi)*.

Mheshimiwa Spika, kambi ya timu sasa inahamia Karatu, mahali penye utulivu zaidi na ukimya ili wamalizie maandalizi yao kabla ya kwenda Nchini Uturuki. Hivyo, Serikali kwa kushirikiana na wadau ikiwemo Shrikisho la Mpira wa Miguu Tanzania *(TFF)* itahakikisha kuwa timu hiyo inaendelea kupatiwa malezi na mafunzo yanayostahili ili kuweza kufanya vizuri katika mashindano hayo ya dunia yanayotarajiwa kuanza tarehe 28/09/2022 hadi tarehe 09/10/2022 nchini Uturuki ambapo Tanzania itaungana pamoja na nchi nyingine kutoka Bara la Afrika ikiwemo Morocco, Misri na Angola nazo zitashiriki mashindano hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu ni mwendelezo wa mafanikio lukuki yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka mmoja tangu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, aingie madarakani na hii inatokana na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau wa michezo ndio zimesababisha kufikia hatua hii ya kufuzu

kushiriki katika michuono ya Kombe la Dunia nchini India kwa *Serengeti Girls* na nchini Uturuki kwa *Tembo Warriors.*

Mheshimiwa Spika, pia Wizara kwa kushirikiana na *TFF* tutaendelea kuzisimamia vyema timu zetu zote za Taifa ili kuweza kufanya vizuri katika mashindano yao mbalimbali. Mkakati wa Wizara ni kwenda kubadilisha fikra na mitazamo ya Watanzania ya kuwa michezo ni sehemu ya burudani pekee, la hasha, duniani kote michezo ni ajira, michezo ni biashara, michezo ni utajiri.

Mheshimiwa Spika, nami nakuthibitishia kupitia programu yetu ya michezo ya mtaa kwa mtaa tunakwenda kusaka na kuibua vipaji vya wanamichezo watakaokwenda kucheza michuono ya kulipwa huko duniani, hususan *soccer* la kulipwa nchi za ulaya. Majirani zetu tayari wameshapiga hatua kwa kutoa wachezaji wengi wanaocheza *soccer* la kulipwa Ulaya na kujiingizia fedha nyingi za kigeni sambamba na kuziimarisha timu zetu za Taifa zinazoundwa na wachezaji wengi na nguli wanaocheza vilabu vya kulipwa ulaya, nasi tunakwenda huko. Aidha, nazipongeza timu zetu zote zilizotutoa kimasomaso kwa hatua hii iliyoandika historia mpya kwa Taifa na inayoitangaza nchi yetu duniani kote sambamba na kuipa heshima nchi yetu ikiwa ni sehemu ya *Post Royal Tour,* hakika tumefungulia njia.

Mheshimiwa Spika, wito wangu kwa Watanzania wote ni kuunga mkono jitihada hizi na kujitoa kwa wingi kwa hali na mali kuzishabikia ili kuziongezea ari, hamasa na kuzitia moyo timu zetu za Taifa. Serikali kupitia Wizara yangu itaandaa utaratibu maamul um na mahususi kwa ajili ya kuratibu ushiriki mpana kwa Watanzania katika mashindanio hayo makubwa ya dunia.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nachukua fursa hii kumpongeza tena Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa dhati kabisa kwa kuwa nasi katika safari yote hii ya mafanikio katika Wizara hii na kutuwezesha leo kusimama hapa katika Bunge lao hili tukufu kwa ufahari kabisa. Alitupa moyo, alituwezesha na zaidi kabisa yupo karibu nasi kufuatilia maendeleo ya timu kila uchwao, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninawashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wote kwa kutuunga mkono na ahsanteni sana kwa kunisikiliza. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge pongezi alizozitoa Mheshimiwa Waziri na taarifa aliyoitoa ni yetu sote. Leo alikuwa hazungumzi kwa niaba ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, tumsikie sijui ni Kepteni atazungumza au nani mmemchagua azungumze kwa niaba yenu nyote? Ni Kepteni?

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Ndiyo.

**SPIKA:** Haya, hebu msindikize hapo mbele aje aseme na Wabunge na wananchi wote. *(Makofi)*

*(Hapa Kapteni wa Timu ya Tembo Worriors alisindikizwa na Msaidizi wa Bunge kwenye kipaza sauti)*

**KEPTENI WA TIMU YA TAIFA YA WATU WENYE ULEMAVU *TEMBO WARRIORS*:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii. Hizi ni salamu za Kepteni wa Timu ya Taifa

ya *Tembo Warriors* ya Mpira wa Miguu kwa Watu Wenye Ulemavu Tanzania. Tembo!

**WACHEZAJI WA *TEMBO WARRIORS*:** *Warriors*

**KEPTENI WA TIMU YA TAIFA YA WATU WENYE ULEMAVU *TEMBO WARRIORS*:** Tembo.

**WACHEZAJI WA *TEMBO WARRIORS*:** *Warriors! (Makofi)*

**KEPTENI WA TIMU YA TAIFA YA WATU WENYE ULEMAVU *TEMBO WARRIORS*:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa yote kwa kutufikisha salama hapa Dodoma. Nakiri kwamba hii ni mara yangu ya kwanza kabisa kukanyaga ndani ya sehemu hii ya Bunge, nina uhakika na wenzangu pia. Hii ni heshima kubwa sana kwangu na wachezaji wenzangu ambao nimeambatana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushindi tuliopata wakati tuliposhiriki mashindano ya Afrika ya mpira wa miguu kwa Watu Wenye Ulemavu *(CANAF 2021)* yaliyofanyika nchini ndiyo yaliyosababisha timu yetu ya *Tembo Warriors* kuungana na nchi nyingine tatu kutoka Afrika ambapo tutawakilisha katika mashindano ya Kombe la Dunia nchini Uturuki mwaka huu. Ushindi huu ulifanya Tembo *Warriors* kuweka historia kuwa timu ya kwanza kushiriki katika Fainali ya Kombe la Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushindi ulitokana na chachu ya Serikali ya Awamu ya Sita iliyoongozwa na Mpendwa wetu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ambaye kwa hakika anaijali sekta ya micherzo kwa kuhakikisha Wizara

inakuwa bega kwa bega na timu zetu za Taifa. Aidha, Rais wetu mpendwa alimtuma Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutuletea Shilingi Milioni 150 kwa ajili ya kusaidia katika mashindano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alipokuja Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kutufikishia salamu za mpendwa Rais wetu tulimpelekea ahadi ya kupambana mpaka kuhakikisha kuwa timu yetu inakuwa ya kwanza kushiriki katika mashindano ya Kombe la Dunia. Ahadi ambayo tunamshukuru Mungu tuliitimiza, tunakwenda kuupiga tena mwingi Uturuki na kutangaza *Royal Tour. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Mbariki Rais wetu mpendwa ambae tunaona kabisa anatupeleka mbali kwenye sekta yetu ya michezo. Ahsanteni sana. Tembo!

**WACHEZAJI WA *TEMBO WARRIORS*:** *Warriors, warriors* juu! *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mkumbuke tulikuwa tumetengua Kanuni, kwa hiyo ni sawa hiki anachokifanya. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na pongezi alizozitoa Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, nami kwa niaba ya Bunge na mkishafika hapa ndiyo mmeshafika, nchi yote iko hapa. Kwa hiyo, nchi nzima inawapongeza sana Tembo *Warriors* kwa heshima kubwa ambayo mmeipatia nchi yetu kwa kufuzu kwenda huko kushiriki Kombe la Dunia. Heshima hii mmepewa na Bunge kama nchi yote kwa sababu, tunawatazama na

tunawategemea kwamba, mlivyofanya vizuri ngazi hii mtaenda kufanya vizuri zaidi ngazi inayofuata. *(Makofi)*

Kuingia kwenu hapa ni ahadi kwamba kombe mtarudi nalo, kwa hiyo, tunawatakia kila la heri katika michezo iliyo mbele yenu na hapa Mheshimiwa Waziri tunakushukuru wewe pia kwa kuhusika moja kwa moja kwenye jambo hili kuhakikisha vijana wetu wanakuwa kwenye kambi ili wawe katika hali nzuri. Huko ulikowapeleka ndiyo kwenyewe, watakuwa na pumzi za kutosha watakapoenda huko kwenye Kombe la Dunia.

Pia, najua wameambatana hapa na viongozi mbalimbali, tunawashukuru pia, kwa kuendelea kuilea timu hii, mkiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dkt. Abbas, tunaamini mtaendelea kushirikiana nao kwa kila hali na kila hatua ili wakafanye vizuri zaidi. *(Makofi)*

Kipekee kabisa tumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa karibu na wanamichezo, lakini siyo tu kuwa karibu kwa kujitoa, maana bila fedha jamani haya mambo tunayoyasema haya, kwenda Poland hatuendi na bajaji, lazima upande ndege na kule uandaliwe usafiri na mambo kama hayo na ukae hoteli ule mambo yaende vizuri. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhakikisha timu hii inafanya vizuri. Tunaamini kwa morali aliyowapa na kwa namna anavyoendelea kushirikiananao mtafanya vizuri. *(Makofi)*

Ndugu Wachezaji, kama mnavyofahamu nchi nzima hapa inasema Rais anaupiga mwingi na sisi Wabunge tunajua Rais anaupiga mwingi sasa muende

na ninyi huko kwenye Kombe la Dunia mkaoneshe Tanzania kuna Rais anayeupiga mwingi, kwa hiyo, tunawatakia kila la heri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tumefanya hili ni tukio lingine katika baadhi ya timu zetu ambazo zimeshinda kwenda kushiriki Kombe la Dunia. Waliingia hapa *Serengeti Girls* wanaenda kushiriki Kombe la Dunia na sasa wanaingia Tembo *Worriors* kwa kuwa wanaenda kushiriki Kombe la Dunia, kwa ajili ya kuweka usawa hapa nchini, pia morali kwa ajili ya wachezaji wote timu yoyote nyingine ya Taifa itakayofuzu kwenda kucheza Kombe la Dunia italetwa hapa Bungeni ili tuipe baraka zetu za kwenda huko. Kwa hiyo, hata timu zingine zisijione wanyonge hivi Hapana, zikae mkao sawa tu Bunge tuko tayari kutoa morali ya namna hii ya watu kuja kukalia viti vya Waheshimiwa Wabunge na wao kwa sasa ni Waheshimiwa Wabunge kwa muda, kwa majina yao. Kwa hiyo, tutafanya hivi kwa kila timu ambayo itakuwa inafuzu kwenda kucheza Kombe la Dunia. Kwa hivyo, tunawatakia kila la kheri Twiga *Stars*, tunawatakia kila la kheri Taifa Stars, tunawatakia kila la kheri timu za *netball*, nimesema jamani timu ya Taifa maana hapa tusije tukachanganya mambo, hapa ni timu za Taifa naona watu wa Yanga wanataka Yanga iingie humu ndani.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo na ili sasa turuhusu ratiba yetu iendelee tunawashukuru sana na tunawatakia kila la kheri katika ratiba iliyoko mbele yenu na sasa *Sergeant-At-Arms* muwafuate ili muweze kuwatoa hapa na kwa kipindi hiki cha dakika chache mtakachokuwa mnatoka na ninyi ni Waheshimiwa wachezaji wa Tembo *Warriors* tunawatakia kila la kheri ahsanteni sana. *(Makofi)*

*(Hapa Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Watu wenye Ulemavu ya Tembo Warriors waliondoka Ukumbini)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa wakati tunajiandaa kuendelea na ratiba yetu niwakumbushe tu jana kwa wale ambao walihudhuria mdahalo tulikubaliana tuendelee na utaratibu wetu wa kupongeza, utaratibu wetu wa kupongeza kwa kugonga meza na siyo kupiga makofi, ndiyo utamaduni wetu Bunge la Tanzania tunapiga meza wengine wanazungumza Mabunge mengine wanazungumza kwa mdomo kila watu wana utaratibu wao. Sasa hapa katikati tumeanza kuchanganya tamaduni zote, tunapiga kigelegele cha mdomo, tunapiga makofi, tunapiga na meza. Sasa lazima tuwe nalo moja na nadhani tulilolizoea ni la meza, kwa hiyo tuendelee na meza tusipige makofi wala vigelegele vya mdomo, ndivyo tulivyokubaliana jamani Waheshimiwa Wabunge na makubaliano yetu ndiyo hayo.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, nimuite sasa Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa kabla hatujaanza majadiliano tutaisikiliza kwanza Kamati yetu ya Bajeti inasemaje kuhusu hotuba ya Hali ya Uchumi pia hotuba ya Bajeti ya Serikali halafu tutaanza uchangiaji. Sasa nimuite Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti Mheshimiwa Daniel Sillo Baran.

**MHE. DANIEL B. SILLO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 124(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023, pamoja tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022, na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Naomba taarifa yote ya Kamati iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa asubuhi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuthibitisha kwa vitendo uchapakazi wake, uadilifu wake na uaminifu wake kwa Taifa la Tanzania. Kamati inaamini Mheshimiwa Rais amekuwa ni mfano bora wa kuigwa na watu wote wanaopewa dhamana ya uongozi katika nchi yetu. Ameyaishi maneno yake aliyoyasema wakati wa uapisho kwamba miradi iliyoachwa na mtangulizi wake ataiendeleza na atahakikisha anaikamilisha. Mheshimiwa Rais ameonesha uwezo mkubwa katika kupigania Diplomasia ya uchumi na mafanikio yake yameonekana na yanaendelea kuonekana.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isidory Mpango kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika majukumu yake. Vilevile, Kamati inampongeza, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kusimamia na kuratibu shughuli zote za Serikali kikamilifu. Aidha, Kamati inakupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa uongozi wako mahiri uliojaa weledi na uzoefu wa kutosha katika kuliendesha Bunge hili la Kumi na Mbili (12) la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa kushiriki kikamilifu katika kuisaidia Kamati kwenye utekelezaji wa majukumu yake. Sisi Kamati ya Bajeti tunaishukuru miongozo yenu na ushirikiano mnaotupatia katika kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge, Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mbunge, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa kushirikiana vyema na Kamati wakati wote tulipowahitaji kwenye Kamati. Aidha, Kamati inawashukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango Ndugu Emmanuel Tutuba, Manaibu wake, Gavana wa Benki Kuu Prof. Florence Luoga, na Manaibu Gavana, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania Ndugu Alphayo Kidata, Wakuu wa Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Mheshimiwa Spika, muundo wa taarifa; Taarifa hii inatoa tathmini ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/22 na uchambuzi wa Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2022/23 kwa kuangalia viashiria mbalimbali vya uchumi, miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali pamoja na mwenendo wa mapato na matumizi. Pia, Taarifa hii imeainisha maeneo mbalimbali ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla kwa mwaka 2021. Hali ya Uchumi wa Dunia; kwa mujibu wa Taarifa ya Mwenendo wa Hali ya Uchumi wa Dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa Mwezi Aprili, 2022 (*World Economic Outlook Report*, April 2022) uchumi wa dunia kwa mwaka 2022 unakadiriwa kukua kwa asilimia 3.1 ikilinganishwa na makadirio ya ukuaji wa asilimia 6.0 yaliyotolewa mwezi Julai 2021. Makadirio ya ukuaji kwa kiwango cha chini yanatokana na ukuaji mdogo wa uchumi kwa nchi zilizoendelea za Marekani pamoja na nchi zinazoibukia kiuchumi kama China. Ukuaji mdogo wa uchumi kwa nchi zilizoendelea umechagizwa na sababu mbalimbali, ikiwemo vita baina ya Urusi na Ukraine iliyoathiri uchumi wa dunia kwa kiwango kikubwa, ugonjwa wa UVIKO-19 unaosambaa duniani na hivyo kusababisha kufunga maeneo ya uzalishaji na vituo vya biashara. Itakumbukwa kwamba Taifa la China linakaribia 15% ya biashara zote duniani.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hiyo pia inaonyesha kwamba Katika kipindi cha mwezi Agosti 2021 hadi mwezi Februari 2022 bei za bidhaa za msingi (*Primary*

*Commodities*) katika soko la dunia zimepanda kwa asilimia 24 kwa mchanganuo ufuatao:-

i. Bidhaa za chuma za msingi yaani *base metal* zimeongezeka kwa asilimia 2;

ii. Bidhaa za madini ya thamani *precious metal* zimeongezeka kwa asilimia 3;

iii. Bidhaa za kilimo zimepanda kwa asilimia 11 na hii ni kutokana na kupanda kwa bei za nafaka katika soko la dunia kwa asilimia 21.8. Aidha bei ya ngano katika soko la Dunia imeongezeka kwa asilimia 26.4; na

iv. Mahitaji ya mafuta duniani yameongezeka kwa mapipa milioni 99.7 kwa siku hali inayopelekea bei ya mafuta ghafi ya petroli kupanda kwa asilimia 36. Hivyo bei ya Mafuta ghafi inatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 55 mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi zinaonyesha wazi kwamba tatizo la mfumuko wa bei lililopo nchini siyo suala la kulaumu Serikali kwa sababu suala hilo limetokana na hali halisi ya uchumi wa Dunia.

Mheshimiwa Spika, hali ya ukuaji wa uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021; Taarifa kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu inaonyesha kwamba katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Pato la Taifa liliongezeka kwa wastani trilioni 135.517 toka shilingi trilioni 129.130 ya mwaka 2020, sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 4.9. Shughuli za uchumi zilizokuwa na mchango katika ukuaji wa uchumi kwa kiwango cha 4.9 ikilinganishwa na 4.8 kwa mwaka 2020. Vilevile shughuli zilizokuwa na ukuaji mkubwa ni sanaa asilimia 19.4, umeme asilimia 10.0, madini asilimia 9.6 na habari asilimia 9.1.

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo ni kati ya sekta pekee ambayo pamoja na uwepo wa ugonjwa wa UVIKO-19 na madhara ya Vita baina ya Urusi na Ukraine imeweza kukua na kuongeza mchango wake katika Pato la Taifa. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawekeza kwa kiasi kikubwa kwenye sekta ya kilimo na sekta nyingine kama vile utalii wa ndani na nje ili zichangie katika uchumi na hivyo kuwa na uchumi usiotegemea sekta chache.

Mheshimiwa Spika, akiba ya fedha za kigeni; Hadi kufikia mwezi Machi, 2022 akiba ya fedha za kigeni ilikuwa Dola za Kimarekani Milioni 5,581.6, kiwango kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi Mitano hadi Sita. Aidha, kiwango hiki kimeshuka toka dola za Marekani Milioni 6,557.9 kilichoripotiwa na Benki Kuu Machi 2021, ambacho kilikuwa kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi Sita hadi miezi Nane. Kamati inaishauri Serikali badala ya kuendelea kuwa na kiwango cha akiba za fedha za kigeni kinachozidi uagizaji wa bidhaa na Huduma kutoka nje kwa zaidi ya miezi Minne badala yake ziada ya zaidi

ya miezi Minne iwe inatumika katika kuikopesha Serikali ili kupunguza gharama ya ukopaji kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, biashara ya nje; Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba hadi kufikia mwezi Machi, 2022 urari wa malipo kwa sekta ya nje ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani Milioni 1,315.9 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani Milioni 351.9 katika kipindi hicho hicho kwa mwaka 2021. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kujielekeza zaidi katika Sekta ambazo zinaweza kuongeza mauzo yetu nje ya nchi kama Kilimo, Mifugo, Uvuvi pamoja na Madini ili ziweze kupunguza nakisi ya urari wa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Deni la Serikali; Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba hadi mwezi Machi 2022, deni la Serikali lilikuwa ni Shilingi Trilioni 69.44 kati ya kiasi hicho deni la nje lilikuwa Shilingi Trilioni 47.07 na deni la ndani lilikuwa ni Shilingi Trilioni 22.37 ukilinganisha na Deni la mwezi Machi 2021 la Shilingi Trilioni 64.46 sawa na ongezeko la asilimia 7.73. Ongezeko la deni limetokana na ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo na malimbikizo ya riba ya deni la nje hususan nchi zisizo wanachama wa kundi la Paris (Non-Paris *Club members*) ambazo Serikali inaendelea kujadiliana nazo kuahirisha ulipaji wa madeni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba deni letu ni himilivu kwa viwango vyote vya kimataifa. Kamati inaendelea kuishauri Serikali masuala yafuatayo:-

i. Kuangalia uwezekano wa kujipima uhimilivu wa deni kwa kutumia kiashiria cha makusanyo ya mapato ya ndani kwa ulipaji wa deni. Hii ni kwa sababu deni la

Serikali hulipwa na makusanyo ya ndani na ni malipo ya lazima (*first charge)* katika matumizi ya Serikali;

ii. Kwa kuwa Tanzania ilipata *The Debt Service Suspension Initiatives – DSSI* toka benki ya Exim ya China (US$ 99.5 Million) na *French Development Agency* (US$2.6 Million). Hivyo Kamati inaishauri Serikali kulipa madeni haya mara tu muda wa kulipa utakapofika ili kuondoa tatizo la malimbikizo ya madeni.

iii. Kamati inatambua hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kukamilisha suala la *credit rating*, hata hivyo ni vyema kukamilisha haraka mchakato wa nchi yetu kufanyiwa tathmini ya uwezo wa ukopaji na ulipaji *(credit rating)* ili kuiwezesha Serikali kupata mikopo yenye masharti nafuu na kwa urahisi;

iv. Mikopo yenye masharti ya kibiashara ielekezwe katika miradi yenye sura ya kibiashara ili miradi hii ikamilike kwa wakati na kuanza kurejesha gharama za mikopo hiyo;

v. Kuboresha mikakati ya kukusanya kodi ili kuhakikisha sehemu kubwa ya bajeti inagharamiwa na mapato ya ndani pamoja na kupunguza matumizi yanayoweza kuepukika; na

vi. Serikali kutafuta mikopo yenye masharti ya kati (*Semi concessional loans*) ambayo masharti yake ni nafuu ikilinganishwa na mikopo ya kibiashara.

vii. Izingatiwe kwamba gharama za mikopo ya biashara zitaongezeka sana kutokana na kuongezeka kwa mfumuko wa bei na viwango vya riba kwa nchi zilizoendelea.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa viwango vya riba na huduma za kibenki mwezi Machi 2022, riba katika mabenki ya kibiashara ilitozwa kwa wastani wa asilimia 16.28 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 16.63 ya kipindi kama hicho mwaka 2021. Hali hii imetokana na jitihada za Serikali katika kuyaongezea mabenki yetu nchini ukwasi hivyo kusababisha viwango vya mikopo ya riba nchini kuendelea kushuka. Vilevile riba inayotozwa kwenye amana za mwaka mmoja ni kati ya asilimia 6.94 na asilimia 8.21 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 6.83 na asilimia 8.57 kwa mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza ukwasi katika mabenki ili kushusha viwango vya riba za mabenki na amana. Hata, hivyo Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya masharti yaliyowekwa kwenye Mkopo wa Shilingi Trilioni Moja kwa mabenki ili yaweze kukopesha sekta mbalimbali za uchumi ikiwemo kilimo kwa kati ya asilimia Tisa hadi asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya hali ya umaskini nchini; Viashiria vya kupima hali ya umaskini nchini hupatikana kwa kutumia taarifa za utafiti wa mapato na matumizi ya kaya binafsi, utafiti unaofanyika kila baada ya miaka mitano. Matokeo ya utafiti ya mwaka 2017/2018 yanaonyesha kwamba kaya zenye idadi ndogo ya watu zina kiwango kidogo cha umaskini kuliko kaya zenye idadi kubwa ya watu. Kiwango cha umaskini wa mahitaji ya chakula na ya msingi ni kikubwa kwa kaya zinazoongozwa na wakuu wa kaya wenye elimu ndogo. Hivyo, Serikali iendelee kusimamia vema Sera yake ya Elimu Msingi bila ada na kutekeleza Sera ya Idadi ya Watu ya mwaka 1992 ambayo inaelekeza wananchi kuzaa watoto wanaoweza kuwahudumia. Kamati inaendelea

kusisitiza kwamba Serikali iwekeze zaidi katika sekta ambazo zinahusisha wananchi wengi kama vile kilimo, mifugo na uvuvi ili kuwakwamua kutoka kwenye umaskini.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022 hadi Aprili 2022 Serikali ilikusanya na kutumia jumla ya Shilingi Trilioni 29.84 sawa na asilimia 78.55 ya lengo la mwaka. Kati ya fedha hizo Shilingi Trilioni 12.06 ni fedha za matumizi mengineyo ikijumuisha malipo ya Deni la Serikali, Shilingi Trilioni 6.73 ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi Trilioni 10.61 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mwenendo wa Mapato ya Kodi; Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania iliweza kukusanya jumla ya Shilingi trilioni 17.20 dhidi ya lengo la kukusanya Shilingi Trilioni 21.78 sawa na asilimia 78.97. Mapato ya kodi kwa mwaka 2021/2022 yameongezeka kwa asilimia 18.5 ukilinganisha na kipindi kama hicho mwaka 2020/2021. Nitumie fursa hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiari na kutoa kibali cha kuajiri watumishi takribani 2,000 na Pili Nimpongeze Ndugu Alphayo Kidata Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania pamoja na Watendaji wote wa *TRA* kwa ukusanyaji wa kodi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Mwenendo wa Matumizi; hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya Shilingi Trilioni 29.40 zimetolewa sawa na asilimia 77.4 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, Shilingi Trilioni 18.79 zilitumika kwa ajili matumizi ya kawaida ambayo yalijumuisha Shilingi Trilioni 6.73 kwa ajili ya mishahara, Shilingi Trilioni 4.79 Matumizi Mengineyo na

Shilingi Trilioni 7.27 kugharamia deni la Serikali. Aidha, jumla ya Shilingi Trilioni 10.61 sawa na asilimia 70.76 ya lengo la mwaka zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamia vyema Sera za Matumizi kwa mwaka 2021/22.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2021/2022 na mapendekezo ya mpango wa maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023. Kamati ingependa kutoa maoni na mapendekezo yake kuhusu utekelezaji wake kwa mwaka 2021/2022 na mapendekezo ya Mpango kwa Mwaka 2022/2023 katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tathmini ya Utekelezaji; Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, Serikali ilikuwa imetumia jumla ya shilingi trilioni 10.72 ambayo ni sawa na asilimia 85.3 ya bajeti iliyokuwa imetengwa ya shilingi trilioni 14.99 kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kati ya fedha hizo Shilingi Trilioni 10.72 zilizopokelewa, shilingi trilioni 9.14 ni fedha za ndani na shilingi trilioni 1.46 ni fedha za nje. Hatua hii inaonyesha dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutumia fedha za ndani kuliletea Taifa letu maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Afya; Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya afya, huduma za kibingwa, upatikanaji wa vifaa tiba, kinga, dawa na vitendanishi. Serikali imeweza kufanya ujenzi na ukarabati mkubwa wa vituo vya Afya 304 ili kuviwezesha kutoa huduma kwa wajawazito wanaopata uzazi pingamizi wakati wa kujifungua. Hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya vituo vya Afya 250 sawa na asilimia 82.2 vilikuwa vimeanza kutoa

huduma kamili ikiwa ni pamoja na upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni. Vilevile Serikali imefanikiwa kukamilisha Vyumba/Wodi za Watoto Wachanga Mahtuti 30 katika hospitali za Halmashauri na hivyo kuwezesha kuwepo kwa jumla ya vituo 165.

**1.0.**

**2.0.** Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imefanikiwa kupunguza vifo vya watoto wachanga kutoka vifo 8,190 mwaka 2020 hadi vifo 6,741 mwaka 2021, vifo vya Watoto wa chini ya mwaka mmoja vimepungua kutoka vifo 2,657 mwaka 2020 hadi vifo 1,092 mwaka 2021 na vifo vya watoto wa umri chini ya miaka mitano vimepungua kutoka vifo 3,482 mwaka 2020 hadi vifo 1,512 mwaka 2021. Changamoto kubwa zinazoikabili sekta hii hivi sasa ni ukosefu wa watumishi katika miundombinu iliyojengwa na Serikali, ununuzi na usambazaji wa dawa na vifaa tiba pamoja na baadhi ya maeneo kutokuwa na vituo vya afya na zahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kuharakisha mchakato wa uanzishwaji wa Sheria ya Bima kwa wote ili isaidie wananchi wa hali ya chini katika kupata huduma za afya. Nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye hadi mwezi Aprili alikuwa ametoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa madawa na vifaa Tiba kupitia *MSD* vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 129.85.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Elimu; Kama kuna sekta ambayo imepiga hatua kubwa za maendeleo katika ujenzi wa miundombinu ya Msingi ya Kufundishia na kujifunza ni sekta ya elimu. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kutekeleza Mpango ni kama ifuatavyo:-

Kurejesha wanafunzi wa kike 3,333 masomoni kupitia mpango wa kurejesha wanafunzi, kuendelea na ujenzi na ukarabati wa Vyuo vya VETA katika Mikoa 25 ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, jumla ya Shilingi 304,000,000,000 zilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta ya elimu ambapo Shilingi 240,000,000,000 ni kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 12,000 vya madarasa katika Shule za Sekondari, na shilingi 60,000,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 3,000 vya madarasa ya shule shikizi na shilingi 4,000,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni 50 katika shule za msingi zenye wanafunzi wenye mahitaji maaalum, pia vitabu 18,200 vilisambazwa kwa watoto wenye uoni hafifu. Kamati inatambua kwamba Serikali ipo katika hatua ya kuajiri walimu ili kupunguza upungufu uliopo. Suala hili liende sambamba na kurejea mitaala yetu ili iendane na wakati na kuangalia namna bora na namna ya kutoa mikopo kwa vyuo vya ufundi kama ilivyo kwa Vyuo Vikuu. Kamati inaamini hivi sasa tunahitaji wataalam wengi kutoka vyuo vya kati.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Kilimo; Kamati inampongeza Mheshimiwa Suluhu Hassan kwa kuongeza Bajeti ya Kilimo kutoka shilingi 294,000,000,000 mwaka 2021/2022 hadi shilingi 954,000,000,000 kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kilimo ni moja ya sekta ambazo ni nguzo kuu ya maendeleo ya viwanda kwa sababu ndiko malighafi za viwandani zinapopatikana. Aidha, kilimo ndicho kinaajiri takribani asilimia 65 ya Watanzania wote. Mafanikio yaliyopatikana katika sekta hii ni pamoja na:-

Kuwezesha uzalishaji wa Tani 18.6 za chakula ukilinganisha na mahitaji ya tani 14.8 hivyo kuwa ziada ya

tani 3.8 za chakula sawa na asilimia 126. Kuongezeka kwa matumizi ya zana bora za kilimo kama vile matrekta kutoka asilimia 23 mwaka 2020/2021 hadi asilimia 25 kwa mwaka 2021/2022, na Kuongeza mbegu mpya aina 18 zilizogunduliwa na kuzalishwa na taasisi za umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo sekta hii bado inakumbwa na changamoto mbalimbali kama vile ardhi ya kilimo kuendelea kupungua kutokana na kuvamiwa kwa ajili ya makazi, kuendelea kuagiza mazao ya nafaka kama ngano na shairi ambayo yanaweza kuzalishwa nchini, utaratibu usioridhisha wa uagizaji na usambazaji wa mbolea zinazotoka ndani na nje. Aidha, imekuwa vigumu kwa sekta ya kilimo kupata mikopo kwa ajili ya kuiendeleza kutokana na vihatarishi vyake. Kamati inaamini masuala haya yakifanyiwa kazi Kilimo kinaweza kuwa sekta inayoweza kulitoa Taifa hapa lilipo kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maji; Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji mijini na vijiji. Pongezi hizi zinatokana na utolewaji wa fedha kwa miradi ya maji kupitia mfuko wa maji, Bajeti Kuu ya Serikali na nyongeza ya Bajeti kupitia Fedha za UVIKO-19 ambapo zina jumla ya Shilingi Bilioni 733.28 hadi mwezi Machi zilikuwa zimetolewa jumla ya Shilingi Bilioni 522.44 sawa na asilimia 71.2. Hata hivyo, pamoja na juhudi hizi ni vema Serikali ikaongeza juhudi katika usimamizi wa miradi yake inayoitekeleza ili ilete tija inayotazamiwa na kwa kujengwa kwa ubora na kwa kuzingatia thamani ya fedha.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Miundombinu. Bandari; Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kuboresha

bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga pamoja na bandari zilizopo katika maziwa makuu na bandari kavu kila kanda mfano Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Mwanza, Mtwara, Mbeya na Tanga. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba Mamlaka ya Bandari badala ya kuendelea kuwekeza ili kuwe na ufanisi katika uondoshaji wa shehena Bandarini inafikiria kutumia makampuni ya nje kama vile *DP World* na *TICTS*. Hatua hii inaweza kuleta mafanikio ya ufanisi lakini itapunguza kwa kiasi kikubwa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mfano, kuna baadhi ya mizigo haiwezi kushushwa na *TPA* kwa sababu hawana kifaa kiitwacho *N-GEN* na badala yake makontena yanayohitaji kifaa hicho hutumia gati ambazo ziko chini ya *TICTS*. Kifaa hicho kina kazi ya kutoa taarifa za wakati yaani *real time* wakati wa upakiaji na upakuaji wa makasha.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utalii; Sekta ya utalii ni miongoni mwa sekta za kiuchumi ambazo zilikumbwa na changamoto za ukuaji katika kipindi cha mwaka 2020/2021 kutokana na janga la Homa Kali ya Mapafu lililoikumba dunia kuanzia mwishoni mwa mwaka 2019 hadi mwaka 2020. Mwaka 2021/2022 Kamati ilishauri Serikali kuangalia namna ya kutangaza utalii wetu ili kurejesha biashara ya utalii iliyokuwa imeathirika kwa kiasi kikubwa. Aidha Kamati ilishauri Serikali kutafuta fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya hifadhi yetu iliyokuwa imeharibika kutokana na mvua.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchukua uamuzi madhubuti wa kuandaa filamu ya *The Royal tour* ili

kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini. Aidha, kupitia fedha za Mkopo kutoka *IMF* sekta hii ilipewa mgao wa Shilingi Bilioni 90.2 ili kukarabati na kujenga miundombinu ya msingi pamoja na kununua mitambo itakayokuwa ikikarabati miundombinu hiyo mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya utekelezaji wa bajeti za mifuko; Kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti Sura 439 Kifungu cha 9 (f) kinaipa mamlaka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kukutana na Mashirika ya Umma ili kuangalia mizania yao ya fedha pamoja na kuangalia endapo mashirika hayo yanafuata misingi ya sheria za fedha za umma na sheria nyingine za Nchi.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Bajeti ya Mifuko Maalum *(Ring fenced Funds)* Mfuko wa Maji. Mfuko wa maji una chanzo kikuu kimoja cha fedha zinazotokana na tozo ya mafuta ya petroli na dizeli. Kamati imebaini kwamba utolewaji wa fedha za kutekeleza miradi ya maji kwa miaka miwili mfululizo umekuwa ukitegemea zaidi chanzo cha tozo ya Mafuta ya petroli na Dizeli kuliko fedha kutoka Mfuko mkuu wa Serikali. Fedha kutoka mfuko mkuu wa Serikali zimekuwa hazitolewi kama zilivyoidhinishwa na Bunge isipokuwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo sekta hiyo ilipokea fedha za UVIKO19 Shilingi 139,000,000,000. Fedha zilizotolewa kutoka kwenye tozo ya mafuta kwenda kwenye mfuko wa maji ilikuwa asilimia 78.4 ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba shida iliyoko katika Wizara ya Maji hivi sasa si uhaba wa fedha bali ni tatizo la ukosefu wa rasilimali watu wa kusimamia miradi ya maji. Mfuko wa Barabara. Changamoto kubwa ambayo Kamati imebaini katika utekelezaji wa Mfuko huu ni baadhi ya barabara

kujengwa chini ya kiwango na hivyo kuhitaji matengenezo makubwa ndani ya muda mfupi. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuboresha kitengo cha ukaguzi wa barabara yaani *road inspection* ili kuhakikisha kwamba barabara zinafanyiwa matengenezo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa *REA*, hadi mwezi Aprili 2022, Serikali ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 407.045 sawa na asilimia 98.3 ya bajeti ya Mfuko kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mfuko. Hadi mwezi Aprili 2022 mfuko wa *REA* ulikuwa na jumla ya Shilingi *trilioni* 1.24 hata hivyo miradi haikutekelezwa kutokana na changamoto mbalimbali kama vile kupanda kwa bei za vifaa na mikataba isiyoruhusu mabadiliko ya bei pamoja na usimamizi usioridhisha. Kamati inaamini masuala hayo yakifanyiwa kazi miradi itatekelezwa kwa haraka na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya Utendaji Kazi wa baadhi ya Mashirika ya Umma pamoja na utekelezaji wa bajeti za Mashirika hayo. Tunaanza na Shirika la *Petrol* Tanzania - *TPDC*. Kamati imebaini kwamba shirika halitekelezi ipasavyo mikataba ya ugawanaji mapato hasa baada ya kuchangia gharama za uwekezaji ili inufaike na mapato. Kutokana na hali hiyo shirika limekuwa likinufaika na ada na tozo mbalimbali na faida kubwa kuchukuliwa na wawekezaji. Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kubadilisha Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi ya Mwaka 2015, ili kuruhusu *TPDC* kutumia sehemu ya mapato yanayotokana na shughuli za utafutaji na uzalishaji wa gesi kutumika katika uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Kamati ilibaini kwamba *TPDC* haina vituo vya kutosha vya kusambaza mafuta, hivyo Kamati inaishauri Serikali kuiruhusu *TPDC* kuingia ubia na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikali *GPSA* ili kutumia vituo vyao kwa mpito wakati *TPDC* ikiendelea na mchakato wa kujenga vituo vyake.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma *PPRA*. Sheria ya Ununuzi Sura ya 410 imeipa *PPRA* Mamlaka ya Kuanzisha, Kusimamia na kuendesha Mfumo wa Ununuzi kwa njia ya Mtandao Kamati imebaini kwamba Mfumo wa Ununuzi wa Umma kwa njia ya Mtandao unatumia lugha moja ya Kingereza na hivyo kuwa ngumu kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine katika mfumo huo. Hivyo ni wazi kwamba mfumo huu unakiuka moja ya nguzo Tano za ununuzi wa Umma ambayo ni kuwezesha makampuni ya ndani kushiriki katika zabuni. Aidha, matumizi ya lugha ya kingereza pekee yanakiuka nguzo ya haki, usawa pamoja na fursa kwa wote. Kwa msingi huo Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba mfumo huu unatumia lugha zote kubwa duniani kama vile, Kiswahili, Kifaransa, Kichina na Kireno. Na kwa kuwa, mfumo wa *TANePS* haukujengwa na Watanzania, Kamati inaishauri Serikali ianze mchakato wa kujenga mfumo kwa kutumia wataalam wa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Matokeo ya Mashauriano baina ya Serikali, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na Kamati ya Uongozi. Kanuni ya 124(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Juni, 2020 kanuni hiyo inaelekeza kwamba, baada ya Bunge kukamilisha mjadala wa Makadirio ya Wizara zote, ndani ya siku sita kabla ya hotuba ya Bajeti kusomwa Bungeni, Serikali kwa kushauriana na Kamati ya Bajeti itafanya majumuisho

kwa ajili ya kuzingatia hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha unaoisha, na Makadirio ya Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kanuni hii ilianzisha mjadala wa mabadiliko wa muundo wa uwasilishaji wa bajeti kutoka uliokuwepo awali ambapo ilianza kuwasilisha bajeti kuu ya Serikali na kufuatia na Mafungu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hoja zilizojadiliwa. Kamati ya Bajeti ilikutana na Serikali kwa kipindi cha siku Sita kuanzia tarehenane hadi Tarehe 13 mwezi Juni ili kushauriana kuhusu hoja 12 zilizojitokeza katika Wizara mbalimbali wakati wa majadiliano ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2021/2022 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2022/2023, baadhi ya hoja hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Kuongeza fedha kwa ajili ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ujenzi wa mifumo na ununuzi wa magari,

(ii) Kuangalia uwezekano wa kutoza kwa kiwango cha asilimia sifuri Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mafuta yaliyochujwa mara mbili yanayotokana na mbegu za pamba, mchikichi na alizeti yanayozalishwa ndani ili yaweze kushindana katika soko,

(iii) Mlundikano wa mapingamizi ya kodi yaliyoko kwenye Bodi ya Rufaa za Kodi, Mahakama ya Rufaa ya Kodi pamoja na Mahakama ya Rufaa ambayo hadi tarehe 31 Disemba, 2021 kulikuwa na kesi zenye Thamani ya shilingi trilioni 5.184,

(iv) Changamoto ya upatikanaji wa Ofisi za Wabunge Majimboni,

(v) Utatuzi wa Changamoto za utekelezaji wa Miradi ya Umeme Vijijini *REA* kutokana na kukosekana kwa vifaa kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi,

(vi) Serikali kuangalia uwezekano wa kuwalipa mishahara Waheshimiwa Madiwani pamoja na Wenyeviti wa Mitaa na vijiji,

(vii) Kuangalia uwezekano wa kuongeza maeneo yanayozunguka Bunge ili kuimarisha ulinzi na usalama wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, maamuzi baada ya mashauriano; Baada ya mashauriano Kamati ilikubaliana na majibu ya Serikali kwa hoja Sita na hoja Tano zilihitaji ufafanuzi wa ziada. Baadhi ya hoja hizo zimefanyiwa kazi kupitia hotuba ya bajeti ya Serikali iliyowasilishwa Tarehe 14 Juni, 2022. Aidha, hoja hizo ambazo zilihitaji ufafanuzi wa ziada Mheshimiwa Spika aliagiza kwamba zifanyiwe kazi na mrejesho kuwasilishwa kwa Kamati katika muda tofauti tofauti. Vilevile, kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya umeme vijiji Serikali iliagizwa kuleta mrejesho Bungeni kabla ya kuipigia kura Bajeti Kuu ya Serikali Tarehe 24 Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, Sura ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imepanga kukusanya na kutumia jumla ya Shilingi Trilioni 41.48 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 8.1 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2021/2022 ya Shilingi Trilioni 37.99. Kati ya fedha hizo, Shilingi Trilioni 26.54 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni asilimia 63.8 ya bajeti yote na Shilingi Trilioni 15 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo sawa na asilimia 36.2 ya bajeti. Aidha, bajeti ya maendeleo inajumuisha SHILINGI

TRILIONI 12.31 fedha za ndani na Shilingi Trilioni 2.7 fedha za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sera za mapato; Kwa upande wa misaada na mikopo kutoka kwa washirika wa maendeleo, Serikali inategemea kupokea kiasi cha shilingi trilioni 4.15 sawa na ongezeko la asilimia 40.56 ikilinganishwa na shilingi trilioni 2.95. Aidha, Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 5.35 kutoka soko la ndani ambapo shilingi trilioni 3.30 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva na kiasi cha shilingi trilioni 2.05 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Vilevile Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 2.86 kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya miundombinu, hivyo Kamati inashauri Serikali kuendelea kufanya mazungumzo na washirika wa maendeleo na kuwashawishi ili kuendelea na utaratibu wa awali wa *General Budget Support*.

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuondokana kabisa na utegemezi wa kibajeti hasa kipindi hiki ambapo hali ya uchumi wa nchi za wahisani zimetetereka kutokana na ugonjwa wa UVIKO-19 pamoja na vita ya Urusi na Ukraine na hivyo kuwepo na uwezekano mkubwa wa nchi hizo wahisani kushindwa kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mikopo ya ndani na nje mwaka 2022/2023 Serikali imepanga kukopa katika soko la ndani kiasi cha Shilingi Trilioni 2.05 sawa na ongezeko la asilimia 11.72 ikilinganiswa na Shilingi Trilioni 1.84 mwaka 2021/2022. Kamati inaishauri Serikali kupunguza kukopa zaidi kwenye soko la ndani ili

isisababishe kukosekana kwa mikopo kwa sekta binafsi. Badala yake inashauriwa kuangalia vyanzo vya mikopo ya nje yenye masharti nafuu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, sera za matumizi; katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imepanga kutumia kiasi cha shilingi trilioni 41.48 sawa na ongezeko la asilimia 8.1 ukilinganisha na shilingi trilioni 37.99 mwaka 2021/2022 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Takwimu zinaonesha kuwa mapato ya ndani yanazidi matumizi ya kawaida kwa kiasi cha shilingi trilioni 3.03. Hii maana yake ni kwamba mapato yote ya ndani yanaweza kugharamia matumizi ya kawaida peke yake na asilimia 8.3 tu ya miradi yote ya maendeleo. Kufuatia uchambuzi huu Kamati inaishauri Serikali kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani ili walau yawe na uwezo wa kugharamia miradi ya maendeleo angalau kwa asilimia 40.

Mheshimiwa Spika, hatua za kikodi zinazopendekezwa na Serikali kwa mwaka Fedha 2022/2023. Nianze kwa kutoa pongezi kwa Serikali ambayo kwa kiasi kikubwa imechukua na kuzingatia mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Bajeti, hatua hii inaonyesha utayari wa Serikali kupokea mapendekezo na kuyafanyia kazi, chini ya uongozi bora wa Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan. Kamati imefanya uchambuzi wa hatua hizo na kubaini kwamba mabadiliko yaliyofanyika yanalenga maeneo yaliyobainishwa katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu hatua mbalimbali za kikodi**.** Pamoja na kwamba Kamati ya Bajeti itapata fursa ya kutoa maoni

na mapendekezo yake kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2022, naomba uniruhusu kwa uchache nitoe maoni kuhusiana na hatua zilizopendekezwa.

Moja; mabadiliko yaliyofanyika katika Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Afrika Mashariki. Kwa mara ya kwanza katika historia ya Kamati ya Bajeti ilipata fursa ya kupitishwa kwenye mapendekezo ya mabadiliko ya sheria hii na Kamati ilitoa maoni yake. Hata hivyo, utaratibu huu haupo kikanuni wala kisheria hivyo ni muhimu kwa Bunge kuhakikisha kwamba tunafanya mabadiliko katika Sheria ya Bajeti Kifungu cha 9 (1) ili kuongeza jukumu kwa Kamati ya Bajeti kupitia, kuchambua na kutoa maoni juu ya mabadiliko ya Sheria ya Ushuru wa Forodha, kwa sababu mabadiliko hayo huidhinishwa na Bunge la Afrika Mashariki, endapo Bunge hili halitaridhia mabadiliko hayo ni lazima yarejeshwe katika Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Waziri wa Fedha na Mipango kwa kusikiliza vema maoni na mapendekezo ya Kamati na kuyafanyia kazi. Uchambuzi wa kina wa kila hatua ya kikodi iliyowasilishwa na Serikali utafanyika wakati wa kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2022 na Maoni ya Kamati yatawasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/2023. Moja uanzishwaji wa Ofisi ya Msuluhishi wa Masuala ya Kodi *(Tax Ombudsman),* Mwaka 2019 Serikali ilifanya mabadiliko katika Sehemu ya 3(A) ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 438 kwa kuongeza vifungu vipya vya 28A hadi 28G ambavyo vilianzisha Ofisi

ya Mpokea Malalamiko ya Kodi. Aidha, Kamati inatambua kwamba kupitia Tangazo la Serikali Na. 106 la Tarehe 04 Machi, 2022 zilitangazwa Kanuni zenye lengo la kubainisha sifa za Mtendaji Mkuu wa Ofisi hiyo, majukumu yake, utendaji kazi wa Ofisi na namna ya kushughulikia malalamiko ya kodi. Pamoja na Kanuni hizo kukamilika na kutangazwa hivi sasa, Ofisi hiyo haijaanzishwa. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha uanzishwaji wa Ofisi hiyo ambayo ni muhimu sana katika usuluhishi wa migogoro ya kodi kama ilivyoahidi Ofisi hiyo kuanza kazi Julai, 2022.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara kwa kutumia mfumo wa *EPC+F,* wakati Waziri wa Fedha na Mipango akiwasilisha Bajeti ya Serikali Bungeni alilitaarifu Bunge kwamba baadhi ya barabara katika mwaka ujao wa fedha zitatumia mfumo wa usanifu, utangazaji wa zabuni, kujenga na kutafuta fedha za ujenzi *(Engineering Procurement Construction and Finance)*. Mfumo huu una faida mbalimbali kama vile vihatarishi vyote vya mradi vinakuwa chini ya kampuni iliyofanya kazi kwenye hatua zote za usanifu, zabuni, ujenzi na utafutaji wa fedha na pili ni kuirahisishia Serikali utafutaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya barabara.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mfumo huu una faida kubwa pale ambapo barabara zinazojengwa ama zinalipiwa *(road toll)* au zinazalisha mapato makubwa ya moja kwa moja, vinginevyo mfumo huu ni aghali sana kwa sababu Serikali itabaki na jukumu la kulipa mkopo uliochukuliwa na kampuni husika kwa ajili ya ujenzi na utalipwa pamoja na riba hivyo una athari ya moja kwa moja na Deni la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba ni miaka 10 hadi hivi sasa hatuna mradi hata mmoja wa *PPP*

hivyo itakuwa ni vigumu kwa *EPC+F* kuwa na manufaa kwa muda mfupi. Endapo tutaharakisha ujenzi wa barabara kwa *EPC+F* bila kufanya tathmini ya kina ya mapato yetu na Deni la Serikali ni wazi kwamba kutakuwa na athari kubwa sana kwenye mapato yetu ya ndani.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji na uendelezaji wa mifumo ya kukusanyia kodi chini ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*. Ulimwengu tulionao hivi sasa ni ulimwengu wa TEHAMA ambao umerahisisha masuala mengi sana ikiwemo ulipaji na ukadiriaji wa kodi. Kamati imefanya uchambuzi wa mifumo mbalimbali ya Mamlaka ya Mapato kama Vile *TANCIS, ITAX* na E-*FILLING* na kubaini kwamba mifumo hii inahitaji kuhuishwa ili isomane na iendane na wakati wa sasa. Hivyo, tathmini ya awali inaonyesha kwamba Mamlaka ya Mapato inahitaji Shilingi 560,000,000,000 ili kuboresha mifumo hii pamoja na kujenga mifumo mipya kama *IDRAS*. Mifumo hii ina manufaa yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuondoa rushwa kwa kupunguza muingiliano baina ya Mlipakodi na Afisa wa Mamlaka, Pili ni kupunguza mapingamizi ya kodi yanayotokana na ukadiriaji na mwisho ni kurahisisha ulipaji wa kodi. Kamati inaishauri Serikali kukopa au kutenga fedha/Bajeti kwa ajili ya Mamlaka ili iweze kuhuisha, kujenga na kuiendeleza mifumo yake ili iendane na wakati.

Mheshimiwa Spika, kupanua wigo wa ukusanyaji kodi wa Mapato ya Serikali; Kodi zipo za aina mbili kodi za moja kwa moja na kodi zisizo za moja kwa moja. Ni vigumu sana kukwepa kodi zisizo za moja kwa moja kwa sababu mara nyingi kodi hizi zipo kwenye matumizi ya

huduma na bidhaa mbalimbali na ili uzikwepe ni lazima uamue kuacha kutumia bidhaa au huduma husika. Kodi ambayo ni rahisi kukwepa kwa mazingira yetu ya Tanzania ni kodi za moja kwa moja ambazo zinazotokana na mapato. Mfano, kuna wamiliki wengi wa nyumba za kupangisha na hakuna kodi yoyote ya mapato wanayolipa. Hali hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na ukubwa wa sekta isiyo rasmi nchini ambayo inakadiriwa kuwa asilimia 75 ya biashara zote nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kwamba ifanye *pilot project* kwa kuweka Maafisa Kodi katika Kata zenye shughuli nyingi za kiuchumi ili kuweza kutambua na kusajili biashara na walipa kodi wapya na pia zoezi hili litakuwa kwa nchi nzima, hatua hii itakuwa na mafanikio makubwa sana katika kupanua wigo wa kodi. Mfano mzuri ni wanafunzi wa Chuo cha Kodi waliofanikiwa kuwaandikisha walipa kodi wapya 20,000 katika Wilaya ya Ilala pekee mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania; pamoja na kutambua hatua nzuri zilizochukuliwa na Serikali ni dhahiri kwamba Taifa letu bado linakabiliwa na mazingira yasiyoridhisha ya ufanyaji biashara na uwekezaji. Ripoti ya Dunia ya Ufanyaji Biashara inayoandaliwa inatuweka katika nafasi ya 141 kati ya nchi 190 duniani kwa mazingira bora ya biashara. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa *blueprint* ili nchi yetu iwe kati ya nchi 100 zenye mazingira bora ya ufanyaji biashara duniani ifikapo mwaka 2025 kama lilivyo kwenye lengo la Mpango wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kuandaa Sera ya Taifa ya Ufuatiliaji na Tathmini na Baadaye kutunga Sheria; Ufanyaji wa Ufuatiliaji na Tathmini ni zoezi la kitaalam ambalo lina malengo makuu matatu. Moja ni kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa, mbili ni kuhakikisha kunakuwa na thamani ya fedha na tatu ni kurekebisha upungufu wakati wa utekelezaji wa mradi au shughuli yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Miradi kwa Njia ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi yaani *Public Private Partnership*; katika Hotuba ya Bajeti ya Hali ya Uchumi, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alilieleza Bunge kwamba katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2022/2023 utaratibu wa ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi utatumika katika kutekeleza miradi. Pamoja na kwamba utaratibu huu una manufaa makubwa sana kwa Taifa, ni miaka zaidi ya 12 sasa tangu ilipotungwa Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2010 pamoja na mabadiliko yake ya mwaka 2018. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini changamoto zinazosababisha kutokuwepo na miradi *PPP* ambayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kiwango cha chini cha mtaji unaotambulika kisheria kwa ajili ya Miradi ya *PPP* ni dola za Marekani milioni 20, sawa na Shilingi za Kitanzania bilioni 40;

(ii) Mwamko mdogo wa Wizara, Idara na Taasisi za umma kutekeleza miradi kwa njia ya ubia;

(iii) Mazingira yasiyoridhisha ya uwekezaji ambayo hayavutii uwekezaji kwenye miradi ya aina hii; na

(iv) Ugumu uliopo wa kisheria wa kutekeleza miradi kwa njia hii hasa miradi ambayo inaibuliwa na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inatanzua vikwazo vilivyobainishwa ili lengo la utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia iweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kutoshirikiana wakati wa Utekelezaji wa Miradi; Kamati katika uchambuzi wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo imebaini kwamba baadhi ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali hazifanyi kazi kwa kushirikiana. Mfano, Mradi wa Umeme Vijijini unatekelezwa na Wakala wa Umeme Vijijini lakini jambo la kushangaza ni pale ambapo tathmini ya maeneo yanayohitaji kuunganishiwa umeme inafanyika na taasisi za umma kama vile shule, hospitali na zahanati hazijumuishwi. Eneo lingine ni pale ambapo halmashauri inapanga kujenga hospitali ya wilaya lakini Wakala wa Barabara Vijijini *(TARURA)*, *TANESCO* na Mamlaka ya Maji ya eneo husika kutokuwa na mpango wala bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kupeleka huduma muhimu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kufanya Marejeo ya Mikataba ya Kikodi ya Kimataifa Baina ya Serikali na Mataifa mengine; Mikataba ya makubaliano ya kodi baina ya nchi mbili ina malengo makuu mawili:-

(i) Kuondoa uwezekano wa mapato ya mtu mmoja kukatwa kodi mara mbili kwenye shughuli moja ya kiuchumi; na

(ii) Kuondoa uwezekano wa biashara moja kutozwa kodi ya aina moja katika nchi mbili.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo nchi hukubaliana nani atatoza kodi ipi kwenye shughuli gani. Tanzania hivi sasa ina mikataba tisa ya kodi na mikataba hiyo ni kama ilivyoainishwa katika taarifa ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe kwanza kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu.Vilevile nimpongeze Naibu Spika Mheshimiwa Mussa Azan Zungu kwa kuwa msaidizi mwema kwako. Aidha, napenda kumshukuru, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nimshukuru Katibu Mkuu Ndugu Emmanuel Tutuba, Manaibu Makatibu Wakuu, Makamishina na wataalam wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za uandaaji wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa napenda nimshukuru Mheshimiwa Omari Kigua, Makamu

Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipa wakati wote wa kupitia na kuchambua Bajeti Kuu ya Serikali na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi ya Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa Mwihambi *(ndc)* pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati hii kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti, Ndugu Michael Kadebe, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Mathew Kileo na Makatibu wa Kamati Ndugu Emmanuel Rhobi, Ndugu Maombi Kakozi na Ndugu Wilfred Akasi kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii kwa wakati. Napenda pia kuwashukuru Watendaji wote wa Idara na Vitengo vyote vya Ofisi ya Bunge, kwa kuhakikisha kwamba taarifa hii inawasilishwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2021, TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2021/22, MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2022/23, PAMOJA NA MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### 3.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 124(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021, Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/23 pamoja na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/23.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Juni 2020, pamoja na Sheria ya Bajeti Sura 439. Aidha, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba Serikali imekuwa ikitoa ushirikiano wa kutosha kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa shughuli za kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapenda kutoa pongezi za dhati kwa Mhe. Samia Suluhu Hassani Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuthibitisha kwa vitendo uchapakazi wake, uadilifu wake na uaminifu wake kwa Taifa la Tanzania. Kamati inaamini Mheshimiwa Rais amekuwa ni mfano bora wa kuigwa na watu wote wanaopewa dhamana ya uongozi katika nchi yetu.

Ameyaishi maneno yake aliyoyasema wakati wa uapisho kwamba miradi iliyoachwa na Mtangulizi wake ataiendeleza na atahakikisha anaikamilisha. Aidha, Rais ameonyesha uwezo mkubwa katika kupigania Diplomasia ya uchumi na mafanikio yake yameonekana na yanaendelea kuonekana.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isidory Mpango kwa kuendelea kumsaidia Mhe Rais katika majukumu yake. Vilevile, Kamati inampongeza, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kusimamia na kuratibu shughuli zote za Serikali kikamilifu. Aidha, Kamati inakupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa uongozi wako mahiri uliojaa weledi na uzoefu wa kutosha katika kuliendesha Bunge hili la Kumi na Mbili (12) la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika umelithibitishia Bunge kwamba kanuni ndio msingi mkuu wa uendeshaji wa shughuli za Bunge. Vilevile, napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa kushiriki kikamilifu katika kuisaidia Kamati kwenye utekelezaji wa majukumu yake. Sisi Kamati ya Bajeti tunaishukuru miongozo yenu na ushirikiano mnaotupatia katika kutekeleza majukumu yetu.

**Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii pia kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, (Mb) Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, (Mb) Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa kushirikiana vyema na Kamati wakati wote tulipowahitaji kwenye Kamati. Aidha, Kamati inawashukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango Ndg. Emmanuel Tutuba na Manaibu wake, Gavana wa Benki Kuu Prof. Florence Luoga, na Manaibu Gavana, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato

Tanzania Ndg. Alphayo Kidata na Wakuu wa Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

### 3.1. Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hii inatoa tathmini ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/22 na uchambuzi wa Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2022/23 kwa kuangalia viashiria mbalimbali vya uchumi, miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali pamoja na mwenendo wa mapato na matumizi. Pia, Taarifa hii imeainisha maeneo mbalimbali ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii imegawanyika katika maeneo makuu nane (8). Eneo la kwanza ni Utangulizi; Eneo la pili ni Tathmini ya Mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla; Eneo la tatu ni Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/22; Eneo la nne ni Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2021/22 pamoja na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/23; Eneo la Tano linahusu Mapitio ya Utendaji Kazi wa Baadhi ya Mashirika ya Umma pamoja na Utekelezaji wa Bajeti za Mashirika ya Umma; Eneo la Sita linahusu Sura ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/23; Eneo la Saba linahusu Hatua za Kikodi zinazopendekezwa na Serikali; Eneo la Nane ni Maoni na Mapendekezo ya Kamati na mwisho ni Hitimisho.

## 4.0. TATHMINI YA MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI JUMLA KWA MWAKA 2021

### 4.1. Hali ya Uchumi wa Dunia

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Taarifa ya Mwenendo wa Hali ya Uchumi wa Dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa Mwezi Aprili, 2022 (World Economic Outlook Report, April 2022) uchumi wa dunia kwa mwaka 2022 unakadiriwa kukua kwa **asilimia 3.1** ikilinganishwa na makadirio ya ukuaji wa **asilimia 6.0** yaliyotolewa mwezi Julai 2021. Makadirio ya ukuaji kwa kiwango cha chini yanatokana na ukuaji mdogo wa uchumi kwa nchi zilizoendelea za Marekani pamoja na nchi zinazoibukia kiuchumi ikiwemo China. Ukuaji mdogo wa uchumi kwa nchi zilizoendelea umechagizwa na sababu mbalimbali ikiwemo vita baina ya Urusi na Ukraine iliyoathiri uchumi wa dunia kwa kiwango kikubwa, Ugonjwa wa UVIKO-19 unaosambaa duniani, na hivyo kusababisha kufunga maeneo ya uzalishaji na vituo vya biashara.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hiyo pia inaonyesha kwamba Katika kipindi cha mwezi Agosti 2021 hadi mwezi Februari 2022 bei za bidhaa za msingi (Primary Commodities) katika soko la dunia zimepanda kwa asilimia 24, kwa mchanganuo ufuatao

i. Bidhaa za chuma za msingi yaani *base metal* zimeongezeka kwa **asilimia 2**;

ii. Bidhaa za madini ya thamani *precious metal* zimeongezeka kwa **asilimia 3**;

iii. Bidhaa za kilimo zimepanda kwa **asilimia 11** hii ni kutokana na kupanda kwa bei za nafaka katika

soko la dunia kwa **asilimia 21.8.** Aidha bei ya ngano katika soko la Dunia imeongezeka kwa asilimia 26.4; na

iv. Mahitaji ya mafuta duniani yameongezeka kwa mapipa **milioni 99.7** kwa siku hali inayopelekea bei ya mafuta ghafi ya petroli kupanda kwa **asilimia 36**. Hivyo bei ya Mafuta ghafi inatarajiwa kuongezeka Kwa **asilimia 55** mwaka 2022.

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu hizi zinaonyesha wazi kwamba tatizo la mfumuko wa bei lililopo nchini si suala la kulaumu Serikali kwa sababu suala hilo limetokana na hali halisi ya uchumi wa Dunia.

**4.2. Uchumi wa Nchi Kusini mwa Jangwa la Sahara**

**Mheshimiwa Spika**, Katika nusu ya mwisho ya mwaka 2021 uchumi wa nchi za kusini mwa jangwa la Sahara ulitarajiwa kukua kutoka **asilimia 3.7** hadi **asilimia 4.5**. Japokuwa hali ilibadilika mwanzoni mwa mwaka 2022 na hivyo uchumi unatarajiwa kukua kwa **asilimia 3.8** hii ni kutokana na madhara ya vita vya Urusi na Ukraine pamoja na ugonjwa wa UVIKO-19. Matukio haya yamesababisha mfumuko mkubwa wa bei kwa bidhaa mbalimbali ikiwemo mafuta, gesi na vyakula. Vilevile nchi hizi zimekumbwa na tatizo la uhitaji mdogo wa bidhaa zao zinazouzwa nje ya nchi (*low demand of goods)* toka kwa washirika wao wakubwa wa kibiashara (*trade partners)*.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hiyo pia inaonyesha kwamba nchi nane zilizo kusini mwa jangwa la Sahara zinazozalisha mafuta zitanufaika kutokana na kupanda kwa bei za

mafuta na gesi ulimwenguni. Vilevile uchambuzi wa IMF unaonyesha kwamba nchi zinazozalisha madini aina ya dhahabu, almasi, shaba zitanufaika na kupanda kwa bei za madini haya katika soko la dunia. Kwa upande wa nchi 37 zilizo kusini mwa jangwa la Sahara ambazo hazizalishi mafuta na gesi uchumi wake unatarajiwa kuyumba kutokana na kupanda kwa bei ya nishati hizo.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na taarifa za hali ya uchumi wa dunia na uchumi wa nchi zilizo kusini mwa jangwa la Sahara, Kamati ina maoni na ushauri ufuataao:-

i. Kwa kuwa bei ya mazao ya kilimo katika soko la dunia imepanda kwa **asilimia 11** ikichangiwa na kupanda kwa bei ya nafaka kwa **asilimia 21.8**. Kamati inaishauri serikali kwamba Wizara ya Kilimo ishirikiane na TANTRADE kutafuta masoko hasa ya nafaka zenye mahitaji makubwa duniani na kuhamasisha kilimo cha kisasa cha nafaka hizo. Hii italisaidia taifa kupata fedha za kigeni na kuimarisha urari wa kibiashara na kupunguza kasi ya mfumuko wa bei pamoja na kukuza uchumi wa wakulima wetu.

ii. Kwa kuwa Nchi za kusini mwa jangwa la Sahara ikiwemo Tanzania zinategemea **asilimia 85** ya ngano kutoka nje, na kwa kuwa bei ya ngano katika soko la dunia imeongezeka kwa **asilimia 26.4** hali iliyosababishwa na vita vya Urusi na Ukraine pamoja na hali ya ukame uliokithiri nchini Canada. Kamati inaishauri Serikali kufufua na kuimarisha mashamba ya ngano yaliyopo nchini hususani mashamba ya Basotu yaliyoko mkoani Manyara ili kuzalisha ngano ya kutosha na ikiwezekana kuuza nje ya nchi pamoja na

kuhamasisha kilimo hiki kwa maeneo mengine ambayo zao hili linastawi.

iii. Kwa kuwa, mfumuko wa bei kwa mwaka 2022 unatarajiwa kuongezeka kwa wastani wa **asilimia 12.2** kwa nchi za kusini mwa jangwa la sahara. Kamati inaishauri Serikali kupitia Benki kuu ya Tanzania na Wizara ya Fedha na Mipango kuweka mikakati ya muda mfupi na muda mrefu ya jinsi ya kukabiliana na mfumuko wa bei ili kutokuathiri uchumi wa Taifa letu.

iv. Kwa kuwa, nchi zenye mafuta na gesi zinatarajiwa kunufaika na ongezeko la bei katika soko la Dunia, hii ni fursa ya Tanzania kutumia vyema gesi asilia tuliyonayo ili iweze kulinufaisha Taifa. Aidha, nchi 37 zilizo kusini mwa jangwa la Sahara ambazo hazizalishi mafuta na gesi uchumi wake unatarajiwa kuyumba. Huu ni wakati muafaka kwa Tanzania kunufaika na sekta ya Kilimo na Gesi asilia.

## 4.3. Hali ya Ukuaji wa Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Benki kuu ya Tanzania inaonyesha kwamba katika mwaka wa fedha 2021/22 uchumi wa Tanzania ulikua kwa wastani wa **asilimia 4.9** ikilinganishwa na **asilimia 4.8** katika kipindi hicho hicho kwa mwaka 2020/21. Ukuaji huu umetokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na madhara ya janga la UVIKO-19 ikiwemo mkopo toka IMF. Hali hii inaashiria kwamba Tanzania inazidi kujikwamua dhidi ya madhara ya kiuchumi yaliyosababishwa na ugonjwa wa UVIKO-19.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa Mwezi Aprili, 2022 (World Economic Outlook Report, April 2022) inaonyesha kwamba nchi nane zilizo kusini mwa jangwa la Sahara zinazozalisha mafuta zitanufaika kutokana na kupanda kwa bei za mafuta na gesi ulimwenguni. Vilevile, uchambuzi wa IMF unaonyesha kwamba nchi zinazozalisha madini aina ya dhahabu, almasi, shaba na Palladium zitanufaika na kupanda kwa bei za madini haya katika soko la dunia. Aidha, ni wakati muafaka wa kusimamia vizuri masoko yetu ya madini ili tunufaike na ongezeko la bei. Vilevile, Benki kuu inashauriwa kuharakisha utaratibu wa kutunza dhahabu ili inapotokea fursa kama hii iweze kulinufaisha Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu inaonyesha kwamba katika kipindi cha mwaka 2021, Pato la Taifa liliongezeka kwa **shilingi trilioni 135.517** toka **shilingi trilioni 129.130** ya mwaka 2020, sawa na ongezeko la wastani wa **asilimia 4.9**. Shughuli za uchumi zilizokuwa ukuaji mkubwa ni sanaa **(asilimia 19.4)**, umeme **(asilimia 10.0)**, madini **(asilimia 9.6)** na habari **(asilimia 9.1)**.


**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Kilimo ni kati ya sekta pekee ambayo pamoja na uwepo wa ugonjwa wa UVIKO-19 na madhara ya Vita baina ya Urusi na Ukraine imeweza kukua na kuongeza mchango wake katika Pato la Taifa. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawekeza kwa kiasi kikubwa kwenye sekta ya kilimo na sekta nyingine kama vile utalii wa ndani na nje ili zichangie katika uchumi na hivyo kuwa na uchumi usiotegemea sekta chache.

## 4.4. Mfumuko wa Bei

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021 mfumuko wa bei ulikua kwa wastani wa **asilimia 3.7** ikilinganishwa na **asilimia 3.3** mwaka 2020. Ongezeko hili la mfumuko wa bei linatokana na kuongezeka kwa bei za bidhaa, hususani bei za mafuta ya kula na petroli pamoja na bidhaa za walaji katika soko la dunia. Hata hivyo mfumuko wa bei uko ndani ya wigo wa asilimia 5.0 kwa mujibu wa vigezo vya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), na wigo uliowekwa na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wa kati ya **asilimia 3** na **asilimia 8.** Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, Fahirisi za Bei za msingi (Core inflation) zimekuwa na mwenendo imara kutoka mwezi Aprili, 2021 hadi mwezi Aprili, 2022.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Mfumuko wa bei nchini umesababishwa kwa kiasi kikubwa na kupanda kwa bei za mafuta ya kula na petroli na bidhaa za walaji katika soko la dunia, na kwa kuwa mfumuko wa bei duniani unatarajiwa kuongezeka **kwa asilimia 5.7** kwa nchi zenye uchumi ulioendelea na **asilimia 8.7** kwa nchi zinazoendelea, ni dhahiri kwamba kwa mwaka wa fedha 2022/23 mfumuko wa bei utaendelea kuongezeka nchini hivyo Kamati inaishauri Serikali kutilia mkazo katika njia mbalimbali za kudhibiti mfumuko wa bei ili kuleta unafuu wa maisha kwa wananchi.

**Kielelezo Namba 1: Mwenendo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei Kutoka Mwezi Aprili, 2021 hadi Aprili, 2022. (2020 = 100)**




## 4.5. Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji fedha

**Mheshimiwa Spika,** licha ya kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi iliyosababishwa na janga la UVIKO-19 na vita ya Urusi na Ukraine, thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani na sarafu nyingine za washirika wakuu wa biashara ulimwenguni imeendelea kuwa tulivu. Hali hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji thabiti wa sera ya fedha, usimamizi imara katika kuhakikisha uwazi na utaratibu mzuri katika soko la kubadilisha fedha za kigeni, na kuimarika kwa urari wa biashara. Katika kipindi cha Machi, 2021, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa **shilingi 2,309.58** ikilinganishwa na **shilingi 2,306.20** kipindi kama hicho mwaka 2020 sawa na kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola kwa **asilimia 0.14**. Hali hii imechangiwa na mfumuko wa bei unaosababishwa na kupanda kwa bei za mafuta ya kula na petroli katika soko la dunia. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha tunanufaika na ongezeko la bei kwa bidhaa tunazoweza kuziuza nje ya nchi kama gesi na dhahabu. Pili kuhakikisha bidhaa ambazo tunauwezo wa kuzizalisha

ndani ya nchi tunafanya hivyo ili kuepuka mfumuko wa bei kutoka nchi nyingine (Imported Inflation).

### 4.6. Akiba ya Fedha za Kigeni

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi, 2022 akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za kimarekani **milioni 5,581.6,** kiwango kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha **miezi 5** hadi **6**. Aidha, kiwango hiki kimeshuka toka dola za marekani **milioni 6,557.9** kilichoripotiwa na Benki kuu Machi 2021, ambacho kilikuwa kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha **miezi 6** hadi **8.** Kamati inaishauri Serikali badala ya kuendelea kuwa na kiwango cha akiba za Fedha za Kigeni kinachozidi uagizaji wa bidhaa na Huduma kutoka nje kwa zaidi ya miezi 4 badala yake ziada ya zaidi ya miezi 4 iwe inatumika kuikopesha Serikali ili kupunguza gharama ya ukopaji kutoka nje.

**Jedwali Na. 1. Mwenendo wa Akiba ya Fedha za Kigeni kwa mwezi Desemba kuanzia mwaka 2015 hadi 2022**

| | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kiasi (USD million)** | 4,093.7 | 4,325.6 | 5,900.3 | 5,044.6 | 5,554.4 | 4,767.7 | 6,557.9 | 5,581.6 |
| **Uwezo (miezi)** | 5.1 | 5.0 | 6.6 | 4.9 | 6.4 | 5.6 | 6.8 | 5.6 |

***Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania***

### 4.7. Biashara ya Nje

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa kamati ulibaini kwamba hadi kufikia mwezi Machi, 2022 urari wa malipo kwa sekta ya nje ulikuwa na nakisi ya dola za **Marekani**

**milioni 1,315.9** ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani **Milioni 351.9** katika kipindi hicho hicho kwa mwaka 2021. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kujielekeza zaidi katika Sekta ambazo zinaweza kuongeza mauzo yetu nje ya nchi kama Kilimo, Mifugo, Uvuvi pamoja na Madini ili ziweze kupunguza nakisi ya urari wa ujumla. Vilevile Serikali kupitia Benki Kuu isimamie masoko ya ubadilishaji fedha nchini ambayo itapelekea utulivu wa thamani ya shilingi na akiba ya kutosha ya fedha za kigeni kwa kuweka mazingira rafiki yanayozingatia sheria.

**4.8. Deni la Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa kamati ulibaini kwamba hadi mwezi Machi 2022, deni la Serikali lilikuwa ni **Shilingi trilioni 69.44** Kati ya kiasi hicho deni la nje lilikuwa **shilingi trilioni 47.07** na deni la ndani lilikuwa ni **shilingi trilioni 22.37** ukilinganisha na Deni la mwezi Machi 2021, la **Shilingi trilioni 64.46** sawa na ongezeko la **asilimia 7.73** (**Shilingi trilioni 4.98).** Ongezeko la deni limetokana na: Ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo na malimbikizo ya riba ya deni la nje, hususan nchi zisizo wanachama wa kundi la Paris (Non-Paris Club members) ambazo Serikali inaendelea kujadiliana nazo kuahirisha ulipaji wa madeni (The Debt Service Suspension Initiatives).

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kwamba deni letu ni himilivu kwa viwango vyote vya kimataifa. Kamati inaendelea kuishauri Serikali masuala yafuatayo:

viii. Kuangalia uwezekano wa kujipima uhimilivu wa deni kwa kutumia kiashiria cha makusanyo ya mapato ya ndani kwa ulipaji wa deni. Hii ni kwa sababu deni la Serikali hulipwa na makusanyo ya

ndani na ni malipo ya lazima (first charge) katika matumizi ya Serikali;

ix. Kwa kuwa Tanzania ilipata *The Debt Service Suspension Initiatives* – DSSI toka benki ya Exim ya China (**US$ 99.5 million**) na *French Development Agency* (**US$2.6 million**). Hivyo Kamati inaishauri Serikali kulipa madeni haya mara tu muda wa kulipa utakapofika ili kuondoa tatizo la malimbikizo ya madeni;

x. Kamati inatambua hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kukamilisha suala la credit rating, Hata hivyo ni vyema kukamilisha haraka mchakato wa nchi yetu kufanyiwa tathmini ya uwezo wa ukopaji na ulipaji (credit rating) ili kuiwezesha Serikali kupata mikopo yenye masharti nafuu na kwa urahisi;

xi. Mikopo yenye masharti ya kibiashara ielekezwe katika miradi yenye sura ya kibiashara ili miradi hii ikamilike kwa wakati na kuanza kurejesha gharama za mikopo hiyo;

xii. Kuboresha mikakati ya kukusanya kodi ili kuhakikisha sehemu kubwa ya bajeti inagharamiwa na mapato ya ndani pamoja na kupunguza matumizi yanayoweza kuepukika; na

xiii. Serikali kutafuta mikopo yenye masharti ya kati (Semi concessional loans) ambayo masharti yake ni nafuu ikilinganishwa na mikopo ya kibiashara. Izingatiwe kwamba gharama za mikopo ya

biashara zitaongezeka kutokana na kuongezeka kwa riba za mikopo katika mataifa yaliyo endelea pamoja na mfumuko wa bei

**Jedwali Na 2. Mwenendo wa Deni la Serikali kati ya mwezi Aprili 2021 na Aprili 2022**

| | Hadi Kufikia Aprili 2022 | | Hadi Kufikia Juni 2021 | | Tofauti ya Deni | | Tofau katik Asilim |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | TZS Bilioni | USD Milioni | TZS Bilioni | USD Milioni | TZS Bilioni | USD Milioni | |
| Deni la Nje | 47,074.66 | 20,376.70 | 45,521.45 | 19,703.10 | 1,553.21 | 673.60 | 3.31% |
| Deni la Ndani | 22,369.80 | 9,731.15 | 18,934.33 | 8,236.14 | 3,435.47 | 1,495.01 | 15.36 |
| Deni la Serikali Kuu | 69,444.46 | 30,107.85 | 64,455.78 | 27,939.24 | 4,988.68 | 2,168.61 | 7.20% |

*Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango*

**4.9. Mwenendo wa Viwango vya Riba na Huduma za Kibenki.**

**Mheshimiwa Spika,** mwezi Machi 2022, riba katika mabenki ya kibiashara ilitozwa kwa wastani wa **asilimia 16.28** ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 16.63** ya kipindi kama hicho mwaka 2021. Hali hii imetokana na jitihada za Serikali katika kuyaongezea mabenki yetu nchini ukwasi hivyo kusababisha viwango vya mikopo ya riba nchini kuendelea kushuka. Vilevile riba inayotozwa kwenye amana za mwaka mmoja ni kati ya **asilimia 6.94** na **asilimia 8.21** mwaka 2022 ikilinganishwa na **asilimia 6.83** na **asilimia 8.57** kwa mwaka 2021

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza ukwasi katika mabenki ili kushusha viwango vya riba za mabenki na amana. Hata, hivyo kamati inaishauri

Serikali kuangalia upya masharti yaliyowekwa kwenye Mkopo wa shilingi trilioni 1 kwa mabenki ili yaweze kukopesha sekta mbalimbali za uchumi ikiwemo kilimo kwa kati ya **asilimia 9** hadi asilimia 10. Masharti yalivyo hivi sasa ni vigumu kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa sababu Benki zitakazonufaika na mkopo huo ni benki kubwa tu. Aidha, kamati inaishauri Serikali kuendelea kusimamia sekta hii ili kuhakikisha kwamba riba zinazotozwa zinaendena na vihatarishi pamoja na mfuko wa bei.

### 4.10.Tathmini ya Hali ya Umaskini Nchini

**Mheshimiwa Spika,** viashiria vya kupima hali ya umaskini nchini hupatikana kwa kutumia taarifa za Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi (Household Budget Survey - HBS) utafiti unaofanyika kila baada ya miaka mitano. Matokeo ya Utafiti ya mwaka 2017/18 yanaonyesha kuwa kaya zenye idadi ndogo ya watu zina kiwango kidogo cha umaskini kuliko kaya zenye idadi kubwa ya watu. Na kiwango cha umaskini wa mahitaji ya chakula na ya msingi ni kikubwa kwa kaya zinazoongozwa na wakuu wa kaya wenye elimu ndogo. Kamati inatambua kuwa mojawapo ya hatua kubwa ya maendeleo sio tu kukua kiuchumi lakini pia kuhakikisha umaskini wa mahitaji ya msingi na umaskini wa chakula unapungua. Hivyo, Serikali iendelee kusimamia vema Sera yake ya Elimu Msingi bila ada na kutekeleza Sera ya Idadi ya Watu ya mwaka 1992 ambayo inaelekeza wananchi kuzaa watoto wanaoweza kuwahudumia. Kamati inaendelea kusisitiza kwamba Serikali iwekeze zaidi katika sekta ambazo zinahusisha wananchi wengi kama vile kilimo, mifugo na uvuvi ili kuwakwamua kutoka kwenye umaskini.

## 5.0. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2021/22 Serikali ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 37.99** kutoka katika vyanzo vya ndani na nje. Kati ya fedha hizo mapato ya ndani yalikadiriwa kuwa **shilingi trilioni 24.83**, Mapato ya Halmashauri yalikuwa **shilingi bilioni 863.86**, misaada na mikopo yenye mashati nafuu yalikuwa **shilingi trilioni 4.25** na Mikopo ya ndani ilikuwa **Shilingi trilioni 8.03**. Hadi Aprili, 2022 Serikali ilikusanya na kutumia **shilingi trilioni 29.84** sawa na **asilimia 78.55** ya lengo la mwaka. Kati ya fedha hizo **shilingi trilioni 12.06** ni fedha za matumizi mengineyo ikijumuisha malipo ya Deni la Serikali, **shilingi trilioni 6.73** ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi trilioni 10.61** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

### 5.1. Mwenendo wa Mapato.

**6.0.** Mapato ya Kodi

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania iliweza kukusanya jumla ya **Shilingi trilioni 17.20** dhidi ya lengo la kukusanya **shilingi trilioni 21.78** sawa na **asilimia 78.97**. Mapato ya kodi kwa mwaka 2021/22 yameongezeka kwa **asilimia 18.5** ukilinganisha na kipindi kama hicho mwaka 2020/21. Mwenendo huu unaonesha wazi kwamba Mamlaka ya Mapato inaweza kukusanya kati ya **asilimia 85 hadi 90** ya lengo. Nitumie fursa hii kwanza kumpongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiari na kutoa kibali cha kuajiri watumishi takribani 2000 na Pili Nimpongeze Ndg. Alphayo Kidata Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania

pamoja na Watendaji wote wa TRA kwa ukusanyaji wa kodi kwa ufanisi. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha inaiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa rasilimali watu na fedha ili ifanye kazi zake kwa ufanisi na tija.

**Jedwali Na.2.Ulinganisho wa Makusanyo ya Kodi kuanzia Julai hadi Aprili kwa mwaka 2019/20, 2020/21 na 2021/22 (Tanzania Bara)**

| Mwezi | Makusanyo Halisi 2019/20 | Makusanyo Halisi 2020/21 | Makusanyo Halisi 2021/22 | Asilimia za Ukuaji |
|---|---|---|---|---|
| Julai | 1,232,189.51 | 1,267,684.68 | 1,406,285.05 | 10.93% |
| Agosti | 1,315,495.03 | 1,376,047.61 | 1,622,783.06 | 17.93% |
| Septemba | 1,708,501.52 | 1,681,595.98 | 1,687,435.10 | 0.35% |
| Oktoba | 1,445,098.98 | 1,314,921.71 | 1,640,509.53 | 24.76% |
| Novemba | 1,446,408.00 | 1,317,311.47 | 1,659,300.09 | 25.96% |
| Disemba | 1,906,284.26 | 2,087,934.57 | 2,300,446.13 | 10.18% |
| Januari | 1,476,474.76 | 1,288,372.39 | 1,729,390.26 | 34.23% |
| Februari | 1,303,475.53 | 1,296,990.58 | 1,618,832.38 | 24.81% |
| Machi | 1,539,061.34 | 1,625,196.77 | 1,965,755.82 | 20.95% |
| Aprili | 1,167,545.20 | 1,258,130.60 | 1,568,242.03 | 24.65% |
| **JUMLA** | **14,540,534.13** | **14,514,186.37** | **17,198,979.45** | **18.50%** |

***Chanzo**: Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)*

**7.0.** Mapato yasiyo ya Kodi

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Aprili, 2022 Mapato yasiyo ya Kodi yalifikia **shilingi trilioni 2.03**, sawa na **asilimia 65.56** ya lengo la kukusanya **shilingi trilioni 3.05** kwa mwaka. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba Wizara na

Idara zote zinazo kusanya Maduhuli ya Serikali zinafanya hivyo kwa kutumia mifumo ya kieletroniki ili kuleta ufanisi.

**8.0.** Mapato ya Serikali za Mitaa

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Aprili 2022 Mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani vya Mamlaka za Serikali za Mitaa yalifikia **shilingi bilioni 759.0** sawa na **asilimia 87.86** ya lengo. Pamoja na mafanikio haya bado kuna changamoto kubwa ya uchache wa mashine za POS (Point of Sale) na matumizi yake kwa Serikali za mitaa ili kuhakikisha hakuna ubadhirifu wa mapato yanayokusanywa unaotokana matumizi ya mashine hizo.

**9.0.** Misaada na Mikopo ya Masharti Nafuu kutoka Nje

**10.0.**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2021/22 Serikali ilitarajia kupokea jumla ya **shilingi trilioni 4.27**. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022 Misaada na mikopo nafuu iliyopokelewa ilikuwa **shilingi trilioni 3.93** sawa na **asilimia 92.0** ya lengo. Hali hii inaonyesha kwamba kwa mwaka wa fedha 2021/22 wahisani wamejikita zaidi kutoa mikopo nafuu. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo kwa kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano (Development Cooperation Framework-DCF) ambao umeonyesha matumaini makubwa kimaendeleo katika kipindi kifupi.

**11.0.**Mikopo ya ndani

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2021/22 Serikali ilikusudia kukopa jumla ya **shilingi trilioni 4.99.** Hadi kufikia mwezi Aprili 2022 mikopo kutoka vyanzo vya ndani ilifikia **shilingi trilioni 4.12** sawa na **asilimia 82.57** ya lengo. Kamati inaishauri Serikali kupunguza kukopa ndani ili kuipa nafasi sekta binafsi kupata mikopo kwa riba nafuu ili

kuchochea uwekezaji na hatimaye kukuza uchumi wa nchi.

## 11.1.Mwenendo wa Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/22 Serikali ilikusudia kutumia **shilingi trilioni 37.98** ambapo **shilingi trilioni 23** ni matumizi ya kawaida na **shilingi trilioni 14.98** ni matumizi ya maendeleo. Hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya **shilingi trilioni 29.40** zimetolewa sawa na **asilimia 77.4** ya lengo. Kati ya kiasi hicho, **shilingi trilioni 18.79** zilitumika kwa ajili matumizi ya kawaida ambayo yalijumuisha **shilingi trilioni 6.73** kwa ajili ya mishahara, **shilingi trilioni 4.79** Matumizi Mengineyo na **shilingi trilioni 7.27** kugharamia deni la Serikali. Aidha, jumla ya **shilingi trilioni 10.61** sawa na **asilimia 70.76** ya lengo la mwaka zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamia vyema Sera za Matumizi kwa mwaka 2021/22.

## 12.0.TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2021/22 NA MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2022/23

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2022/23 ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wa 2021/22 – 2025/26. Dhima ya Mpango huu ni *Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu*. Mpango huu utakuwa na maeneo makuu matano ya kipaumbele ambayo ni: (i) kuchochea uchumi shindani na shirikishi; (ii) kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; (iii) kukuza biashara; (iv) kuchochea maendeleo ya watu; na (v) kuendeleza rasilimali watu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kutoa maelezo ya utangulizi hapo juu, Kamati ingependa kutoa maelezo, ushauri na maoni yake katika maeneo yafuatayo: -

**12.1.Tathmini ya Utekelezaji**

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, Serikali ilikuwa imetumia jumla ya **Shilingi trilioni 10.72** ambayo ni sawa na **asilimia 85.3** ya Bajeti iliyokuwa imetengwa ya **Shilingi trilioni 14.99** kwa mwaka wa fedha 2021/22. Kati ya fedha hizo **Shilingi trilioni 10.72** zilizopokelewa, **Shilingi trilioni 9.14** ni fedha za ndani na **Shilingi trilioni 1.46** ni fedha za nje. Hatua hii inaonyesha dhamira ya dhati ya Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutumia fedha za ndani kuliletea Taifa maendeleo.

**Jedwali Na. 3 Utolewaji wa Fedha za Maendeleo hadi Tarehe 30 Aprili, 2022**

| BAJETI | MWAKA 2021/22 | FEDHA ZILIZOTOLEWA | ASILIMIA YA BAJETI |
|---|---|---|---|
| Fedha za Ndani | 10,723,022,999,999 | 9,141,606,071,313 | 85.25 |
| Fedha za Nje | 4,266,573,553,001 | 1,464,679,893,004 | 34.33 |
| **JUMLA** | **14,989,596,553,000** | **10,606,285,964,317** | **70.76** |

**13.0.** Sekta ya Afya

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya afya, huduma za kibingwa, upatikanaji wa vifaa tiba, kinga, dawa na vitendanishi. Serikali imeweza kufanya ujenzi na ukarabati mkubwa wa vituo vya Afya 304 ili kuviwezesha kutoa huduma kwa wajawazito wanaopata uzazi

pingamizi wakati wa kujifungua (CEmONC). Hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya vituo vya Afya 250 sawa na asilimia 82.2 vilikuwa vimeanza kutoa huduma kamili ya CEmONC ikiwa ni pamoja na upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni. Vile vile Serikali imefanikiwa kukamilisha Vyumba/Wodi za Watoto Wachanga Mahututi (Neonatal Intensive Care Unit - NICU) 30 katika hospitali za Halmashauri na hivyo kuwezesha kuwepo kwa jumla ya NICU 165. Aidha, Serikali imefanikiwa kupunguza vifo vya watoto wachanga kutoka vifo 8,190 mwaka 2020 hadi vifo 6,741 mwaka 2021; vifo vya Watoto wa chini ya mwaka mmoja vimepungua kutoka vifo 2,657 mwaka 2020 hadi vifo 1,092 mwaka 2021 na vifo vya Watoto wa umri chini ya miaka mitano vimepungua kutoka vifo 3,482 mwaka 2020 hadi vifo 1,512 mwaka 2021.

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto kubwa zinazoikabili sekta hii hivi sasa ni ukosefu wa watumishi katika miundombinu iliyojengwa na Serikali, ununuzi na usambazaji wa dawa na vifaa Tiba pamoja na baadhi ya maeneo kutokuwa na vituo vya afya na zahanati. Aidha, kamati inaendelea kusisitiza Serikali kuharakisha mchakato wa uanzishwaji wa Sheria ya Bima kwa wote ili isaidie wananchi wa hali ya chini katika kupata huduma za afya. Nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambae hadi mwezi Aprili alikuwa ametoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa madawa na vifaa Tiba kupitia MSD vyenye thamani ya **Shilingi bilioni 129.85.**

**14.0.**Sekta ya Elimu

**Mheshimiwa Spika,** Kama kuna sekta ambayo imepiga hatua kubwa za maendeleo katika ujenzi wa miundombinu ya Msingi ya Kufundishia na kujifunza ni

Sekta ya Elimu. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kutekeleza Mpango ni kama ifuatavyo:-

i. Kurejesha wanafunzi wa kike 3,333 masomoni kupitia mpango wa kurejesha wanafunzi;

ii. Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa vyuo vya VETA katika mikoa 25 ya Tanzania Bara;

iii. Jumla ya **Shilingi bilioni 304.00** zilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta ya elimu (elimu msingi) ambapo **Shilingi bilioni 240.00** ni kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 12,000 vya madarasa katika Shule za Sekondari, **Shilingi bilioni 60.00** kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 3,000 vya madarasa katika Vituo Shikizi na **Shilingi bilioni 4.00** kwa ajili ya ujenzi wa mabweni 50 katika Shule za Msingi zenye wanafunzi wenye mahitaji maaalum; na

iv. Vitabu 18,200 vilisambazwa kwa Watoto wenye uoni hafifu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kwamba Serikali ipo katika hatua ya kuajiri walimu ili kupunguza upungufu uliopo. Suala hili liende sambamba na kurejea mitaala yetu ili iendane na wakati na kuangalia namna ya kutoa mikopo kwa vyuo vya ufundi kama ilivyo kwa vyuo vikuu. Kamati inaamini hivi sasa tunahitaji wataalamu wengi kutoka kwenye vyuo vya kati kuliko wenye shahada.

**15.0.** Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi

**15.1.1.1. Kilimo**

**Mheshimiwa Spika,** Kilimo ni moja ya sekta ambazo ni nguzo kuu ya maendeleo ya viwanda kwa sababu ndiko malighafi za viwandani zinapopatikana. Aidha, kilimo ndicho kinaajiri takribani **asilimia 65** ya watanzania wote. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika sekta hii ni pamoja na:-

i. Kuwezesha uzalishaji wa **Tani 18,665,217** za chakula ukilinganisha na mahitaji ya **tani 14,835,101** hivyo kuwa ziada ya **tani 3,830,116** za chakula sawa na utoshelevu wa chakula wa **asilimia 126;**

ii. Kuongezeka kwa matumizi ya zana bora za kilimo kama vile matrekta kutoka **asilimia 23** mwaka 2020/21 hadi **asilimia 25** kwa mwaka 2021/22; na

iii. Kuongeza mbegu mpya aina 18 zilizogunduliwa na kuzalishwa na Taasisi za Umma na sekta binafsi.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mafanikio hayo sekta hii bado inakumbwa na changamoto mbalimbali kama vile ardhi ya kilimo kuendelea kupungua kutokana na kuvamiwa kwa ajili ya makazi, kuendelea kuagiza mazao ya nafaka kama ngano na shairi ambayo yanaweza kuzalishwa nchini, utaratibu usioridhisha wa uagizaji na usambazaji wa mbolea zinazotoka ndani na nje. Aidha, imekuwa vigumu kwa sekta ya kilimo kupata mikopo kwa ajili ya kuiendeleza kutokana na vihatarishi vyake. Kamati inaamini masuala haya yakifanyiwa kazi Kilimo kinaweza kuwa sekta moja itakayolitoa Taifa hapa lilipo.

### 15.1.1.2. Sekta ya Mifugo

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya mifugo ni miongoni mwa sekta zilizofanya vizuri katika mwaka wa fedha 2021/22.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba katika mwaka 2021/2022 idadi ya mifugo hapa nchini imeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2020/2021 ambapo idadi ya ng'ombe imeongezeka kutoka **milioni 33.9** hadi **milioni 35.3**. Vilevile uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka **lita bilioni 3.1** mwaka 2020/2021 hadi kufikia lita **bilioni 3.4** katika mwaka 2021/22. Aidha, uzalishaji wa nyama umeongezeka kutoka tani **738,166** mwaka 2020/2021 hadi tani **769,966.7** mwaka 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia **4.3.** Pia uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai **bilioni 4.5** mwaka 2020/2021 hadi mayai **bilioni 4.9** mwaka 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 8.8.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza tija katika sekta ya mifugo Kamati inapendekeza mambo yafuatayo yafanyiwe kazi;

i. Kwa kuwa Sekta ya Mifugo inauhitaji wa maafisa ugani wa mifugo 14025 na waliopo ni 3642. Ni dhahiri kwamba wafugaji wengi nchini wanakosa huduma ya ugani. Kamati inaishauri Serikali kuongeza maafisa ugani wa mifugo katika sekta hii ili kuongeza tija na kuwafikia wafugaji wengi;

ii. Kuimarisha taasisi zilizo chini ya Sekta ya mifugo kama vile Kampuni ya Ranchi za taifa inayokumbwa na uhaba wa bajeti na migogoro ya ardhi, Bodi ya maziwa na Bodi ya nyama zinazokumbwa tatizo la urasimu wa vibali na usajili kwa wadau wake;

iii. Kudhibiti tatizo la utoroshaji wa mifugo nje ya nchi kwa masoko na vituo vilivyo mipakani;

iv. Kuboresha mazingira ya ufanyaji wa biashara ya mifugo kwa kujenga na kuboresha minada ya mifugo ili

kuongeza thamani ya mifugo na hivyo kumpa faida mfugaji na kuleta tija katika taifa;

v. Kutoa fedha za kutosha katika vituo vya taifa na kikanda vya uhimilishaji wa mifugo, ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa mitamba ya nyama na maziwa; na

vi. Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) izijengee uwezo Jumuiya za Wafanyabiashara wa nyama na maziwa nchini juu ya namna bora ya kusimamia shughuli zao ndani na nje ya Nchi.

**15.1.1.3. Sekta ya Uvuvi**

**Mheshimiwa Spika,** sekta ya Uvuvi ni miongoni mwa sekta muhimu za uchumi nchini inayochangia katika Pato la Taifa na kuondoa umaskini. Katika mwaka 2021, Sekta ya Uvuvi ilikua kwa asilimia **2.5** na ilichangia asilimia **1.8** kwenye Pato la Taifa. Aidha, Sekta ya Uvuvi inatoa ajira kwa watanzania takriban Milioni **4.5** katika mnyororo mzima wa thamani ambapo ajira za moja kwa moja kwa wavuvi ni **194,804** na wakuzaji viumbe maji ni **31,998**. Hadi kufikia mwezi April 2022, jumla ya tani **415,880.64** za samaki zenye thamani ya **Shilingi trilioni 2.80** zilivunwa, ikilinganishwa na tani **422,859.78** za samaki zenye thamani ya **Shilingi trilioni 2.62** zilizovunwa katika kipindi kama hiki mwaka 2020/2021

**16.0.**Sekta ya Maji

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji mijini na vijiji. Pongezi hizi zinatokana na utolewaji wa fedha kwa miradi ya maji kupitia mfuko wa maji, Bajeti Kuu ya Serikali na nyongeza ya Bajeti kupitia Fedha za

UVIKO-19 ambapo zina jumla ya **Shilingi bilioni 733.28** hadi mwezi machi zilikuwa zimetolewa jumla ya **Shilingi bilioni 522.44** sawa na **asilimia 71.2**. Hata hivyo, pamoja na juhudi hizi ni vema Serikali ikaongeza juhudi katika usimamizi wa miradi yake inayoitekeleza ili ilete tija inayotazamiwa na kwa kujengwa kwa ubora na kwa kuzingatia thamani ya fedha.

**17.0.**Sekta ya Miundombinu

## 17.1.1.1. Barabara

### a) TARURA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha chanzo maalumu kupitia tozo ya mafuta ili fedha zitakazopatikana zielekezwe TARURA kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara za Vijijini. Hadi mwezi Machi 2022 TARURA ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 660.96** sawa na **asilimia 66** za Bajeti ya **Shilingi trilioni 1.01.** Kati ya fedha zilizopokelewa **asilimia 48.74** zinatokana na tozo ya mafuta na **asilimia 51.26** zinatoka katika vyanzo vingine. Hivyo Kamati haitarajii kuona kwamba Serikali ina nia ya kufuta tozo hii hasa ukizingatia urefu wa barabara za TARURA na umuhimu kwa sekta ya Kilimo na wananchi wa Vijijini. Aidha, kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kujenga barabara za teknolojia nafuu za vijijini ili kupunguza matengenezo ya kila mwaka.

**Jedwali Na 4. Utolewaji wa Fedha hadi Mwezi Machi 2022 kwa Wakala wa Barabara Vijijini-TARURA**

| Na | CHANZO | BAJETI 2021/22 | ZILIZOTOLEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mfuko wa Barabara Matengenezo | 243,146,889,329 | 178,742,266,043 | 73.51 |

| Na | CHANZO | BAJETI 2021/22 | ZILIZOTOLEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 2. | Mfuko wa Barabara Maendeleo | 23,546,749,770 | 15,055,000,115 | 63.94 |
| 3. | Nyongeza Mfuko Mkuu wa Serikali | 127,500,000,000 | 107,215,000,000 | 84.09 |
| 4. | Tozo ya Mafuta | 322,158,200,000 | 205,917,635,697. | 63.92 |
| 5. | Mapato parking & hifadhi ya barabara | 30,447,063,548 | 19,802,332,760 | 65.04 |
| 6. | Barabara Mji wa Serikali Mtumba | 30,447,063,548 | 15,043,595,891 | 49.41 |
| 7. | Miradi Ahadi za Viongozi | 14,517,109,419 | 31,427,919,342 | 216.49 |
| 8. | Agri Connect | 22,263,192,571 | | 0. |
| 9. | Mishahara (PE) | 31,665,784,000 | 19,802,332,760 | 63 |
| 10. | DMDP | 156,031,456,038 | 82,609,000,000 | 53 |
| | **JUMLA** | **1,006,024,057,039** | **675,615,082,610** | 70.42 |

*Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wakala wa Barabara Vijijini.*

### 17.1.1.2. Bandari

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kuboresha bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga pamoja na bandari zilizopo katika maziwa makuu na bandari kavu kila kanda mfano Dar es salaam, Morogoro, Dodoma, Mwanza, Mtwara, Mbeya na Tanga. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba Mamlaka ya Bandari badala ya kuendelea kuwekeza ili kuwe na

ufanisi katika uondoshaji wa shehena Bandarini inafikiria kutumia makampuni ya nje kama vile *DP world* na TICTS. Hatua hii inaweza kuleta mafanikio ya ufanisi lakini itapunguza kwa kiasi kikubwa mapato ya Serikali. Mfano kuna baadhi ya mizigo haiwezi kushushwa na TPA kwa sababu hawana kifaa kiitwacho N-GEN na badala yake makontena yanayohitaji kifaa hicho hutumia gati ambazo ziko chini ya TICTS. Kifaa hicho kina kazi ya kutoa taarifa za wakati yaani *real time* wakati wa upakiaji na upakuaji wa makasha. Aidha, kamati imebaini kwamba Mamlaka ya Bandari imekuwa haikamilishi mifumo yake kwa wakati ili kukusanya mapato kwa ufanisi. Kamati inaamini masuala hayo yakifanyiwa kazi kutakuwa na ufanisi mkubwa na ongezeko la mapato kwa Bandari zetu zilizo chini ya TPA.

**18.0.** Sekta ya Viwanda na Biashara

**Mheshimiwa Spika**, Dhima ya ujenzi wa uchumi wa viwanda na Ushindani inaonekana katika Mpango wa I, II na III wa Maendeleo ya Taifa. Hata hivyo utekelezaji wake umekuwa ni wa kusua sua kutokana na mazingira mabovu ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kukamilisha haraka mchakato wa kuleta Bungeni Sheria ya Kuwezesha Ufanyaji Biashara nchini yaani **Business Facilitation Act** ili isaidie utekelezaji wa *Blue print* pamoja na wadau wengine.

**Mheshimiwa Spika,** Moja ya eneo ambalo linaathiri sana Sekta ya Viwanda nchini ni bisahara ya magendo katika mipaka yetu. Ukubwa wa mipaka yetu umekuwa ni mwiba kwa viwanda vya ndani. Hivyo, Kamati inaitaka serikali kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa vifaa pamoja na watumishi ili waweze kusimamia

vyema mipaka yetu na kuzuia biashara hii haramu ya magendo.

**19.0.**Sekta ya Utalii

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya utalii ni miongoni mwa sekta za kiuchumi ambazo zilikumbwa na changamoto za ukuaji katika kipindi cha mwaka 2020/21 kutokana na janga la Homa Kali ya Mapafu lililoikumba dunia kuanzia mwishoni mwa mwaka 2019 hadi mwaka 2020. Mwaka 2021/22 kamati ilishauri Serikali kuangalia namna ya kutangaza utalii wetu ili kurejesha biashara ya utalii iliyokuwa imeathirika kwa kiasi kikubwa. Aidha kamati ilishauri Serikali kutafuta fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya hifadhi yetu iliyokuwa imeharibika kutokana na mvua.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nimpongeze Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchukua uamuzi madhubuti wa kuandaa filamu ya *The Royal tour* ili kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini. Aidha, kupitia fedha za Mkopo kutoka IMF sekta hii ilipewa mgao wa **shilingi bilioni 90.2** ili kukarabati na kujenga miundombinu ya msingi pamoja na kununua mitambo itakayokuwa ikikarabati miundombinu hiyo mara kwa mara. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kuweka mazingira bora ya uwekezaji katika malazi ili kuvutia watalii wengi zaidi.

**20.0.** Sekta ya Ardhi na Mazingira

**20.1.1.1. Ardhi**

**Mheshimiwa Spika**, Ardhi ni maliasili isiyoongezeka, hivyo, ni muhimu kuwa na mipango bora ya matumizi ya ardhi

kwa vizazi vya sasa na Vizazi vijavyo. Endapo hatutapanga matumizi bora ya ardhi kwa kuangalia ongezeko la watu ni wazi kwamba vizazi vijavyo havitakuwa na maeneo ya hifadhi za misitu, makazi na maeneo ya shughuli za kiuchumi. Hivyo, ni lazima maamuzi yafanyike sasa ya kulinda misitu, mabonde na rasilimali maji ambazo zitaimarisha ustawi wa mazingira ambayo ni kiungo muhimu katika maendeleo endelevu. Vilevile, Serikali ione umuhimu wa kuingiza kilimo na uhifadhi wa misitu katika miji *(urban agriculture and urban forestry)*.

### 20.1.1.2. Mazingira

**Mheshimiwa Spika,** Utunzaji wa mazingira ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa lolote. Uharibifu wa mazingira unagharama kubwa sana kutokana na majanga yanayoweza kujitokeza kama vile ukame, mvua zilizopita kiasi, upepo mkali na ongezeko la joto. Hivyo, Kamati inaushauri Serikali kuhakikisha Sheria ya Mazingira Sura ya 191 inasimamiwa kikamilifu. Aidha, Inashauriwa kufanya marekebisho Sheria ya Mazingira sura ya 191 iliyoanzisha mfuko wa Mazingira ili kuwezesha kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kutafuta vyanzo vya fedha za kufadhili miradi ya kutunza na kuboresha mazingira.

## 21.0.TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA MIFUKO

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti Sura 439 kifungu cha 9 (f) kinaipa mamlaka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kukutana na Mashirika ya Umma ili kuangalia mizania yao ya fedha pamoja na kuangalia endapo mashirika hayo yanafuata misingi ya sheria za fedha za umma na sheria nyingine za Nchi. Kutokana na takwa hilo la kisheria Kamati ilikutana na kufanya

Tathimini ya utendaji kazi wa mifuko maalumu na Mashirika ya Umma. Masuala yafuatayo yalibainika:-

**21.1.Utekelezaji wa Bajeti ya Mifuko Maalumu (Ring-fenced Funds)**

**22.0.**Mfuko wa Maji

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa maji una chanzo kikuu kimoja cha fedha zinazotokana na tozo ya mafuta ya petroli na dizeli. Kamati imebaini kwamba utolewaji wa fedha za kutekeleza miradi ya maji kwa miaka miwili mfululizo umekuwa ukitegemea zaidi chanzo cha tozo ya Mafuta ya petroli na Dizeli kuliko fedha kutoka Mfuko mkuu wa Serikali. Fedha kutoka mfuko mkuu wa Serikali zimekuwa hazitolewi kama zilivyoidhinishwa na Bunge isipokuwa kwa mwaka wa fedha 2021/22 ambapo sekta hiyo ilipokea fedha za Uviko-19 **shilingi bilioni 139**. Fedha zilizotolewa kutoka kwenye tozo ya mafuta kwenda kwenye mfuko wa maji ni **asilimia 78.4** ya lengo la mwaka. Mwenendo wa utolewaji wa fedha wenye tija kama huu ulijitokeza kwa mwaka wa fedha 2020/21 ambapo Tozo ya mafuta kwenda kwenye Mfuko wa maji ilikuwa ni **asilimia 97.1** (Rejea Jedwali Na 5 Hapo chini linaonyesha mwenendo huu.)

**Jedwali Na. 5 - Mwenendo wa Bajeti ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Maji**

| **Chanzo** | **Bajeti 2020/21** | **Fedha zilizotolewa hadi aprili 2021** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| Tozo ya mafuta | 175,912,837,000 | 170,848,841,709.00 | **97.1** |
| **chanzo** | **2021/22** | **Hadi mwezi Machi 2022** | |
| Tozo ya mafuta | 175,912,837,000.00 | 137,956,116,703.40 | **78.4** |

***Chanzo: Wizara ya Maji***

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba shida iliyoko katika Wizara ya Maji na Umwagiliaji hivi sasa si uhaba wa fedha bali ni tatizo la ukosefu wa rasilimali watu wa kusimamia miradi ya maji. Kamati inaishauri Serikali kuipatia Wizara hii wataalamu wa kutosha ili kuongeza ufanisi wa upatikanaji wa maji kwa wananchi.

**23.0.**Mfuko wa Barabara

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Mfuko wa Barabara inatambua vyanzo vya mapato vya Mfuko huu ni tozo ya mafuta ya petroli na dizeli (Fuel Levy); ushuru wa magari ya kigeni yanayotumia barabara za Tanzania (*Transit Fees*); tozo ya uzidishaji wa uzito (*overloading charges*) pamoja na fedha kutoka Serikali kuu. Kamati imebaini kwamba chanzo kutoka Tozo za mafuta kimekuwa kikifanya vizuri kwa **asilimia 97** tofauti na vyanzo vingine.

**Jedwali Na.6 Bajeti na Mgawo wa Fedha za Mfuko wa Barabara (Shilingi)**

| | Bajeti | Mgawo | Mafanikio |
|---|---|---|---|
| **2020/21** | | | |
| TANROADS | 572,604,616,096.20 | 541,633,349,000 | 94.6% |
| TARURA | 245,401,978,709.34 | 232,128,578,505 | 94.6% |
| MoWT | 63,622,735,121.80 | 60,181,483,222 | 94.6% |
| PO-RALG | 27,266,886,523.26 | 25,792,064,278 | 94.6% |
| RF Admin. | 7,884,312,549.40 | 7,457,862,704 | 94.6% |
| **Jumla** | **916,780,529,000** | **867,193,337,709.75** | **94.6%** |
| **2021/22** | | | |
| TANROADS | 567,342,742,235.00 | 473,578,215,492.59 | 83.5% |
| TARURA | 243,146,889,529.00 | 202,962,092,353.39 | 83.5% |
| MoWT | 63,038,082,471.00 | 52,619,801,721.82 | 83.5% |
| PO-RALG | 27,016,321,059.00 | 22,551,343,595.21 | 83.5% |
| RF Admin. | 7,811,860,706.00 | 6,520,797,354.87 | 83.5% |
| **Jumla** | **908,355,896,000.00** | **758,232,250,518.00** | **83.5%** |

***Chanzo: Bodi ya Mfuko wa Barabara***

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto kubwa ambayo Kamati imebaini katika utekelezaji wa Mfuko huu ni baadhi ya barabara kujengwa chini ya kiwango na hivyo kuhitaji matengenezo makubwa ndani ya muda mfupi. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuboresha kitengo cha ukaguzi wa barabara (road inspection) ili kuhakikisha kwamba barabara zinafanyiwa matengenezo kwa wakati.

**24.0.**Mfuko wa Maendeleo ya Reli

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 68 cha Sheria ya Reli Na. 10 ya mwaka 2017 (Railways Act, No. 10 of 2017) kinatambua uwepo wa Mfuko wa Reli. Mwenendo wa utolewaji wa fedha kwa miaka miwili katika mfuko huu umekuwa ni wa kuridhisha. Kwa wastani kati ya Mwaka 2020/21 na 2021/22 Mfuko wa reli ulipokea fedha kutokana na tozo ya mafuta kwa wastani wa **asilimia 85.92.** Kamati ilifanya uchambuzi wa matumizi ya mfuko wa reli na ikabaini kwamba kwa kiasi kikubwa matumizi ya mfuko huu kwa mwaka 2021/22 yameelekezwa kwenye Malipo kwa ajili ya mkandarasi wa ujenzi wa njia ya reli ya kisasa *Standard Gauge Railway* kwa kipande cha Morogoro hadi Makutupora (Km 722) pamoja na matengenezo ya njia ya reli ya Meter Gauge katika maeneo mbalimbali nchini. Kamati inashauri kwamba ni vyema Serikali ikaendelea kugawanya rasilimali fedha kwenye maeneo mengine ya miundombinu ya reli ili kuhakikisha huduma ya reli inatolewa bila changamoto hasa katika reli ya kati ambapo mizigo bado inasafirishwa kupitia reli hiyo. Jedwali Na. 7 hapo chini linaonesha mwenendo wa makusanyo ya Mfuko wa Reli.

**Jedwali Na 7: Mwenendo wa makusanyo na fedha zilizotolewa kwa Mfuko wa Reli**

| **Mwaka wa Fedha** | **Bajeti 2020/21** | **Fedha zilizotolewa 2020/21** | **Asilimia %** |
|---|---|---|---|
| Jumla ya Fedha | 289,678,923,000 | 249,721,849,202.79 | 86.21 |
| Mwaka wa Fedha | 2021/22 | 2021/22 (Hadi Machi) | Asilimia % |
| **Jumla ya Fedha** | **294,801,622,000.00** | **252,409,967,180.00** | **85.62.** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya TRC*

**25.0.**Mfuko wa REA

**Mheshimiwa Spika,** Vyanzo vikuu vya mapato ya Mfuko wa Nishati Vijijini ni tozo ya mafuta, tozo ya umeme (*electricity fees*) pamoja na misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2021/22, Mfuko wa Nishati Vijini (REF) uliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 414.27** kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umeme na usambazaji wa umeme vijijini. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **shilingi bilioni 363.11** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 51.16** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Aprili 2022, Serikali ilikusanya jumla ya **shilingi bilioni 407.045** sawa na **asilimia 98.3** ya bajeti ya Mfuko kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mfuko. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **shilingi bilioni 253.552** kinatokana na makusanyo ya tozo ya mafuta na umeme (*electricity fees*) na kiasi cha **shilingi bilioni 153.492** ni fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zinazopelekwa moja kwa moja katika miradi (Direct Project Fund).

**Mheshimiwa Spika,** Hadi mwezi Aprili 2022 mfuko wa REA ulikuwa na jumla ya **Shilingi trilioni 1.24** hata hivyo miradi haikutekelezwa kutokana na changamoto mbalimbali kama vile kupanda kwa bei za vifaa na mikataba isiyoruhusu mabadiliko ya bei pamoja na usimamizi usioridhisha. Kamati imebaini kwamba tozo ya mafuta ndio chanzo pekee cha uhakika kwa ajili ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya umeme vijijini. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inasimamia vizuri mikataba ya utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini kwa sababu ndio chanzo kikuu cha ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi. Kamati inaamini masuala hayo yakifanyiwa kazi miradi itatekelezwa kwa haraka na kwa ufanisi.

**Jedwali Na.8 linaonesha utekelezaji wa bajeti ya Mfuko wa Nishati Vijijini (REF) kwa mwaka wa fedha 2021/22**

| Na | CHANZO | BAJETI 2021/22 | FEDHA ILIYOTOLEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Tozo ya Mafuta | 363,108,000,000 | 253,552,628,561 | 69.8 |
| 2. | Tozo ya Umeme | 51,164,100,000 | 153,492,854,609 | 300 |
| **3.** | **JUMLA** | **414,272,100,000** | **407,045,483,170** | **98.3** |

***Chanzo**: Wizara ya Nishati*

## 25.1.MAPITIO YA UTENDAJI KAZI WA BAADHI YA MASHIRIKA YA UMMA PAMOJA NA UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA MASHIRIKA YA UMMA.

### 25.1.1. Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba shirika halitekelezi ipasavyo Mikataba ya Ugawanaji Mapato *(Production Sharing Agreements, PSA)* hasa ya kuchangia

gharama za uwekezaji ili inufaike na mapato. Kutokana na hali hiyo shirika hilo limekuwa likinufaika na ada na tozo mbalimbali na faida kubwa kuchukuliwa na wawekezaji. Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kubadilisha Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi ya Mwaka 2015, ili kuruhusu TPDC kutumia sehemu ya mapato yanayotokana na shughuli za utafutaji na uzalishaji wa gesi kutumika katika uwekezaji. Vilevile, Kamati ilibaini kwamba TPDC haina vituo vya kutosha vya kusambaza mafuta, hivyo Kamati inaishauri Serikali kuiruhusu TPDC kuingia ubia na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikali (GPSA) ili kutumia vituo vyao kwa mpito wakati TPDC ikiendelea na mchakato wa kujenga vituo vyake.

**25.1.2. Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA).**

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini [GPSA] ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala Na. 30 ya mwaka 1997. Kuanzishwa kwa GPSA ni matokeo ya Program za uboreshaji wa utendaji katika sekta ya umma (Public Service Reforms Program-PSRP) ambapo katika maboresho hayo iliyokuwa Bohari kuu ya Serikali ilifutwa na baadhi ya majukumu pamoja na miundombinu yake vilichukuliwa na GPSA.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya kikao na Wakala na kubaini changamoto zinazoikumba taasisi hii, hivyo Kamati inatoa ushauri ufuatao;

i. Serikali iunganishe GPSA na watengenezaji pamoja na wasambazaji wa magari ili wakala huyo aweze kununua magari na mitambo moja kwa moja

kutoka kwa wazalishaji kwa bei nafuu tofauti na hivi sasa ambapo analazimika kupitia kwa wakala mwingine;

ii. Serikali kusimika mitambo ya kujaza gesi ya (Compressed Natural Gas - CNG) kwenye vituo vya GPSA kwaajili ya matumizi ya magari ya Serikali katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza ili kupunguza gharama za matumizi ya mafuta kwa magari ya Serikali;

iii. Kupitia upya sheria ya TASAC ili kuhakikisha kazi ya ugomboaji wa mizigo bandarini na mipakani inafanywa GPSA tofauti na ilivyo hivi sasa ambapo kazi hiyo inafanywa na GPSA pamoja na TASAC; na

iv. Serikali kuweka utaratibu utakao rahisisha misamaha ya kodi kwa mizigo inayohitaji misamaha ili mizigo hiyo isikae muda mrefu bandarini.

**25.1.3. Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA)**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Ununuzi Sura ya 410 imeipa PPRA Mamlaka ya Kuanzisha, Kusimamia na kuendesha Mfumo wa Ununuzi kwa njia ya Mtandao (e-Procurement, e-Submission na e-Signature). Kamati imebaini kwamba Mfumo wa Ununuzi wa Umma kwa njia ya Mtandao (TANePS) unatumia lugha moja ya Kingereza na hivyo kuwa ngumu kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine kutumia mfumo huo. Hivyo ni wazi kwamba mfumo huu unakiuka moja ya nguzo Tano za ununuzi wa Umma ambayo ni kuwezesha makampuni ya ndani kushiriki zabuni za Serikali. Aidha, matumizi ya lugha ya kingereza pekee yanakiuka nguzo ya haki, usawa pamoja na fursa kwa wote. Kwa msingi huo Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba mfumo huu

unatumia lugha zote kubwa duniani kama vile, Kiswahili, Kifaransa, Kichina na Kireno. Na kwa kuwa, mfumo wa TANePS haukujengwa na watanzania, Kamati inaishauri Serikali ianze mchakato wa kujenga mfumo kwa kutumia wataalam wa ndani.

## 26.0.MATOKEO YA MASHAURIANO BAINA YA SERIKALI, KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI NA KAMATI YA UONGOZI.

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 124(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Juni, 2020 inaelekeza kwamba, baada ya Bunge kukamilisha mjadala wa Makadirio ya Wizara zote, ndani ya siku sita kabla ya hotuba ya Bajeti kusomwa Bungeni, Serikali kwa kushauriana na Kamati ya Bajeti itafanya majumuisho kwa ajili ya kuzingatia hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha unaoendelea, na Makadirio ya Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha unaofuata.

### 26.1.Hoja zilizojadiliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti ilikutana na Serikali kwa kipindi cha siku 6 kuanzia tarehe 8 hadi tarehe 13 ili kushauriana kuhusu hoja 12 zilizojitokeza katika Wizara mbalimbali wakati wa majadiliano ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2021/22 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2022/23. Hoja hizo zilihusu maeneo yafuatayo:-

i. Kuongeza fedha kwa ajili ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ujenzi wa mifumo na ununuzi wa magari kutokana na kuongezeka kwa mawanda ya ukaguzi;

ii. Kuangalia uwezekano wa kutoza kwa kiwango cha asilimia sifuri Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mafuta yaliyochujwa walau mara mbili “Double refined” yanayotokana na mbegu za pamba, mchikichi na alizeti yanayozalishwa ndani ili yaweze kushindana katika soko;

iii. Kupunguza mlundikano wa mapingamizi ya kodi yaliyoko kwenye Bodi ya Rufaa za Kodi, Mahakama ya Rufaa ya Mapato ya Kodi na Mahakama ya Rufaa ambayo hadi tarehe 31 Disemba, 2021 kulikuwa na kesi zenye **Thamani ya Shilingi Trilioni 5.184**;

iv. Kufanya mabadiliko katika Sheria ya Ukaguzi wa Umma ili kuleta tija kwenye kitengo cha ukaguzi wa ndani kwa kutatua changamoto zinazosababishwa na sheria hiyo ilivyo hivi sasa;

v. Changamoto ya upatikanaji wa Ofisi za Wabunge majimboni;

vi. Utatuzi wa Changamoto za utekelezaji wa Miradi ya Umeme Vijijini (REA) kutokana na kukosekana kwa vifaa kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi; na

vii. Kupanda bei kwa vifaa vya umeme tofauti na bei ambazo zilikuwa kwenye mikataba na hivyo kusababisha wakandarasi kushindwa kutekeleza Miradi.

viii. Serikali kuangalia uwezekano wa kuwalipa posho waheshimiwa Madiwani pamoja na Wenyeviti wa Mitaa na vijiji;

ix. Kutenga Bajeti kwa ajili ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya maendeleo;

x. Kuongeza fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara;

xi. Kutofanya mabadiliko ya viwango vya bei za bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa ili kuwe na bei himilivu; na

xii. Kuangalia uwezekano wa kuongeza maeneo yanayozunguka Bunge ili kuimarisha ulinzi na Usalama wa Bunge.

**26.2.Maamuzi Baada ya Mashauriano**

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya mashauriano Kamati ilikubaliana na majibu ya Serikali kwa Hoja 6 na Hoja 5 zilihitaji ufafanuzi wa ziada. Baadhi ya hoja hizo zimefanyiwa kazi kupitia hotuba ya Bajeti ya Serikali iliyowasilishwa tarehe 14 Juni, 2022. Aidha, hoja hizo ambazo zilihitaji ufafanuzi wa ziada Mhe. Spika aliagiza kwamba zifanyiwe kazi na mrejesho kuwasilishwa kwa Kamati katika muda tofauti tofauti. Vilevile, kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya umeme vijiji Serikali iliagizwa kuleta mrejesho Bungeni kabla ya kupigia kura Bajeti kuu ya Serikali tarehe 24 Juni, 2022.

**27.0.SURA YA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali imepanga kukusanya na kutumia jumla ya **shilingi trilioni 41.48** ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 8.1** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2021/22 ya **shilingi**

**trilioni 37.99**. Kati ya fedha hizo, **shilingi trilioni 26.54** zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni **asilimia 63.8** ya bajeti yote na **shilingi trilioni 15.0** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo sawa na **asilimia 36.2** ya bajeti. Aidha, bajeti ya maendeleo inajumuisha **shilingi trilioni 12.31** fedha za ndani na **shilingi trilioni 2.70** fedha za nje.

**27.1.Sera za Mapato**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inakusudia kukusanya kiasi cha **shilingi trilioni 28.01**. Kati ya fedha hizo, Mamlaka ya Mapato Tanzania inakadiriwa kukusanya **shilingi trilioni 24.19** sawa na ongezeko la **asilimia 11.1** ikilinganishwa na makadirio ya **shilingi trilioni 21.78** mwaka 2021/22. Mapato yasiyo ya kodi yanakadiriwa kuwa **shilingi trilioni 3.49 mwaka 2022/23** sawa na ongezeko la **asilimia 14.53** ukilinganisha na **shilingi trilioni 3.04**; Mapato ya Halmashauri **shilingi trilioni 1.01** sawa na ongezeko la **asilimia 17.18** ukilinganisha na **shilingi bilioni 863.06** mwaka 2021/22.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, Serikali inategemea kupokea kiasi cha **shilingi trilioni 4.15** sawa na ongezeko la **asilimia 40.56** ikilinganishwa na **shilingi trilioni 2.95**. Aidha, Serikali inatarajia kukopa **shilingi trilioni 5.35** kutoka soko la ndani ambapo **shilingi trilioni 3.30** ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva na kiasi cha **shilingi trilioni 2.05** kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Vilevile, Serikali inatarajia kukopa **shilingi trilioni 2.86** kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara Ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya miundombinu. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuendelea kufanya mazungumzo na Washirika wa

Maendeleo na kuwashawishi ili kuendelea na utaratibu wa awali wa GBS. Aidha, Serikali iendelee kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuondokana kabisa na utegemezi wa kibajeti hasa kipindi hiki ambapo hali ya uchumi ya Nchi za wahisani zimetetereka kutokana na ugonjwa wa Uviko – 19 pamoja na vita ya Urusi na Ukraine na hivyo kuwepo na uwezekano mkubwa wa nchi hizo wahisani kushindwa kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mikopo ya ndani na nje, mwaka 2022/23 Serikali imepanga kukopa katika soko la ndani kiasi cha **shilingi trilioni 2.05** sawa na ongezeko la **asilimia 11.72** ikilinganiswa na **shilingi trilioni 1.84** mwaka 2021/22**.** Kamati inaishauri Serikali kupunguza kukopa zaidi kwenye soko la ndani ili isisababishe kukosekana kwa mikopo kwa sekta binafsi. Na badala yake inashauriwa kuangalia vyanzo vya mikopo ya nje yenye masharti nafuu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**27.2.Sera za Matumizi**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali imepanga kutumia kiasi cha **shilingi trilioni 41.06** sawa na ongezeko la **asilimia 8.1** ukilinganisha na **shilingi trilioni 37.99** mwaka 2021/22 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Takwimu zinaonesha kuwa mapato ya ndani yanazidi matumizi ya kawaida kwa kiasi cha **shilingi trilioni 3.03.** Hii maana yake ni kwamba mapato yote ya ndani yanaweza kugharamia matumizi ya kawaida peke yake na **asilimia 8.3** tu ya miradi yote ya maendeleo. Kufuatia uchambuzi huu Kamati inaishauri Serikali kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani ili walau yawe na uwezo wa kugharamia miradi ya maendeleo angalau kwa asilimia 40.

**Jedwali Na 9: Ulinganisho wa Sura ya Bajeti ya Serikali kati ya Mwaka 2021/22 na 2022/23**

| NA. | | 2021/22 | 2022/23 | TOFAUTI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| | MAPATO | B1 | B2 | B2-B1 | (B2-B1)/B1*100 |
| 1. | Mapato ya Ndani | 24,827,843 | 27,685,782 | 2,857,939 | 11.51 |
| | Mapato ya Kodi (TRA) | 21,778,103 | 24,192,732 | 2,414,629 | 11.09 |
| | Mapato yasiyo ya Kodi (TRA) | 3,049,774 | 3,493,050 | 443,276 | 14.53 |
| 2. | Mapato ya Halmashauri | 863,858 | 1,012,286 | 148,428 | 17.18 |
| 3. | Mikopo/Misaada kutoka Nje | 2,955,923 | 4,154,921 | 1,198,998 | 40.56 |
| | Mikopo ya Masharti Nafuu - GBS | 1,310,650 | 1,240,038 | -70,612 | -5.39 |
| | Misaada na Mikopo ya Miradi | 2,673,617 | 2,792,760 | 119,143 | 4.46 |
| | Misaada na Mikopo ya Kisekta | 270,359 | 122,123 | -148,236 | -54.83 |
| 4. | Mikopo ya Ndani na Nje | 8,034,240 | 8,210,927 | 176,687 | 2.19 |
| | Mikopo ya Nje | 3,045,107 | 2,856,602 | -188,505 | -6.19 |
| | Mikopo ya Ndani | 1,838,796 | 2,054,325 | 215,529 | 11.72 |
| | Mikopo ya Ndani - Rollover | 3,150,337 | 3,300,000 | 149663 | 4.75 |
| | JUMLA YA MAPATO YOTE | 37,980,601 | 41,063,915 | 3,083,314 | 8.1 |
| | MATUMIZI | B1 | B2 | B2-B1 | |
| 5. | Matumizi ya Kawaida | 23,002,951 | 25,542,574 | 2,539,623 | 11.03 |
| | Mfuko Mkuu wa Serikali | 10,699,563 | 11,308,365 | 608,802 | 5.69 |
| | Mishahara | 8,150,509 | 9,740,753 | 1,590,244 | 19.51 |
| | Matumizi Mengineyo (OC) | 4,152,880 | 4,493,456 | 340,576 | 8.20 |
| 6. | Matumizi ya Maendeleo | 14,977,615 | 15,521,341 | 543,726 | 3.63 |
| | Fedha za Ndani | 12,033,639 | 12,122,106 | 88,467 | 0.74 |
| | Fedha za Nje | 2,943,976 | 3,399,236 | 455,260 | 15.46 |
| | JUMLA YA | 37,980,601 | 41,063,915 | 3,083,314 | 8.11 |

| NA. | | 2021/22 | 2022/23 | TOFAUTI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| | MATUMIZI YOTE | | | | |
| | NAKISI YA BAJETI (% OF GDP) | 3.0% | 3.0% | | |

***Chanzo:*** *Wizara ya Fedha na Mipango*

## 28.0.HATUA ZA KIKODI ZINAZOPENDEKEZWA NA SERIKALI KWA MWAKA FEDHA 2022/23.

**Mheshimiwa Spika**, nianze kwa kutoa pongezi kwa Serikali ambayo kwa kiasi kikubwa imechukua na kuzingatia mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Bajeti. Hatua hii inaonyesha utayari wa Serikali kupokea mapendekezo na kuyafanyia kazi, chini ya uongozi bora wa Rais Wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Kamati imefanya uchambuzi wa hatua hizo na kubaini kwamba mabadiliko yaliyofanyika yanalenga maeneo yafuatayo:-

### 28.1.Maeneo yaliyoguswa na Mabadiliko mbalimbali ya Kodi

i. Kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato kwa kuanzisha vyanzo vipya vya mapato;

ii. Kurahisisha ufanyaji biashara na uwekezaji nchini ikiwa ni pamoja na kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini;

iii. Kuchochea uzalishaji katika sekta ya kilimo pamoja na kulinda viwanda vya ndani;

iv. Kupunguza makali ya upandaji wa bei za bidhaa mbalimbali kwa wananchi kama vile mafuta ya kula na ya petroli;

v. Kutengeneza mazingira mazuri ya kufanyia biashara pamoja na kuwawezesha kimtaji Wafanya biashara wadogo maarufu kama Wamachinga; na

vi. Kuchochea uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zinazozalishwa nchini.

**28.2.Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu hatua mbalimbali za kikodi**

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kwamba kamati ya Bajeti itapata fursa ya kutoa maoni na mapendekezo yake kupitia muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2022, naomba uniruhusu kwa uchache nitoe maoni kuhusiana na hatua zilizopendekezwa.

**28.2.1. Mabadiliko yaliyofanyika katika Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Afrika Mashariki**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mara ya kwanza katika Historia ya Kamati ya Bajeti ilipata fursa ya kupitishwa kwenye mapendekezo ya mabadiliko ya sheria hii na kamati ilitoa maoni yake. Hata hivyo utaratibu huu haupo kikanuni wala kisheria hivyo ni muhimu kwa Bunge kuhakikisha kwamba tunafanya mabadiliko katika sheria ya Bajeti kifungu cha 9 (1) ili kuongeza jukumu kwa Kamati ya Bajeti kupitia, kuchambua na kutoa maoni juu ya Mabadiliko ya Sheria ya Ushuru wa Forodha, kwa sababu mabadiliko hayo huidhinishwa na Bunge la Afrika Mashariki. Na endapo Bunge hili halitaridhia mabadiliko

hayo ni lazima yarejeshwe katika Bunge la Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika,** naomba nimpongeze Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba Waziri wa Fedha na Mipango kwa kusikiliza vyema maoni na mapendekezo ya Kamati na kuyafanyia kazi. Uchambuzi wa kina wa kila hatua ya kikodi iliyowasilishwa na Serikali utafanyika wakati wa kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2022 na Maoni ya Kamati yatawasilishwa Bungeni.

## 29.0.MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2022/23

### 29.1.Uanzishwaji wa Ofisi ya Msuluhishi wa Masuala ya Kodi (*"Tax Ombudsman"*)

**Mheshimiwa Spika,** Mwaka 2019 Serikali ilifanya mabadiliko katika Sehemu ya 3(A) ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 438 kwa kuongeza vifungu vipya vya 28A hadi 28G ambavyo vilianzisha Ofisi ya Mpokea Malalamiko ya Kodi. Aidha, Kamati inatambua kwamba kupitia Tangazo la Serikali Na. 106 la tarehe 4 Machi, 2022 zilitangazwa Kanuni zenye lengo la kubainisha sifa za Mtendaji Mkuu wa Ofisi hiyo, majukumu yake, utendaji kazi wa Ofisi na namna ya kushughulikia malalamiko ya kodi. Pamoja na kanuni hizo kukamilika na kutangazwa hadi hivi sasa Ofisi hiyo haijaanzishwa. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha uanzishwaji wa Ofisi hiyo ambayo ni muhimu sana katika usuluhishi wa migogoro ya kodi, kama ilivyoahidi Ofisi hiyo itaanza kazi Julai, 2022.

### 29.2.Ujenzi wa Barabara kwa kutumia Mfumo wa EPC+F (Engineering Procurement Construction and Financing).

**Mheshimiwa Spika**, wakati Waziri wa Fedha na Mipango akiwasilisha Bajeti ya Serikali Bungeni alilitaarifu Bunge kwamba baadhi ya barabara katika mwaka ujao wa Fedha zitatumia mfumo wa Usanifu, utangazaji wa Zabuni, Kujenga na Kutafuta Fedha za ujenzi *(Engineering Procurement Construction and Finance)*. Mfumo huu una faida mbalimbali kama vile vihatarishi vyote vya mradi vinakuwa chini ya kampuni iliyofanya kazi kwenye hatua zote za usanifu, zabuni, ujenzi na utafutaji wa fedha na pili ni kuirahisishia Serikali utafutaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya barabara. Hata hivyo, mfumo huu unafaida kubwa pale ambapo barabara zinazojengwa ama zinalipiwa yaani (road toll) au zinazalisha mapato makubwa ya moja kwa moja. Vinginevyo mfumo huu ni aghali sana kwa sababu Serikali itabaki na jukumu la kulipa Mkopo uliochukuliwa na kampuni husika kwa ajili ya ujenzi na utalipwa pamoja na riba hivyo una athari ya moja kwa moja na Deni la Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaamini kwamba ni miaka 10 hadi hivi sasa hatuna mradi hata mmoja wa PPP hivyo itakuwa ni vigumu kwa EPC+F kuwa na manufaa kwa muda mfupi. Endapo tutaharakisha ujenzi wa barabara kwa EPC+F bila kufanya tathmini ya kina ya mapato yetu na Deni la Serikali ni wazi kwamba kutakuwa na athari kubwa sana kwenye mapato yetu ya ndani.

### 29.3.Utekelezaji wa Miradi ya Umeme Vijiji kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (Rural Electrification Agency - REA).

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ina jumla ya **vijiji 12,318** Hadi kufikia Mwezi Aprili 2022 vijiji vilivyokuwa vimeunganishwa na Umeme ni **vijiji 8,688** sawa na asilimia **asilimia 70.53** ya vijiji vyote nchini. Hivyo ni wazi kwamba ili tuweze kufikia

lengo la kuviunganisha vijiji vilivyobaki 3,630 kwa kipindi cha miaka mitatu iliyosalia ni lazima kuunganisha wastani wa vijiji visivyopungua 443 kila mwaka. Hivyo ni wazi kwamba kwa kasi hii ya utekelezaji wa sasa ni vigumu kufikia malengo ya Mpango ya kukamilisha vijiji vyote vilivyosalia.

**Mheshimiwa Spika,** tofauti ya miradi ya REA na mingine ni kwamba mradi huu hauna changamoto ya fedha ambapo hadi kufikia mwezi Aprili 2022 akaunti ya REA ilikuwa na **shilingi trilioni 1.24** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Changamoto zilizopo ni uwepo wa wakandarasi wasio na uwezo, usimamizi usioridhisha wa miradi, kupanda kwa bei za vifaa na muda mrefu wa maandalizi ya utekelezaji ambao unachukua zaidi ya miezi 6 ya mwaka wa fedha. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwanza inaimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa miradi, pili ni kutafuta wakandarasi wenye uwezo na tatu ni kuangalia uwezekano wa kubadili aina ya mikataba ya utekelezaji wa umeme vijijini ili upandaji wa bei usiwe kikwazo katika utekelezaji wa miradi hii. Hatua hizi zitasaidia kufikia lengo tulilojiwekea la kukamilisha vijiji vyote ifikapo mwaka 2025.

**29.4.Ukusanyaji wa Kodi ya Majengo**

**Mheshimiwa Spika,** ukusanyaji wa kodi ya majengo umepitia mabadiliko mbalimbali. Kwanza, kodi hii ilihamishwa kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa na kupelekwa TRA. Pili, vikaanzishwa viwango mfuto (flat rate) ili kurahisisha ulipaji. Tatu, kodi hii ilianza kulipwa kupitia njia ya luku pamoja na kubadili jina la Sheria inayosimamia kodi hiyo kutoka The Urban Authorities (Rating) Act, Cap 289 R.E 2019 kwenda kwenye Local Government Authorities (Rating) Act, Cap 289 R.E 2019, ili

kujumuisha maeneo mengine ambayo sio miji yaanze kutozwa kodi hii. Mabadiliko yote haya hayajaweza kuongeza mapato kwa kiwango kikubwa kama ilivyotarajiwa au ukilinganisha na Fedha zilizokuwa zikikusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika,** Mwaka 2015/16 wakati Serikali inahamisha Kodi ya majengo kutoka Serikali za Mitaa; zilikuwa na uwezo wa kukusanya zaidi ya **Shilingi bilioni 64** kwa mwaka. Kiasi hiki hakijafikiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa Miaka yote sita ambayo imepewa kukusanya Kodi hii. Katika kipindi cha miaka mitatu Mamlaka ya Mapato Tanzania imeweza kukusanya kiasi cha **Shilingi bilioni 44.769** katika kipindi cha miaka mitatu. Ufanisi huu hautokani na udhaifu wa Mamlaka ya Mapato kukusanya mapato ila unatokana na kutofanyika kwa uthamini wa majengo ili yatozwe kodi hiyo kulingana na thamani yake badala ya kutumia viwango mfuto. Kiasi cha fedha kilichokusanywa na Mamlaka ya Mapato kwa miaka mitatu kinaweza kukusanywa katika Wilaya 3 tu za Mkoa wa Dar es salaam endapo uthamini utafanyika. Kamati inaushauri yafuataο kwa Serikali ili kuongeza mapato ya kodi yatokanayo na Kodi ya majengo:-

i. Kufanya uthamini wa majengo kupitia wanafunzi wa Chuo cha Ardhi kipindi wanapokuwa katika mazoezi kwa vitendo na majengo yatakayofanyiwa uthamini yaondolewe kwenye mfumo wa viwango mfuto;

ii. Kuangalia uwezekano wa kushirikiana na Serikali za Mitaa katika kufanya uhakiki wa majengo kwa kutumia Luku ili kutambua nyumba pamoja na thamani yake; na

iii. Mita namba za Luku zitumike kama namba ya mlipa kodi wa jengo yaani *TIN number* na mfumo wa luku uendelee kutumika kwa kukusanyia kodi hii kama ilivyo hivi sasa.

**Mheshimiwa Spika,** endapo uthamini utafanyika chanzo hiki kwa mwaka kina uwezo wa kuiongezea Serikali mapato ya kodi kati ya **shilingi billioni 100 hadi 200**.

**29.5.Uboreshaji na Uendelezaji wa Mifumo ya kukusanyia Kodi chini ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)**

**Mheshimiwa Spika**, Ulimwengu tulionao hivi sasa ni ulimwengu wa Tehama ambao umerahisisha masuala mengi sana ikiwemo ulipaji na ukadiriaji wa Kodi. Kamati imefanya uchambuzi wa mifumo mbalimbali ya Mamlaka ya Mapato kama Vile TANCIS, ITAX na E-FILLING na kubaini kwamba mifumo hii inahitaji kuhuishwa ili isomane na iendane na wakati wa sasa. Hivyo, tathmini ya awali inaonyesha kwamba Mamlaka ya Mapato inahitaji **shilingi bilioni 560** ili kuboresha mifumo pamoja na kujenga mifumo mipya kama IDRAS. Mifumo hii ina manufaa yafuatayo; kwanza ni kuondoa rushwa kwa kupunguza muingiliano baina ya mlipa kodi na Afisa wa Mamlaka, Pili ni kupunguza mapingamizi ya kodi yanayotokana na ukadiriaji (Assessment) na mwisho ni kurahisisha ulipaji wa kodi. Kamati inaishauri Serikali kukopa au kutenga Bajeti kwa Mamlaka ili iweze kuhuisha, kujenga na kuiendeleza mifumo yake ili iendane na wakati.

**29.6.Kupanua wigo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali (Widening Tax Base)**.

**Mheshimiwa Spika,** Kodi zipo za aina mbili kodi za moja kwa moja “Direct taxes” na kodi zisizo za moja kwa Moja “Indirect taxes”. Ni vigumu sana kukwepa kodi zisizo za moja kwa moja kwa sababu mara nyingi kodi hizi zipo kwenye matumizi ya huduma na bidhaa mbalimbali na ili uzikwepe ni lazima uamue kuacha kutumia bidhaa au huduma husika. Kodi ambayo ni rahisi kukwepa kwa mazingira yetu ya Tanzania ni kodi za moja kwa moja ambazo zinazotokana na mapato. Mfano kuna wamiliki wengi wa nyumba za kupangisha na hakuna kodi yoyote ya mapato wanayolipa. Hali hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na ukubwa wa sekta isiyo rasmi nchini ambayo inakadiriwa kuwa **asilimia 75** ya biashara zote nchini. Kamati inaishauri Serikali kwamba ifanye pilot project kwa kuweka Maafisa Kodi katika kata zenye shughuli nyingi za kiuchumi ili kuweza kutambua na kusajili biashara na walipa kodi wapya na pia zoezi hili litakuwa kwa nchi nzima, hatua hii itakuwa na mafanikio makubwa sana katika kupanua wigo wa kodi. Mfano mzuri ni wanafunzi wa Chuo cha Kodi waliofanikiwa kuwaandikisha walipa kodi wapya 20,000 katika Wilaya ya Ilala pekee mwaka huu.

**29.7.Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania *(Blue Print for Regulatory Reforms to Improve Bussiness Enviroment)***

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kutambua hatua nzuri zilizochukuliwa na Serikali ni dhahiri kwamba Taifa letu bado linakabiliwa na mazingira yasiyoridhisha ya Biashara na uwekezaji. Ripoti ya Dunia ya Ufanyaji Biashara (World Doing Business Report) inayoandaliwa na UNCTAD imetuweka katika Nafasi ya 141 kati ya nchi 190 Duniani kwa mazingira bora ya Biashara. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa BLUEPRINT ili nchi yetu

iwe kati ya nchi 100 zenye mazingira bora ya kufanya biashara duniani ifikapo mwaka 2025 kama lilivyo lengo la Mpango wa Taifa.

**29.8.Kuandaa Sera ya Taifa ya Ufuatiliaji na Tathmini na Baadaye kutunga Sheria yake.**

**Mheshimiwa Spika,** Ufanyaji wa Ufuatiliaji na Tathmini ni zoezi la kitaalamu ambalo lina malengo makuu matatu moja ni kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa, mbili ni kuhakikisha kunakuwa na thamani ya fedha na Tatu ni kurekebisha mapungufu wakati wa utekelezaji wa mradi au shughuli yoyote. Kwa miaka mitatu mfululizo Kamati imekuwa ikishauri Serikali kuandaa Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini ili baadaye itungiwe sheria. Kutokufanya hivyo kumeacha ombwe katika ufuatiliaji na Tathmini na badala yake Serikali imekuwa ikiziba ombwe hilo kwa kuandaa miongozo kwaajili ya ufuatiliaji na Tathmini. Sababu za Msingi za Kuomba uwepo wa Sera na Sheria ni kuhakikisha kwamba majukumu ya kila mmoja yanabainishwa na adhabu zake. Hatua hii itaondoa changamoto zilizopo katika utekelezaji wa miradi.

**29.9.Upimaji, Uendelezaji na Umilikishaji wa Ardhi;**

**Mheshimiwa Spika,** upimaji na uendelezaji wa ardhi ni jambo la muhimu sana katika kuleta maendeleo endelevu. Aidha, kutopima na kumilikisha ardhi kunanyima wananchi wa vijijini fursa ya kutumia ardhi yao kwaajili ya kujiendeleza kiuchumi. Kamati inaishauri Serikali kutafuta fedha ili kupima, kuendeleza na kumilikisha ardhi kwa sababu mapato yanayotokana na ardhi hayachukui muda mrefu kuonekana.

## 29.10. Utekelezaji wa Majukumu ya Bodi ya Kusimamia Ajira kwenye Sekta Binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 12 Aprili, 2022 jijini Dodoma ilizinduliwa Bodi ya Mishahara kwa Sekta Binafsi na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Prof. Joyce Ndalichako. Moja ya jambo alilosisitiza kwa Bodi hiyo ni kufanya Utafiti wa mishahara kwa Sekta Binafsi na kutoa mapendekezo ya Kima cha Chini cha Mishahara kwa Sekta Binafsi. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba kazi ya utafiti inakamilika mapema iwezekanavyo ili Serikali iweze kutangaza kima cha chini cha mishahara kwa sekta binafsi kwa kuzingatia hali ya sasa ya uchumi.

## 29.11. Kipidi maalum cha Msamaha wa Kodi, ada tozo na riba kwa Makampuni ya Utalii (Tax Amnesty in Tourism Sector)

**Mheshimiwa Spika,** Sote tunafahamu kwamba moja ya Sekta ambayo iliathirika kwa kiasi kikubwa na Janga la Uviko 19 ni Sekta ya Utalii. Idadi ya Watalii ilipungua kutoka **watalii 1,527,230** mwaka 2019 hadi **watalii 620,867** mwaka 2020 sawa na kupungua kwa **asilimia 59.3**. Hata hivyo, pamoja na anguko hilo makampuni mengi yanayojishughulisha na utalii ama yalilazimika kupunguza wafanyakazi au kusimamisha biashara zao kutokana na anguko la biashara hiyo. Kutokana na hali hiyo kuna baadhi ya makampuni ambayo yanadaiwa kodi, riba, ada na tozo mbalimbali ambazo yalishindwa kulipa kutokana na anguko la biashara. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kutoa msamaha wa Kodi "*Tax Amnesty*" kwa kipindi maalum hasa kwa kodi, riba, ada na tozo ambazo zilitakiwa zilipwe kati ya mwaka 2019 na 2020.

## 29.12. Matumizi ya Rasilimali za Ndani kwa ajili ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Taarifa ya Benki ya Dunia iitwayo *Reinvigorating Growth in Resource-Rich Sub-Saharan Africa* ya mwaka 2018 inaonyesha kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi 10 Afrika zenye rasilimali nyingi. Hata hivyo, uwepo wa rasilimali si kigezo pekee cha kuwa na maendeleo. Ili maendeleo yapatikane ni lazima rasilimali hizo zitumike kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Kuendelea kuwa na rasilimali ambazo hazitumiki hakulihakikishii Taifa maendeleo. Hivyo ni muhimu sana kama Taifa kufanya mabadiliko katika matumizi ya rasimali tulizonazo.

**Mheshimiwa Spika,** Nchi nyingi hivi sasa zinahama katika matumizi ya nishati zinazozalisha hewa ukaa na kwenda kwa nishati jadidifu. Hivyo kuna baadhi ya rasilimali tusipozitumia hivi sasa huko mbeleni zinaweza zisiwe na thamani, mfano makaa ya mawe. Ni vyema sasa Serikali ihakikishe rasilimali hizi zinavunwa kwa uangalifu na kwa maslahi mapana ya taifa. Kamati inashauri magari ya Serikali yawe na mfumo wa kutumia gesi asilia kama ilivyo kwa malori ya kampuni ya Dangote. Hatua hii sio kwamba itapunguza uagizaji wa mafuta kutoka nje vilevile itapunguza nakisi ya urari wa jumla wa malipo na biashara.

## 29.13. Utekelezaji wa Miradi kwa Njia ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (Public Private Partnership).

**Mheshimiwa Spika,** Katika Hotuba ya Bajeti ya Hali ya Uchumi, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alilieleza Bunge kwamba katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo

wa Mwaka 2022/23 utaratibu wa ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi utatumika katika kutekeleza miradi. Pamoja na kwamba utaratibu huu una manufaa makubwa sana kwa Taifa ni miaka zaidi ya 12 sasa tangu ilipotungwa Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2010 pamoja na Mabadiliko yake ya mwaka 2018. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini changamoto zinazosababisha kutokuwepo na miradi PPP changamoto hizo ni:-

i. Kiwango cha chini cha mtaji unaotambulika kisheria kwa ajili ya Miradi ya PPP ni dola za marekani milioni 20 sawa na Shilingi za Kitanzania bilioni 40;

ii. Muamko mdogo wa Wizara, Idara na Taasisi za umma kutekeleza miradi kwa njia ya ubia;

iii. Mazingira mabovu ya uwekezaji ambayo hayavutii uwekezaji kwenye miradi ya aina hii;

iv. Ugumu uliopo kisheria wa kutekeleza miradi kwa njia hii hasa ile miradi ambayo inaibuliwa na Sekta binafsi (Unsolicited proposal) na inayopendekezwa ifanyike kwa ubia na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inatanzua vikwazo vilivyobainishwa ili lengo la utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia lifanikiwe.

**29.14. Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kutoshirikiana wakati wa Utekelezaji wa Miradi**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika uchambuzi wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo imebaini kwamba baadhi ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali hazifanyi kazi

kwa kushirikiana. Mfano Mradi wa Umeme vijijini unatekelezwa na Wakala wa Umeme vijiji lakini jambo la kushangaza ni pale ambapo tathmini ya maeneo yanayohitaji kuunganishiwa umeme inafanyika na taasisi za Umma kama vile mashule, Hospital na Zahanati hazijumuishwi. Eneo jingine ni pale ambapo Halmashauri inapanga kujenga Hospital ya Wilaya lakini Wakala wa barabara Vijijini (TARURA), TANESCO na Mamlaka ya Maji ya eneo husika kutokuwa na mpango wala bajeti iliyotengwa kwaajili ya kupelekea Huduma hizo muhimu katika hospital. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba pale ambapo kuna miradi ya umma ni vyema Taasisi zote zikashirikiana ili kupunguza gharama za mradi na kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati.

**29.15. Kufanya Marejeo ya Mikataba ya Kikodi ya Kimataifa Baina ya Serikali na Mataifa mengine (Double Taxation Agreement).**

**Mheshimiwa Spika,** Mikataba ya makubaliano ya kodi baina ya nchi mbili ina malengo makuu mawili;-

i. Kuondoa uwezekano wa mapato ya mtu mmoja kukatwa kodi mara mbili kwenye shughuli moja ya kiuchumi; na

ii. Kuondoa uwezekano wa biashara moja kutozwa kodi ya aina moja katika nchi mbili.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na changamoto hizo nchi hukubaliana nani atatoza kodi ipi kwenye shughuli gani. Tanzania Hivi sasa ina mikataba 9 ya Kodi mikataba hiyo ni Canada - Tanzania Income and Capital Tax Treaty (1995), Denmark - Tanzania Income and Capital Tax Treaty (1976), Finland - Tanzania Income and Capital Tax

Treaty (1976), India - Tanzania Income Tax Treaty (1979), Italy - Tanzania Income Tax Treaty (1973), Norway - Tanzania Income and Capital Tax Treaty (1976), South Africa - Tanzania Income Tax Treaty (2005), Sweden - Tanzania Income and Capital Tax Treaty (1976) na Tanzania - Zambia Income Tax Treaty (1968)

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kwamba mikataba hii inamanufaa kwa Taifa, changamoto yake ni fursa iliyoko kwenye mikataba hii ni ukwepaji wa kodi ambao mfanyabiashara au muwekezaji anaweza kunufaika nao na hivyo asilipe kodi katika mataifa yote mawili "*Treaty shopping*". Mikataba yote niliyoitaja awali ina miaka kati ya 17 hadi 54 hivyo kuna haja ya kufanya marejeo ya Mikataba hii ili kuangalia masuala yafuatayo:-

i. Mazingira ya sasa je tunahitaji mikataba ya kodi na nchi hizo;

ii. Je mikataba hiyo imekuwa na manufaa kwa Taifa au imelisababishia Taifa hasara;

iii. Je, tunahitaji kuendelea kuwa na mikataba hiyo ama tuifanyie marejeo na kuangalia uwezekano wa kuwa na mikataba mingine; na

iv. Endapo tunahitaji kuendelea nayo tuendelee nayo jinsi ilivyo ama ipitiwe upya.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaamini hayo yakifanyiwa kazi tunaweza kuwa na mikataba michache yenye manufaa kwa Taifa sio kama ilivyo hivi sasa.

**29.16. Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (Tanzania Shipping Agencies Corporation-TASAC).**

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (Tanzania Shipping Agencies Corporation – TASAC) lilianzishwa chini ya Kifungu cha 4 cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Sura 415. TASAC ilianza rasmi kutekeleza majukumu yake tarehe 23 Februari, 2018 baada ya Tangazo la Serikali Na 53 la Mwaka 2018. Mara tu TASAC ilipoanza, ilitekeleza majukumu ya udhibiti wa usafiri majini na usimamizi wa ulinzi na usalama wa usafiri majini na kuzuia uchafuzi wa mazingira utokanao na shughuli za usafiri majini. Majukumu hayo awali yalikuwa chini ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) na yalihamishiwa TASAC kama ilivyoelekezwa katika kifungu cha 68 cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Sura ya 415.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha Sheria ya TASAC majukumu yake ni pamoja na kufanya kazi za uwakala wa meli, uhakiki wa shehena, uhudumiaji wa nyaraka za uwakala wa meli na uwakala wa forodha kwa shehena na maeneo yenye maslahi kwa Taifa (Shipping Business Functions). Majukumu haya yameleta taharuki kubwa kwenye tasnia ya uwakala wa forodha nchini kwa sababu TASAC ambae ni msimamizi (Regulator) wa masuala ya uwakala wa forodha naye anafanya kazi za uwakala wa forodha kwa misingi ya utawala bora suala ambalo kamati inaona si sawa. Kamati inaishauri Serikali kwamba kufanya mabadiliko kwenye kifungu cha 7 (1), a cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Sura 415. Kwa lengo la kuweka ukomo kwa TASAC kujishughulisha tu na mizigo na bidhaa nyeti za Serikali kama vile Silaha, Nyara za Serikali, Madini, na Mitambo inayohusiana na Madini katika Uchimbaji na

Uandaaji. Shughuli nyingine za masuala za uwakala wa forodha ziendelee kwa sekta binafsi na TASAC aendelee na shughuli zake za usimamizi.

## 30.0.HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe kwanza kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Maoni ya kamati Mbele ya Bunge lako Tukufu.Vilevile nimpongeze Naibu Spika Mhe. Mussa Azan Zungu kwa kuwa msaidizi mwema kwako. Aidha, napenda kumshukuru, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mb, Waziri wa Fedha na Mipango na Mhe. Hassan Chande, Mb, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nimshukuru Katibu Mkuu ndugu Emmanuel Tutuba, manaibu makatibu wakuu, makamishina na wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za uandaaji wa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kupitia na kuchambua Bajeti Kuu ya Serikali na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi ya Bunge (Hansard):-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Joseph George Kakunda, Mb | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| 9. | Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Jonas William Mbunda, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Juma Hamad Omar, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Riziki Said Lulida, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Halima James Mdee, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Mariam Nasoro Kisanji,Mb | Mjumbe |
| 23. | Mhe. Shamsi Vuani Nahodha, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** mwisho naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu wa Bunge, **Ndg. Nenelwa Mwihambi,** *ndc* pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Mathew Kileo na Makatibu wa Kamati Ndg. Emmanuel Rhobi, Ndg. Maombi Kakozi na Ndg. Wilfred Akasi kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii kwa wakati. Napenda pia kuwashukuru Watendaji wote wa Idara na Vitengo vya Ofisi ya Bunge, kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inawasilishwa kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Sillo Daniel Baran, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**
16 Juni, 2022

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Bajeti kwa kuwasilisha maoni ya Waheshimiwa Wabunge wa Kamati hii na nadhani atatupa mwongozo mzuri katika kuishauri Serikali kwenye hali ya uchumi, lakini pia kwenye Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo orodha hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia kwa siku ya leo kwa sababu uchangiaji wetu utaenda mpaka siku ya Ijumaa wiki ijayo tutakapokuwa tunahitimisha kwa kupiga kura, lakini ninalo tangazo hapa la Mwenyekiti wa wavaa mawigi Bungeni, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza anaitisha kikao kasema sasa hajasema wapi ila kasema mtawasiliana kwa njia zenu, Waheshimiwa Wabunge mnaovaa mawigi, kuna kikao. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Mheshimiwa Zulfa Mmaka Omar atafuatiwa na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha na Mheshimiwa Miraji Mtaturu, ajiandae.

Mheshimiwa Zulfa hayupo, basi Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Mtaturu na Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu, ajiandae.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu nitazungumzia mambo matatu. Jambo la kwanza falsafa ya uongozi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka mmoja cha uongozi wake Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ameonyesha kuwa ni kiongozi msikivu, mpole, mtulivu na

anayetumia hekima kubwa sana katika kufanya maamuzi yenye maslahi makubwa kwa Taifa letu. Nitatoa mfano wa mambo manne; moja, Mheshimiwa Suluhu Hassan amefufua na kuimarisha mahusiano ya Tanzania na nchi za nje na kukuza hadhi na heshima ya Taifa letu katika medani ya kimataifa. Pili, Serikali anayoiongoza ina mpango wa kuanzisha Chuo kipya cha Teknolojia, Habari na Mawasiliano hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa dunia imo katika awamu ya nne ya mapinduzi ya teknolojia, mapinduzi ambayo yanashuhudia matumizi makubwa ya sayansi ya kompyuta na hasahasa matumizi ya kompyuta zinazofikiri kama binadamu, roboti, mitambo inayojiendesha yenyewe bila kumtegemea binadamu. Bila shaka maendeleo haya yanahitaji vijana wenye ujuzi, maarifa, utaalam katika masuala ya sayansi ya habari na teknolojia ya habari na mawasiliano kwa ujumla na bila shaka wazo la Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuanzisha Chuo cha Teknolojia ya Habari limekuja katika wakati muafaka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan amefufua Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Kisasa ya Bagamoyo na nne, Rais Samia amefufua Mradi wa Kusindika Gesi Asilia huko Mtwara.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nchi yetu inawekeza fedha nyingi kila mwaka kwa ajili ya ujenzi wa barabara lakini kwa bahati mbaya sana barabara hizi zinaharibika katika kipindi kifupi sana. Kwa hiyo, nchi yetu inalazimika kutenga fedha nyingine kwa ajili ya kuzifanyia marekebisho na matengenezo barabara hizo. Kwa kawaida barabara inahitaji kufanyiwa matengenezo makubwa katika kipindi cha miaka kumi mpaka ishirini,

lakini kwa upande wetu hali ni tofauti sana katika kipindi kisichozidi miaka mitatu barabara zetu nyingi zinaharibika na hatimaye tunalazimika kutenga fedha nyingi kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo. Nchi yetu ni maskini na haiwezi kumudu gharama za namna hii. Ili kuepuka matengenezo ya mara kwa mara ya barabara, hivyo, napendekeza mambo mawili yafuatayo:-

(i) Serikali iteue wahandisi waadilifu na wenye weledi wanaoweza kuwasimamia wakandarasi wa barabara ili barabara zijengwe kwa kiwango na ubora unaotakiwa. *(Makofi)*

(ii) Naunga mkono hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti; Serikali iimarishe Kitengo cha Ukaguzi wa Barabara ili kubaini uharibifu mapema na hatimaye kufanya matengenezo yanayohitajika kwa wakati. Jambo hili litatusaidia sana katika kudhibiti matumizi makubwa ya fedha katika matengenezo ya barabara zetu kama Waingereza wasemavyo *a stitch in time saves nine,* kwa Kiswahili usipoziba ufa utajenga ukuta. *(Makofi)*

(iii) Mwaka 1987 marehemu Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere alipokuwa akihutubia Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa alisema maneno yafuatayo:-

"*Iwapo nchi yetu inataka kupiga hatua kubwa za maendeleo na za haraka, hatuna budi tuzitumie rasilimali zetu kikamilifu.*"

Mheshimiwa Spika, kwa mawazo yangu bado hatujauzingatia ushauri huu wa Mwalimu ipasavyo hasa katika sekta ya gesi asilia. Mwenyezi Mungu ametubariki na kutujalia gesi ipatayo trilioni 57 za ujazo, lakini kwa bahati mbaya sana tumeweza kutumia kiasi hiki cha gesi

kwa kiasi kidogo sana. Iwapo tunataka kukabiliana kikamilifu na kupanda kwa bei za mafuta zinazotokea kila wakati tunapaswa kuimarisha uchumi wa gesi. Kwa hiyo, napendekeza Serikali ifanye mambo yafuatayo:-

(i) Serikali iongeze matumizi ya bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam. Kwa bahati mbaya hivi sasa Serikali imetumia bomba hili kwa asilimia 10 tu. Habari hizi si njema hata kidogo, tunapaswa kuongeza matumizi ya bomba hili. *(Makofi)*

(ii) Serikali ihakikishe mipango na matumizi ya nishati ya gesi katika matumizi hasa katika kuendesha magari ya Serikali na mizigo ili kupunguza gharama ya usafiri na usafirishaji.

(iii) Serikali iharakishe mipango ya kutekeleza mradi wa kusindika gesi asilia kule Lindi.

Mheshimiwa Spika, hapana shaka tukichukua hatua hizi nilizozieleza tutaweza kupunguza uagizaji wa mafuta kutoka nje kwa kiasi kikubwa na naamini hali hii itatusaidia sana kupunguza makali ya maisha kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Miraji Mtaturu atafuatiwa na Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, ajiandae.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyopo mezani kwetu ambayo ni hoja ya Bajeti Kuu ya Serikali

mwaka 2022/2023. Nianze kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na kukutana asubuhi ya leo. Pili, nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuiletea nchi yetu maendeleo. Tumeona kwa vitendo mambo mbalimbali ambayo yanajitokeza baada ya kuwa yeye ametoa kauli na kuonyesha utashi wake wa kweli katika kuiletea Tanzania maendeleo. *(Makofi*

Mheshimiwa Spika, hata leo hii bajeti ambayo imesomwa na kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha imeonyesha wazi maono yake, imeonyesha wazi dhamira yake na imeonyesha wazi namna ambavyo anaitekeleza vizuri Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa nimetoa shukrani kwa Mheshimiwa Rais, sasa nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri mtoa hoja, kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa kazi nzuri aliyoifanya kutuletea hoja hii ambayo imeonyesha wazi bajeti hii itakwenda kuondoa maumivu yaliyokuwepo kwa wananchi. Bajeti hii imegusa nyanja mbalimbali za kimaendeleo, bajeti hii imegusa sekta zote kwa umakini mkubwa, lakini zaidi imeonyesha waziwazi kwamba imeenda kumgusa mnyonge chini kabisa pale. Kwa hiyo, naamini kabisa kama bajeti hii itaenda kufanyiwa kazi itaenda kuleta mabadiliko na kufanya mapinduzi makubwa ya uchumi wa nchi yetu. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake ndugu yangu Mheshimiwa Chande na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kushukuru sana, nimeona kwenye bajeti hii pamoja na bajeti za kisekta ambazo tumekuwa tumepitisha, tumeona katika Jimbo langu, Wilaya yangu ya Ikungi tumeona namna ambavyo tumepata mgao wa fedha, tumepata mgao kwenye maeneo ya afya, maji, elimu huduma mbalimbali za kijamii zinaenda kuguswa, lakini kama haitoshi tumeona namna ambavyo miundombinu ya barabara itaenda kuletewa fedha kwa ajili ya kutengeneza lami katika maeneo ya Mji wa Ikungi ambapo tunapata kilometa mbili, zitaenda kujengwa pamoja na taa zitawaka katika mji wetu. Hii italeta mabadiliko makubwa sana, hivyo, tunaishukuru Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru kwa namna ambavyo imeamua sasa kujenga barabara ile ya Singida - Kwa Mtoro – Ugashi - Tanga ambayo imekuwa tukisemea kwa muda mrefu. Kilometa 462 zikienda kujengwa itaenda kuchachua uchumi wa wananchi wetu na tutaona maendeleo ya haraka yatapatikana. Tumekuwa tukisema Bungeni na leo nashukuru Mheshimiwa Waziri ameitaja barabara hii, tunaamini wananchi wanaisubiri na tunaomba sana mchakato ufanywe mapema, tupate mkandarasi ili barabara iende kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo, naomba niende kwenye eneo ambalo nimesoma katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, eneo la ukuzaji wa uchumi. Eneo hili tumeelezwa vizuri mpango wa Serikali namna ambavyo tutakuza uchumi, lakini tumeelezwa kwamba ukuaji wa uchumi wanategemea mpaka mwakani 2023 tutafikia wastani wa ukuaji wa pato la Taifa kwa asilimia 5.3, wakati huo wastani wa Ilani wa CCM inasema asilimia 6.9. Kama Serikali ikiangalia vizuri tumekuwa tunapanda

kwa taratibu sana kwa sababu kuna baadhi ya vyanzo vya mapato hatujaviangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nitazungumzia sana sekta ya uchumi wa makaa ya mawe pamoja na chuma kilichopo kule Ludewa. Tumekuwa na changamoto kubwa ya kuwa tunatamka lakini hatuchukui hatua. Eneo hili tumekuwa tukilizungumza kwa miaka mingi, lakini leo tutaangalia kwamba kwenye Ilani ya CCM imeeleza wazi kwamba mapinduzi ya uchumi kwa maendeleo ya watu, Ibara ile ya 17, imeelekeza waziwazi kwamba kutumia rasilimali za Taifa kwa ajili ya maendeleo na manufaa ya Watanzania. Leo hii tunavyoongea makaa yale yalioko pale Ludewa hatujayachimba, leo tunavyozungumza tunazo leseni tulizowapa *NDC* ambao wamepewa leseni zipatazo nane, lakini wamezishikilia tu, hawajawahi kufanya utafiti, hawajawahi kuchimba, mali iko pale ardhini haijawahi kuguswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ukienda utasikitika, Kamati yetu ilifika kule, imeona namna ambavyo yale makaa ya mawe huhitaji kuchimba wala kutumia nguvu kubwa. Unachukua chepe tu, unachimba, unachukua yale makaa ya mawe unaenda kuuza. Hayahitaji kutumia fedha nyingi. Leo hatujaweza kuyachimba, hivi ninavyoongea, *NDC* wamepewa leseni nane kama nilivyosema, *PL* 6986 ya mwaka 2012, *PL* 6710 ya mwaka 2010, *PL* 10263 ya mwaka 2014 pamoja na ya 2015, zote hizi hazijawahi kuchimbwa mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, leo hii kwa sababu ni kampuni ya Serikali, ni vizuri waruhusu sekta binafsi waingie kwenye uchimbaji wa madini haya ambayo kimsingi wataenda kwa kasi kwa sababu wao wanaangalia faida. Inawezekana hawa *NDC* kwa kuwa wao ni Serikali

hawaoni manufaa sana na hawaoni haja hiyo kwa sababu haiko kwenye mipango yake, lakini kama tunataka kuangalia chanzo cha uhakika, lazima tuangalie namna ya kuchimba ile chuma, namna ambavyo tutachimba yale makaa ya mawe ambayo kimsingi yataenda kuleta kwa sababu yana soko nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi, tutaunganisha na namna ambavyo tutakuza bandari hii ya Mtwara. Bandari ya Mtwara itapata mzigo wa kutosha kupeleka nje. Tumeanza kuona saivi kuna meli zinaondoka zinakwenda India kutokea Bandari ya Mtwara. Kwa hiyo, uwekezaji wa Bandari ya Mtwara kama tutaweza kupeleka mzigo wa kutosha, utakuwa na maana na utarudisha fedha ambazo Serikali imewekeza. Kwa hiyo, niombe sana, eneo hili waliangalie kwa makini ili waweze kuona namna ambayo tutaongeza pato la Taifa ambalo kimsingi kwetu ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili niwaombe, kuna barabara ya kutoka pale Njombe kwenda mpaka Manda Ludewa. Barabara ina kilomita 210, Serikali imeanza kujenga kilomita 50 kwa kutumia *concreate,* leo hii wameshajenga kilomita kama 30 na kitu hivi. Kwa hiyo, niombe sana, kilomita zilizobaki ziweze kujengwa kwa sababu kutakuwa na *movement* kubwa ya magari ambayo yatakuwa yanatoka kule kwa ajili ya kupeleka kwenye Bandari zetu za Tanga na eneo lingine. Kwa hiyo, eneo hili tukilifanyia kazi vizuri, tutafikia lengo ambalo liko mbele yetu la kukuza uchumi na kuongeza pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili niongelee sekta ya utalii. Utalii ndiyo unatuingizia fedha nyingi kuliko sekta yoyote

katika nchi yetu. Utalii huu ambao tumepewa kama tunu na Mwenyezi Mungu, lazima tulinde rasilimali tulizonazo na vivutio ambavyo tunavyo. Mheshimiwa Rais amefanya kazi nzuri ya kutangaza vivutio vyetu kupitia *royal tour*. Tunaona matokeo yake, watu wanakuja kuona. Hivi leo hii tukitangaza vivutio ambavyo kesho havipo, inakuwa haina maana hata juhudi zote za kutangaza vivutio hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii tunasema wote kwa pamoja, utalii unatuingizia fedha. Tunawavutia watalii waje waone, hivi wakialikwa, wakaja kukuta vivutio vimekwisha itakuwa na maana gani? Niombe sana Serikali ijikite katika kulinda rasilimali zetu. Isiache watu wachache ambao hawana nia njema wakaharibu vivutio vyetu, kwa sababu tu ya lengo, wengine wanakuja na sababu ndogo tu, kwamba Serikali inajali wanyama kuliko wananchi, si kweli. Wote wanaishi nchi hii, lazima tuwe na vipaumbele, tulinde vivutio na huku tunalinda na binadamu, ndiyo maana wanapewa huduma. Hatuwezi kuruhusu hali hii kwa sababu eti kuna watu fulani wataona wanaonewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Pori la Loliondo lilianzishwa mwaka 1951. Mpaka leo kama ingekuwa hatujatunza vizuri, maana yake leo hii tungekuwa hatuna vivutio hivyo. Hatuwezi kuacha watu wachache wakatuharibia, tena bahati mbaya wanatumika na nchi zingine kuharibu kwa sababu ya ushindani wa utalii. Niombe sana Serikali iwe makini kuhakikisha inalinda ili tuendelee kuwa na hali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusipoangalia hili jambo, tutaanza kuingia kwenye huruma ambazo nyingine hazina sababu, wengine wana ajenda zao na kwa

hakika leo hii pori lile lilikuwa na ukubwa wa kilomita za mraba 4,000. Serikali imepunguza 2,500 imewaachia kule wananchi waweze kufanya shughuli. 1,500 ambayo ni chanzo cha ikolojia ya kulinda kule Serengeti ambayo tunasifiwa leo, ni mbuga ambayo inasifika duniani. Watu wengi wanataka kuja kuona pale Serengeti, leo hii tukiua ile, ikolojia ile ya kutunza wale wanyama, nyumbu wanapita kila mwaka kwenda pale wanazaliana. Nyumbu zaidi ya 600,000 wa ndama wanapatikana pale, kupitia ikolojia hii ya njia hiyo. Leo hii tukiacha pale, vyanzo vya maji ambavyo vinapatikana kwenda kutunza kule Serengeti vinapitia pale Loliondo. Leo hii tukianza kuja na sababu ndogo ndogo tu, nyingine hazina mashiko, hatutafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi ni kubwa, kama kunaonekana watu eneo lile hawana sehemu nzuri ni ukame na nini, wapatiwe eneo lingine la kwenda kuishi, Tanzania bado ni kubwa. Ardhi hii iko chini ya Mheshimiwa Rais. Aruhusu waende popote, waweze kuacha eneo lile liweze kulindwa na liweze kuhifadhiwa na tuweze kuendelea kupata utalii kama ambavyo tumeendelea kulinda katika miaka yote, toka mwaka 1951.

Mheshimiwa Spika, sekta ya utalii bado sisi tunaendelea kuona kama ndiyo mboni ya jicho letu. Serikali isisite, ichukue hatua, isimamie na wale waliopewa kazi hii ya kuhifadhi, wafanye kazi yao kwa mujibu wa sheria. Eneo hili naomba sana kama kuna watu ambao wanafanya tofauti na haki za binadamu, wachukuliwe kama wao siyo ionekane kama Serikali nzima haijatenda haki kwa wananchi wale. Kwa hiyo, nilitaka nieleze eneo hili ili tukuze uchumi wetu. Zaidi naomba nirudie tena

kushukuru sana na kuipongeza Serikali kwa kuleta bajeti ambayo leo inaenda kutuheshimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo na Mheshimiwa Zulfa Mmaka Omar ajiandae.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba; Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa maandalizi ya hotuba nzuri ya bajeti. Nawapongeza vilevile kwa sababu wametuletea bajeti nzuri ambayo inaleta matumaini kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti hii inalenga kukuza uchumi. Nataka kuanza na Mkoa wa Kagera. Mkoa wa Kagera, uchumi umeanguka, uchumi umekwenda chini sana. Ukiingia leo hii kwenye mitandao wale wakazi wa Kagera na wazaliwa wa Kagera wameunda makundi mengi, wote wanajadili hali mbaya, hali ya kuanguka kwa uchumi Mkoani Kagera. Hata wewe mwenyewe ukiwa unapita kule vijijini, ukaangalia wale watu, unaona kabisa kwamba uchumi umeenda chini na unaona kabisa kwamba umasikini umeongezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu inayotoa orodha ya mikoa *against GBP per capita* ambalo ni pato la Taifa kwa kila mtu,

inaonesha kwamba Mkoa wa Kagera sasa ni wa 23 katika Mikoa ya Tanzania Bara. Sisi tunashangaa mkoa ambao una misimu miwili ya mvua, mkoa ambao mvua wastani wake kwa mwaka ni milimita 500 mpaka 1,000. Kwa hiyo, ina maana kwamba mazao mengi yanaweza kuota, lakini unakuwa karibu kwenye mkia kiuchumi katika Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, nina uhakika Serikali inaliona hili, nina uhakika na nyie mnapita kwenye mtandao mnaona yale majadiliano yanayoendelea kuhusu Mkoa wa Kagera. Tunaomba sasa na nategemea kwamba Serikali inakwenda kuja na mkakati wa maksudi wa kuunusuru Mkoa wa Kagera. Ili kuinua uchumi wa Mkoa wa Kagera ninayo mapendekezo kadhaa.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Serikali iwezeshe biashara ya mipakani. Kagera *Region is strategical located,* imezungukwa na Nchi nyingine kama vile Burundi, Rwanda, Uganda, vilevile ina mpaka kwa kupitia maji Kenya. Hata hivyo, pia ukiangalia wakazi wa *East Africa* ambao kuna *South Sudan,* Burundi, Rwanda, Kenya na Uganda *population* yake ni watu karibu milioni 195. Hilo ni soko kubwa sana ambalo tukilitumia vizuri tunaweza kuinua uchumi wa Tanzania na tunaweza tukainua uchumi wa Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tufungulie masoko ya mpakani pale Kabanga, Ngara kwenye mpaka wa Burundi, Rusumo kwenye mpaka wa Rwanda, Mutukula kwenye mpaka wa Missenyi, Nyakanazi, Murongo kwenye mpaka wa Kyerwa. Vilevile yako maeneo mengine kama Kashenye, Rubafu, wakiyafungua yale masoko pale, masoko makubwa ya ndizi, masoko makubwa ya mazao mbalimbali, minada mikubwa ya mifugo, utakuta

kwamba tutakuwa tumefungua uchumi wa Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa ukienda kwenye hiyo mipaka niliyoizungumzia, upande wa nchi jirani unachangamka kibishara, lakini ukiangalia upande wetu wa Tanzania umedorora. Kwa hiyo, hapa kinachohitajika ni kuondoa vikwazo vya kikodi na visivyo vya kikodi kwenye sheria za biashara ili ziweze kuwa nzuri, ziwavutie wenzetu wapende kufanya biashara kwenye upande wa kwetu.

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu Mkoa wa Kagera uko mbali sana na Dar es Salaam. Vifaa vingi kwa mfano vya ujenzi vinatoka Dar es Salaam, kwa sababu ya umbali ule unakuta *by the time* ile *product* inafika Mkoa wa Kagera gharama imeshakuwa kubwa sana. Kwa mfano, mfuko wa *cement* unakwenda mpaka unafikia hata Sh.23,000 au Sh.25,000. Kwa hiyo, napendekeza Mkoa wa Kagera upewe upendeleo maalum, *differential treatment* kwenye sheria, kwenye sera, kwenye kanuni za kibiashara ili sasa kuweza kuvutia wawekezaji na kuwekeza nchi za jirani ili wapende kufanya na sisi biashara.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera ni mkoa wa wakulima, wafugaji na wavuvi na Mwenyezi Mungu alitujalia akatupa Ziwa Victoria. Naomba Wizara zinazohusika wawawezeshe watu waweze kufuga samaki kwenye ziwa kwa kutumia vizimba *(cage fishing),* lakini vilevile hata kwenye mabwawa, watuwezeshe waweke viwanda vya kuzalisha mbegu, kwa sababu hata wale wanaofuga samaki kwenye mabwawa inafika mpaka miezi tisa bado kasamaki ni kadogo kwa sababu hawana mbegu bora.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa kilimo, Mkoa wa Kagera ni namba moja kwenye kilimo cha ndizi, lakini zile ndizi hazina soko maalum ambalo linaeleweka. Kwa hiyo, unakuta wakati wa kiangazi ambapo ndizi ni nyingi, mkungu bei inaporomoka mpaka Sh.2,000. Kwa hiyo, huyu mkulima anaenda kupata hasara. Tunaomba wapewe Maafisa Ugani wafundishwe matumizi sahihi ya mbolea, mboji, samadi na mbolea za viwandani, lakini watafutiwe soko.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani mpaka leo Kagera tukaendelea kulima mazao yaleyale, kahawa, ndizi, ndizi, kahawa. Lazima tubadilike, hatuwezi kuendelea na *traditional crops* peke yake. Naomba Serikali waende wahamasishe, tuweze kuanzisha haya mazao mbadala, kwa mfano *vanilla*, michikichi, parachichi, alizeti, vyote vinaweza kuota Mkoa wa Kagera, hili linaweza likachechemua ukuaji wa uchumi ndani ya Mkoa wa Kagera. Tusiwaache watu wakalima tu. Kwanza tutafute masoko kusudi watakaokuja kulima mazao hayo walime kwa *standards* zinazohitajika kwenye soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya ni kwamba labda na uchumi uliendelea kuporomoka Mkoa wa Kagera kwa sababu hakuna zao hata moja la biashara ambalo lina bei nzuri. *On that note,* napenda nimpongeze sana na nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimshukuru Waziri wa Kilimo kwa juhudi zao za dhati ambazo wamezionesha. Waziri Mkuu ameenda zaidi ya mara tatu, mara nne kuangalia kama anaweza kuchechemua na kuongeza bei ya zao la kahawa. Kwanza alienda kukemea ile ya kuuza *butura*, kudhibiti *butura*, wakaondoa tozo kibao kwenye bei ya kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wametuletea mfumo mzuri wa manunuzi kupitia minada na kwa mara ya kwanza katika historia ya Mkoa wa Kagera namna iliyofanyika *last time,* kilo moja ya kahawa ya arabika imeweza kuuzwa kwa Sh.3,740 ambako tumezoea Sh.1,000 au Sh.1,200. Sasa hivi tulikuwa tunasubiri kuona sasa itakuwaje kwenye hii robusta ambayo ni kahawa ambayo inalimwa na wengi kama na bei na yenyewe inaweza ikapanda vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa jinsi anavyowapenda Watanzania. Kwa sasa hivi ametuletea bajeti nzuri, bajeti ya wananchi, kwa sasabu pamoja na matatizo yote yanayoendelea duniani, ambayo yanatokana na athari za UVIKO na vita vinavyoendelea *Ukraine* huko, lakini yeye ameweza ku-*inject* ruzuku ya bilioni 100 kupunguza bei ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumeona bajeti ya kilimo, sekta ambayo inagusa watu wengi, bajeti yake inapanda kutoka kwenye bilioni 264 kwenda kwenye bilioni 954. Mifugo bajeti yake inapanda kwa bilioni 100. Serikali imenunua boti zaidi ya 250 za kisasa zile za faida, zinaenda kupelekwa kwa wavuvi. Vilevile, wale watumishi wa Serikali ambao wamefikia hadhi ya kupewa magari wanaenda kukopeshwa na hii itaipunguzia Serikali gharama kwa bilioni 500.

Mheshimiwa Spika, vilevile amepandisha mshahara, kitu kilichowafurahisha Watanzania kima cha chini kikapanda kwa asilimia 23.5. Pia wastaafu ile hela yao ya mwisho wanayopewa ya mkupuo imepanda kutoka kwenye asilimia 23 mpaka 33.

Mheshimiwa Spika, elimu ni bure, watoto wetu wanasoma tangu awali mpaka kidato cha sita bila ada. Naishukuru sana Serikali kwa sababu bajeti hii inaenda kuondoa umaskini, bajeti hii inaenda kuongeza uchumi, bajeti hii inaenda kuongeza ajira, bajeti hii inaenda kupunguza makali ya maisha, kweli ni bajeti ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Zulfa Mmaka Omar na Mheshimiwa Twaha Mpembenwe ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hoja hii muhimu. Awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwanza kwa kuaminiwa kuongoza Wizara hii nyeti, lakini pia kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na hasa kwa kuleta bajeti ya matumaini makubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii kwa maoni yangu ni kweli kabisa imezingatia lile azimio la nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwamba tuwe na bajeti ambazo zinachochea kukua kwa uchumi wa nchi na kuwapunguzia wananchi ugumu wa maisha. Naiona sura hiyo katika bajeti yetu kwa kiasi kikubwa. Hii ni bajeti shirikishi ambayo imeanzia chini kabisa kwenye halmashauri zetu, ikapanda ikatufikia huku juu, kwa hiyo ni rahisi hata utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona jinsi ambavyo bajeti hii imesisitiza juu ya kuongeza pato la Taifa kwa kuweka

msisitizo mkubwa katika sekta ya kilimo, madini na hata sekta ya utalii na pia kuongeza mzunguko wa fedha kwa kutenga fedha za kulipa madeni hasa ya wakandarasi na wazabuni wengine na pia fedha kwa ajili ya miradi mikubwa ya kimkakati iliyokuwa inaendelea. Hii itainufaisha sana nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pia yako marekebisho ya sheria na baadhi ya tozo ambazo zimeondolewa na nini zote zikielekezwa katika kuchochea sekta binafsi ambayo ni muhimu sana kwa ajili ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pia suala zima la kusisitiza juu ya *value for money* yaani thamani ya kazi kwa fedha zinazotolewa. Nimeona kwa namna pekee kabisa, Ofisi ya CAG inaongezewa wataalam wa fani zingine ili kuipa nguvu zaidi katika kuhakikisha kwamba miradi inakaguliwa kwa uhakika zaidi na kwamba tuendelee kupata thamani halisi ya fedha ambazo tunatoa. Nimewahi kulisema hili katika Bunge hili kwamba hata matumizi yetu ya *force account* kwenye halmashauri zetu na maeneo mengine yanahitaji sana kupelekewa wataalam wa fani zote ili kwamba tunapofanya kazi hasa za ujenzi tuweze kupata kitu ambacho ni cha uhakika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, iko hofu ambayo inaendelea duniani kote juu ya hili suala la *inflation* na mdororo wa uchumi. Ukiangalia sana kinacholeta hofu hii ni vita ya *Ukraine* na Urusi, lakini nasema vita ya *Ukraine* na Urusi, risasi hazifiki huku, kinachofika huku ni madhara yanayotokana na bei za mafuta na suala zima la chakula. Kwa upande wa bei za mafuta naweza nikasema ni changamoto, lakini upande wa chakula kwetu inaweza ikawa fursa vilevile.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu tukijikita kwenye kilimo kwa nguvu zote ikawa kama vita, kuhakikisha kwamba kila ardhi inayofaa kulimwa, inalimwa na inalimwa mazao ambayo kitaalam yamekubalika kwamba yatatuletea tija, tutafika mahali pazuri. Hata ardhi ya mtu ambaye hajaitumia, kama hailimi sasa *either* ikodishwe alipwe *rent* ilimwe au apewe hisa kwa mwekezaji ambaye ataingia pale ili ardhi yote inayofaa kulimwa, ilimike.

Mheshimiwa Spika, mwaka 45 yuko mpiga kura wangu mmoja wa enzi hizo kabla sijawa Mbunge alikuwa anaitwa *Reverent* Silas Msangi alitunga ule wimbo unaosema Tanzania, Tanzania nakupenda kwa moyo wote. Akaelezea jinsi ambavyo watu watakuja kukimbilia Tanzania ili waweze kupigana kwa ajili ya kupata uhuru kwao. Unabii huo unaweza ukatimia tena na hilo lilitimia kwa sababu ule wimbo ule ulitungwa mwaka 45 ikaja kutimia mpaka kesho asubuhi. Hata sasa hivi tukijikita vizuri kwenye sekta ya kilimo watu watakuja kufatuta chakula kwetu na nchi hii itaendelea kukimbiliwa na watu kama sehemu pekee ambayo itakuwa inapatikana chakula kwa sababu kama ni ardhi tunayo kubwa kuliko ya Ukraine, kama ni hali ya hewa, ni nzuri na hatuna uhaba wa wataalam, watu wamesoma vizuri na uwezo wa kufanya kazi wanao.

Mheshimiwa Spika, nashauri, tujikite kwenye sekta ya kilimo kwa nguvu kama ambavyo tuliingia kwenye sekta ya miundombinu tukaanzisha miradi ambayo ilikuwa ni ya kufikirika na ikatimia. Kwa hiyo, tukiingia kwenye sekta ya kilimo kwa nguvu kwa kiasi hicho tunaweza tukafika mahali pazuri sana. Tusiende tu kwenye hali ile ya kusema, tumetenga fedha nyingi lakini tunaziingiza

kwenye miradi kama, sisemi vibaya lakini kilimo kwanza labda na nini ambayo tunaishia kuongeza matrekta ambayo yanaharibika siku mbili. Twende kwenye hali halisi, mazao gani yanafaa hapa, ardhi kiasi gani ipo, yalimwe, yasimamiwe ili tuweze kutoka sisi na kuitoa *East Africa* yote katika matatizo haya ya chakula.

Mheshimiwa Spika, tunakushukuru sana jana ulituletea wataalam kutoka Benki Kuu pamoja na Taasisi za Fedha, wakatoa mawasilisho yao. Ukiangalia yale mawasilisho yao yameendana kabisa na *review* ya *PricewaterhouseCoopers* wanaofanya juu ya bajeti hii. Jambo kubwa sana la msingi lililojitokeza ni juu ya ukweli kwamba *inflation* kwa sisi Tanzania tuko vizuri kuliko Nchi zote za Afrika Mashariki pamoja na *SADC*. Wataalam hawa wasingeweza kudanganya. Jambo hili si jambo la kuchuliwa kwa mchezo mchezo, ni jambo ambalo ni la muhimu sana, tukianzia hapa tunaweza kufika mbali.

Mheshimiwa Spika, sasa ukiacha hapa tulipofikia, pamoja na changamoto za *corona* na za vita vya Ukraine, bado taarifa zinakuja kwamba hoteli zetu na *booking* zetu za utalii zimejaa na hii itakuwa endelevu kwa sababu ya *royal tour*. Tukiipokea hii vizuri, Tanzania itapaa na ikipaa tusitegemee mazuri tu, tutegemee na maadui pia wa kiuchumi. Tumeona hapa kiongozi mkubwa wa nchi moja jirani wa cheo cha *Senator* anatoa kauli za kashfa kashfa za kuingilia suala la ndani ya nchi yetu. Inasemekana basi kama taarifa za kwenye mtandao ni za kutegemea sana, kwamba nchi yetu imepelekwa *ICJ*. Siamini kwa sababu sioni kwamba lililotokea linaweza kupelekwa *ICJ* kwa sababu *ICJ* ina mamlaka za aina mbili. Kwanza, ni juu ya *contentious matters* ambazo ni ugomvi wa mipaka, ambayo ni

magomvi kati ya nchi nan chi, ambalo sasa sio hilo. Lingine labda ni kwenda kutafuta ushauri tu.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba jambo hilo linachochewa na nchi nyingine, inaonesha kabisa kwamba hii ni vita ya kiuchumi ambayo inatokana na hali hii tunayoisema, Tanzania hii tunayoijua ambayo watu wamekuwa wakiitazama kwa jicho kama vile sisi sio watu wa kupiga hatua sana, lakini leo hii tukiambiwa kwamba *inflation* yetu ipo chini kuliko Nchi zote za Afrika Mashariki na *SADC,* lazima wajitokeza maadui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani Vyuo Vikuu vilipoanza hapa Afrika Mashariki, Kitivo cha kwanza kilikuwa ni cha Sheria, kwa hiyo naamini kimejizatiti, hata wakienda *ICJ* twendeni, nina hakika tutajieleza vizuri na tutashinda na tutaendelea kukuza uchumi wetu kwa njia hizo za utalii, kilimo, madini na hata sekta zingine kama za ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, amezungumza vizuri Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha juu ya ubora wa barabara zetu na kadhalika na kadhalika. Ukweli tumekuwa tukisema Serikali iwape kipaumbele wakandarasi wazalendo, lakini pia na wao ni vizuri wakaji-*link* na juhudi kubwa za *innovation* ambazo zinafanyika katika sekta ya ujenzi duniani ambazo zinahusisha makundi matatu. Kundi la kwanza, ni watengenezaji wa *materials* za ujenzi na kundi la pili ni wateja pamoja na wajenzi. Teknolojia imepanda sana, hata kama tutajaribu kuwa-*favour* watu wetu kwa kuwapa mitaji na kadhalika lakini kama watakuwa hawajaweza kuifahamu teknolojia iliyopo sasa, bado wanapokuja watu wa nje kwenye miradi wataonekana bei zao zipo chini na wataweza kupata miradi na miradi yao itakuwa bora zaidi kwa sababu ya teknolojia.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kusema hayo, kusisitiza kwamba tunahitaji kwenda na teknolojia ya dunia na sasa hivi tunaishukuru Serikali, nimeona kwenye bajeti ya Waziri wa Fedha amezunguma juu ya suala la kuzingatia masuala ya TEHAMA katika kuendesha nchi, atatupunguzia gharama na atatuongezea na ubora wa kazi.

Mheshimiwa Spika, lingine ni hili la ku-*take advantage* ya hali ya uchumi ilivyo sasa hivi, tunataka tuvuke kwenda mbele lakini tujipange pia kuwa maadui watakuwepo hasa kwa hili ambalo limejitokeza. Nimeona kabisa kwamba hili limejitokeza kwenye sekta ya utalii, sijiingizi kusema kwamba nani yuko sahihi na wapi, lakini suala zima la kuingiliwa na nchi ya nje katika mipango ya utekelezaji wa sheria zetu za ndani sio sahihi.

Mheshimiwa Spika, nilipata kusoma mahali kwamba masuala kama haya ya Loliondo na Ngorongoro mradi tu yanafanyika kwa mujibu wa sheria zetu, hakuna matatizo yoyote, ni jambo la kawaida ambalo linafanyika kila wakati katika maeneo mbalimbali ya Tanzania, wala halina sura ya ukabila wala ya uonevu, lakini sasa anayeingilia kutoka nje hapo ndiyo inabidi tujipange kwamba kwa kweli hii sasa ni vita. Mara nyingi mti ambao hauna matunda huwa haupigwi jiwe hata na mtoto mdogo, kwa hiyo ukiona mawe yameanza ujue mti wetu una matunda.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba Wabunge wenzangu waunge mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zulfa Mmaka Omar atafuatiwa na Mheshimiwa Twaha Mpembwenwe na Mheshimiwa Janejelly James Ntate ajiandae.

**MHE. ZULFA MMAKA OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia leo. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na uhai wake na kuweza kuwepo katika Bunge hili Tukufu na kutupa pumzi za kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa jinsi anavyofanya kazi zake kwa weledi, umahiri na kwa utulivu kabisa kwa kuzingatia kwamba sisi tunamtegemea na tunampenda, kwa hiyo nimpongeze sana kwa kazi hizo nzuri ambazo anazifanya. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii ya Fedha kwa jinsi wanavyofanya kazi zao katika kuinua uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na suala zima la ukusanyaji wa mapato kule *TRA*. Mimi ni balozi wa kodi ambaye kwa uwezo wangu nafasi hii niliipokea katika bajeti tunayoimalizia kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Nimpongeze sana kwa uteuzi huu na nimwambie kwamba kazi ile ambayo alinituma naifanya na ni kazi nzuri, nimejifunza mengi na naendelea kujifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na suala zima la mipakani. Wakati tupo katika ziara zetu tulibahatika kutembea katika mipaka mingi ya Tanzania. Katika mipaka hiyo tulienda katika mpaka mmoja wa Rombo Tarakea. Hii ni sehemu ambayo wanakusanya pesa nyingi, wanazalisha pesa nyingi, wanafanya kazi nzito na sehemu ile inafanya kazi kubwa, ila wanafanya katika

mazingira mazito. Pale hakuna kituo ambacho wanafanya kazi kwa pamoja kama katika Vituo vingine kama cha Namanga, ambao wao wana Kituo cha Pamoja ambacho kinarahisisha ufanyaji kazi na kinawarahisishia wale ambao wanakwenda kufuata huduma pale, kuipata huduma ile kwa muda mfupi na huduma nzuri. Kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri vituo hivi avitembelee, vinakusanya mapato makubwa lakini wanafanya kazi nzito kwa sababu hakuna vitendea kazi, hawana usafiri, hawana majengo mazuri hata huduma ya afya katika vituo vile kwa kweli haiko vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia katika bajeti ya uanzishaji wa Ofisi za TRA tulikuta kwamba kuna baadhi ya maeneo kama eneo la Kotoro katika Mji wa Kahama kuna kilomita tisini kutoka mjini ambapo watu watafuata kwa ajili ya huduma hii. Hiki kinapelekea wananchi kuwa na uzito kidogo wa kufuata huduma hizi katika vituo vile na uzito ule unapelekea kutokulipa kodi na kodi ya nchi yetu kushuka kidogo. Kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri katika bajeti hii aiangalie vizuri bajeti ya uanzishaji wa ofisi ili waweze kukusanya mapato kama ambavyo tumejipangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende katika ukurasa wa 54, hapa kuna jambo zuri ambalo limefanywa na mama yetu na sisi hatuna budi kumpongeza kwa sababu tunaona kuna vifaa vya afya ambavyo vimeandikwa pale vinavyoenda kununuliwa kwa ajili ya wananchi. Hivi vyote vinatokana na kodi ambazo zinakusanywa. Vifaa hivi ni kama *x-ray machines* 130 ambazo zitanunuliwa, *CT scan* pamoja na mashine za oksijeni. Hili ni jambo zuri na tunampongeza sana mama yetu kwa kujali afya za wananchi wake na sisi tumwambie kwamba malipo haya

atayakuta kwa Mwenyezi Mungu na tutakuwa naye bega kwa bega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee pia kuhusu suala zima la Kitengo cha Elimu kwa Mlipakodi, katika kazi ambayo inatakiwa kuongezwa na kuzidisha kuifanya ni suala zima la elimu. Tunakuta kwamba wananchi wengi hawana elimu hasa ya ulipaji wa kodi. Unakuta anakwambia kwamba hela nyingi inakwenda kwa ajili ya kununua mashine, ila sasa wanapopata ile elimu kwamba hela ile ambayo tunanunua mashine mwisho wa siku ukienda kulipia kodi inaangaliwa ulitoa shilingi ngapi, baada ya hapo ndiyo unapigiwa hesabu ambayo imebakia kwa ajili ya ile mashine, wataelewa. Hivyo, tunasema kwamba elimu bado inahitajika kwa wananchi, kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kile Kitengo cha Elimu kwa Mlipakodi akiongezee bajeti yake ili iweze kuwafikia wananchi wengi kwa haraka na kwa ufanisi. Kwa hiyo, naamini kwamba kwa kazi ambayo wamefanya na kwa asilimia ambayo wameipata ya ukusanyaji wa kodi atazidi kuwaangalia zaidi watu hawa ili elimu izidi.

Mheshimiwa Spika, niende katika suala zima la pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, tunaona kwamba ni jinsi gani anawapenda wananchi wake wakubwa na wadogo. Kitendo cha kufuta malipo kuanzia elimu ya chini hadi kidato cha sita ni suala kubwa sana. Hili halijawahi kutokea na sisi tumwambie Mama Samia kwamba tunamshukuru sana kwa sababu mzigo huu hata sisi Wabunge ulikuwa unatuhusu pamoja na wananchi lakini sasa katutua mzigo huu mzito. Kwa sababu tunafahamu kwamba malipo yale yanakwenda moja kwa moja kwa mzazi na wazazi wengi sana ambao wanaumia na haya mambo ni

wanawake. Kwa hiyo sisi wanawake tunamshukuru kwa kututua mzigo huu na tunamtakia kila la kheri katika masuala ya uendeshaji wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende katika suala la ufutaji wa kodi. Tumeona kuna mambo mengi sana ambayo yamefutiwa kodi zake. Yapo yale ambayo yalipandishwa kodi zake kama masuala ya urembo kama vile nywele. Kwa kweli hili ni suala zuri kwamba Mheshimiwa Rais anataka tuwe *natural*. Kwa hiyo, hili suala nalichukulia kwamba ni zuri kidogo kwa sababu naamini kwamba haya masuala yatakapopandishwa kidogo kodi tutazidi kuwa *natural*, tutazidi kuwa wazuri na uhalisia wetu watazidi kuuona. Kwa hiyo nipongeze sana suala hili ambalo litaleta tija kwa watu wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata wewe tunakuona hapa uko *natural*, kwa hiyo naamini kwamba ni jambo zuri la kuiga na ni jambo zuri ambalo hata wewe unatupa mfano na unapendeza. Kwa hiyo hili ni suala zuri na tuwapongeze kutaka kutupeleka huko kwa njia rahisi hii ya kupandisha haya mambo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pia nipongeze sana kwa kufuta asilimia 40 ya tozo katika mashine za *EFD*. Hili ni jambo zuri kwa sababu wafanyabiashara wengi walikuwa wanalalamika kuhusu suala la ulipaji au ununuaji wa hizi mashine, lakini sasa hivi baada ya kufuta hizo tozo, naamini kwamba wafanyabiashara watakwenda kununua mashine zile na wataweza kuzitumia bila malalamiko, kwa sababu tunafahamu kwamba ukinunua unatakiwa udai risiti na ukiuza unatakiwa kutoa risiti. Kwa kauli mbiu hii ya *TRA,* naamini sasa inaenda kufanyika kiurahisi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zulfa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nampa taarifa tu Mheshimiwa Zulfa kwamba lengo la Serikali kuweka kodi kwenye hizi nywele bandia; mosi; ilikuwa ni kuhakikisha kwamba inalinda viwanda vya ndani. Hapa tunavyoongea kuna viwanda vya ndani ambavyo vinazalisha hizi nywele bandia. Sasa kwa kauli anayoitoa Mheshimiwa Zulfa ambaye amesema ni balozi wa kodi, akihamasisha watu wawe *natural* ina maana vile viwanda vyote vya ndani vitakufa na Serikali itakosa kodi, sasa sijui huo ubalozi utaenda wapi.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kumpa taarifa hiyo tu. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zulfa unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ZULFA MMAKA OMAR:** Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba viwanda vya ndani vinakusanya kodi, lakini sasa nirudie kumwambia dada yangu kwamba *natural* ni bora kuliko kwenda huko ambako anafahamu yeye. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, naona Mheshimiwa Zulfa anataka kunikatishia jitihada na juhudi zangu.

Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Twaha Mpembenwe na atafuatiwa na Mheshimiwa Janejelly Ntate na Mheshimiwa Jerry William Silaa ajiandae.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bajeti yetu hii na Hali nzima ya Uchumi wa Nchi. Kabla sijaanza kuchangia bajeti hii naomba kwanza nichukue fursa hii kwa heshima, taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaendelea kuifanya katika Taifa hili ili kuleta maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda moja kwa moja katika kuchangia bajeti hii nilikuwa naomba…

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha samahani kidogo, uniwie radhi, kaa kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, samahani, kuna wageni ambao natakiwa niwatangaze ili waweze kwenda kuendelea na ratiba zingine. Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 150 na Walimu 10 kutoka Shule ya *Macedonia Nursery and Primary School* ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana Bungeni, karibuni sana Dodoma na tunawatakia kila la heri katika masomo yenu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Twaha Mpembwene.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba niendelee nilipoishia, naomba

nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaendelea kuifanya katika Taifa hili. Sambamba na hili kabla sijachangia bajeti hii sina budi kuzungumza yale mazuri ambayo Mheshimiwa Rais ameweza kuyafanya mpaka hivi sasa na hasa nataka nizungumze miradi mikubwa mikubwa.

Mheshimiwa Spika, katika miradi mikubwa mikubwa ambayo Mheshimiwa Rais aliweza kuirithi kutoka kwa *predecessor* wake tunazungumzia Mradi wa Rufiji *Hydroelectric Power*, mradi ule fedha zipo, mkandarasi yupo *site* na shughuli zinaendelea. Sambamba na hilo, kuna Mradi ule wa SGR Dar es Salaam – Morogoro pamekamilika, Morogoro – Dodoma pako vizuri, Dodoma – Makutupora kwenda Tabora, Mheshimiwa Rais tayari ameshaini mkataba wa trilioni 4.41 na hivi ninavyozungumza shughuli zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sio hivyo tu, katika barabara kubwa kubwa zile na madaraja Mheshimiwa Rais ameweza ku-*sign off certificate* ya mwisho na kumlipa mkandarasi na amefungua Daraja la Tanzania pale Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, sio hivyo tu lakini marafiki zangu, wajomba zangu kule Wasukuma pale Busisi -Kigongo daraja lile linaendelea kujengwa na shughuli zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amekwenda mbali zaidi, katika suala zima la usafirishaji wa anga, tayari amesaini mkataba wa kununua ndege tano zikiwemo mbili zile kubwa kubwa na mambo mazuri yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, niliona ni vema kuyazungumza haya kwa sababu Mheshimiwa Rais ameweza ku-*prove doubt as wrong*, kuna wengi walikuwa na wasiwasi kwamba itakuwa vipi, lakini kwa kufanya hivyo tu, Mheshimiwa Rais amekwenda mbali zaidi, ameanzisha miradi yeye mwenyewe ambayo miradi hiyo historia yake ni ya ajabu sana, niseme tu katika moja kubwa ambalo Mheshimiwa Rais amelifanya ni kusaini mkataba wa *LNG* trilioni 70, fedha ambazo kwa namna moja au nyingine ni historia ambayo itaendelea kukumbukwa ndani ya Taifa hili. Nani kama Mama Samia?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee mbele. Naomba sasa nijikite katika bajeti hii. Bajeti hii malengo yake makubwa ni matatu. Lengo la kwanza ni kuweza kufufua uchumi; lakini lengo la pili ni kuboresha sekta za uzalishaji na lengo lingine ni kuhakikisha kwamba bajeti inakwenda kusaidia kasi ya maisha.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli ulio wazi kabisa, hakuna ambaye anapinga, dunia imekumbwa na msukosuko mkubwa katika suala zima la mambo ya kiuchumi, tukianza na suala zima la *corona* na vile vile katika vita vinavyoendelea hivi sasa. Kwa tafsiri hiyo maana yake ni nini? Ni kwamba gharama za maisha zimekuwa kubwa sana duniani sio Tanzania tu. Bajeti hii naomba niseme tu, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, inamfanya awe *very popular Finance Minister* japokuwa mwenyewe huwa anasema kwamba hii bajeti inamfanya asiwe *popular Finance Minister*. Kwa tafsiri hiyo maana yake ni nini? Imemfanya kuwa *very popular Finance Minister* kuliko kumchukua mtendaji fulani akampeleka katika timu

fulani ambayo haipo hata katika kumi bora Barani Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee mbele, bajeti hii imekwenda kugusa maeneo makubwa mawili; katika *level* ya kwanza kwenye *level* ya *micro economy* na *level* ya pili katika *micro economy* Kitaifa zaidi. Ninapozungumza katika eneo la *micro economy*, bajeti hii ni bajeti ya wananchi kweli kweli kwa sababu:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameweza kuongeza mishahara kwa watumishi na sasa hivi tunakwenda kuzungumzia asilimia 23. Hili ni jambo la msingi sana. Tunajua gharama za maisha zimeongezeka, kwa tafsiri hiyo hiyo ni lazima vile vile tuweze ku-*mitigate* na mambo mazima ya mshahara na hilo limefanyika katika bajeti hii. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, bajeti hii vile vile imekwenda kugusa wananchi wa kawaida sana, nini maana yake? Hivi tunavyozungumza wanafunzi wanakwenda kusoma bure *form five and six*. Hii inatuambia kwamba, sasa sisi Watanzania kwa raha zetu. Kazi yetu ukipata mtoto, hangaika naye kulea mpaka miaka saba, akitoka hapo darasa la kwanza mpaka la saba bure. Akitoka hapo *form one* mpaka *form four* bure. Akitoka hapo *form five* mpaka *form six* bure. Akitoka hapo kwenda Chuo Kikuu kuna fedha bilioni mia tano na sabini Mheshimiwa Rais ameziweka zinasubiri vijana kwenda kuchukua mikopo, nini maana yake? Maana yake ni kwamba, wanafunzi kutoka Mbeya, wanafunzi kutoka Songwe, wanafunzi kutoka Handeni, wanafunzi kutoka Kibiti, wanafunzi kutoka Mtama kwa Wamakonde kule, wote wanakwenda Chuo Kikuu bila shida yoyote nani kama Mama Samia. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee mbele, bajeti hii katika mambo mengine makubwa na mazuri ambayo imeweza kuyafanya imekwenda vilevile kugusa katika ngazi ile ya *micro* Kitaifa zaidi. Tafsiri hiyo maana yake ni nini, Mheshimiwa Rais amekwenda mbali zaidi, katika Sekta nzima ya Kilimo na inajulikana wazi kabisa Tanzania asilimia 65 tunategemea kilimo. Pale Mheshimiwa Rais amekwenda kutumbukiza fedha takribani shilingi bilioni 954, nani kama Mama Samia. Kwa kufanya hivyo tafsiri yake ni nini, tunakwenda sasa kuboresha sekta nzima ya mambo ya uzalishaji. Kwani tunajua kule kwenye kilimo ndipo tutakapokwenda kupata malighafi ambazo zitakwenda kusaidia kuzalisha *products* nyingine zikiwepo vilevile za mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Mheshimiwa Rais ameenda mbali zaidi katika kuhakikisha kwamba tunakwenda ku-*protect* viwanda vyetu vya ndani, amefanya jambo kubwa sana, kuna baadhi ya bidhaa ambazo zimekwenda kuongezewa tozo. Kwa kufanya hivyo nini tafsiri yake? Tafsiri yake ni kwamba, tunakwenda ku-*discourage importation* na kwa maana hiyo tunakwenda ku-*stimulate* uchumi ndani ili wazalishaji wetu waweze kuendelea. Kwa tafsiri pana ya kiuchumi maana yake ni nini, wale waliosoma *commerce* wanajua, hapa kinachokwenda kufanyika tunakwenda kufanya *mitigation* kwenye *balance of trade* ili twende kwenye *balance of payment*. Nimwambie tu Mheshimiwa Mwigulu, bajeti hii ni bajeti ya kisayansi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee mbele. Pamoja na yote haya naomba niweke nukta zifuatazo vizuri zaidi. Mheshimiwa Waziri wakati ana-*present* bajeti hapa alizungumza suala la vijana wenye miaka 18 waanze kulipa kodi. Niki-*quote* hapa kwa ruhusa yako, kwenye chombo kimoja cha habari cha *Global Publish* kinasema, samahani na-*quote:*

"*Waziri Mwigulu - kila Mtanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 kuanza kulipa kodi*".

Mheshimiwa Spika, hii imeweza kuleta tafaruku kubwa katika mitandao, lakini Serikali na Mheshimiwa Waziri kwa nini namwambia bajeti hii imemfanya awe *very popular Finance Minister*, hapa kinachoenda kufanyika siyo kwamba mwanafunzi akifika umri wa miaka 18 alipe kodi. *Determine factor* hapa tunayoizungumza ni suala zima la kipato. Kwa hiyo kwa tafsiri hiyo, nilipa bahati ya kuishi kwa Wamakonde pale Uingereza, wao wanachokifanya, unapofika umri wa miaka 18 unapewa kitu kinachoitwa *National Insurance Number Card*, nini tafsiri yake? Tafsiri yake ni kwamba unapokuwa tayari ume-*graduate* umemaliza masomo, unapokwenda kufanya kazi tayari mfumo unakufahamu na hiki ndicho kilichoweza kufanyika katika bajeti hii. Kwa hiyo naomba niliweke hili liwe wazi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na haya yote, naomba vilevile niweze kuweka nukta nyingine sawa na nukta hii ninayoiweka sawa ni nukta inayohusiana na suala zima la *Royal Tour*. Mheshimiwa Rais amefanya kitu kikubwa sana katika kuifungua Tanzania, kwenye *Royal Tour* tunajua kwamba tunakwenda kupata mapato makubwa sana kule katika suala zima la utalii. Naiomba tu Serikali, Wizara husika zote lazima ziweze kuchukua nafasi yake, *royal tour*

kama *royal tour* siyo kazi peke yake ya Wizara ya Utalii; Wizara ya Ardhi lazima sasa muweze kuhakikisha mnakwenda kupima ardhi katika maeneo husika ili wawekezaji wanapokuja siyo wanakwenda kwa Mwenyekiti wa Kijiji kwenda kuomba ardhi kwa ajili ya kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, kama hivyo haitoshi, Wizara vilevile inayohusiana na mambo ya Miundombinu lazima wahakikishe kwamba wanakwenda kufungua miundombinu katika sehemu tofauti, siyo mwekezaji anataka kwenda kuwekeza katika maeneo kama Kibiti maana yake Mukuranga sasa hizi kumeshajaa viwanda, watu wanaanza kuhangaika na mambo ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si hayo tu katika Sekta nzima ya mambo ya Mawasiliano, pale ni lazima tuhakikishe tunakwenda kuweka mikonga ambayo itatusaidia. Wawekezaji watakapokuja siyo waanze kusumbuka, mtu kwenda kupiga simu anaenda kupanda katika mti halafu anaanza kupiga simu. Kwa kusema hivi niseme tu, Wizara husika lazima wayaangalie haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, vilevile Wizara ya Nishati lazima wawe makini kuhusu kupeleka umeme kwenye sehemu husika. Wawekezaji wanapokuja siyo tena tuanze kuhangaika kuchukua majenereta na kuanza kuwasha umeme.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya, naomba niweke jambo vizuri sana na hili ndiyo la msingi kwelikweli. Pamekuwa na chokochoko kidogo zinaendelea katika mitandao ya kijamii na suala hili linahusiana na suala zima la mambo ya Ngorongoro.

Kwanza naomba niipongeze sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweza kutenga eneo kwa wenzetu ambao wameamua kuhama kwa hiari kwenda kuishi katika maeneo ya Handeni.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, naomba niongee kwa dhati kabisa, sisi Watanzania wote kwa ujumla wake tunajua wafugaji waliopo katika eneo la Ngorongoro ni Watanzania wenzetu na hatukubali waweze kupata shida, lakini pia tunajua Serikali kama Serikali ina nia nzuri kabisa ya kulitatua tatizo hili *amicably*. Kwa hiyo naomba nisisitize, wale wenzetu majirani katika kipindi cha mwaka 1974 mpaka 1978, wakati huo akili yangu ilikuwa inafanya kazi, zilianza chokochoko kama mzaha hivihivi, kuna watu fulani fulani walikuwa wanataka kuchukua mipaka yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima kwa Kanuni zetu sitoweza kutaja jina la nchi yoyote ile, lakini niseme tu wale majirani zetu ambao wanajaribu kutuingilia katika mambo yetu ya ndani, wakome mara moja, hii hakubaliki. Hii ni Tanzania, sisi tuna uwezo wa kuamua mambo yetu ya ndani, hatuhitaji msaada wa kutoka sehemu nyingine yoyote ile. Inashangaza sana leo hii ukiangalia kwenye mitandao huko utakuta kabisa kwamba kuna maandamano yameandaliwa katika maeneo fulani ya majirani zetu. Sitaki kutaja jina, lakini niseme tu vita hii ni vita ya kiuchumi, Watanzania tuamke, Watanzania lazima walielewe hili, tuweze kushikamana na wenzetu waliopo Ngorongoro, tuweze kuisaidia Serikali ili tuweze kutatua matatizo yaliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge niwaombe Mawaziri mliopo muwape taarifa Naibu Mawaziri na Mawaziri walioko Dodoma waje Bungeni. Hoja ya Bajeti ni Bajeti Kuu ya Serikali na zinajadiliwa hoja za kila Wizara na kila Wizara itapewa fursa ya kujibu hoja zake kwenye hoja hii. Kwa hiyo, Waheshimiwa Mawaziri mliopo, naomba muwaite Naibu Mawaziri na Mawaziri waliopo Dodoma ambao hawana ruhusa ya kutokuwepo Bungeni, lakini pia hawajasafiri na Mheshimiwa Rais wala hawajasafiri kwenda popote waje Bungeni. Bajeti Kuu ni Bajeti ya Serikali yote na kila mtu achukue hoja zinazomhusu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Janejelly James Ntate, atafuatiwa na Mheshimiwa Jerry William Silaa na Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, ajiandae.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu ndiyo ananipa uwezo wa kusimama hapa leo kuongea.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru pia Mheshimiwa Rais ambaye ndiye Kiongozi wa Chama Cha Mapinduzi kwa kuja na Sera ya kupunguza ada kwa wanafunzi wetu wa *form five* na *form six*. Vile vile nampongeza kwa kuangalia maslahi ya watumishi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara ya Fedha, wamekuja na Bajeti ambayo ni nzuri, bajeti inayogusa wananchi, bajeti ambayo imeangalia kila kona na bajeti ambayo inaenda kuleta maendeleo. Pamoja na kuja na bajeti nzuri nitakuwa na ushauri katika bajeti hii. Nianze na ushauri waliokuja nao wa kupunguza mishahara ya

watumishi wale wanaokuwa wamepewa vyeo vya madaraka, kwamba madaraka yanapotoka mshahara wake uondolewe. Hili kwa kweli halitaleta tija bali linaenda kuleta mgogoro kati ya watumishi na Serikali yao. Wanakwenda kumletea mgogoro Mheshimiwa mama Ndalichako na Vyama vya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Sheria ya Utumishi Na.8 kifungu cha 3 kinaongelea mishahara ya mtumishi na haki zake za kimshahara. Ndiyo maana tukihamisha mtumishi kutoka Taasisi, tunajua Taasisi zina mishahara mikubwa, tukimleta Serikalini huwa hatupunguzi mshahara wake, anaendelea na mshahara wake binafsi, lakini kwa hawa wateule tunasema tuwapunguze mishahara. Hapa naomba nishauri kitu cha kufanya, kaumri kangu haka ni Serikali ya Awamu ya Kwanza ndio sijafanya nao kazi, lakini Serikali zilizobaki zote nimefanya nazo kazi. Zamani uteuzi wa *District Executive Directors*, *District Administrative Secretaries* na *Regional Administrative Secretaries*, uteuzi wote walikuwa wanaenda kwa watumishi ambao wameshakomaa ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mtumishi alikuwa akifika cheo cha Muundo cha mwisho *Principal* Serikalini, mnaanza kumtania kwamba wewe subiri mwenye mamlaka akuone, kwa sababu hawezi kwenda popote na huyu ameiva kabisa, lakini tuangalie sasa hivi tunawatumia? Hatuwatumii. Kwa hiyo unakuta mtu anaweza akateuliwa kuwa *DED* au *DAS* amemaliza Chuo Kikuu tu, hajapata uzoefu ndani ya Serikali, huyu akienda lazima mambo hayatakwenda vizuri na huyu akirudi sasa ndiyo hawa Wakurugenzi Mheshimiwa Waziri ametaja kwamba tunao 300, wamekuja kwa muundo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zamani hawa wateule, walikuwa wanachujwa na Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ndiyo kazi yake kuchuja hawa wateule na walikuwa wakienda wanafanya kazi kwelikweli, lakini hawa tunaopeleka sasa hivi watu wamekuwa wateule wa Mheshimiwa Rais. Unakuta *DC* anamwambia *DED* mimi ni mteule wa Rais, *DED* naye anamwambia mimi ni mteule wa Rais, kazi zinaanza kushindwa kwenda hapa. Sasa ili waweke vizuri lazima mmoja atapigwa chini, sasa huyu anayepigwa anaongeza idadi hiyo ambayo Mheshimiwa Waziri amekuja nayo.

Mheshimiwa Spika, sasa leo tunasema tuanze kuwashusha mishahara, kushusha mshahara mtumishi inatakiwa uunde Tume, umfungulie mashtaka, Tume ije na majibu kusema anatakiwa kati ya adhabu tatu apate mojawapo. Moja huwa ni kushushwa cheo ambayo mmeshampa sasa, mmepiga chini; pili ni kupunguziwa mshahara na tatu ni kufukuzwa kazi. Sasa hizi adhabu tunazoenda kuwapa za kuwapunguzia mishahara Tume gani tumeunda ikakwambia huyu anafaa kupunguziwa mshahara. Hapa naomba Serikali iliangalie kwa mapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imesema viongozi wakopeshwe magari, nakubaliana nalo kabisa, lakini tunaweza tukaenda kupoteza viongozi. Awamu ya Tatu ilijaribu wakakopeshwa magari lakini tulipata ajali nyingi sana za viongozi. Anatoka Ofisini amechoka anajiendesha kurudi nyumbani anagonga, saa zingine anawaza Mkuu wake wa Kazi kashampa mikakati ya ajabu, ataifanyaje mwisho wanagonga magari. Tuliwahi kumpoteza Kamishna mmoja alikuwa Kamishna wa Madini, kwa ajali ya kutoka usiku kazini, tuliangalie nalo kwa mapana.

Mheshimiwa Spika, pia imesema *CAG* wanamwongezea nguvu. Twende tuangalie hayo matumizi, tuwabane kwenye matumizi, tuwabane kwenye manunuzi, ndiko kunakoharibu fedha nyingi ya Serikali, lakini siyo kusema kwamba tuwape magari, tuliwapa halafu baadaye tukaendela kuwapa magari ya Serikali, hapo sioni kama tutaweza kwenda napo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishauri kwenye ukusanyaji wa mapato. Tumeangalia tu ukusanyaji wa mapato, lakini tumejisahau kwenye maduhuli ya Serikali na haya ndiyo makubwa zaidi na hapo ndipo tunapopoteza mapato. Maafisa Masuuli wetu wamepewa mamlaka ya kusimamia matumizi, lakini kwenye mapato wanapasahau. Sasa sijui utasimamiaje matumizi kama hutafuti hayo mapato ili uje kuyatumia. Niishauri Serikali tu Mlipaji Mkuu wa Serikali aingie mikataba na Maafisa Masuuli ya kukusanya maduhuli, asipofikia kiwango cha kukusanya, basi matumizi wasimpe, kwa sababu hakusanyi anachotaka kuja kutumia na mianya inayoleta maduhuli haya yasikusanywe ipo mingi.

Mheshimiwa Spika, twende kwenye *pass* za kusafiria, *passport* ambayo ni haki ya kila Mtanzania kuipata nchini humu, angalia utaratibu wake wa kuitafuta, unajaza mafomu, ukijaza ukifika Uhamiaji kwenye *counter* pale, unakutana na Maafisa wanakwambia hii *font* uliyotumia, mjazo uliojaza siyo wa kiuhamiaji, rudi ukaanze upya, lakini wanakuelekeza nenda hapo nje. Ukienda Kurasini pale nje, *stationery* zipo kama uyoga, Ofisi za Wanasheria zipo kibao, unaenda kuanza upya. Sasa kuanza upya kama huyu raia hana safari anarudi nyumbani anaachana navyo kwa sababu alishapanga Sh.20,000 ya

Mwanasheria mara ya kwanza amelipa imeharibika, kulipa tena hawezi na muda wake unapotea.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napiga hesabu kidogo tu ya kujumlisha na kutoa, Watanzania 2,000,000 wakirudi nyumbani bila kuendelea na *pass* hizo 50 mara 2,000,000 tunapoteza bilioni 100 hapo za maduhuli zinaondoka, lakini sasa aliyepenyeza akapata hiyo *passport* ikiisha, akirudi anaanza utaratibu uleule wa usumbufu, lakini hii si ni elektroniki, ukiweka kitambulisho changu cha *NIDA* si unaona rekodi zangu zote. *TRA* wanawezaje, mbona ukienda leseni imeisha, wakiweka ile leseni, wanatoa wanakuona rekodi zako, unalipa 70,000 wanakupa leseni yako mpya unaondoka. Huku kwenye *passport* tunashindwaje, kuweka ile *NIDA* tukaona rekodi za huyo raia, tukampa *pass* yake ya kusafiria. Kwa hiyo sasa *pass* imebaki siyo Sheria ya Kikatiba kwamba tuna haki ya kumiliki *pass* za kusafiria, imebakia unaitafuta wakati unataka kusafiri. Hapa ukitupa safari ndiyo tutahangaika kutafuta *pass* kwa sababu unaona unahangaika bure, hapo tunapoteza mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuje *NIDA*, *NIDA* napo kuna mapato yanapotea kwa kuzungusha raia kupata vitambulisho vya *NIDA* na penyewe ukichukua tu watu 2,000,000 waone huu usumbufu waache waende pembeni, kwa 20,000 tunapoteza bilioni 40, hapo ni kwenye *NIDA* napo pia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, niongeze dakika mbili tu nimalizie.

**SPIKA:** Mbili utakuwa unampunguzia mwenzako mwenye muda wake, sekunde 30 malizia sentensi.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Twende kwenye *NIKONEKT* ya *TANESCO* waliyoanzisha, si rafiki kwa raia. Napeleka kadi ya *NIDA* wanaweka namba, lakini ile fomu ina maswali, inakuuliza mpaka babu wa bibi yako. Babu wa bibi yako nani? Jina lako nani? Shule ya msingi umesoma wapi? Wakiweka namba za *NIDA* si wanaona hivyo vitu. Naomba wafanye hii mitandao yote isomane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga hoja mkono, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jerry William Silaa, atafuatiwa Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, tutamaliza na Mheshimiwa Judith Kapinga.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu kwenye hii Bajeti Kuu na nianze mchango wangu kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa bajeti nzuri. Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara ya Fedha, bajeti hii imeenda kujibu vilio vingi vya Watanzania na niseme naipongeza sana.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Serikali kuondosha ada ya kidato cha tano na cha sita kimeenda kujibu vilio

vya wananchi wengi. Mimi mwenyewe binafsi yuko kijana mmoja, mjukuu wa mama mmoja maarufu kule tulikokulia, marehemu Kibibi ilikuwa nimlipie ada wiki hii, kwamba kauli hii na mimi mwenyewe hela yangu imepona, naipongeza sana Serikali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi kwenye kilimo, mifugo na uvuvi inaenda kuwatengenezea Watanzania maeneo mengi zaidi ya kujishughulisha kwenye shughuli zao na sasa tunaenda kupata matokeo chanya kwenye Sekta ya Kilimo, kwenye Sekta ya Mifugo na Sekta ya Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza nitakalolisemea ni eneo la kodi na mimi nimpongeze kidhati Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kauli yake aliyoitoa pale Bukoba kwenye ziara yake ya Mkoa wa Kagera. Kauli ile imepokelewa vizuri sana na wafanyabiashara wa nchi hii. Kumekuwa na dhana na tumekuwa tukisema hapa kwamba Serikali kwa kukusanya kodi anajikuta ni mbia asiyechangia mtaji kwenye biashara ya Mtanzania. Kwa hiyo tumekuwa tukiishauri sana Serikali ukusanyaji wao wa kodi, taratibu zao za makusanyo ziwe rafiki na elimu itolewe kwa wafanyabiashara na wasitengeneze dhana ya kugombana na wafanyabishara na kufunga biashara zao. Kauli ile ya Mheshimiwa Rais yuko rafiki yangu mmoja ambaye najua kabisa hata mimi hakunipigia kura mwaka 2020 alinitumia *speech* ile na akaniandikia Mama Samia Suluhu Hassan amepata kura yangu 2025.

Mheshimiwa Spika, niiombe sana Serikali, niwaombe sana *TRA* waende wakatekeleze maagizo yale. Tuliongea hapa, wako wafanyabiashara wadogo hawa *presumptive tax regime* ambapo naona sasa hapa tena wamewekewa asilimia 3.5 ya *turn over*. Asilimia 3.5 ya

*turn over* siyo hela ndogo, lakini hawa ndiyo wenye mitaji ya Sh.1,000,0000 au Sh.500,000, unapomwambia aende akanunue mashine ya Sh.500,000 ni ngumu kuweza kutekelezeka. Sasa kama Serikali ni mbia wa kodi ni lini Serikali itaona ni wajibu wake kumpa mtu mashine ya *EFD* bure ili mashine ile sasa iweze kuweka rekodi za kodi Serikali iweze kupata kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yako marekebisho mengi ya kodi ambayo Serikali imeelekeza yafanyike. Nitachangia kwa uchache na nadhani nitachangia vizuri kwenye *Finance Bill*. Unapoweka *withdrawing tax* ya asilimia mbili kwenye *small scale miners*, maana yake unaongeza pale ilipokuwa *loyalty* na ile *inspection charge* ya asilimia sita na moja sasa unaenda kwenye asilimia tisa.

Mheshimiwa Spika, as *we speak right now* dhahabu nyingi inayochimbwa na wale wachimbaji wadogo wale wa kushika na *mercury* inatoroshwa nchini. Unapoongeza kodi Serikali hamuendi kuongeza mapato mnakwenda kuongeza utoroshaji wa dhahabu na ziko nchi zinanufaika na utoroshaji huo. Mwaka jana hapa iliwekwa *withholding tax* kama hii kama kwa wakulima, Bunge la mwezi wa Agosti liliiondosha. Sasa niwaombe sana Serikali tusingoje tufanye jambo tupate kilio, tuje tena kubadilisha sheria wakati jambo tunaliona halitatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, muda ni mchache lakini ukichukua *turn over* za *corporates* kubwa Tanzania *Breweries Limited*, *Vodacom Tanzania, TIGO* ukaangalia na *corporates tax* wanayolipa ni chini ya hiyo asilimia 3.5. Mwaka huu wa fedha *Vodacom ime-declare loss*, *TIGO wame-declare loss,* kwa hiyo hawajalipa *corporate tax*, unapotaka hawa *presumptive tax measure* walipe 3.5

*percent* ya *gross* huendi kuwatendea haki na nadhani utekelezaji wake utakuwa ni mgumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu Serikali niiombe na niishauri iongeze nguvu kwenye *communication*. Tulikwenda kule Amani Muheza kwa Mheshimiwa MwanaFA tulikuta wale wasafirishaji wa vipepeo wanaathirika na lile katazo la Serikali la kusafirisha wanyama hai nje *as if* wanyama simba wanafanana na vipepeo. Juzi Serikali ikatoa kauli hapa kauli, nilivyoielewa ni kusaidia wale wa vipepeo na wale wanaoshika mijusi na wanyama wengine wadogo wadogo, lakini kwa sababu haikuwa *communicated* vizuri ikatengeneza taharuki, Waziri naye alivyopata taharuki akajaa upepo, akafuta lile agizo. Kwa hiyo, wale waliokuwa wanasherehekea maskini wa Mungu wale *Conservators* wa misitu wa kule Amani ambao wanasaidia kutunza misitu kwa ajili ya vipepeo na wao wamerudi tena kwenye *back to square one* 2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hili la *TIN Number,* kwa tabia za *TRA* za ukusanyaji wake wa kodi ukimwambia mwananchi naye apewe *TIN Number* lazima ataruka kimanga, anajua tunarudi kule kule wanakofanyiwa wafanyabiashara, sasa tutafanyiwa Watanzania wote. Naomba Serikali ifanye *communication,* ielimishe wananchi na ndio maana Mheshimiwa Twaha amesema ziko nchi zinaita *Insurance Number*, ziko nchi zinaita *Social Security Number,* kikubwa Mtanzania leo tunavyozungumza hapa alipo mwenyewe ni mlipakodi. Anaponunua pembejeo ile *transaction* inatakiwa ilipiwe kodi, anapolipa nauli kwenye daladala, anapopanga chumba, anaponunua chakula zote zile ni *transaction* za kibiashara ambazo huyu mwananchi angekuwa na

namba yake zingeingia kwenye taarifa zake. Tunapoongelea *universal worthy insurance* ndio atajikuta ametumia kiasi gani kwa mwaka apate bima ya maisha yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa wanaiweka *TIN Number* limebutuka huko la kwao hilo, kazi yao kwenda kuelimisha wananchi kwamba namba hii ya *NIDA* ikitumika kuweka miamala yako inakusaidia wewe mwenyewe, kama tunagawa pembejeo za ruzuku tunajua wewe ni mnunuaji mzuri na matumizi yako na kilimo chako upate pembejeo. Sasa naamini Serikali italifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kifupi, niombe mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, niombe na niipongeze Serikali imemwongezea fedha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali *(CAG)* kukagua matumizi ya Serikali. Imepokea ushauri wa Kamati ya Bunge, imeongeza meno kwa *Internal Auditors* kusimamia matumizi. Sasa niiombe iendelee kupokea ushauri wa kuweka mifumo ya TEHAMA. Mifumo ya TEHAMA ndio itasaidia kupunguza matumizi ya Serikali na mifumo hii ya uangalizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nia yangu ni nini? *Let the Government be the Government*, *let corporate be corporate and let the Parliament be Parliament*. Huwezi ukaendesha Serikali kama shirika la kibiashara *this is not a profit-making organization,* yaani leo Kamishna wa Ardhi akopeshwe *Prado* akitaka kwenda kukagua mgogoro wa ardhi anajiendesha mwenyewe, haitakaa itokee. Tusipende kutengeneza vitu ambavyo vitatengeneza mkwamo kwenye utendaji wa Serikali. Serikali ijiendeshe, matumizi yabanwe, *controls* ziwepo, mifumo iwepo, lakini

uendeshaji wa Serikali ni ngumu kulinganisha na sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kifupi kwenye *custom duty,* matairi ya bodaboda yameongezwa toka asilimia 10 mpaka asilimia 25. Kule juu wakulima tumewaangalia, wafugaji tumewaangalia, wavuvi tumewaangalia, hebu tuwatambue na hawa bodaboda na wenyewe kama Watanzania na tupunguze kodi kwenye matairi ya bodaboda kwa sababu uendeshaji wa bodaboda sio anasa bali na yenyewe ni ajira kama eneo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko eneo Serikali *ina-propose* kupunguza mikopo ya halmashauri ya asilimia 10, ambayo ni mikopo inayokopesha makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, eti ibaki asilimia tano. Tunawathamini sana Wamachinga na sisi ni wapiga kura wetu kule mijini, Serikali itafute mahali kwingine fedha ya kujenga miundombinu lakini sio kwa Wamachinga. Mikopo hii asilimia 10 ibaki, hapo ilipo yenyewe haitoshi, kama mnavyogawa pembejeo bure kwa wakulima na sisi wa mjini mikopo hii inasaidia wapiga kura wetu. Hili naomba kushauri na hatutokubali lifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona *hotel levy* ilikuwa asilimia 20 imekuja asilimia 10 inakwenda asilimia tano. *Hotel levy* ilikuwa ni suluhu ya wale wanaokimbia *VAT* asilimia 18, wanakuja kwenye *hotel levy* na ndio maana *ika-balance* kwenye asilimia 20, haya ni mapato ya *Local Government,* naomba tuyaangalie.

Mheshimiwa Spika, vile vile niombe jambo moja *property tax* ilichukuliwa ikapelekwa *TRA* haikukusanywa

na taarifa ziletwe hapa, haikuwahi kukusanywa *effective* kama mamlaka za Serikali za Mitaa zinavyokusanya. Mwaka jana wakachukua wakapeleka kwenye LUKU, nyumba ya Masaki inalipa Sh.1,000 kwa mwezi Sh. 12,000 kwa mwaka. Niombe kwenye bajeti hii kodi ya majengo irudishwe kwenye halmashauri, ikirudishwa kwenye halmashauri itengenezwe *retention scheme* asilimia tano ibaki kwenye mtaa, asilimia tano ibaki kwenye kata, isaidie uendeshaji, isaidie mafunzo, ujenzi wa ofisi, posho za Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji na za Madiwani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tusitengenezeane fitina ya kisiasa kwa jambo ambalo linawezekana kwa kudhani mishahara ya Madiwani inatakiwa kutoka Serikali Kuu; na kama Serikali haina uwezo basi isijibu suala hilo wakati maeneo mengine wanafanya. Fedha hazikusanywi, hawa viongozi wanatakiwa kuwa ni chachu ya ukusanyaji wa mapato ukisoma *Local Government Authority Act* na Kanuni za Kudumu za Halmashauri, Madiwani wanapaswa kuwa ni watu wa kuchochea maendeleo na kusimamia shughuli za kijamii kwenye maeneo yao. Waturejeshee kodi ya majengo, watuwekee malengo, mifumo ya kukusanya ipo watuwekee *retention scheme*. Kuna kata zitanunua magari, zitajenga ofisi za magorofa, zitalipana posho, kuna Kata na Mitaa wananchi wataacha kutozwa Sh.1,000 za barua kwa fedha itakayobaki kwenye maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda la mwisho na sio kwa umuhimu hizi kodi ndogo ndogo mara kwa king'amuzi, mtu kashachoka kashatumika siku nzima, karudi nyumbani anataka kuangalia mpira wake wa Yanga anaambiwa king'amuzi tena kilipiwe na tozo. Niombe

sana tutengeneze mifumo ya kodi ambayo ni rafiki inayoweza kukusanyika kirahisi ambayo itasaidia Watanzania wapende kodi na wapende Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Judith Kapinga na kama muda utakuwepo Mheshimiwa Jafari Chege.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara hii. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja, lakini niipongeze sana Wizara, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa jinsi alivyoitengeneza hii bajeti, inaonekana hakika ni bajeti ya Watanzania. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jambo jema alilolifanya la kuongeza elimu bure mpaka kidato cha sita. Hii inaonesha ni jinsi gani Ilani ya CCM inavyotekelezwa na ziada maana huu hakika ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, lakini ni jinsi gani Mheshimiwa wetu Rais anaonesha anawajali Watanzania na hasa akinamama, maana akinamama ndio wenye mzigo mkubwa ndani ya familia. Hili jambo ni zuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niishauri Serikali kutokana na suala hili zuri liongezeke pia suala la ajira kwa Walimu ili wawe wengi kwa ajili ya kuleta tija kutokana na hii elimu bure. Isije tu ikawa elimu bure lakini madarasani Walimu hawatoshi. Ni wananchi wengi sana ambao hawana ajira wako mtaani, kutokana na suala hili mimi ninaamini kabisa Serikali imelenga huko huko, japokuwa tu tunashauri na sisi kama Wabunge, lakini naamini kabisa

lengo la Serikali pia hapa ni kuongeza ajira kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee pia suala kama aliloongea Mheshimiwa Mbunge mwenzangu kuhusiana na hili suala la asilimia 10. Serikali iangalie sehemu ya kutoa hii fedha asilimia hii kwa ajili ya shughuli inayotakiwa kufanyika. Ni jambo zuri na ni jambo jema, lakini naamini kabisa wajasiriamali wengi mtaani ni vijana, akinamama lakini pia wamepunguza idadi ya mambo ambayo yangefanyika hasa kwa hawa vijana ambao wanajiajiri wenyewe ambao labda wangefanya uhalifu, uharibifu, lakini wamejiajiri kutokana na hii mikopo midogo midogo.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali ikiwaondolea tena hii asilimia itabaki nini kwa maana moja au nyingine ile asilimia waliyokuwa wanapata vijana asilimia nne akinamama asilimia nne na walemavu asilimia mbili na hapo sasa hatuoni kitu cha kubaki. Sidhani kama mimi ni mmojawapo wa ku-*support* suala hili. Kwa kweli tuiombe Serikali iondokane na wazo hili la kuondoa hii fedha ibaki pale pale na ikiwezekana bajeti ijayo wawaongezee, hii fedha ni kidogo sana haitoshi, huko mtaani watu hawana ajira na wamejiajiri wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende pia kwenye suala la kumpongeza sana mama yangu Mheshimiwa Rais kwa hili suala la kuanzisha Chuo Kikuu cha TEHAMA hapa Dodoma. Ameupiga mwingi sana, kwa kweli amefanya jambo zuri sana kwa sababu pia itaongeza ajira kwa vijana. Hata hivyo, niishauri Serikali na ombi langu kwa Serikali, Mkoa wa Mara ni Mkoa ambao unatakiwa uangaliwe kipekee kwa sababu ni mkoa uliomtoa muasisi wa Taifa hili Hayati Nyerere. Katika mazingira hayo kutokana na nchi za wenzetu tunavyoziona mikoa kama

hii ya watu muhimu kama hawa huwa ni mikoa ya kihistoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutukubalia suala la kuweka eneo la historia au eneo la utalii pale Butiama, lakini haitoshi na sisi pia Mkoa wa Mara tunapaswa kuwa na vyuo vya ziada ambavyo vitakuwa ni mfano, lakini vitakuwa ni vyuo ambavyo vinaonesha kabisa muasisi wa Taifa hili ametokea Mkoa wa Mara; na sisi pia Mkoa wa Mara tungeomba basi baadaye tuletewe Chuo cha TEHAMA ili kusudi kuutambulisha Mkoa wa Mara kwamba ndio mkoa aliotoka muasisi wa Taifa hili na vyuo vingine pia vya mahesabu, lakini pia na vyuo vikuu mbalimbali. Kwa hili nimpongeze sana mama yangu lakini ombi hili kwa Serikali naomba sana lizingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hili suala la matatizo yaliyotokea kwa wenzetu. Niwaombe ndugu zetu au majirani zetu wa nchi Jirani, sisi Watanzania tuna amani yetu ya kutosha, lakini wanapaswa kujua kabisa kwamba Tanzania ni nchi huru nchi inayojitegemea. Masuala ya kuingilia uhuru wetu haiwahusu wao washughulikie matatizo yao, sisi kama ni furaha yetu tutashughulikia wenyewe, kama ni matatizo yetu tutashughulikia wenyewe kama nchi, wao hawapaswi kuingilia masuala ya Tanzania na kuleta chokochoko zao Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hiki ni kitendo ambacho tunakilaani sana na sisi Watanzania au wawakilishi wa Watanzania tunawaambia wasirudie tena na hasa wale wenzetu ambao pia wanafikia hatua hata ya kumtusi Mheshimiwa Rais wetu, wajue kwamba yule ndio kiongozi wa nchi yetu. Wanapomtusi Mheshimiwa

Rais wanatutusi sisi wenyewe Watanzania. Watanzania tushikamane kwa pamoja tuiangalie nchi yetu tukijua kabisa hii ni vita ya kiuchumi, mbona haya hayajatokea kabla mama hajaanza kutangaza *Royal Tour*? Wameona sasa Tanzania tunakwenda juu sana katika utalii wameona sasa waanze kuleta chokochoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tuseme tuko pamoja Watanzania tuungane kwa pamoja matatizo yetu tutayamaliza wenyewe na mambo ya Tanzania tutayashughulikia wenyewe, hatumhitaji mtu yeyote wa nchi ya jirani kuja kushughulikia matatizo ya Tanzania au kuendelea kuleta matatizo ndani ya Tanzania.

*Mheshimiwa Spika, tunawaambia wakae wakijua Tanzania ina Majeshi ya kutosha, lakini Tanzania ni nchi ambayo iko imara, wakituletea chokochoko, Mheshimiwa Rais akija akisimama akisema, wajue kabisa watakiona na wasirudie tena kumtusi Mheshimiwa Rais. (Makofi)* ***[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]***

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ili kuyaweka mambo yetu sawa, hapa nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Judith Kapinga atamalizia dakika zake 10, kwa sababu muda wetu uliobaki ni dakika tano, kwa hiyo itabidi tumvumilie kidogo. Mheshimiwa Judith Kapinga.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi ya upendeleo. Awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa maono yake makubwa na kwa *dedication*

na dhamira ya dhati aliyonayo kwenye masuala mazima ya TEHAMA. Tumeona mipango yake mizuri kwenye masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu, kwa kweli nimpongeze Mheshimiwa Rais na nimwambie tu kwamba anawatendea haki Watanzania. Takwimu zinatuonesha kwamba ikifika mwaka 2065 katika nchi zote za Afrika, Nchi za Afrika Mashariki ndizo zitakazoongoza kwa idadi kubwa ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu zinatuambia katika nchi nne za Afrika Mashariki ikifika mwaka 2065 idadi kubwa ya watu watakuwa ni vijana yaani tutakuwa tuna *the most youthful population* Afrika nzima. Takwimu zinatuambia ikifika mwaka 2065 tutakuwa tumekwenda mara tatu ya idadi ya watu ambayo tunayo sasa hivi. Yaani kwa mfano Kenya watatoka milioni 56 watafika milioni 115, Uganda watatoka milioni 48 watakwenda milioni 141, Rwanda watatoka milioni 11 watakwenda milioni 25 na sisi Watanzania tutatoka milioni 60 mpaka milioni 186. Sasa takwimu hizo zinatuambia katika idadi hii ya watu asilimia 62 watakuwa ni vijana kuanzia miaka 18 mpaka miaka 35. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna nyingine takwimu zinatuambia hawa ndio watakuwa walipakodi wetu wakubwa. Idadi hii ya watu katika umri huu ndio ambao watakuwa tegemezi la Taifa letu kwa miaka kadhaa ijayo. Sasa nasema haya kwa sababu kwanza ningependa niwapongeze vijana wenzangu katika Taifa hili, pamoja na changamoto za ajira, vijana wanamuunga mkono Mheshimiwa Rais kwa kujiajiri kwa shughuli ndogo ndogo. Kwa kweli niwapongeze sana, pamoja na changamoto mbalimbali za miundombinu, lakini vijana wa Taifa hili hawajaacha kupambana kwenye kujiajiri ili kusaidia shughuli za maendeleo ya Taifa

lao. Niwatie shime vijana wenzangu na niwaambie waendelee katika kutafuta mbadala wa ajira bila kuchoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vijana hawa wanajitahidi sana, ningependa nimwombe Mheshimiwa Waziri awafute jasho vijana. Awafute jasho vijana kwenye kuwasaidia kutengeneza faida kwenye shughuli za kimaendeleo wanazozifanya, kwa kuondoa vikwazo vidogo vidogo vya kibiashara ambavyo vinawarudisha nyuma. Wote tunafahamu katika vitu ambavyo vitasaidia kuondoa changamoto ya ajira katika Taifa hili ni teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna *applications* ndogo ndogo zinatumika ambavyo zimeajiri mamia ya vijana, wote tunaifahamu *taxify* pamoja na changamoto zake imewaondoa vijana mtaani imeajiri Malaki ya vijana, wanapata ajira ndogo ndogo. Kwa hiyo, tunafahamu kumbe *application* moja ikiajiri vijana karibu laki moja, tukiweka mazingira wenzeshi ina maana vijana wengi sana wataajirika kwenye hiyo, lakini sasa changamoto ni moja. Kama *applications* hizi zinaleta ajira tunajiuliza kwa nini vijana wengi sasa hawaleti ubunifu ili *application* hizi ziajiri wengine? Bunifu wanazo, tatizo ni uwezeshaji wa kimiundombinu, hawana fedha za kusimamisha biashara zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mikopo tunayotoa leo tunataka vijana wetu waende wakajenge matofali, wakafanye ujenzi, wasage unga, haiwezekani ajira hizi haziwezi kuajiri vijana wengi kwa wakati mmoja. Kuna tatizo gani la hatimiliki za *application* za vijana kutumika kama dhamana ya mikopo yao? Kwa sababu ni vitu ambavyo ndio vinawaletea fedha. Duniani kote

*intellectual property* inatumika kama dhamana kwenye mikopo, lakini hii mikopo yetu ya halmashauri nani ametuwekea uzio tusiwape vijana wabunifu mikopo ili iweze kuwasaidia? Kwa hiyo, nadhani tuanze kufikiria tofauti, sio lazima tu tufanye kazi hizi *physical* katika kuwapa vijana mikopo, tufikirie na hawa vijana ambao bunifu zao zitaajiri vijana wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka pia nishauri jambo moja, nimeliongea hapa Bungeni mara nyingi sana na nitaongea kwa masikitiko makubwa sana. Nilisema vijana wa Kitanzania wanapambana sana, lakini kuna mifumo ambayo ipo kwenye mikono ya Mheshimiwa Waziri, kanuni Mheshimiwa Waziri ndiye mwenye mamlaka nazo, suala la *PayPal* itatuingizia kodi, *PayPal* itaongeza fedha kwenye Serikali yetu, sasa kigugumizi kiko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilivyofuatilia kuhusu *PayPal* nikaambiwa kwamba, *PayPal* wenyewe wanasema hawana soko Tanzania. Jamani, Tanzania ndio inaongoza kwa idadi kubwa ya watu Afrika Mashariki, soko lipo Tanzania, tatizo jirani yetu ni janjajanja sana, ndio maana anataka fedha zetu zipitie kwake. Sasa wataalam wetu wasipoenda hatua mbele zaidi kugundua vikwazo kama hivi vya majirani zetu ambao wanatufinya ili vijana wetu wasiweze kupata fursa kama hizi, inakuwa ni shida. Ndio maana leo hapa tunawalaani kwa kuingilia kwenye masuala yetu kama ya Loliondo.

Mheshimiwa Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri suala la *PayPal,* Tanzania *is the biggest market,* kwa hiyo, tusipoenda hatua mbele kujua kwamba, jirani yetu anatuwekea janjajanja ili fedha zetu tuzipitishe kwake, vijana wetu wataendelea kutaabika kwa kiasi kikubwa mno kwa sababu, kama kweli hamna biashara kwa nini

wanaruhusu tuwalipe kupitia *application* yao? Kwa nini wao hawaruhusu sisi tusilipe kupitia *application* yao? Yaani tunalipa, lakini hatuwezi kulipwa, hatuwatendei haki vijana wa Kitanzania. Naongea kwa masikitiko makubwa kwa sababu, suala hili lina miaka 10 nyuma, hatuwezi kukaa hapa kila Bunge tukazungumza masuala ya *PayPal*. Mheshimiwa Spika alililitolea maelekezo mwaka jana, nilitegemea mpaka kufikia kipindi hiki tutakuwa tumepiga hatua kwenye masuala ya mustakabali wa vijana wa Taifa hili, wanaohangaika kutafuta ajira na kujiajiri. Hatuwezi kukubali wakwamishwe na vikwazo vidogo vidogo ambavyo vikitatuliwa vitaleta nafuu kwa wao pamoja na Taifa lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri kwenye suala la *PayPal* naomba alitafutie muarobaini kwa sababu, kama kuongea tumeshaongea sana. Labda sasa watuambie tufanye nini? Sisi kama vijana hatuwezi ku-*match* kwenda kwenye Makao Makuu ya *PayPal* kwa sababu, uwezo hatuna. Tunaamini Serikali yetu kama inataka kodi itatuwekea mazingira wezeshi ya kutusaidia ili tuweze kufanya biashara na tuweze kupata malipo ya kulipa kodi. Kama suala ni wao kuja kuweka *physical presence in Tanzania* wanaweza wakashirikiana na makampuni mengine kwa ajili ya kuwa wawakilishi wao hapa nchini kwetu Tanzania. Pia kama suala ni kodi, Serikali inaweza ikapata kodi kupitia mwakilishi ambaye ni kampuni. Kwa hiyo, kwa kweli kwenye suala la *PayPal* naomba Mheshimiwa Waziri alivalie njuga. Sisi tunalipa hatulipwi, hatuwezi kwenda kupitisha fedha kwa jirani. Naongea hili suala la *PayPal l* kwa uchungu kwa sababu tulishaliongea sana, Mheshimiwa Waziri naomba atusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kwenye suala lingine la masuala ya ubunifu. Vijana wa Kitanzania hawajaanza kubuni magari leo, wameanza kubuni magari siku nyingi sana, lakini tujiulize kwa nini haviendelei? Hata hivyo, juzi alitokea mbunifu mmoja akabuni watu wote wakaenda kwake. Ni vizuri, lakini tumesahau vijana wa Taifa hili wameanza bunifu siku nyingi mno, lakini kuna vikwazo vya kibiashara na vikwazo vinaanzia *TRA*. Tunataka tu-*recognize* vitu tu ambavyo vinatoka nje ya nchi, yaani mpaka uthibitishwe kwamba, bidhaa yako uliyobuni inafaa kwa matumizi ya Watanzania, unasota ile mbaya. Sasa hawa vijana ambao wanabuni tunawarudisha hatua 10 nyuma, yaani mifumo nyetu yenyewe inatambua vitu vya wenzetu kuliko vitu vyetu sisi wenyewe.  Naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri. Kama kweli tunataka mabadiliko kwenye masuala ya sayansi na teknolojia, lazima tuanze kwenye kubadili mifumo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize na jambo la mwisho kuhusiana na uwezeshwaji wa vijana. Wote tunafahamu maendeleo makubwa kwenye nchi mbalimbali yameletwa na viongozi ambao ni vijana, ikiwemo sisi hapa Tanzania; Uhuru wa Taifa letu, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliupambania akiwa na umri wa kijana. Kwa hiyo, nasema hivyo kwa maana moja, naunga mkono kwamba, yatupasa tuwe na vijana ambao wametayarishwa kwa ajili ya kushika nafasi za kimaamuzi, lakini haimaanishi vijana wa Taifa hili hawawezi kushika nyadhifa za uongozi katika Taifa hili, vijana wanaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningependa nishauri kwenye hili suala zima la nafasi za teuzi, pale ambapo wanashushwa nafasi. Huyu mtu kama alikuwepo Serikalini,

ana nafasi yake ya mwisho, kuna nafasi ya mwisho ya juu kabisa kwenye *rank* husika. Kwa mfano, kama ulikuwa *lawyer,* nafasi ya mwisho kabisa pale juu kwenye *lawyer* basi arudishwe pale juu, lakini sio nafasi zote za teuzi ni kwa ajili ya watu ambao wako Serikalini peke yake, kuna watu wa sekta binafsi. Kwa hiyo, leo hii tukisema vijana wasipewe nafasi kisa tu hawakufanya kazi Serikalini, hatutendi haki na vilevile ikifika 2065 *population* kubwa ni vijana *whether* tunataka ama hatutaki, lazima tuwa-*groom* waweze kuja kuwa viongozi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwahakikishie vijana wanafaa kuwa viongozi wa Taifa hili, *let's groom them,* tuwatayarishe kuja kushika nafasi za kimaamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa sehemu yetu ya kwanza ya Bunge.

Mambo mawili; la kwanza, wakati Mheshimiwa Agness Mathew Marwa akichangia alieleza kwamba, nchi yetu inayo majeshi ya kutosha, akiwa anaelekeza hayo maneno kwenye mchango wake ambao alisema kuna majirani wana chokochoko. Sasa kwa sababu, hapa ni Bungeni na hii ni taasisi ambayo kimsingi ndio ambayo kama tangazo la vita likitoka litakuja hapa, sasa mambo kama hayo hayaruhusiwi. Kwa hiyo, sehemu hiyo ya mchango wake itaondoka kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine; wakati tukiendelea na huu mjadala wa hoja yetu ya Bajeti Kuu, haya maneno ya chokochoko nimeyasikia, Waheshimiwa Wabunge wameshayasema sana hapa, lakini kwa

sababu hii ni taasisi, ni Mhimili wa Bunge na huko tunakosema chokochoko zimetoka zimekuja kwa njia ya mitandao. Kwa namna hiyo, hatuwezi sisi tukataka kujibu chokochoko za mitandao kwa kutumia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu, itaonekana kama tuna mawasiliano hivi na taasisi maalum ama husika kutoka kwenye nchi yoyote ya jirani inayojihusisha na mambo hayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, hoja zetu bado zitaendelea kwenye maeneo yetu ya nchi yetu, tunataka maendeleo kwenye kila sekta, lakini hii ya kuwajibu watu kwenye mitandao huko tutakuwa kidogo, kama Bunge, ni kama hatujielekezi kwenye zile hoja zilizo mbele yetu hapa. Kwa hiyo, niwaombe wale waliochangia wameshatupa picha na sisi kwa sababu tumeiona tunaweza kuwafuata huko kwenye mitandao ili tukawajibie huko, lakini kwa hapa ndani tujielekeze kwenye hoja hii ya utalii kwa namna inayofaa kwa sababu, kwa taarifa zilizopo mpaka sasa ni kwamba, nchi yetu pamoja na majirani wanaotuzunguka tuko vizuri. *(Makofi)*

Kama wako watu wanaojitokeza hapa na pale, basi tutafute namna ya kuwajibu katika maeneo yale ambayo tunaona kwamba, tunataka kuwajibu, lakini kwa upande wa Bunge, nafikiri mpaka sasa Bunge taarifa lililonayo ni ile aliyotoa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapa Bungeni. Hiyo ndio taarifa ya Serikali kuhusu jambo la Ngorongoro na Loliondo, taarifa ndio hiyo tunayo hapa Bungeni. Kwa hivyo, hizi taarifa nyingine tushughulike nazo kwa kadiri zinavyojitokeza huko ambako zinajitokeza, ili iwe rahisi hata hao watu kupata ujumbe, kama tunafikiri wataupata huo ujumbe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwataje Wabunge wachache ambao tutaanza nao mchana kwenye mjadala huu. Kama ambavyo nilikwishakusema huko nyuma, wachangiaji kila mchangiaji anachangia dakika zake 10 na tutaendelea na utaratibu uleule wa kutoa kipaumbele kwa Wabunge ambao hawajapata fursa. Kwa hivyo, inawezekana kabisa katika mpangilio wa majina wako ambao walishachangia mara nyingi, wasipopata nafasi leo si kwamba, hawatapata kabisa ni kwa sababu, asubuhi tulikuwa na mambo mengi kidogo, kwa hiyo, orodha ya leo haitakwisha na kwa hivyo, watahamia kesho, lakini kule kuhamia kesho haimaanishi wao watapewa kipaumbele kwa sababu, hawajachangia leo.

Nafafanua kwa sababu, si lazima mimi ndio niwe nimekaa hapa, ili mtu asije akasema nilibaki jana, sasa mbona leo sijapewa kipaumbele, hapana. Kama majina yatakuwa mpaka jioni hatujaweza kukamilisha, orodha itaenda siku nyingine. Tutaendelea kufanya hivyo na tunaamini katika hizi siku zote za kuchangia kila Mbunge atapata nafasi. Kila Mbunge atapata nafasi na kwa sababu sote tuko Dodoma tusiwe na wasiwasi, atakayechangia leo au atakayechangia kesho. Naamini Waheshimiwa Wabunge hilo limeeleweka. *(Makofi)*

Sasa Wabunge ambao tutaanza nao mchana ni Mheshimiwa Jafary Chege, Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mheshimiwa Assa Nelson Makanika, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga na wengine wataendelea kutajwa kadiri muda utakavyokuwa unakwenda.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni ambao hawakuwepo wakati tukitangaza asubuhi, hawakupata nafasi ya kuingia humu ndani. Tunao wanafunzi 100 na Walimu 10 kutoka *Nyamata Pre and Primary School* ya Jijini Dar-es-Salaam wakiongozwa na Mkuu wa shule hiyo Mwalimu Isack Lumuli. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi 114 na Walimu 10 wa Shule ya Sekondari Kintinku ambao wanatoka Mkoani Singida. Karibuni sana vijana wetu na Walimu wenu. *(Makofi)*

Vile vile tunao viongozi 23 wa Tawi la CCM Mji Mpya kutoka Jijini Dar-es-Salaam. Karibuni sana, hawa wanaongozwa na Ndugu Francis Mahundi na Fidelis Mbunda. Karibuni sana Bungeni, karibuni sana na tumaini mmepata kujifunza mawili matatu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka Saa 11.00 kamili, jioni leo.

*(Saa 7.11 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano na wachangiaji wetu wa kwanza watakuwa ni Mheshimiwa Jafari Chege, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa kwanza kwa jioni ya leo. Nianze tu kwa kusema naunga mkono hoja ya Bajeti ya Serikali, lakini pia nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wasaidizi wake wote Makamu wa Rais, Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wa Wizara hii kwa bajeti nzuri ambayo kimsingi imekidhi mahitaji na matakwa ya wananchi, lakini pia wame-*consider* kwa kiasi kikubwa sana maoni ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza mchango wangu nimwombe tu Mheshimiwa Waziri atakapopata nafasi aweze kuielezea ile *factor* ya kusema kwamba mtumishi hasa watumishi wa kuteuliwa atakapokuwa amepoteza nafasi yake basi anarudi nyuma kukidhi kwa maana ya kuchukua mshahara ule ambao alikuwa analipwa mwanzo. Yaani maana yake ni kwamba kama mtu alikuwa ni Afisa Mtendaji wa Kata mamlaka zikamwona kutokana na utendaji wake mzuri, akateuliwa akawa Mkuu wa Wilaya, baada ya mwaka mmoja au miaka miwili akapanda akawa Mkuu wa Mkoa, kwa sababu utendaji wa kazi ndiyo unamfanya apande hizo nafasi na namna mamlaka zinavyomwona, lakini pale utumishi wake unaposita anarudi kuchukua mshahara ule wa Mtendaji wa Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kuna miaka mitatu hapa amepoteza, nataka nijue anarudi kwenye mshahara upi? Kwenye mshahara ule wa awali kipindi anateuliwa kwenda kuwa Mkuu wa Wilaya au atarudi kwenye mshahara upi? Kwa sababu hapo miaka mitatu naamini wenzake pia kuna mishahara imeongezeka. Sasa nataka nijue tu na Mheshimiwa Waziri atakapopata nafasi aielezee kwa sababu hii ndiyo watumishi wengi

hasa hawa ambao wanakumbwa na nafasi za uteuzi wametengeneza taharuki hiyo. Mtu alikuwa ni Mwalimu analipwa Sh.400,000, ameonwa na mamlaka amekuwa Mkuu wa Wilaya ana-*stop* Ukuu wake wa Wilaya anarudi kwenye mshahara wa Sh.400,000 ule ule au wata-*consider* na ile miaka yote ambayo amepoteza kwenye nafasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijikite kwenye mchango wangu na nitachangia katika maeneo matatu. Eneo la kwanza, kama nilivyoanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, nimesoma vizuri sana bajeti hii na nimekesha vizuri, nimeisoma kwa kiwango kikubwa, lakini niseme na kwa kumkumbusha sekta ya ardhi kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha hajaiweka. Sekta ya Ardhi haijapewa kipaumbele kama zilivyopewa sekta nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikisema na tumekuwa tukishauri hapa, ukisoma yale maeneo yote ambayo fedha za Serikali zinakwenda kwenye mahitaji muhimu kwenye sekta mbalimbali, ardhi haijaguswa na nimekuwa nikisema na tumekuwa tukisema hapa Mheshimiwa Waziri atakumbuka ardhi ni rasilimali asilia, ardhi ni mtaji, lakini ardhi pia ni chanzo cha mapato. Bahati nzuri kwenye bajeti hii Mheshimiwa Waziri amesema kwamba dhima ya bajeti ni kwenda kujenga uchumi shindani wa viwanda na maendeleo ya watu. Huwezi kujenga uchumi shindani wa maendeleo ya watu kwenye viwanda kama ardhi haijazungumzwia kwa kiwango hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri atakapopata nafasi mwishoni wakati wa majumuisho yake, aje aizungumzie ardhi kama sekta

ambayo ni sekta mtambuka, ni sekta ambayo haya mengine yote tunayoyafanya ya uchumi wa maendeleo ya viwanda hayawezi kufanyika bila kuwekeza kwenye ardhi. Ningetamani Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anazungumza ajikite kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kwa kutambua umuhimu wa sekta ya ardhi, mwaka jana alitoa zaidi ya bilioni 50 kwa ajili ya kwenda kwenye mamlaka za upangaji na upimaji kwa maana halmashauri na ilikwenda kazi ya kupanga, kupima na kurasimisha. Ukisoma kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri haizungumzwi. Pia tunatambua mwaka huu ametenga zaidi ya bilioni 345 ambayo inakwenda kwa ajili ya kuhakikisha hizo kazi za kuboresha miundombinu ya sekta ya ardhi kupanga na kupima na maeneo mengine ningetamani nayo aielezee kwa maana sekta ya ardhi ni sekta mtambuka na kwa kutoa maelekezo namna fedha hizi zitakavyoenda kunufaisha sekta ya ardhi na maeneo mengine. Siyo hivyo tu, tuna zaidi ya bilioni 130 ambazo zimetoka Korea, hii yote ni michango ya Mheshimiwa Rais. Ukisoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ardhi ni kama vile haijaguswa kwa ukubwa unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho mwishoni aiweke na aizungumze ili angalau mamlaka za upangaji na upimaji na wananchi na wadau wengine wa sekta ya ardhi, lakini wajue ni namna gani ambavyo Serikali imejipanga kwenda kuboresha kwenye sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ni miradi ya kimkakati pamoja na vyanzo vya mapato ya halmashauri. Kwa kuwa Wizara ya Mheshimiwa Waziri ndiyo imekuwa ikijikita sana kwenye kupanga matumizi

na kupeleka fedha za miradi ya kimkakati, zipo halmashauri ambazo ni za kimkakati lakini mapato yake ni madogo sana. Mathalan, Wilaya yangu ya Rorya, ndiyo maana tuliwahi kushauri hapa, ni vema Wizara ya Fedha ikafanya mchanganuo wa halmashauri ambazo zipo mipakani, mapato yake ni madogo, siyo *stable,* haya-*sustain* na wakati mwingine wanakusanya kwa kujinyima kweli kweli, hawa ndiyo wapewe fedha za miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukaona kwenye mapendekezo ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba sasa tunakwenda kuiboresha, kuichanganua ile 10% iliyokuwa inatoka, kwamba itoke asilimia tano, asilimia mbili mbili. Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi, kuna halmashauri ambazo kwa mwezi wanakusanya milioni 40 peke yake, mfano kwangu Rorya, ukikusanya milioni 40 Rorya, ukitoa asilimia kumi ni milioni nne, ukianza kuigawanya kwa kipindi hiki kwa sasa kwa asilimia 4:4:2, maana yake unaweza ukaona kwamba vijana walikuwa wanapata milioni 1.6 peke yake, Sh.1,600,000 kikundi cha watu 10 wanaitumia vipi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa umeenda tena umeinyambulisha, umeigawa, unasema itakwenda 2%, yaani maana yake wale waliokuwa wanapata Sh.1,600,000, kikundi cha vijana 10 wanapata 800,000 kwenye halmashauri zenye mapato madogo kama Rorya. Kwa hiyo naomba kama kuna uwezekano tuiache ile10% iende vile vile 4:4:2, ile fedha 5% ambayo ilikuwa inakwenda kwa ajili ya Wamachinga, tuendelee na mkakati ambao Mheshimiwa Rais ameshatusaidia, amepeleka zaidi ya bilioni 10 kwenye kila mkoa, ziende zikaboreshe maeneo ya Machinga, tusiguse kule, kwa sababu ukigusa kule kwa sababu ukigusa kule, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi vijana sasa kwa

kasi inayokwenda, kwa *growth rate* ambayo inakwenda mpaka kufika 2025 kutakuwa na vijana wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tulipo kuna msururu wa vijana, makundi ya vijana wameomba mikopo kwenye halmashauri zetu, lakini hawajapewa. Sasa ukipunguza kile kiwango kwenye halmashauri inayopokea milioni 40, wapo watu 10 wanapokea milioni nane, haitafaa hata kidogo. Kwa hiyo naomba nishauri kwenye hilo, tuone namna ya kulifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, ni namna ya kuboresha kwenye maeneo ya mipaka. Niliwahi kuchangia hapa kutumia fursa za kimpaka kati ya halmashauri ambazo ziko ndani ya nchi na nchi. Kwangu Rorya, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami nimekuwa nikisema hapa tuna Bandari ya Sota, pale ndani ya wilaya yangu, lakini hatujawahi kuona namna gani inanufaisha uchumi wa nchi yetu. Tuna mipaka yetu pale Kirongwe, nichukue nafasi kwanza kuwashukuru watu wa *TRA*, baada ya kuona nimezungumza kwa muda mrefu, sasa wameweza angalau kuboresha sehemu ile, lakini tukumbuke ndani ya kilometa 35 hakuna udhibiti wowote. Niliwahi kusema hapa kuna ng'ombe wanavuka, wanapita ndani ya mpaka ule kwa siku siyo chini ya ng'ombe 200 au 300, Serikali inapoteza fedha pale, ningetamani kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri aone namna ya kusaidia haya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia kwenye maeneo ya mnada wa upili kwenye maeneo ya mipaka kupitia Wizara ya Mifugo, nimekuwa nikisema vile vile zaidi ya kilometa 35 mpaka 40 ili uweze kutembea pako wazi, pale chochote kinafanyika, inawezekana ninavyozungumza kuna watu wanavusha mifugo, Serikali

inapoteza mapato mengi sana pale, niombe sana nalo hili liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kwenye suala la kulipa kodi, nimpongeze na nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa namna ambavyo ameona kwamba sasa vijana wote ambao wanafikisha miaka 18 waweze kuwa na *TIN* Namba. Nimekuwa nikisema hapa na ningetamani mwishoni nalo pia alitolee maelezo, tunazo Taasisi za umma ambazo zinadaiwa zaidi bilioni 78 na Wizara ya Ardhi kama kodi ya ardhi, hawana tofauti hawa watu na mwananchi mnyonge ambaye tunamwambia nenda kalipe kodi yako leo na wakati tunayo mataasisi ya umma, mashirika ya umma yanadaiwa zaidi ya milioni 78. Yaani kama ndiyo hivyo kama tunashughulika na mwananchi kumwambia nenda kalipe kodi, haya mashirika yetu ambayo tunayo zaidi ya 114, lini wanalipa hizo hela?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema nimpongeze Waziri namna alivyosema kwamba Wakurugenzi wa hizi Taasisi wawe wanaingia kwa kufanya *interview,* lakini naomba asiishie hapo tu, aende awaambie Mkurugenzi asiyeweza kulipa kodi ya Serikali kama ambavyo tunashughulika, wao ndiyo wanatakiwa wawe mfano, hawalipi zile fedha, matokeo yake ni kwamba, Wizara ya Ardhi kila mwaka ikipanga bajeti zaidi ya 35% ya bajeti ya Wizara ya Ardhi kwenye kodi ya ardhi inategemewa kupatikana kutoka kwenye mashirika ya umma. Halafu ndani ya 35% hayo mashirika hayalipi hiyo fedha, kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri aikazie hii, haya mashirika ya umma yanayodaiwa fedha za Serikali, walipe tusiwe tunakwenda tunamng'ang'ania tu mwananchi kulipa halafu tunayo mashirika ndani yetu na hayalipi kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kwa umuhimu wake, niombe sana Mheshimiwa Waziri wanapopanga hii bajeti na wanapokwenda kutengeneza mipango waangalie mazao ya kimkakati ya kila mkoa. Nilikuwa naona hapa kwenye kilimo Mkoa wangu wa Mara kila nikiusoma sioni, nilikuwa natamani sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alione hili, hatuna zao la kibiashara la kimkoa ambalo tunatakiwa litunyanyue sisi kama mkoa, tunaona mikoa mingine inavyokwenda, lakini Mkoa wa Mara hatujafika mahali tukaona namna gani Serikali imepanga mikakati ya kutengeneza zao la kibiashara na likasimamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo maeneo mengi ya kiuchumi kama viwanda vimekufa, Bandari ya Musoma imekufa, tulitamani angalau na sisi kupitia kilimo tuone ni zao gani ambalo Wizara imefanya utafiti na twende kutoa elimu kwa wananchi ili angalau liwe ni zao la kutubeba watu wa Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jafari Chege. Tunaendelea na Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, Mheshimiwa Assa Nelson Makanika na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji wajiandae.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii. Nianze kwanza kwa kuipongeza Serikali kwa bajeti nzuri sana ambayo kwa kweli imeleta matumaini makubwa kwa Watanzania na hasa wanyonge. Pia nimpongeze Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu

Hassan, kwa jinsi ambavyo amekuwa akituletea maendeleo. Vile vile niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mwigulu pamoja na Naibu wake kwa kutusomea bajeti nzuri sana yenye matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siyo mchumi, lakini nizungumze kidogo kuhusu mambo ya *inflation*. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Mwigulu, Waziri wa Fedha ni kwamba hali ya uchumi sasa hivi kidunia imepungua kwa asilimia 3.1, badala ya matarajio ambayo ilikuwa ni asilimia 6.0. Katika hilo hilo suala la *inflation* wanasema kwamba mpaka hapa tulipo katika soko la dunia bidhaa nyingi zimepanda kwa asilimia 24, lakini mfumuko wa bei kwenye soko la dunia kwamba umeongezeka kwa asilimia 5.7 kwa nchi zilizoendelea na kwa nchi zinazoendelea ni asilimia 8.7, maana yake ni kwamba bidhaa zitaendelea kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa zimetolewa sababu nyingi ambazo kwamba mojawapo ni hii ambayo ni ya vita ya Ukraine na Russia, lakini na suala la UVIKO 19, tunashukuru Mheshimiwa Spika alituletea wale wataalam jana ambao wengine walikuwa wametoka BoT na wengine wa Serikalini kwa ajilli ya kutupitisha sehemu mbalimbali katika kuangalia mambo ya uchumi. Moja ya kitu ambacho kinahitaji elimu ya kutosha, ni pale waliposema kwamba hata kusingekuwa na vita ya Ukraine na Russia, bado bei kwa mfano za bidhaa zilizopo sasa zingeendelea kuwepo hapa zilipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mwananchi wa kawaida inatakiwa kutolewa elimu ya kutosha ili ajue tunafikaje hapo, kwa sababu hawa wataalam wetu pia ndiyo wanapita na mitaani na wananchi pia

wanawasikiliza, kwa hiyo siyo kitu cha ajabu kumwona mwananchi wa kawaida akisema uchumi huu kudorora au bei kupanda siyo kwa sababu ya vita ya Russia na Ukraine, ni kwa sababu ya elimu kama hii. Kwa hiyo kuna umuhimu wa kutoa elimu ya kutosha ili watu waelewe maana ya mfumuko wa bei ni nini, lakini pia kuwapa wananchi njia mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuna suala pia la umwagiliaji kwenye kilimo. Kwa kuwa hali ya hewa si nzuri sana kwa nchi yetu na huenda kukawa pia hatutarajii lakini pengine sehemu zingine zikapata upungufu kidogo wa chakula, kuna umuhimu sana wa kuimarisha hizi skimu za umwagiliaji ili tuweze kufanikiwa katika kujihami na suala la chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Sekta ya Afya Mheshimiwa Mwigulu alituambia kwamba sasa hivi baada ya miundombinu kuboreshwa, tatizo kidogo limekuwa kwenye upungufu wa wahudumu wa afya. Tunaomba hiyo miundombinu ambayo tayari imejengwa kwa muda sasa na iko kwenye mafanikio mazuri, ili iweze kuwa na ufanisi, basi Serikali ifanye jitihada za kutosha kupatikana kwa hawa wahudumu wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la elimu, Serikali imefanya vizuri, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwarudisha mashuleni wale watoto wa kike ambao walikuwa na changamoto mbalimbali zikiwemo za ujauzito. Hata hivyo, pia kumekuwa na changamoto, kwenye elimu pia kuna upungufu mkubwa sana wa Walimu na hasa vijijini. Sehemu nyingi vijijini bado kuna upungufu wa Walimu, Serikali ifanye mkakati wa kutosha na ikiwezekana hata kurekebisha baadhi ya kanuni au

Sheria za kuwalazimisha Walimu wakae vijijini. Vinginevyo hili tatizo litakuwa ni la kudumu na tutaendelea kuliimba kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu bure mpaka kidato cha sita tunaipongeza sana Serikali kwa kuamua hivyo. Hata hivyo, Serikali iangalie uwezekano wa kutoa chakula, kama haiwezekani kwa shule zote, basi angalau shule ambazo ziko kwenye *remote areas* ambako wanafunzi kupata chakula inakuwa siyo rahisi. Miaka ya nyuma iliwezekana, mimi binafsi shule ya msingi nilisoma chakula kilikuwepo shuleni, wale ambao mmesoma miaka ambayo na mimi nimesoma, ile ya 1970, tulikuwa tunakula chakula shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunakula chakula ambacho kama mnakumbuka, tulikuwa tunakula mpaka ngano, tulikuwa tunaita *bulga*. Kulikuwa na siku maalum ya kula *bulga* lakini pia tulikuwa tunaletewa chakula na watu wale wa chakula barafu walikuwa wanatuletea samaki wale ambao wamegandishwa. Kwa hiyo tulikuwa tunapata elimu ya namna hiyo, lakini hata madaftari likiisha ulikuwa unampelekea Mwalimu, anaangalia kama limejaa anakupa daftari lingine. Kwa hiyo tunaomba pia Serikali iangalie kutoa nafuu za namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie suala hili la utalii, utalii ndugu zangu ni muhimu na nchi yetu imepiga hatua kubwa sana sasa hivi kuhusu utalii. Mheshimiwa Rais ametuongoza vizuri katika eneo hili. Utalii wetu umekua kwa kiwango kikubwa, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu Hassan na hasa hili suala la *Royal Tour*. Kama ilivyo kawaida penye mafanikio hapakosi changamoto, wenzetu wameanza kutuchafua ili

tusifanye vizuri. Katika hili niko tofauti kidogo na wenzangu kwenye kuchangia eneo hili. Naona hapa nia siyo watu kuhamishwa au watu kuhama, hapa wanalenga utalii wetu ili wale wenzetu ambao wanakuja kwenye kufanya huo utalii waone kule Tanzania kuna sehemu haina amani. Hawa wenzetu Wzungu na watalii wengine, mara nyingi hawaendi sehemu ambayo wanajua kuna machafuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wenzetu hawa wanaotumia lugha hizi mbalimbali za kwamba kuna kitu fulani kinafanyika watu wanahamishwa, tena watu wenyewe wanahamishwa kwa hiyari yao wala siyo vurugu, lakini bado wanaingilia kutupakazia. Nchi hii siyo mara ya kwanza kuhamisha watu, kulikuwepo na suala la *operation* vijiji miaka ya 70, watu walihamishwa mpaka kupelekwa Gezaulole na Mwanadilatu, hatukuona watu wakiingilia na kusema hawa wamehamishwa kinyume cha sheria. Vile vile bomoa bomoa nyingi zimepita, ardhi ya nchi hii ni mali ya umma chini ya udhamini wa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanahamishwa kwa kutumia taratibu na wanakuwa *compensated*. Sasa leo anapotokea mtu anaingilia kitu ambacho ni cha nchini mwetu; na ninaomba kidogo ninukuu, hii ni *sovereign*. Hii *term* inatumika kimataifa na maana yake naomba noisome. Maana yake ni *the supreme absolute uncontrollable power by which an independent state is governed and from which or specific political powers are delivered*. Inaendelea kusema, *the international independence of a state, combined with rights and powers of regulating its internal affairs without foreign interference*. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tuna *regulate* mambo yetu wenyewe na tuna taratibu ambazo hatujakiuka *any international law* yoyote. Kwa hiyo, ndiyo maana nimesema wanalenga utalii wetu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na hasa Wizara yetu ya Utalii, hapa tunachafuliwa, kulenga namba ya wale watalii ambao wanaongezeka hapa nchini. Hata hili alilolianzisha Mheshimiwa Rais, la *Royal Tour,* haya ndiyo yanayolengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuwe waangalifu, wanataka paonekane kwetu hapana utulivu ili waweze kutupunguzia idadi yetu ya Utalii… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwakasaka. Muda mrefu kengele ilishapigwa.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwakasaka. Tunaendelea na Mheshimiwa Assa Nelson Makanika, na baadaye Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, ajiandae.

**MHE. ASSA N. MAKANIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia bajeti hii ambayo ni Bajeti Kuu ya mwaka 2022 kuelekea 2023. Mheshimiwa Waziri ametuwasilishia bajeti hii ambayo imekuja na vitabu vinne, nimeipitia na kwa kweli lengo kubwa ni kutafuta, na namna gani

tukishatafuta, tuweze kutumia. Nami nimepata jambo la kuweza kusema ili kumshauri Mheshimiwa Waziri aweze kuangalia namna gani anaweza akayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti hii smeelezea vipaumbele ambavyo ndivyo atakavyoviweka mbele na ambavyo vitamwezesha katika kukusanya na wapi atapata mapato hayo. Kipaumbele cha kwanza amesema mwenyewe kwenye bajeti yake *page* ya 33, amezungumza kwamba atafanya kipaumbele cha kwanza kuwa ni kilimo na atakifanya sana sana kilimo cha Chikichi kuwa Kigoma ndiyo iwe kitovu kikubwa cha kilimo hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *palm economy* ndiyo uchumi wenyewe sasa hivi ambao unaweza ukaleta majibu makubwa ya *inflation* yoyote ambayo inaweza ikapatikana kwenye bei ya *cooking oil.* Changamoto hii inaweza ikatatuliwa na *palm oil* peke yake tu. Kabla ya kwenda mbele kabisa nimwoneshe Mheshimiwa Waziri kwamba, sisi wenyewe hata kwenye ripoti yake ya hali ya uchumi amezungumza hili jambo, lakini Waziri mwenye dhamana amezungumza hili jambo kwenye bajeti yake, Bwana Bashe. Nimepitia sana hii bajeti yake *page* namba 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bashe anatuonesha kwamba mazao ambayo yanazaa mbegu hizi za mafuta katika namna zilivyozaa kuanzia mwaka 2017 mpaka mwaka 2020, kwenye Jedwali namba 12 ameonesha Waziri mwenye dhamana ya kwamba zao ambalo limeonesha kuzaa kwa *negative* ndani ya miaka mitano, ni alizeti; na limeshuka kwa asilimia 26.3 kutoka mwaka 2017 mpaka mwaka 2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipomfuatilia Waziri, anaonesha kabisa jitihada kubwa bado ameiweka kwenye alizeti. Mheshimiwa Waziri na Mwenyekiti ukija ukatazama Jiografia ambapo alizeti inamea ni *semidesert,* yaani ni nusu jangwa. Kwa maana hiyo ukienda kuweka matumaini ya Taifa kwamba ulilishe Taifa mafuta ya kula kutoka kwenye alizeti, unaliweka Taifa kwenye hali ya hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Kigoma tuna hali ya Jiografia safi kabisa, mvua hazina changamoto hata kidogo kwetu. Siyo hivyo tu, alizeti ni zao ambalo linaweza likapandwa kwa mwaka na baadaye likishavunwa haliwezi tena kuvunwa mpaka lipandwe tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini chikichi, ukiipanda; sisi tumezaliwa tunakuta michikichi ya miaka 80; mpaka sasa hivi miaka 30 bado ipo.  Haja kubwa ipo katika kutazama zao la Chikichi. Jaribu kuangalia, hata juzi tumehudhuria semina hapo, watu wa Benki ya Dunia wameonesha wengi kuwa na *statements* mbili tofauti, lakini *statement* moja ambayo hata sisi tunajichanganya, wengi wanasema mfumuko wa bei kwenye mafuta ya kula ni kwa sababu ya vita vya Ukraine; uongo mkubwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema, mfumuko wa bei kwenye mafuta ya kula unasababishwa na mipango yetu sisi wenyewe kama nchi, wala siyo vita hata kidogo, kwa sababu hivi ni vitu ambavyo tunaweza tukazalisha wenyewe endapo tutaweza kuweka mipango madhubuti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jaribu kutazama kwenye jambo hili; ikiwa tunaweza tukakusanya fedha zetu

wenyewe, hizi za madafu, tukatenga Shilingi bilioni 480 tukaenda kuagiza mafuta haya kutoka nje, kiasi kikubwa kama hicho, na kule tunapoagiza ndiko kwa watu waliokuja kujifunza hiki kilimo cha Chikichi kwetu; tunatoa fedha zetu tunazipeleka kule kwao, tunakuwa tumepeleka vitu vingi sana, hatujapeleka fedha tu. Tumepeleka fedha za kigeni, tumepeleka ajira za watu wetu, tumewahamishia wale watu waliopata akili mapema wakaweza wakaweka mipango Madhubuti, ndiyo tunakwenda kununua kule. Tunakuwa tumenunua na vingi, tumebadilishana na vingi kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nikufahamishe tu jambo usilolijua au mwingine anaweza asilifahamu, mafuta yote tunayokula hapa Tanzania, asilimia 98 yanatokana na Mawese. Ukichukua Korie, ni zao la Mawese. Ni nini kinachofanyika ambacho kinatufanya tuweze kutumia kitu ambacho tunaweza tukazalisha wenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo teknolojia mbili tu duniani ambazo Malaysia na Indonesia wanazitumia. Hata sisi wenyewe wafanyabiashara wetu wanakwenda kuchukua kule kutoka kwa hao watu wanakuja huku wanafanya *packaging* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mawese wanachokifanya, wanatumia teknolojia ambayo inaitwa *deodorization,* wanaondoa harufu ya yale mafuta ya mawese. Wakimaliza pale, wanafanya teknolojia ya pili inaitwa *colorization,* wanaondoa ile rangi ya mawese unayoiona. Ikishatoka pale, ni Korie halisi, tayari kwa *packing,* inakwenda kutumika kwenye soko letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri jambo hili analiweza sana, na kuliweza ni yeye tu, amezungumza kwenye hali ya kubana matumizi, hata hapa mpaka sasa anaweza aka-*cutoff* kwenye hii bajeti nusu tu, itazaa viwanda vikubwa sana Mkoani Kigoma ili tuweze kuzalisha kwa asilimia kubwa na hatutaagiza mafuta nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu jambo moja ya kwamba kwa kuweza kujibana hata mwaka mmoja katika bajeti zetu, tunaweza tukapunguza lita hizo tunazoagiza nje kwa kiwango kikubwa sana. Ni sisi tu kuamua leo. Mheshimiwa Waziri na Wizara yako, chukueni uamuzi leo mweze kulifanyia kazi hili, tutakuwa tumekwenda kurekebisha katika mfumuko huu na hali ya mafuta ya kula ambayo inasumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa gharama hiyo hiyo, hata *technical team* imefanya *research* yake, ipo Ofisi ya Waziri Mkuu na ninadhani na Mheshimiwa Waziri utakuwa umeipata. Hii *technical team* inaongozwa na Mzee mmoja yupo pale Kigoma, wameweza kuangalia namna gani ambavyo kama Kigoma na maeneo mengine ambayo yamezungumzwa kwenye bajeti ikiwemo Mkoa wa Kagera na Mikoa mingine ya jirani katika bonde lile la Mto Tanganyika likitumiwa kwa bajeti hii hii, tunakwenda kuweka mabadiliko makubwa kwenye hali hii ya mafuta ya kula tunayoagiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende hoja ya pili, ni suala la reli. Mheshimiwa Waziri, kwanza tunakushukuru sana na tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa jambo kubwa hili alilolifanya. Sisi tulikuwa na hofu sana. Kwa mchumi yeyote kwa mpango ule wa kwanza uliokuwepo, tulikuwa tuna hofu nchi yetu inakwenda kutengeneza

*uneconomic hub* kwenye nchi jirani. Ila kwa kitendo Mheshimiwa Rais alichokifanya, akaleta ile reli ikaenda kupita pale Uvinza ipande Msongati, iende Gitega, iende Bujumbura na baada ya hapo itokee pale pale Uvinza ifike mpaka Kindu nchini Kongo, ni jambo la kupongezwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunasema Mheshimiwa Rais ameweza kupaona hapo. Wale walikuwa wametutega, kwa sababu tunakwenda kutengeneza *hub* katika nchi yetu wenyewe. Watu wa Kigoma tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hilo aliloliona, nasi tunasema tutakuwa pamoja naye na tutamuunga mkono. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Assa.

**ASSA N. MAKANIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, nilimtaja Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji na Mheshimiwa Oran Manase Njeza, ajiandae.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa hii. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia kuwa na hali ya uzima na afya. Pia nakushukuru wewe Mwenyekiti, kwa wakati huu kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia katika Bunge lako hili tukufu leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri wangu wa Fedha kwa mpango wake huu aliouleta humu Bungeni ambao sasa hivi tunaweza kuuchangia Wabunge humu ndani, na sote tumesimama tunachangia suala hili lake kuhusu Mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu, naye anafanya kazi kubwa sana nchini, anafanya kazi kila mahali, Mwenyezi Mungu amjaalie hatua, ampe wepesi, ampe kila la heri na amuoondolee shari, ampe heri *Inshaallah*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea, nizungumzie suala la kuboresha huduma ya mama na mtoto. Huduma ya Mama na Mtoto, nashauri iendelee kutolewa. Akina mama wahudumiwe na akina baba, na hao akina baba waweze kuwahudumia akina mama. Maana ndiyo kama ninavyosema, tunawapenda sana akina baba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la watoto. Watoto wetu nao wanatakiwa kuhudumiwa, lakini kuna janga sasa hivi limejitokeza au tunasema changamoto. Kuna changamoto ya kiafya juu ya watoto wetu imeingia hapa nchini, nalo ni ugonjwa wa figo kwa watoto. Huu ugonjwa unaathiri sana watoto wetu huu. Ninavyokwambia watoto wengi wameshafariki kwa ugonjwa huu wa figo. Huu ugonjwa wa figo sio Watoto tu, hata sisi watu wazima; na huu ugonjwa unaleta changamoto ya haja ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaposhikwa haja ndogo unatakiwa ufukuzie kwenda chooni, kwa sababu unapohitaji kwenda haja ndogo, basi ile figo inaathirika

mle ndani. Kwa hiyo, figo inaumia sana; lakini kwa watoto imezidi kuwaathiri. Kwa hiyo, kwa mpango huu, nasema kwamba wanawake tupewe kipaumbele pamoja na hawa watoto waweze kushughulikiwa ili hili janga lililojitokeza kuhusu figo litazamwe kwa kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ulinzi; kuna suala la Mambo ya Ndani ya Polisi kwamba Polisi wanafanya kazi vizuri, wanaendelea kushughulikia mambo ya usalama nchini, wanafanya kazi kusema ukweli. Kutwa kucha wao wamo ndani kwa kutulinda sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Polisi ukiwatazama, wale watu wamekuwa wanyonge sana, hawana kipato cha kuweza kuwasaidia hawa ndugu zetu Polisi hasa wanapostaafu, mafao yao yanakuwa kidogo, hayawakidhi maisha yao wakasema kwamba hapa sisi tujenge au waweze kufanya miradi ya kuweza kuwasaidia mpaka hapo watakapofika kwa Mwenyezi Mungu. Fedha yao inakuwa ndogo. Kwa hiyo, katika huu mpango, namwomba Mheshimiwa Waziri, hawa ndugu zetu Polisi nao waweze kusaidiwa katika suala hili ili wafanye kazi vizuri na wajisikie kama wapo katika nchi yetu hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea, kuna ulinzi wa Jeshi hivi sasa. Hapa sasa! Ulinzi wa Jeshi nao niwapongeze; jeshi linafanya kazi vizuri, linatulinda, lipo kila pembe, lipo kila rika, wanaangalia kila mahali, lakini ukija ukazingatia Jeshi wanavyofanya kazi humu nchini, kwetu sisi ukiingia katika Mkoa wa Kusini kwenye Jimbo la Tunguu, kuna vijiji ambavyo vimevamiwa na Jeshi, ni kilio. Kuna sintofahamu kubwa sana ya wananchi kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiri, kuna eneo moja la Ubago lile limekwenda na maji, watu toka enzi ya ukoloni wapo pale; wamelima, wana minazi, wana majumba wamehamishwa hawapo, kilio kimewafika, hadi sasa hivi haijajulikana hii sitofahamu itafikia wapi? Siyo Ubago tu, ukija Dunga nako liko hilo suala, lakini siyo Dunga, mambo yote yapo hapo Kijiji cha Kikungwi. Kijiji cha Kikungwi Uwandani wapo wananchi wanalima ndimu pale, wana minazi, wana mazao mbalimbali kule wanalima. Matokeo yake, juzi tu wameambiwa wajiorodheshe majina. Wakajiorodhesha majina, kumbe kile Kijiji tayari kinachukuliwa na Jeshi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuwalipa.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Eh!

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake kilichojitokeza, wale wananchi wanaendewa na wale Waarabu wanye madevu makubwa yanayoning'inia hapa, kweli hawa ni Jeshi? Hiki kijiji kweli kimevamiwa na Jeshi hiki? Kwa nini waende wale Waarabu? Ndio wanakwenda kule kuangalia na wanasema *khel khel khel,* wanazungumza mle. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wana sintofahamu, wanasema hiki kijiji pengine sio jeshi hawa, jamani kilio hiki Mheshimiwa Waziri hebu kama unaona uongo, tufuatane twende kwenye hicho Kijiji cha Kikungwi ukaone hali halisi iliyokuwepo kule.  Hatari hii kwa sababu kila mahali Ubago, Jeshi; Nunga, Jeshi; sasa hivi Kikungwi, Jeshi; kuna Unguja Kuu, kuna Cheju, huko kote ni mahali pa Jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashangaa kwamba Kikungwi wamekwenda kuorodheshwa watu kuhusu mazao yao. Mwisho wa Habari, wanakwenda Waarabu sasa. Haya, tuseme nini hapo? Kweli hilo ndiyo Jeshi? Jamani Serikali, mwangalie, tusije tukavamiwa hapa, ikaja ikawa balaa imetutokea hapa, akina mama wenyewe kama mnavyotujua, hatuna nguvu hizo na wengi kule ndio wanaolima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu kwa mpango huu ipangwe siku waende wakaangaliwe wale watu kwenye Kijiji kile cha Kikungwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuhusu Watumishi wa Umma wastaafu. Kama ninavyokwambia, watumishi wa Umma wamefanya kazi Serikali hii miaka mingi mpaka wamefikia kipindi kile cha kustaafu, miaka yao 60 au 65 au 55, sheria ipo hiyo. Wamefanya kazi, lakini mwisho wa Habari, stahiki zao bado wengine mpaka leo hawajalipwa ingawa Serikali inawalipa. Naishukuru Serikali yangu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inafanya kazi kubwa sana kuwalipa hawa wastaafu ambao walistaafu katika nchi yetu, lakini bado wanasikitika, wanasema mafao yao hawajapewa. Hili nalo naomba liangaliwe kwa kina, hawa wenzetu walipwe stahiki zao kwa mujibu wa sheria inayohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, mimi hapa pamenitosha. Naunga mkono hoja asilimia mia moja kwenye bajeti yangu hii ya mpango iliyowasilishwa hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, nilimtaja Mheshimiwa Oran Manase Njeza na Mheshimiwa Joseph Kakunda, ajiandae.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana nami kupata fursa hii ya kuchangia na kutoa maoni yangu kwenye bajeti hii ya Serikali. Nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Tanzania na Serikali nzima kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani yetu imetekelezwa vizuri mno na kwa asilimia nzuri mno, na nina imani katika kipindi hiki kinachoishia mpaka Juni kwa kweli tutakuwa tumefanya yale ambayo hayakutegemewa kutokana na changamoto za kidunia zilizokuwepo. Wengi hatukutegemea kuwa bajeti hii itatekelezwa kwa kiwango hiki hasa kutokana na vita ambayo imetukumba dunia sasa hivi, pia na ugonjwa wa UVIKO. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana vilevile kwa Serikali na Mheshimiwa Rais kwa kuja na hii bajeti. Hii bajeti ni ya kimapinduzi, hii bajeti tunaweza kusema ni ya kimapinduzi au kwa lugha nyingine wanasema *transformation budget*, imetuonesha mwelekeo mzuri mno na ukiangalia dhima ya mpango wetu ni kujenga uchumi shindani na viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ina maana kubwa mno kwa vile uchumi shindani hatushindanishi mazao yetu au mashirika yetu hapa, lakini tunashindana *globally,* tunashindana dunia nzima. Kwa hiyo, uchumi wetu tunapouangalia kibajeti, tuangalie sisi je, ni sehemu gani

ya dunia ambayo tumeimega na nchi yetu inahakikisha kuwa inakuwa na ushindani ambao ni mzuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hii bajeti, kwa kweli kwa kiasi kikubwa imekidhi. Ukuaji wa *GDP* imeonesha kuwa katika kipindi cha *COVID* nchi yetu ilifanya vizuri, lakini hata hiki kipindi tunachokwenda, ukuaji wa asilimia 5.3 ni wajuu kuliko nchi zote za Kusini mwa Jangwa la Afrika. Hiyo rekodi ni kubwa sana ukilinganisha na wastani wa 4% tu ambapo nchi nyingine zote ni 4%, sisi tuna asilimia 5.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia vile vile, tunaendelea kuhakikisha uchumi wetu unaendelea kuwa imara. Mfumuko wa bei ambao ni kati ya 3% mpaka 5% na sasa hivi ni chini ya 4%, hiyo ni rekodi nzuri sana. Kwa sababu katika hiki kipindi ambacho mfumuko wa bei duniani ni mkubwa, hata nchi zilizoendelea zimeshindwa kuhimili kuweza ku-*contain* hiyo *inflation* yao, lakini unashangaa Serikali yetu chini ya Mheshimiwa Rais, ni maajabu gani wanayoyafanya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia utulivu wa Shilingi, nilikuwa najaribu kuangalia kwa mazoea tulizoea kuona *exchange rate* ya dola ilikuwa inalingana na bei ya *petrol* kwenye kituo cha mafuta, lakini leo hii mafuta ni zaidi ya 3,000, lakini *exchange rate* ni Shilingi 2,300/=. Ina maana Benki Kuu na Serikali kwa jumla wanafanya vizuri mno. Kwa hiyo, hata ile *imported inflation* nayo bado haijatuathiri kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Mheshimiwa Waziri umefanya kazi nzuri sana na timu yako, na nimefurahi zaidi nilipoona bajeti yako imeweka kipaumbele cha kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kinaajiri asilimia 65 ya Watanzania, lakini kilimo kinachangia asilimia 25 tu ya uchumi. Kwa kweli huo uwiano siyo mzuri, haiwezekani Watanzania zaidi ya asilimia 65 wachangie tu asilimia 25 ya uchumi. Hiyo siyo dalili nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza Serikali iangalie, pamoja na bajeti ya kilimo kuongezeka kutoka Shilingi bilioni 294 mpaka karibu Shilingi bilioni 954, ongezeko hilo ni kubwa mno; ni mara tatu. Kwa hiyo, tunategemea mchango wa kilimo uende mara tatu; na ukienda mara tatu nchi hii itakuwa imefika mahali pazuri mno. Mchango wa kilimo ulikuwa mdogo kwa sababu ya ufanisi, lakini tunashukuru kwa mpango aliokuja nao Waziri wa Kilimo, unatuonyesha kuwa unaweza kututoa hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kwa sababu, bila kuhakikisha kuwa kilimo kinatutoa hapa tulipo, nchi yetu itakuwa ni maajabu tukipata hayo maendeleo tunayoyafikiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za kigeni tunazitegemea kutokana na mazao ya kilimo, madini na utalii, lakini zaidi zaidi tunategemea kwenye kilimo. Kwa hiyo, tunaomba nguvu kubwa iende kwenye kilimo. Tunashukuru kwa ruzuku ya mbolea, lakini hii ruzuku ya mbolea iliyooneshwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa 80, kile kiasi alichokitaja mwanzoni na hata alichokitaja Waziri wa Kilimo hakijaonekana. Amezungumzia tu ya kwamba katika kilimo kutakuwa na ruzuku ya pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunakuomba ruzuku ya pembejeo ya mbolea ilenge kupunguza bei ya

mbolea zote wanazotumia wakulima kwa mazao ya biashara na vilevile mazao ya chakula. Hiyo itatupeleka mahali pazuri zaidi, kwa sababu sasa hivi *commodity prices* zinakwenda vizuri sana. na kwasababu *commodity prices* zinakwenda vizuri, tukizalisha tunahitaji masoko, na masoko yanahitajika ya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba *commodity exchange market* iimarishwe. Hii itasaidia uhakikika wa masoko ya mazao yetu, lakini unapoimarisha hii, uimarishe pia *warehouse receipt finance*. Ni muhimu kwa vile zinaenda pamoja. Pamoja na hiyo, tunaomba usajili wa ma-*warehouse* yote na sheria ibadilike ili kulinda hizi *warehouses* na hii biashara yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana, kuna huu mfumo mpya wa ujenzi wa barabara wa *EPC and finance*. Huu mfumo inabidi uwe *coordinated* vizuri kwa sababu inawezekana Wizara ya Ujenzi ikaenda na huu mfumo ikategemea labda ni *free lunch,* yaani ni kitu ambacho tutapewa bure, Hapana. Huu ni mkopo. Kwa hiyo, tuangalie hii mikopo tutailipa namna gani? Kwa hiyo, zile *securities,* zile *mortgages* ambazo tutazifanya, tuwe waangalifu kwa kuangalia nchi za wenzetu walifanya nini mpaka wakaangukia kubaya kwa ajili ya hii mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetajwa barabara ya Tanzam kipande cha Igawa - Mbeya mpaka Tunduma. Hiki kipande ni muhimu sana kwa ajili ya biashara ya bandari. Naomba sana, inawezekana huu mfumo haujawa tayari, lakini katika hii barabara kuna kipande cha Uyole - Songwe *bypass* wananchi hawajalipwa fidia mpaka leo. Hebu walipeni fidia wale wananchi tunaposubiri hii mipango. Naomba ujenzi wa hii barabara

upewe kipaumbele, na barabara zote za Isionje - Kikondo - Makete nayo ipewe kipaumbele kwani ilishaanza, na ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mbalizi - Makongorosi ipewe kipaumbele; na barabara ya Mbalizi - Shigamba ipewe kipaumbele. Vilevile kumalizia ujenzi wa uwanja wa ndege wa Songwe uliopo Mbeya upewe kipaumbele. Hii itaenda pamoja kuhakikisha kuwa mazao yetu yanafika kwenye masoko ya kidunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Oran Manase Njeza. Nilimtaja Mheshimiwa Mheshimiwa Joseph Kakunda na Mheshimiwa Jackson Kiswaga, ajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi kwa pole mbili; pole ya kwanza, unapoisoma ile hali ya uchumi iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha jana asubuhi, unaona kabisa kwamba kuna mazingira magumu kabisa ya uendeshaji wa uchumi katika dunia; na kwa sababu Tanzania siyo kisiwa, nasi tumefikiwa na matatizo makubwa sana ya uendeshaji wa uchumi wetu hususan kutokana na matatizo haya ya UVIKO-19 na matatizo haya yaliyoletwa na vita vya Urusi na Ukraine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli naipa pole sana Serikali, lakini naunga mkono juhudi za Serikali ambazo zimetajwa na Waziri wa Fedha. Hongera sana kwa juhudi hizo, nakuunga mkono sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pole ya pili; ni ushawishi mbaya dhidi ya juhudi za Serikali kulinda rasilimali zetu hususan maliasili na utalii, hasa hasa kwenye eneo letu la Ngorongoro. Tunaona kwamba Rais amefanya juhudi kubwa sana, ameongoza filamu ya *Royal Tour* ili tuongeze watalii, lakini ushawishi mbaya unaweza ukasababisha watalii wakaogopa kuja Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana sana, tunahitaji kulinda maliasili na utalii wetu kwa nguvu zote. Hapa msisitizo niweke kwenye Ngorongoro, nikitoa takwimu kidogo. Hifadhi ya Ngorongoro ni sehemu ya ikolojia kuu tatu za hifadhi. Kwanza ni ikolojia ya Serengeti; pili ni ikolojia *Nato-Longido and Events Amboseli* na tatu ni ikolojia ya Manyara – Tarangire. Hizi zinahusiano wa moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikolojia hizo ni muhimu kwa mazalio na *movements* za wanyama wanaokaribia karibu milioni tatu kwa eneo hilo. Eneo hilo la Hifadhi ya Ngorongoro linatambuliwa na *UNESCO* kama urithi wa dunia. Kwa hiyo, ni lazima tuulinde urithi wa dunia ambao ndiyo urithi wa Watanzania wote. Maana yake tunapozungumzia habari ya maliasili ipo mahali fulani, siyo mahali hapo tu, bali maliasili hiyo ni ya Taifa zima. Kwa hiyo, kupinga juhudi za Serikali kama zilivyoelezwa humu Bungeni na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hiyo haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye eneo la pongezi. Kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Rais na timu yake yote ya Mawaziri kwa utekelezaji mzuri sana wa Ilani ya Uchaguzi. Sisi tunatembea kifua mbele, hata Jimboni kwangu kule natembea kifua mbele, kwani miradi mingi imetekelezwa kwasababu ya mawasiliano

mazuri kati ya Madiwani na mimi Mbunge na kati ya mimi na Serikali kupitia Mawaziri kwenda kwa Rais. "Usione vyaelea vimeundwa." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya watu wanajaribu kuwatoa Madiwani kwenye mafanikio, wasiwatoe Madiwani. Kuna watu wanamtoa Mbunge kwenye mafanikio, wasimtoe Mbunge. Kuna watu wanamtoa Rais; nasema hivi "usione vyaelea, vimeundwa." Ushirikiano kati ya Diwani, Mbunge na Rais ndiyo umesababisha kufanyika yote hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi ya pili katika uchumi wa kisasa, ili tuendelee tunahitaji kuendeleza uwekezaji katika sekta za uzalishaji, biashara na viwanda, na sekta nyingine. Wawekezaji wanahitaji maeneo manne muhimu. Eneo la kwanza, wanahitaji gharama nafuu za usafiri na usafirishaji. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Serikali nzima kwa jinsi alivyowasilisha hapa mipango ya kujenga barabara, mipango ya kujenga reli, mipango ya kujenga bandari, mipango ya kujenga *airport*, mipango ya kujenga usafiri wa majini. Kwa hiyo, hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili, wawekezaji wanahitaji gharama ndogo za huduma za uendeshaji wa mitambo. Napongeza juhudi za Serikali katika kuboresha upatikanaji wa mafuta, kueneza umeme na maji. Haya yanahitaji wawekezaji. Eneo la tatu, wawekezaji wanahitaji malighafi ya uhakika. Napongeza juhudi za Serikali za kuboresha Sekta ya Kilimo ambayo bajeti ya kilimo imeongezwa, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wanahitaji wafanyakazi wenye ujuzi. Kwa hiyo, napongeza sana

juhudi za Serikali kupitia hotuba ya bajeti ambayo imesema itajenga vyuo vya ufundi katika Wilaya zote vyuo vya *VETA*, hongera sana. Naipongeza Serikali sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napongeza Serikali kuondoa mfumo wa mapato kwenye sheria ya kodi. Nawapongeza Serikali kuboresha mfumo wa ununuzi wa umma kwa ajili ya kupunguza udanganyifu, hongera sana. Nawapongeza Serikali kuendeleza matumizi ya TEHAMA kwenye kazi za Serikali ili kupunguza matumizi, hongera sana. Napongeza juhudi za Serikali kuanza maandalizi ya Sera ya Taifa ya ufuatiliaji wa Tathmini, naipongeza sana. Naipongeza Serikali kuboresha ukaguzi wa ndani na kujenga uwezo zaidi wa *CAG,* napongeza sana sana, hongera sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nina maeneo matano ya ushauri na ninaomba mnisikilize. Eneo la kwanza ambalo nashauri; Serikali imeondoa ada ya Kidato cha Tano na cha Sita; hiyo ni safi kabisa, hongera sana. Ila wakati wanapofanya uchaguzi wa vijana kwenda *Form Five* na *Form Six,* ndiyo kipindi hicho hicho Serikali hufanya uchaguzi wa vijana wanaokwenda kusomea kozi za kati za ujuzi. Kwenye vyuo vya kati; kwa manesi, mafundi maabara na nini, hao nao wanahitaji msamaha wa ada, tumewasahau. Naomba sana Serikali izingatie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili; Serikali imependekeza kupunguza asilimia 10 ya mikopo ya akina mama walemavu na vijana kwenye Halmashauri. Kama unatoa asilimia tano Sikonge unaileta kwenye TAMISEMI halafu ikajenge soko la wamachinga

Dodoma Mjini, hapa unakuwa hujawatendea haki watu wa Sikonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba yale majiji na manispaa ambayo wana mipango ya kujenga hayo mabanda ya wamachinga, ndiyo hao wapatiwe hiyo asilimia tano iende kule, lakini Halmashauri za Wilaya ambazo hazina mpango wa kujenga mabanda ya wamachinga, waachiwe asilimia 10 zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa tatu; wakulima wanapouza mazao yao, naomba walipwe ndani ya wiki moja. Kule Sikonge imejitokeza wakulima wa tumbaku wameuza mazao yao mwezi wa Tano, kuna mtu anatangaza anasema watalipwa mwezi wa Nane. Naomba sasa Serikali iingilie kati wakulima wetu walipwe haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne; wananchi wa vijijini wanaotaka kupimiwa ardhi zao, labda wanahitaji mikopo kwenye benki, hawawezi kupima ardhi zao. Naomba sana Waziri wa Fedha anapoleta *Finance Bill* aainishe maelekezo kwamba anaelekeza kupitia Sheria ya Fedha kwamba mtu yeyote anayetaka kuwekeza vijijini kwa kuomba mkopo, ardhi yake ipimwe bila kusubiri mpango wa matumizi bora ya ardhi ya Kijiji iishe, isipokuwa tu maombi yake yawe yameidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji, Halmashauri yake pamoja na Mkuu wa Wilaya, hapo apimiwe ili kusudi tupate maendeleo vijijini na watoto wa vijijini waweze kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kwa uratibu wa Mkuu wetu wa Mkoa; tuna Mkuu wetu wa Mkoa mzuri sana, siyo kwa sura tu, hata kwa kazi, Dkt. Batilda Buriani anafanya vizuri. Ameanzisha mpango wa kujenga Chuo

Kikuu cha Tabora. Wale ambao wanafahamu historia ya elimu ya nchi hii, watakubaliana nami kwamba Chuo Kikuu cha Tabora kilikuwa kijengwe miaka 50 iliyopita. Sasa kwa sababu tumechelewa, naomba Serikali iunge mkono juhudi za Mkuu wetu wa Mkoa kujenga Chuo Kikuu cha Tabora haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Kakunda. Nilimtaja Mheshimiwa Jackson Kiswaga na Mheshimiwa Munde Tambwe ajiandae.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hoja hii muhimu ya bajeti kuu ya Serikali. Kwanza nianze kumshukuru Rais kwa kazi nzuri anayoifanya hasa kwa kutengeneza ile filamu ya *Royal Tour* ambayo tumeshuhudia na tumepata taarifa kwamba tayari wageni wengi wanaanza kumiminika hasa Kanda hii ya Kaskazini kwa sababu ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimnukuu Isaac Newton alisema, "*an object will remain at its original state or rest until a relevant force is applied.*" Kwamba kitu kitakaa katika hali yake ya kawaida au katika eneo lake la asili mpaka nguvu fulani itumike kukisukuma na ndiyo hicho ambacho Rais amefanya, amesukuma utalii wetu na sasa tunaona matokeo. Ni kweli kulikuwa kuna sababu ya kuutangaza utalii kwa sababu katika sehemu nyingi za dunia wenzetu wamekuwa wakitumia fursa hasa ya kutangaza Mlima Kilimanjaro na maeneo mengine kupita njia za nchi za jirani ili kuingia kwenye nchi yetu. Kwa hiyo, hiki ni kitu kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wamekuwa wakilalamika kwamba sasa kwa nini utangazwe utalii kwa wakati huu na tuko kwenye mfumuko wa bei na mambo mengi? Nimnukuu tena mwanaharakati mwingine ambaye anaitwa John Mason wa *Insight International,* yeye alisema hivi, "*in trying times we should not stop try.*" Katika nyakati ngumu na nyakati za majaribu tusiache kuthubutu wala tusiache kujaribu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namshukuru Rais kwa hilo, amethubutu na kwa vile maisha hayaishi leo, ni lazima tuendelee kufanya mambo ambayo yatakayosaidia Taifa liende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiangalia hapo hapo kwenye utalii, kule Iringa tunayo ile Mbuga ya Ruaha *National Pack,* ukiangalia kitakwimu ni kwamba ile mbuga ni ya pili hapa Tanzania ikiwa na eneo kubwa la kilomita za mraba 20,226 ambayo ni ya pili kwa Tanzania. Ilikuwa ya kwanza, lakini sasa Mwalimu Nyerere imeizidi, mwaka 2008 tulivyoongeza lile Bonde la Usangu ilikuwa ya kwanza, lakini sasa ni ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia duniani ni mbuga ya sita, lakini pia wanasema kwamba ni ya 10 duniani kwa kuwa na simba wengi. Hata hivyo mbuga hii ya wanyama inatembelewa na jamii ya ndege wapatao 574; kabila za ndege mbalimbali duniani ambao wanatoka Ulaya, Australia, Madagaska na nchi nyingine za Afrika, wanakwenda Mbuga ya Ruaha kwa nyakati tofauti. Kwa hiyo, kuna kuhama kwa hawa ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ukiangalia katika nchi hii ndiyo mbuga ambayo haitembelewi kabisa.

Sababu ni nini? Sababu ni miundombinu, lakini tunamshukuru Rais, sasa amesaini mkataba ambao utakwenda kujenga barabara ya kwenda *Ruaha National Pack* na hivyo huu utalii utakwenda kukua hata Nyanda za Juu Kusini. Na kama ambavyo tumekuwa tukizungumza mara zote, ni muhimu sana sasa watalii wakatawanywa katika nchi yote ili sasa kupunguza uharibifu unaoendelea kule Kanda ya Kaskazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuhusiana na *Royal Tour* kwamba amefanya sehemu ya kwanza, ni sehemu ndogo, kwa sababu ya mafanikio ambayo tayari tumeanza kuyaona, nashauri kwamba hii *Royal Tour* iwe kwenye *series,* yaani kuwe kuna toleo lingine tena. Hili toleo litakalofuata liingize mbuga za Ruaha ambazo kipekee utakuta kuna mnyama pale anaitwa tandala ambaye hayupo sehemu nyingine; utaingiza Mbuga za Kitulo na maeneo mengine kama *Kalambo Falls* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya namna hiyo, tutakuwa tumeutangaza utalii vizuri na utalii wetu utaendelea kukua. Pia kwenye utalii ni muhimu sana sasa kama nchi tusiangalie utalii wa wanyama peke yake, tuangalie utalii wa namna tofauti. Unaweza ukawa utalii wa mavazi. Kwa mfano, kule Iringa tuna mambo yale ya migolole, ni utalii. Kwa hiyo, tuangalie utalii kwa mapana yake, tusiangalie tu utalii wa wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wenzetu walioko kwenye utalii naomba waweze kuangalia kwa mapana yake. Kule kwetu kuna mapango ambayo Mkwawa alikuwa anajificha; nayo yanaweza yakaingizwa kwenye utalii. Viko vitu vingi. Kwa hiyo, tuwaanchie wao, naona watafikiria namna ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ule mradi wa *Regrow* ambao ulikuwa na mpango wa kuifanya nchi Nyanda za Juu Kusini iwe hadhi ya utalii. Tuna kituo kinatakiwa kijengwe pale Iringa, tunaamini Serikali itakwenda kwa haraka kufanya hivyo, tukiunganisha pamoja na uwanja wa ndege ambao inaonekana kwamba sasa hivi wamegundua kuna mwamba pale chini ambapo inaonesha kwamba tutachelewa kumaliza ule uwanja kwa miezi 36 zaidi. Naiomba Serikali ione namna gani ya kuweza kuharakisha hilo ili tufanye utalii wetu kuwafungamanishi tukiwa na ndege, barabara na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikizungumzia ile Bodi ya Stakabadhi Ghalani. Nimezungumzia kwenye biashara, na pia nilizungumzia kwenye kilimo. Sasa hapa nataka kushauri nini? Wakati tunaanzisha hii Bodi ya Stakabadhi Ghalani mwaka 2005, kulikuwa kuna kipengele katika sheria ambacho kilikuwa kinaipa hii mamlaka kujasili maghala yote yaliyoko nchini. Isipokuwa tulipofanya marekebisho mwaka 2016, hiki kipengele kikaondolewa. Maana yake sasa tumemwondolea mamlaka huyu Mkurugenzi wa Bodi za Maghala, hana meno tena ya kuweza kusajili maghala yote yaliyoko nchini pamoja na yale ya binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ni muhimu kusajiliwa? Ni lazima kwa sababu tukisajili haya maghala yatatusaidia kujua mazao ambayo tunakuwa nayo tangu kutoka kule chini vijijini. Kwa hiyo, naiomba Serikali na Waziri husika kwa wakati unaofaa wailete hii sheria tuifanyie marekebisho ili tumpe meno huyu Mkurugenzi wa Bodi za Stakabadhi Ghalani aanze kusajili maghala yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia jambo lingine, tunazungumzia suala la bajeti, lakini pia kuna changamoto kubwa ambayo imeanza kujitokeza sasa hivi, watu kutotoa hizi risiti za *EFD*. Mtu mmoja mwenye hekima alisema, "*men were created to be controlled and guided.*" Kwa maana gani? Kwamba wanadamu waliumbwa ili wasimamiwe na waongozwe. Tukiwaacha hawa wanadamu, wanafanya mambo wanayotaka. Kwa hiyo, sasa hivi hawatoi risiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna bidhaa nyingi ambazo zinaingia kutoka nje kupitia hii mipaka, ni kama *panya road* fulani hivi, maeneo ya Bagamoyo, Tunduru na maeneo ya mipaka mbalimbali ya nchi. Kwa hiyo, bidhaa nyingi zinaingia kwa njia ya *panya road*. Sasa kama tukiacha hii iendelee, tutafifisha nguvu ya Serikali kuweza kukusanya mapato na kuhudumia wananchi wake na kufanya miradi mingi ambayo Serikali inatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia, tumeongeza ajira nyingi, tumeongeza mishahara, lakini sasa kama hatuwezi kukusanya kodi, itakuwa ni kazi kubwa sana Serikali kuweza kutima malengo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nigusie hili suala linaloendelea kuhusu Ngorongoro. Najua rafiki yangu Mheshimiwa Shangai tumekuwa tukizungumza mambo mengi, lakini nizungumzie suala hili, kwamba ni kweli mchango mkubwa wa utalii kwenye nchi hii unatokana pia na Kanda ya Kaskazini hasa eneo la Ngorongoro. Katika sheria za nchi hii ni kwamba hakuna Mtanzania, mimi au yeyote mwenye haki ya kusema kwamba hii ni ardhi yangu nitakaa milele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anayemiliki ardhi katika nchi hii ni Rais na Serikali inaweza wakati wowote inavyoona inafaa ikaichukua ile ardhi kwa matumizi ambayo yana faida pana kwenye Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama walivyosema wenzangu, mwaka 1974 nchi hii iliamua kuhamisha watu kutoka katika maeneo waliyokuwa wamekaa, wametawanyika, kuwaleta kwenye vijiji. Sababu zilikuwa nyingi, pamoja na kuwapa huduma kwa karibu na mambo mengine. Ila ili nasi tuweze kuendelea kuutunza utalii wetu, iko sababu ya kuendelea kuilinda Ngorongoro na nchi hii kama unavyosema kwamba hakuna kabila ambalo linaweza lika-*claim* kwamba hapa ni pakwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda hata kule Iringa utakuwa Wamasai wengi sana wanaishi kule na wamegombea mpaka Ubunge. Ukiangalia pale Isimani wapo, huwa wanagombea gombea mpaka Ubunge. Kwa hiyo, tusilete chokochoko kuonekana kwamba kuna kabila fulani moja au Wahehe au Wapare wenye uhalali sana kwamba hii ardhi ni ya kwao; *Sukuma land or Hehe land* au *Masai land*. Nafikiri tusilete huu mchanganyiko, tunafanya hili jambo liwe gumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweka uzalendo mbele, tujue kwamba nchi hii ni ya kwetu, na kama kuna chokochoko yoyote ambayo inagusa maslahi ya nchi, ni lazima wote tuungane kwa ajili ya kusudi jema la kuhakikisha kwamba nchi yetu inaimarika kiuchumi na tunakuwa wamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala lingine kuhusu Bandari ya Bagamoyo. Bandari hii ni muhimu sana katika uchumi wa nchi. Ni kweli kumekuwa kuna malalamiko mengi kwamba namna mikataba hii ambavyo ilikuwa imesainiwa ambayo hata sisi hatuijui, ilikuwa ya ovyo. Hata hivyo, bado kuna sababu ya kuendeleza hii Bandari ya Bagamoyo kwa sababu ziko meli kubwa sana duniani ambazo haziwezi kutua katika nchi yetu ya Tanzania, sasa lile eneo la Bagamoyo lina upana mkubwa ambapo tunaweza tukalipanua na tukaleta meli kubwa na uchumi wetu ukaweza kwenda kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali ione ni namna gani inaweza kuendeleza ile Bagamoyo, na mfumo wa uendeshaji wa hizi bandari nashauri uwe kwa mfumo wa kushirikiana kati ya *private sector* na Serikali ili kuweza kuharakisha maendeleo. Kwa sababu *private sector* inavyoingia kwenye kuendesha jambo, maamuzi yake yanakuwa ya haraka. Ila mara nyingi kwenye Serikali zote duniani maamuzi huwa yanakuwa ni ya polepole sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jackson Kiswaga. Nilimtaja Mheshimiwa Munde Tambwe, baadaye Mheshimiwa Yahaya Massare na Mheshimiwa Grace Tendega wajiandae.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia bajeti yetu ya Serikali. Awali ya yote nianze kumpongeza Waziri wa Fedha kwa kazi kubwa anayoifanya. Pia nampongeza Naibu wake, Katibu Mkuu na *management* nzima ya Wizara ya Fedha. Hakika wanafanya kazi kubwa, kazi nzuri na tunaiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitachangia vitu kama vitatu. Nitachangia kuhusu *force account,* lakini mambo ya *TANePS* ambayo yameongelewa kwenye bajeti yetu. Vile vile nitachangia kodi ya ardhi, na muda ukinitosha nitaongeza na *block farm,* maana hii ni ajenda yangu ya kila siku mpaka kieleweke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipate nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa, hakuna mtu asiyejua. Mheshimiwa Rais anapambana usiku na mchana kuhakikisha maendeleo ya Watanzania yanapatikana; lakini tu siyo maendeleo ya vitu au maendeleo ya majengo, anataka maendeleo ya Mtanzania mmoja mmoja aonekane na yeye anaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezoea kusema uchumi umepanda sijui kwa *five point six*, *seven point* ngapi, lakini Mtanzania wa kawaida mfukoni kwake hakuna hela. Nadhani Mheshimiwa Rais amejikita kuleta maendeleo kama Taifa na pia kuleta maendeleo kwa Mtanzania mmoja mmoja. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, anafanya kazi kubwa, tumemwona kwenye *Royal Tour* kule maporini kazi anayoifanya. Yote hiyo ni kuhangaika Watanzania wawe na maisha mazuri. Amekuwa ni Rais lakini ni mama, sisi wote ni watu wake, akituangalia nadhani halali usiku, anaendelea kuhangaika kwenye

Mataifa mbalimbali kuhakikisha hatukwami na mambo yanaenda. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, tunamtakia kila la heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Rais aendelee kusafiri ili watoto wake tuendelee kuneemeka. Yeye ni baba sasa, lazima atoke akahangaike kuhakikisha nchi yake inaenda vizuri. Tunampongeza sana. Kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Rais ungeniuliza mimi ningesema basi Mheshimiwa huyu apate nafasi 2025 Watanzania wote tumuunge mkono bila kuleta mgombea yeyote wa chama chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia na *force account*. Serikali imepeleka pesa nyingi sana za maendeleo kwenye halmashauri zetu, lakini miradi mingi inasimamiwa na *force account*. Sasa tunazungumzia bajeti kupanua wigo wa kodi. Naangalia miradi hii yote iliyofanywa na *force account* mafundi wote wa *force account* hawalipi kodi yoyote ya Serikali. Akishalipwa ile pesa ni ya kwake halipi kodi yoyote ya *TRA*. Sasa niiulize Serikali, kwa nini miradi hii isijengwe na wakandarasi? Mkandarasi atamwajiri huyo fundi anayejenga kwa *force account* ataajiriwa na mkandarasi. Mkandarasi ataajiri vijana wetu, mainjinia waliosoma wako mtaani, ataweka kama mainjinia wake; ataajiri vibarua; pia mkandarasi huyu atalipa kodi ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapopeleka *force account* unakuta halmashauri ina miradi 18 au ina miradi 19 inaiendesha lakini ina injinia mmoja au mainjinia wawili. Hawa mainjinia wawili wanawezaje kwa pamoja kusimamia miradi 19? Unakuta *value for money* haiko sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, sera yetu ni makandarasi, ma-*contractor* kufanya kazi. Rudisheni kazi hizi kwa ma-*contractor*. *Force account* kwanza ilitoka wapi jamani? Yaani mimi hata sijui ilipotokea. Tupelekeni kazi kwa makandarasi, watalipa kodi ya Serikali. Hawa *force account,* mafundi wote mliowaweka hawajawahi kulipa kodi ya Serikali, wala hawalipi, wala hawajulikani kwenye Serikali wala hawajasajiliwa sehemu yoyote, wala hawana leseni, wala hawana *TIN*, wala hawana *VAT*, lakini wanafanya kazi za Serikali na wanalipwa pesa na Serikali. Kwa hiyo, mnapoteza mapato mengi sana kwa miradi yote hii iliyotendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani tumekuwa tunafanya vitu vya ajabu ajabu! Kwa mfano, hela zinakwenda kwenye shule za kujenga madarasa na kadhalika. Anaambiwa Mwalimu Mkuu asimamie majengo yale. Mwalimu Mkuu ana utaalam gani wa kusimamia majengo? Mwalimu Mkuu asimamie zile fedha na atakuja kukaguliwa. Hakusomea Uhasibu Mwalimu Mkuu; lakini shule hiyo ina Walimu saba tu au nane. Mnamtoa Mwalimu Mkuu kwenye kazi yake kwenda kusimamia majengo, na wakati huo huo tunalalamika Walimu wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itafute wataalam wa kufanya hiyo kazi na Walimu waachwe wafanye kazi zao za kiualimu. Naiomba sana Serikali yetu iwe makini sana katika hili jambo. Walimu wamekuwa wanalaumiwa. Kwa mfano, Mwalimu shule yake iko hapa, anayesimamia jengo lake la Walimu ambalo liko labda kilomita moja, nani anampa nauli huyo Mwalimu Mkuu kwenda kusimamia huko hilo jengo? Nani anamlipa posho ya kukaa kule mpaka jioni kusimamia hilo jengo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Serikali, watumishi wengine wanavyokaa maofisini wanavyolipwa posho, basi na Walimu hawa kama mmeshindwa kuweka wataalam basi muwalipe; na muache kuwakamata wanapokuwa wanashindwa kuweka hesabu vizuri kwa sababu siyo masomo yao waliyoyasomea. Wala kujenga majengo wao sio mainjinia. Huwezi kumwambia Mwalimu asimamie ujenzi wa shule, halafu baadaye unakuja kumuuliza…

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munde, subiri taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nataka nimpe taarifa dada yangu Mheshimiwa Munde kwamba *force account* zilikuwa zinasaidia sana. Mpaka sasa zinasaidia kwanza kuokoa fedha za Serikali ambazo zimekuwa zikipotea sana na pia zinawasaidia wale mafundi wetu wa ndani ambao hawawezi kukaa kwenye kampuni kuweza kufanya kazi nyingi ambazo tunaziona zimesaidia sana hii miradi ya Serikali ambayo imetekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munde unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei kabisa, kwa sababu hawa makandarasi pia ni Watanzania, wako hapa hapa na wameajiriwa. Hawa

makandarasi sio mafundi, wana kampuni zao, wanaajiri mafundi hao hao na wanawalipa pesa, lakini wanalipa kodi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunaongelea kuongeza kodi ya Serikali. Tunaongelea kuongeza mapato. Bajeti yetu tuliyonayo sasa hivi asilimia 28 tunategemea wafadhili, lakini tunatamani siku moja tuwe na bajeti yetu asilimia 100 ambayo tutajitosheleza sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naendelea kusema kwamba tunaomba makandarasi wafanye kazi ya ukandarasi kama sera zetu zilivyo, siyo ma-*local* fundi. Hao ma-*local* wataajiriwa na makandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee sasa kuhusu *TANePS*. Sasa mimi sitaki taarifa, muwe mnachangia wenyewe jamani, mnatutuoa kwenye reli.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munde taarifa ni kwa mujibu wa kanuni.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nimekusikia. Niongelee suala zima la *TANePS*. Nimesikia kwenye bajeti ya Waziri amesema sasa hivi ataweka bei *fixed* kwenye *TANePS*. Kwa hiyo, kwenye zile bei kutakuwa hakuna ushindani kama vile kutangaza tenda na watu kushindana. Kutakuwa na bei *fixed* kwenye *TANePS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najiuliza, kwa mfano *ream* ya karatasi Serikali itaweka bei ya Masumini ambaye ndio tajiri au mwenye kiwanda. Mimi nauliza, yule mwenye duka kule Irambo kwa kaka yangu

Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, duka la mtaani, ambaye halmashauri ilikuwa inafanya naye kazi ya kununua *ream* ya Masumini Shilingi 8,000/=, yeye anauza Shilingi 11,000/= au Shilingi 9,000/=. Je, Serikali itaenda kununua kwa Shilingi 11,000/= iache Shilingi 8,000/= kwa Masumini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *local content* iko wapi? Yakija makampuni ya kigeni unaambiwa lazima mwaajiri Watanzania. Nanyi lazima mfanye kazi na Watanzania wote, siyo matajiri tu. Hamwezi kufanya kazi na viwanda; najua hizo bei zitakuwa za viwanda, zitakuwa za ma-*agent* wakubwa. Sasa huyu mfanyabiashara mdogo ambaye alikuwa na *cement* yake kwenye halmashauri atauzaje kwenye Serikali tena? Serikali itanunua kiwandani moja kwa moja ndiyo itakuwa bei *fixed* ambayo iko kwenye *TANePS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa na miradi ya UVIKO walianza hivyo hivyo, tununue moja kwa moja kwenye viwanda. Ndiyo maana nimesema, Mheshimiwa Rais anataka pesa ziingie kwenye Serikali lakini na mtu mmoja mmoja. Akasema pesa hizi zipelekwe halmashauri na vitu vinunuliwe kwenye halmashauri husika, na pesa zilionekana, kwenye Serikali mambo yalionekana, na kwa mtu mmoja mmoja Watanzania walipata pesa. Ila Mheshimiwa Waziri mambo ya kutuwekea bei za *fixed* kwenye *TANePS* mjue kabisa masikini wote hawatauza, watauza matajiri na wenye viwanda tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mkurugenzi wa Halmashauri hawezi kununua pia kwenye halmashauri yake *ream* ya Shilingi 12,000/= wakati Masumini Dar es Salaam ni Shilingi 8,000/=. Sasa napata shida, naangalia bajeti ya Kamati ya Fedha Shilingi 700,000/= pamoja na posho za Madiwani. Anaanzaje kuagiza *ream* za Shilingi

200,000/= kwa Masumini? Maana akinunua hapa itakuwa bei siyo ya kwenye *TANePS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie hili suala vizuri, iache ushindani wa bei. Wameongeza, Mheshimiwa Waziri amesema hapa anaongeza *exchequer auditor,* amewapa pesa ili waongeze kuajiri.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Kazi ya Serikali ni hiyo, kuangalia mapato yake yasivuje, lakini siyo kuwabana Watanzania waache kufanya biashara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munde, kengele ya pili imelia, nilikuachia umalizie sentesi yako.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Munde Tambwe. Tunaendelea na Mheshimiwa Yahaya Massare, nilimtaja halafu Mheshimiwa Grace Tendega ajiandae.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii nami nichangie hotuba hii ya Serikali, Bajeti Kuu. Nami nichukue fursa hii kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambazo amezifanya hapa kati, ametuonesha kwamba fedha kiasi akiutumia mtiririko ambao ameutumia hapa juzi, una matokeo chanya zaidi kuliko mfumo ambao tunautumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alipopata zile Shilingi trilioni 1.3 alizigawa na akatoa maelekezo ya moja kwa moja zikajenge vituo shikizi na hospitali kwa maana ya vituo vya afya na maeneo mengine. Tumeona jinsi ambavyo kwa kutumia *Force Account*, tumejenga vitu vizuri sana na vya thamani na thamani ya fedha imeonekana. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuleta fedha hizi kule kwenye Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Waziri na Naibu Wake, Katibu Mkuu ambaye ni Mlipaji Mkuu wa Serikali, Watumishi wa Wizara ya Fedha na Kamati ya Bajeti kwa kutusaidia. Wameonesha namna ambayo kwa miaka mingi ya nyuma, usikivu wa Waziri wa Fedha umekuwa mkubwa sana kwa kipindi hiki. Amesikia ushauri mkubwa wa Wabunge tuliochangia katika Bajeti za Wizara na Serikali imekuja na majibu mengi ya hoja za Wabunge ambazo tulikuwanazo kipindi cha miaka miwili mitatu hapo nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo ambalo lilikuwa ni mwiba sana, kuunganisha mikoa kwa barabara. Mkoa ambao mimi natoka, Singida, kelele ya miaka mingi kwa Marais zaidi ya wanne nyuma, ilikuwa ni kuunganisha na Mkoa wa Mbeya kwa barabara ya lami. Nashukuru sana sasa Serikali imeitaja moja kwa moja kwenye bajeti. Sasa hivi ninavyozungumza, Mkandarasi ameshapewa na kiwanja cha kujenga kwa ajili ya kupeleka vifaa vya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napongeza sana kwa hatua hii ambayo, wananchi wa Mkoa wa Singida hasa Jimbo ambalo mimi natoka la Manyoni Magharibi, Halmashauri ya Itigi, wanaenda kufurahia matunda ya

Serikali yao. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hii ambayo wananchi wa Itigi wanaanza kufarijika na kuona nao ni wenzao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida bado pia haujaunganishwa na Mkoa wa Simiyu, kitu ambacho kina karaha. Naiomba Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kupitia Waziri wa Ujenzi, kupitia daraja la Sibiti, waone namna ya kuunganisha Mkoa wa Singida na Mkoa wa Mbeya. Wameitaja barabara ile ambayo inakwenda kule Hydom na kwenda kwa Mheshimiwa Flatei huyu mpiga sarakasi ambaye hapa huwa ananisababishia shida. Sasa kipande ambacho kinatakiwa kiwepo katika mpango kutoka Iguguno mpaka Ibaga, tutakuwa tumeiunga mikoa kwa barabara za lami. Pia ni barabara ambazo kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika hotuba yake, kwamba ni barabara za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutaunga barabara hii nayo tayari tutakuwa tumetenda haki kwa watu wa Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo tumeona baada ya kuletea mapesa yale mengi na Mheshimiwa Rais, yamefanya kazi, kuna uchache wa watumishi na hasa Walimu na Watumishi wa Afya. Katika kada hizi mbili kumekuwa na changamoto kubwa. Tumejenga shule ambazo tulikuwa tunaziita shikizi. Vituo shikizi sasa ni shule kamili na zimesajiliwa. Kwenye Jimbo langu tumeshasajili tayari shule 20 mpya zenye madarasa mapya kabisa manane, saba, sita; lakini walimu hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ione hasa katika jimbo langu la Manyoni Magharibi, Halmashauri ya

Itigi, kuona namna ambavyo itaweza kuongeza walimu ili wanafunzi hao wanaoenda kuanza shule hizi, waweze kupata elimu ambayo ni bora. Tumejenga vituo vya afya, na sasa tunajenga Hospitali ya Wilaya pale Itigi, pia tunahitaji watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo halijazungumzwa na Wabunge wengi. Tunaposimamia fedha hizi; Mheshimiwa Kakunda hapa amesema, sisi tunapiga maneno hapa tunaiambia Serikali, Serikali sikivu inapeleka fedha kwenye Halmashauri zetu. Wanaosimamia kule ni Madiwani, lakini Madiwani hawa hatujawaona katika hii bajeti. Madiwani wetu, posho zao baada ya kupelekwa Serikali Kuu na hasa wale ambao Halmashauri zao zinakusanya chini ya Shilingi bilioni tano, vipato vyao ni duni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali kupitia Wizara ya Fedha iangalie jambo hili na ikiwezekana waje na majibu na wenyewe tuwaone. Mheshimiwa Rais ameongeza watumishi kwa asilimia 23, hawa Madiwani hupewa tu posho, basi hata zile posho hatuwezi kuziongeza? Hebu naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapokuja, aangalie basi hawa watu ambao tunapoenda kwenye chaguzi wao ndio wanaomba kura na pia baadaye wanasimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunafika maeneo mengi, Mheshimiwa Rais maeneo mengine hafiki, lakini tunazungumza kule kwamba tunaomba kura mafika matatu, lakini haya mafika mawili tunayafanyia vizuri, hili figa moja mbona tunalisahau? Hebu tuangalie watu hawa ambao kwa hakika wanafanya kazi ya kujitolea kwa kiwango kikubwa sana, na fedha zile kule kwetu hazijaliwa hata senti mbili. Zote zimetumika katika mtiririko

mzuri kwa maana ya usimamizi wao mzuri. Sasa tunawapongezaje watu hawa? Kama watumishi wameongezwa mishahara, nao kwa nini tusiwaone? Naomba niishauri Serikali iangalie katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mwingine, tunapoenda kumaliza kujenga Stiegler's Gorge, tunapoendelea kujenga reli, basi huko baadaye tuangalie ni namna gani tunakabiliana na hali hii ya upandaji wa mafuta? Sisi tunayo fursa hapa kwamba nchi yetu ina gesi. Ni namna ya kuichakata tu ile gesi na kuifanya iweze kutumika kwenye magari madogo. Gesi iliyopo inaweza kutumika kwenye magari makubwa, lakini bado haioneshi dalili. Tumeona hapa magari ya Dangote, wameweza kuichakata ile gesi na kuitumia kwenye magari yao, sasa sisi tunashindwa nini? Kwa nini Serikali nayo isianze kutumia gesi katika magari yake ya Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri, wakati tunasubiri kuchakata *LNG*, hii *CNG* iliyopo ianze kutumika. Tumeshindwa kuisambaza; hapo hapo Dar es Salaam ni viwanda vichache sana vinavyotumia gesi hii. Hebu tuone sasa fursa tuliyonayo ili kupunguza uagizaji wa mafuta tuweze kufanya gesi hii iliyopo nchini mwetu. Kama kuna tatizo la umiliki, mikataba ilikuwa ya ovyo; tumeweza kufumua mikataba katika migodi mikubwa ya dhahabu, tunashindwaje hapa kwenye gesi ili kuinufaisha nchi hii, tupunguze uagizaji wa petroli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunaagizi *LPG*, gesi ya kupikia wakati ambapo tuna *LNG* hapa, tuna *CNG* ambayo tunaweza kutumia direct kwa kupikia. Tunafanyaje kwa namna hii? Kwa nini tusitafute namna ya kuwekeza basi? Najua uwekezaji ni mkubwa,

tulishatumia zaidi ya Dola bilioni tatu, tukatengeneza bomba kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam, leo hatuwezi kutafuta hata bomba dogo likasogea Dodoma au likaenda Mwanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kufikiri tuone tu namna gani wataalam wetu wanaweza kutusaidia ili tuondokane na hali hii tunayokwenda nayo katika kuagiza mafuta ya petroli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahaya Massare, tunaendelea na Mheshimiwa Grace Tendega na Mheshimiwa Deo Sanga na Mheshimiwa Michael Mwakamo, Mheshimiwa Cecilia Paresso na Mheshimiwa Prof. Sospeter Muhongo wajiandae.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia na mimi bajeti hii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Bajeti hii ukiingalia kwenye karatasi ni nzuri, lakini kazi ipo kwenye utekelezaji. Utekelezaji ndiyo changamoto kwa bajeti nyingi, hatujawahi kufikia asilimia 80 ya utekelezaji wa bajeti. Kwa hiyo, hata kama Mama alishasema kwamba yeye hawezi kuzungumza kwa kufoka, lakini tujitafsiri sisi kama Serikali na kama Watanzania kuhakikisha kwamba bajeti hii inatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze kwa kuangalia; hii ni bajeti ya pili kwa mpango wa miaka mitano ambayo ni 2021/2022 – 2025/2026. Dhima yake ilikuwa ni

kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Hiyo ndiyo dhima kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuweka vipaumbele vyake ambapo ameweka kilimo, mifugo, uvuvi, nishati, uwekezaji na biashara. Hivi alivyoviweka kama kipaumbele, kama kweli vitafanyiwa kazi, tuna miaka siyo miwili au mitatu, tutakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niunge mkono suala la mkakati wa kubana matumizi ya Serikali. Naunga mkono kwa sababu Watanzania kwa kweli wana hali ngumu na tumeona. Kwa mfano, masual ya magari, utaona jinsi magari anavyotumika ndivyo sivyo. Tukiangalia wenzetu tu nchi ya Jirani; Uganda, wanatumia magari yao binafsi na wanakwenda wanafanya kazi vizuri. Cha muhimu, lazima kuwe na utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba wale ambao umewaweka katika *categorization* zenu za uongozi basi wawekewe mkakati Madhubuti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la kupunguza ukubwa wa uwakilishi, nalo naliunga mkono katika vikao kusafiri umbali mrefu, kutumia TEHAMA, ni vitu ambavyo ni muhimu, hata alipokuja Mheshimiwa Rais hapa Bungeni tarehe 22/4/2022 alihimiza mambo kama hayo, TEHAMA itumike, na ndiyo vitu ambavyo tunaomba Mheshimiwa Waziri akafanyie kazi vizuri. Pia kufanyia kazi huko kuendane na kuboresha wafanyakazi ambao watakuwepo katika sekta mbalimbali za maeneo ya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tujiulize, mfumo wa kuendesha uchumi wa nchi yetu ni upi? Hamjawahi kututanabaisha kwamba mfumo wetu ni upi? Ni ujamaa na kujitegemea? Ni mfumo gani? Hatuna mfumo ambao

tunaufahamu. Kwa sababu kama huufahamu vizuri, utapanga na utatekeleza vitu ambavyo hujui unakwenda wapi? Tujipambanue na tutafsiri mfumo wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa kujibu hoja, atuambie tuko wapi sasa hivi ili tuweze kujua tunafanya nini? Kwa sababu kila aina ya uchumi inajipambanua. Hata kama ni Bima ya Afya ya Ujamaa ni tofauti na Bima ya Afya ya Ubepari au Bima ya Afya ya kitu kingine. Kwa hiyo, tukijipambanua tutajua tunawekaje mambo yetu yaende sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme, Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere alizungumza kwamba, naomba ninukuu: "Maendeleo lazima yawe na uhusiano na watu." Pia Hayati Rais Benjamin Mkapa, alisema katika kitabu chake, naomba ninukuu, anatamani mfumo wa uchumi ambao ni shirikishi. Hii ina maana gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya asilimia 67 ya watu nchini ni vijana. Kati ya hiyo asilimia 67, asilimia 13 ya hao hawazalishi hata Shilingi 100/=. Tupo kwenye majimbo yetu, tupo katika nchi yetu, nayo ni nguvu kazi. Sasa ni heri kuibua kichwa kimoja chenye ubunifu kuliko madini tuliyonayo. Kwa sababu tunaweza tukayaibua hayo madini lakini watu wa kuja kuyatumia wasiwepo. Tunataka uzalishaji wenye tija. Kama hatujawekeza vizuri kwa vijana hawa, uzalishaji utakuwa ni ndoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji mfumo wa kuinua sekta binafsi ili tuibue mabilionea wengie. Hebu tujiulize Tanzania, tuna mabilionea wangapi Mheshimiwa Waziri wa Fedha? Tunao wangapi? Nchi kama Finland, Ghana, Norway, Ujerumani, zimeweza kuwatumia wazawa wao, zimewawezesha na mpaka wameweza kufanya uchumi

wao unakuwa *stable*. Sasa sisi tunajipambanuaje kwa hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa soko huria la kijamii *(social market economy)* ni mfumo unaochukua mazuri ya Ujamaa na mazuri ya Ubepari kwa pamoja, kisha wanapata mfumo mmoja wa kuhakikisha uchumi wa mtu mmoja mmoja unakua. Sasa hiki ndiyo kitu ambacho kama Serikali itaweza kutumia mfumo huu, tunaweza tukafika mbali. Ila mfumo huu ni endelevu, misingi yake mikubwa, lazima kuwe na sera na sheria zinazotabirika kwa wawekezaji. Hatuna sera zinazotabirika kwa wawekezaji. Rais amejitahidi sasa hivi, lakini tunaomba matokeo ya utekelezaji wa sera hizo. Vile vile kuwe na ushindani, uwajibikaji, soko, umoja, motisha na ushindani mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Tanzania anayeanza biashara leo, mtu kama anataka kuanza biashara leo, anaanza kulipa lini? Tujiulize wote, anaanza kulipa lini? Lazima tuwatengenezee mazingira ambayo huyu mtu anayeanza biashara leo tumpe muda wa kuuza kulipa. Hiyo ndiyo changamoto tunayopata. Pia, kodi kiasi gani? Hiyo kodi atakayolipa itakuwa ni kiasi gani? Lazima tuwashike mkono hao wote ambao watakuja kutaka kuwekeza. Tusipofanya hivyo itakuwa ni changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni wazo langu la mwanzo. Naenda katika kipengele cha Bodi ya Mikopo. Katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri, sijaona mahali ambapo amezungumzuzia kabisa kuongeza posho ya wanafunzi wa vyuo vikuu. Ni jambo jema kwa wanafunzi wa Kidato cha Tano na Sita kusoma bure, sawa; lakini kule chuo kikuu, toka miaka hiyo wanapewa Shilingi

8,500/= wakati Dola bado ni Shilingi 1,600/=, mpaka leo Dola imepanda kuwa Shilingi 2,300/= mpaka Shilingi 2,400/=, bado wanapata kiasi kile kile, Hapana. Tuwaboreshee na hao. Pia mishahara imepanda. Kwa hiyo, tuangalie na hawa vijana tuweze kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine tuwaongezee pia ile capitation grants, tulipanga Dola moja, Shilingi 10,000/= tukawa tunawapa, tuwaongezee nao angalau ifike Shilingi 25,000/= kwa Primary School na Secondary, tuwaongezee hata ifike Shilingi 50,000/=. Hii itawasaidia watoto wetu kuweza kupata huduma bora za kielimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nizungumzie sasa kuhusu usimamizi na udhibiti wa upotevu wa mapato. Kama tunatenga hizi pesa lakini hazina udhibiti mzuri, tunatwanga maji kwenye kinu. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, ameweza kumwongezea fedha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, na vile vile ameweza kuwapa *vote* wale *internal auditors.* Nashukuru kwa sababu kumekuwa na changamoto kubwa katika uwasilishaji wa taarifa za masuala haya. Tukifanya hivyo, ndipo uwajibikaji tutauona, uwazi tutauona, tutaona tija ya fedha zetu ambazo tunazipeleka katika sekta mbalimbali huko katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Grace Tendega. Nilimtaja Mheshimiwa Deo Sanga, halafu Mheshimiwa Michael Mwakamo na Mheshimiwa Cecil Paresso wajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi nami niwe miongoni mwa wachangiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Wabunge wenzangu kwa namna ambavyo tunamshukuru Rais wetu, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea bajeti iliyosomwa na Dkt. Mwigulu, bajeti nzuri yenye mwelekeo mzuri kwa ajili ya Watanzania na Majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunasema Mheshimiwa Rais amefanya kazi nzuri? Moja, mpaka hivi sasa, haki ya Mungu kwa muda wa mwaka mmoja haijawahi kutokea fedha nyingi tunazo katika Halmashauri zetu, nyingi sana. Kwa hiyo, tunakushukuru sana. La pili, tukushukuru Dkt. Mwigulu Nchemba pamoja na Naibu wako na Katibu Mkuu wako na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri mnayoifanya juu ya kuwaletea Watanzania maendeleo. Mama amefungua milango ya nchi yetu. Kwa hiyo, Dkt. Mwigulu unakwenda katika njia hiyo, hongera, fanya kazi, chapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nawapongeza na Mawaziri wote na Manaibu Waziri kwa kazi nzuri mnayoifanya. Mnaiga mfano, mnafanya kazi nzuri sana. Wako watu hapa ambao wanabeza baadhi ya Mawaziri kwa kazi wanazozifanya. Jamani tuache ubinafsi, tuongee ukweli. Mawaziri mnafanya kazi nzuri, nzuri sana, chapeni kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna suala la maji ambalo katika Miji 28, Serikali zote zilishindwa, haijawahi kutokea, Mama ameweza, tunashukuru sana. Miradi hii

ya Miji 28 ikiwepo na Mji wa Makambako, sasa Watanzania na hasa wa Mji wangu wa Makambako, mradi huu ambao tayari umesainiwa, juzi tulikuwa Ikulu, tunashukuru sana. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu hakikisha unasimamia fedha ziende kule Makambako zikafanye kazi ya mradi huu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu kule Kusini wakulima wetu wana tatizo la mbolea hasa ya *DAP* na *UREA*, lakini kutokana na Wizara ya Kilimo, kupitia hili Waziri wa Kilimo alilowasilisha juzi hapa kwamba Serikali sasa itakwenda kutoa ruzuku, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu tunaomba ruzuku hiyo, tunaisubiri kwa hamu ili kusudi mbolea hii iweze kupungua bei. Ni imani yangu kazi hii Mheshimiwa Dkt. Mwigulu utaifanya ili kusudi wananchi wetu waweze kupata mbolea yenye bei nafuu kwa ajili ya wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sikutaka kuchangia, maana bajeti hii inajieleza, iko vizuri. Iko vizuri! Changamoto kwenye Jimbo la Makambako; tuna fidia ambayo imechukua muda mrefu pale Idofi kwa ajili ya kujenga kituo cha *One Stop Center*. Serikali imeshatoa fidia zaidi ya Shilingi milioni 870, bado Shilingi bilioni tatu na *something*. Tunaomba fedha hizo ziende ili kituo cha *One Stop Center* kiweze kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna Kituo cha Polisi Makambako; eneo lile lilozungukwa wananchi pale wanataka kulipwa fidia, zililetwa fedha zaidi ya Shilingi milioni 200, fedha zile baadaye wananchi walipokataa kupokea kwamba ni ndogo na baadaye tulipoongea nao wakakubali fedha zile zikahamishwa zikaenda kujenga Kituo cha Polisi Wanging'ombe. Ombi langu Mheshimiwa Waziri, Hazina toeni fedha sasa walipwe

wale wananchi wanateseka sana, sana sana. Kwa sababu ni eneo ambalo muda mrefu limechukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia nyingine ya tatu ni suala la Soko la Kimataifa. Serikali ilishatoa Shilingi bilioni 3.1, fedha zilizobaki ni ndogo kwa ajili ya wananchi 18 na wananchi hawa walikuwa wanashughulikiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara. Ombi langu sasa, Hazina itoe fedha ili wananchi hawa nao walingane na wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la fidia ni suala la umeme wa upepo. Pia tunaomba Hazina wamalize mazungumzo na *TANESCO* ili wananchi hawa waweze kulipwa fidia za maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kuna miji 45 ambayo inakwenda kujengwa masoko na stendi ikiwepo na Makambako. Tunaomba Mheshimiwa Dkt. Mwigulu miji hii iweze kuanza hasa ukizingatia pale Makambako ndiyo *center* ya kwenda Songea, Mbeya, Malawi, na kadhalika. Kwa hiyo, tunaomba jambo hili lianze mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ambalo limezungumziwa kuhusu kulipa magari; malori, mabasi na kadhalika Shilingi 3,500,000/=. Jambo hili Mheshimiwa Dkt. Mwigulu wananchi wamelipokea, wamenipigia sana simu, wanaomba bei ipungue iwe kati ya Shilingi 2,000,000/= na Shilingi 2,500,000/=. Mmelifanya jambo zuri kwamba sasa litakuwa halina longolongo, watu wakishalipa basi, tunakutana mwaka mwingine. Jambo hili wamelipokea vizuri, lakini wanaomba bei ipungue. Shilingi 3,500,000/= ni fedha nyingi. Tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yako, mkae tena

upya, mpange, bei ipungue ili wananchi waweze kumudu kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile watu wa vituo vya mafuta nao wanaomba iwe kama hii mliyopanga ya magari. Vituo vya mafuta kwa lita moja wanapata faida ya Shilingi 100/=, na katika faida ya Shilingi 100/= ninyi mnachukua Shilingi 20/= wanabaki na Shilingi 80/=. Halafu mnakuja kukokotoa tena kodi. Kwa nini na wenyewe mnapochukua Shilingi 20/= iwe basi, shughuli imeisha? Litakuwa ni jambo jema sana na mambo yatakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la muda mrefu la hawa waliyosambaza pembejeo, wamekuwa wakidai fedha zao kwa muda mrefu. Ombi langu Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kama watu hawa wapo ambao walikuwa waaminifu, walifanya kazi vizuri, walipwe fedha zao kwa sababu jambo hili limechukua muda mrefu, na Serikali hampo kwa ajili ya kuwadhulumu watu, mpo kwa ajili ya kuwalipa. Tunaomba wale ambao mmehakiki fedha zao, wanatakiwa kulipwa, basi walipwe Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu jambo lingine ni mikopo ya benki. Mikopo hii, naiomba Serikali, benki zetu, ukienda benki nyingine riba ni asilimia 21, wengine 18, wengine 19, wengine 17. Kwa nini isiwe moja? Tunaomba kwenye benki, sisi ni wakopaji, tukope asilimia isizidi 15 ili tuweze kumudu kulipa madeni haya ambayo tumekopa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo Sanga. *(Makofi*

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niliweke vizuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante, kengele ilishalia.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sekunde moja.

**MWENYEKITI:** Nilikuongezea, kengele ililia nikaona unaongelea mambo ya muhimu ya benki.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu chapa kazi, fanya kazi na Mama fanya kazi vizuri na Mawaziri wote fanyeni kazi vizuri, mko vizuri na Manaibu Waziri. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Deo Sanga. Tunaendelea Michael Mwakamo, baadaye Mheshimiwa Cecilia Paresso, ajiandae.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia jioni ya leo. Kabla sijaendelea na mchango ambao nimeukusudia unaohusu Jimbo langu, nina jambo la ushauri kwa Serikali ambapo kwenye Hotuba ya Waziri sijaliona, lakini nafikiri ni muda sahihi nami kutoa mawazo yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo moja la Mwenge wa Uhuru. Mwenge wa Uhuru ni jambo jema sana kwenye nchi yetu. Mwenge wa Uhuru unakimbizwa kwa

niaba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mwenge wa Uhuru unakagua miradi mikubwa yenye gharama kubwa ya fedha za Serikali. Naipongeza Serikali kwa kuendelea kuwekeza nguvu na kuhakikisha Mwenge wa Uhuru unakimbizwa nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kwenye eneo hili nina wazo. Wakimbiza Mwenge wanapokwenda kufungua miradi ile, wanaifungua kwa niaba ya Mheshimiwa Rais. Nafikiri kwa ukubwa na wingi wa miradi inayofunguliwa nchi nzima kwa mwaka mmoja kwa Mbio za Mwenge wa Uhuru ingependeza sana tukapitia upya utaratibu wa kuyaandika mawe yale ya miradi yanayozinduliwa. Ingefurahisha sana! Kwangu binafsi kama kila mradi unaozinduliwa na Mbio za Mwenge wa Uhuru, kwa maana ile ile ya kupongeza jitihada anazozitekeleza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tungeandika majina yake katika miradi yote ili iwe kumbukumbu kwa kila Kijiji kutokana na nguvu kubwa anazozitoa kuhakikisha kwamba miradi ile inaonekana na Watanzania wote kwamba ni utekelezaji wake yeye mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu nikiangalia hata kwenye Risala ya Utii ambayo anasomewa Mkimbiza Mwenge, inatamkwa, “Mheshimiwa Rais…” Kwa hiyo, ni busara kabisa kwamba na mawe ya msingi pia yanayozinduliwa yakawekwa kwa jina la Mheshimiwa Rais. Hii ni katika kumpongeza na kumpa morali na nguvu na kuendelea kuzitoa pongezi zetu kwake na Serikali yake kwa namna ambavyo anaelekeza fedha nyingi kwenye miradi mikubwa ambayo inatatua matatizo ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hili, nirudi kujielekeza kwenye kupitia hotuba hii iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri, nikijielekeza sana mambo ambayo yanagusa Jimbo langu. Nimeisoma Hotuba vizuri, nimemsikiliza wakati anaiwasilisha, kwa kweli nimpongeze, ana kiwango kikubwa sana cha kuwasilisha jambo na kueleweka kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo jambo hasa katika masuala mazima ya Ujenzi na Uchukuzi. Kuna eneo kwenye hotuba ile imezungumza ujenzi wa barabara ya kilomita 158 ya mwendokasi inayotokea Dar es Salaam – Mlandizi – Chalinze hadi Morogoro. Barabara hii ni mpya, inakwenda kujengwa kwa ajili ya kurahisisha usafirishaji kwa watu kuingia kwenye barabara hii ya kulipia na kuwa ni barabara ya mwendokasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nategemea tukiwa tunafikiria kuanzisha miradi mipya mikubwa hasa kwenye sekta hii ya barabara, tungejaribu kuangalia miradi mikubwa ya barabara ambazo zipo kwenye mipango kwa muda mrefu ambazo hazijatekelezwa. Tunapokuwa tunaenda kuanzisha mradi huu, maana yake tunautafutia na chanzo cha pesa cha kwenda kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niikumbushe Serikali, upo mradi wa barabara ambayo kila nikisimama naisema, na ninaisema kwa sababu naiona iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi tangu mwaka 2005; barabara ya kutoka Makofia – Mlandizi, Mlandizi – Mzenga, Mzenga – Mwanarumango mpaka Vikumburu. Ni barabara yenye urefu wa kilomita 153. Kwa hiyo, inafanana kabisa na barabara ambayo inafikiriwa kwenda kuanzwa kutekelezwa kwa sasa hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ninayoitaja ipo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi tangu 2005, na kila Ilani inatajwa. Cha kusikitisha, kwenye hotuba ya Wizara husika, barabara hii imetajwa; kwenye hotuba ya Wizara husika ya mwaka 2021 barabara hii ilitengewa na fedha; kwenye hotuba kubwa ya Serikali iliyowasilishwa juzi, barabara hii haipo, inazungumzwa barabara mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii imeshafanyiwa upembuzi yakinifu. Kwa kipande cha kilomita 35 kinachotokea Makofia mpaka Mlandizi kinahitaji fidia isiyopungua Shilingi 9,986,550,000/=, mpaka leo, na upembuzi yakinifu huu umefanyika mwisho kabisa wamemalizia kazi mwezi Kumi mwaka 2018. Watanzania hawa ambao wanaisubiri fidia hii, nyumba zao zinabomoka, wamekaa kwenye nyumba ambazo wanashindwa kuzifanyia ukarabati, hawaelewi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wengine walipoisikia hotuba wanajaribu kuniuliza, Mheshimiwa Mbunge, hebu tuulizie kwa Waziri, kama wanaanzisha wazo la kutengeneza barabara mpya ya kilomita 158 zinazopita kwenye Jimbo hili hili la Kibaha, iweje sisi ambao tulishafanyiwa upembuzi yakinifu iwe hatuna chochote tunachokipa? Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, kama wamesahau kuizungumza, namwomba sana, kwa faraja ya watu wa Jimbo la Bagamoyo, Kibaha Mjini, Kibaha Vijijini na Kisarawe, ni vyema Serikali ikaja na tamko kwenye eneo hili ili watu hawa wajue nini kinafuata baada ya muda mrefu kupita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwenye hotuba ambayo Waziri amesoma, sisi kwenye utekelezaji wa Serikali tuna mambo mawili makubwa tunaenda nayo. Kwanza kuna dhima ambayo inaonekama kwenye

mipango ya Serikali; kwenye Mpango wa Miaka Mitano wa kuanzia 2021/2022 mpaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye bajeti ya mwaka 2022/2023 tunayo dhima ya bajeti hiyo. Hizi dhima mbili ukiziangalia, zote zina lengo la kukuza uchumi, kuondolea wananchi umasikini na kuwaongezea watu maisha bora katika maeneo wanayoishi. Wizara imeweka wazi kabisa, imebainisha vipaumbele ambavyo wanakwenda kuvifanyia kazi; kilimo, mifugo, uvuvi, nishati, uwekezaji na biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuzungumza kwenye eneo hili, lazima tunapokwenda kufikiria kuwaongezea watu uchumi wao, lazima tuanze kutafakari pale ambapo watu hawa wapo, pale ambapo watu hawa walikuwepo na wapi tunataka tuwapeleke kwa sasa? Ukiiangalia bajeti ya Serikali, inajielekeza kwenye kufikiria kuchimba mabwawa makubwa, kutafuta mbolea na kutafuta mbegu bora. Ni lazima tujiulize, wakulima hawa tunaowafikiria kuwapelekea mambo haya, changamoto zao za kawaida za asili ambazo zinawakabili, ni kiasi gani Serikali imezielekezea nguvu kwenye kuzitatua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano wa changamoto moja nyepesi kabisa. Kwenye hotuba hapa, Waziri ametambua, naomba ninukuu kidogo mistari michache sana. Amesema, "kwa ardhi, maji na watu tulionao ni jambo la aibu kwa Tanzania kulia shida ya ngano, shida ya mafuta ya kula kwa sababu ya vita ya Ukraine na Urusi." Sasa kama tunatambua haya, lakini hawa wananchi ambao wanalima kienyeji, kwa kilimo cha zamani kabisa, cha jembe la mkono, tunawafikiaje?

Tunawezaje kwenda kuanza nao pale? Ili uweze kumfikisha mtu mbali, kaanze naye pale alipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaona mpango mkakati wa Serikali kuwashughulikia wakulima wadogo wenye jembe la mkono. Wanamtoaje kwenye jembe la mkono kumpeleka kwenye jembe ambalo anaweza akazalisha ili afikie malengo makubwa ambayo Serikali inayafikiria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukiangalia, wamezungumzia masuala mazima ya kuchimba mabwawa; leo hii tunavyo vyanzo vya maji, nao wamevitambua. Kuna Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, mito mikubwa kama Malagarasi, Ruvuma, Rufiji, Mara, Pangani, Ruvu na kadhalika. Mito hii ipo. Kabla hawajaanza kufikiria kuchimba mabwawa makubwa, wana mkakati gani wa kuyatumia maji haya ambayo tayari yapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza kutafuta fedha za kuchimba mabwawa, wakati huo huo vyanzo hivi vya maji ambavyo vinasimamiwa na Bodi za Maji wameweka taratibu ngumu za wananchi kuyatumia. Sasa tunajichanganya wenyewe. Huku unatafuta kuchimba bwawa la maji, huku una mto umeutambua, una ziwa unalolitambua, lakini maziwa yale na mito ile wananchi ambao wamepakana nayo kando kando kama Mto wa Ruvu watu wanashindwa hata kumwagilia kwa masharti magumu yaliyopo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo maeneo ambayo tunafikiri eti ndiyo tunamsaidia mwananchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Michael Mwakamo. Nilimtaja Mheshimiwa Cecilia Paresso na baadaye Mheshimiwa Profesa Muhongo, ajiandae.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu. Bajeti yoyote inapopangwa na hasa ya Serikali ni makisio au matarajio ya nini kitakusanywa ili yale tuliyojipangia kwa maana ya matumizi na maendeleo yaweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba mfumo wa bajeti yetu hapa nchini ni *cash budget,* kwamba tukusanye, tupate ndiyo tuitumie kwa jinsi ambavyo tumeipitisha. Ila mfumo huo wa *cash budget* inahitaji Serikali kuwa makini na kuweka mikakati ya ukusanyaji kwenye maeneo yote ambayo kodi inapaswa kukusanywa na kuhakikisha hakuna upotevu wowote wa kodi, lakini kuweka mazingira rafiki ambayo kila mlipa kodi atakuwa anatamani kulipa kodi na siyo kwa kulazimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi tumekuwa tukiweka makisio ya bajeti kubwa na hatufikii malengo ya ukusanyaji. Miaka mitano ya fedha iliyopita makisio yetu ya bajeti hayajawahi kufikiwa. Tumetekeleza bajeti hiyo

kwa kukusanya na kupata haya matarajio ya kodi kwa kiasi cha asilimia 78 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika bajeti ya mwaka 2021/2022 ambayo tunaimalizia, lengo lilikuwa ni kukusanya Shilingi trilioni 37.99 kutoka vyanzo vyote, lakini hadi Aprili Serikali imeweza kukusanya Shilingi trilioni 29. Unaona hapo kuna utofauti kati ya Shilingi trilioni nane, lakini hapo hujachukua mwezi wa Tano na wa Sita kwa sababu ripoti inasema ni mwezi wa Nne ndiyo wamekusanya kwa kiwango hicho. Kwa hiyo, hata ukichukua mwezi wa Tano na wa Nne, ukakisia tu labda mtakusanya Shilingi trilioni nne, bado unaona, kuna upungufu wa takribani Shilingi trilioni nne kulingana na makisio ya bajeti ambayo tulijiwekea kwa mwaka uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tunajadili tena bajeti ya mwaka 2022/2023, tunaweka tena malengo makubwa ya Shilingi trilioni 41, wakati kule nyuma tuna upungufu, lakini leo tunaongeza 8% tena ya makisio ya bajeti. Sasa naishauri Serikali kwamba haya makisio mnayoyaweka nadhani mfikirie huko mbele, kutokuweka makisio ambayo hatuwezi kuyafikia. Ni bora hata tuweke pungufu, hata ikija zaidi inakuwa ni bora zaidi kuliko kuweka kwenye makaratasi matarajio makubwa halafu hatuyafikii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya hayo, kuna mambo mengi ambayo yanapaswa kutazamwa ili tuweze kufikia hiki ambacho tunakitarajia. Sasa nini kifanyike? Kuna mianya mingi sana ya upotevu wa kodi. Ukisoma uchambuzi wa Shirika la *Action Aid,* kuna upotevu mkubwa sana kwenye maeneo mengi kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamefanya uchambuzi kati ya mwaka 2013 na mwaka 2021; kwenye sekta isiyo rasmi tunapoteza Shilingi trilioni 6.5. Sasa tukiweka mikakati; mikakati rafiki lakini, siyo ile ya kutumia *task force,* siyo ile ya kubambikiza kodi, hapana. Tuweke mifumo rafiki ya kuzitambua sekta hizi zisizo rasmi, tuwajengee mazingira, tukusanye kodi ambazo zinapotea, tutaweza kufikia haya malengo ambayo tumejiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni misamaha ya kodi isiyokuwa ya lazima. Kuna misamaha ya kodi isiyokuwa ya lazima ya Shilingi trilioni 1.1. Hii ni misamaha mingi sana. Kwa hiyo, ni lazima mfikirie aina ya misamaha inayotolewa kwa hawa wanaopata hii misamaha, na kama hiyo misamaha kweli ina tija, ili tuhakikishe tunapunguza misamaha hii ili hizi fedha ambazo zinachukuliwa kama misamaha basi ziingie kwenda kutekeleza na kufanikisha hilo lengo mlilojiwekea la Shilingi trilioni 41.48. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwenye utakatishaji wa fedha au fedha haramu. Uchambuzi wa *Action Aid* unaonesha kwamba kuna Shilingi trilioni 1.4 ambayo inapotea katika eneo hili. Haya mambo yapo, kuna wachambuzi wanafanya kupitia taarifa zenu wenyewe Serikali, zipo, mzisimamie, mzifanyie kazi ili tuhakikishe haya malengo mliyojiwekea yaweze kufikiwa na Watanzania waweze kupata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni lazima kuhakikisha tunaimarisha ukusanyaji wa ndani kwa kuweka mazingira rafiki, lakini kuweka masharti rafiki na rahisi kuanzisha na kufanya biashara. Tunaposema masharti rafiki, ni kuangalia mazingira ya watu wanaotaka kufanya biashara, yawe ni rafiki. Leo wafanyabiashara wa

maduka ya kubadilishia fedha wakitaka kuomba leseni maana yake, anatakiwa awe na mtaji wa Shilingi bilioni moja. Hii sijui imewahi kutokea wapi? Yaani ni ngumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa nini tusiweke kiwango kidogo ambacho kila mtu ataweza, halafu kama mnahisi kwamba haya maduka ya kubadilishia fedha labda yana tabia ya kuficha fedha au fedha haramu, wekeni mazingira ya kuratibu na *ku-control,* lakini tuweke kodi ambazo mtu akitaka kuanzisha biashara anaweza kwa sababu kuna kiwango kidogo ambacho anakimudu na ataanzisha biashara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuondoe urasimu wa ufanyaji wa biashara au upatikanaji wa leseni. Leo mfanyabiashara labda kwenye Kijiji X akitaka kuanzisha biashara yake, ataenda Halmashauri kukata leseni, atalipia, lakini hatapewa kile kitambulisho cha leseni mpaka arudi *TRA* apate *Tax Clearance*. Atafika *TRA* ata-*print Tax Clearance* halafu atarudi tena Manispaa au Halmashauri na kupewa ile risiti ya leseni ya biashara. Sasa unaona mnavyomsumbua huyu mfanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini mifumo isiongee kwa pamoja? Akienda Halmashauri mtu wa Halmashauri, wajue huyu mtu hadaiwi kodi yoyote, ana *Tax Clearance* ambayo iko kwenye mfumo inaonesha. Au akienda kama anadaiwa basi mfumo uoneshe moja kwa moja. Kwa hiyo, tuweke mazingira ambayo yanaoana (mazingira ya Kiserikali) ambayo mtu akienda eneo hili anapata huduma zote kwa mara moja na siyo kuhangaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, mmeondoa ada kwa Kidato cha Tano na cha Sita, ni vizuri, ni jambo jema, lakini ada ni kitu kidogo katika michango mingine mingi sana iliyopo. Leo mtoto wa Kidato cha Tano na cha Sita anapoenda kuanza, anapelekewa *Joining Instruction* ambayo ina michango mingi kuliko hata ile ada iliyoondolewa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema, mmefanya vyema kwa sababu mnataka kuondoa hiyo ada na kusema elimu bila ada, lakini tukumbuke pia Kidato cha Tano na cha Sita, siyo elimu ya lazima. Kuanzia Darasa la Kwanza mpaka *Form Four* ndiyo elimu ya lazima na kila mwanafunzi aende. Sasa hawa wanaoenda ni *option* tu, lakini kuna hao wengine ambao ni wa Kidato cha Nne kurudi chini, hawa nao hawalipi ada, lakini huku nako kuna michango. Kwa hiyo, ni vyema sana tuboreshe hii ya lazima ambayo inawachukua kila mtu; Darasa la Kwanza mpaka Kidato cha Nne, tupunguze na tuhakikishe pia hata hii ambayo imeondolewa kwenye Kidato cha Tano na cha Sita; na Mheshimiwa Kakunda alisema vizuri pia kwamba tuangalie kwenye vyuo vya kati kuwaondolea ada wabaki labda na michango midogo tu ya kuwezesha utekelezaji wa hizo shughuli za kielimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri kwamba hili jambo ni jema, tumewapunguzia akina mama mzigo ambao kwa namna moja ama nyingine walikuwa wanahangaika kupata ada huko vijijini, lakini tuone pia namna ya kuwapunguzia mzigo kwenye suala la michango, imekuwa mingi mno ambayo inawekwa na shule zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, tumeweka kipaumbele kwenye kilimo na Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti yako umesema kwamba kipaumbele *this time* itakuwa kilimo, ni vizuri mmefanya vizuri kwa sababu kilimo ni ajira, kilimo kinachangia kwenye uchumi wa nchi, kilimo ni kila kitu. Tunamshukuru Mungu kwa sababu tuna ardhi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ardhi ya Tanzania ikitumika vizuri kulingana na kanda zetu, na hali ya hewa kwenye maeneo yetu, kwa kweli sisi ni matajiri sana sana. Tunahitaji kutumia ardhi kupitia kilimo kuhakikisha uchumi wa nchi unakua, uchumi wa mtu mmoja mmoja na uchumi wa jamii unakua. Ila tunahitaji bajeti itosheleze, bajeti za utafiti ziwepo kwenye suala la kilimo, bajeti husika ya Wizara ambayo imeomba ipatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma tuna kilio kikubwa sana, tunapitisha bajeti ya Wizara hapa mfano Kilimo, haiendi kama ambavyo imepitishwa. Kwa hiyo, tunategemea safari hii kama kweli mmesema kilimo ni kipaumbele, tuone basi kwa matendo kwa kuhakikisha kwamba, hiyo bajeti ya WIzara ya Kilimo ambayo tumepitisha hapa Bungeni inatolewa kwa wakati na inakwenda kufanya yale ambayo yamekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye suala la kilimo tunahitaji utashi wa kisiasa. Kama kuna utashi wa kisiasa wa kufanya kilimo ndiyo kipaumbele, tunahitaji kufanya kilimo ndiyo kisaidie uchumi wa mtu mmoja mmoja, kwa jamii na nchi kwa ujumla, basi tuone kwa matendo suala la kilimo mnalipa kipaumbele. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Tayari! Mh!

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Cecilia Paresso.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujamalizia michango yetu ya leo naomba niwatambue wageni ambao wapo jioni hii katika Bunge letu. Kwanza tuna wageni ambao wapo kwenye jukwaa la Mheshimiwa Spika wageni hao ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Jumuiya ya Wazazi Taifa. Hao wanaongozwa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Taifa Dkt. Edmund Mndolwa, karibu sana Mwenyekiti katika Bunge letu. *(Makofi)*

Ndugu Haidary Abdallah Makamu Mwenyekiti wa Wazazi Taifa; pia tuna Ndugu Gilbert Kalima, Katibu wa Wazazi Taifa; pia tuna Ndugu Daniel Shija Naibu Katibu Mkuu Wazazi Tanzania Bara; tuna Ndugu Othman Maulid ambaye pia ni Naibu Katibu Mkuu Wazazi Ofisi Kuu ya Zanzibar. Viongozi hawa wameambatana na wajumbe 155 ambapo tuna Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji Taifa; kuna Wajumbe wa Baraza Kuu la Taifa ambapo katika Baraza Kuu hilo la Taifa wote kwa pamoja kuna Wajumbe wa *NEC*, na Wajumbe wawili wa Baraza la Wawakilishi ndani ya Baraza. *(Makofi)*

Pamoja na hao pia tuna Maafisa ambao wanatoka Makao Makuu Dodoma pamoja na Ofisi Kuu Zanzibar, nao kwa pamoja wasimame wote. Karibuni sana wageni wetu wa Umoja wa Wazazi Tanzania, Jumuiya Kongwe ya Chama cha Mapinduzi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa makofi hayo Wajumbe hawa wana Wawakilishi wawili, mmoja ni Bahati Kenneth Ndingo na mwingine ni Mwenyekiti wenu niliyesimama mbele yenu. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, baada ya kuwatangaza hivyo, kwa vile walikuwa na kikao toka asubuhi wanaweza kuondoka na kwenda kupiga picha na kufanya shughuli nyingine. *(Makofi)*

Pia humu ndani kuna Waheshimiwa Wabunge wengi wanatokana na Jumuiya hii, kwa hiyo tuendelee kuheshimu Jumuiya ya Wazazi. *(Makofi)*

Vile vile tuna wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge ambao wapo Bungeni kwa ajili ya kutembelea Bunge. Wageni hao wa Waheshimiwa Wabunge kama wapo naomba wasimame kwa pamoja, wale pale, wapo juu. Karibuni sana wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Karibuni sana katika Bunge letu, naamini mmejionea mengi na namna gani Bunge linaendeshwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na michango yetu. Nilimtaja Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuongea. Nianze kwanza kwa kusema kwamba bajeti tuliyopewa ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, ni bajeti nzuri, na

mimi kwa Jimbo la Musoma Vijijini miradi yote tuliyoiomba imekubaliwa. Kwa hiyo, hii bajeti naiunga mkono kwa niaba ya wananchi wa Musoma Vijijiji. Kwa hiyo kinachofuata ni namna ya kuboresha au kudumisha uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitachukua picha kubwa zaidi kwa sababu Jimbo limeshapata kila kitu, sasa nifanye kitu cha kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Mheshimiwa Waziri amefanya *presentation* nzuri sana na akatuonesha hali ya uchumi ilivyo duniani. Nitaongezea tu kwamba, kwa hali tuliyonayo ya uchumi sasa hivi, wataalam wabobezi wa uchumi duniani wanasema ni hali kama ilivyokuwa mwaka 1973 na 1974 ambapo mafuta yalipanda bei mara nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1979 na 1980 mafuta yalipanda bei mara mbili, na watu wa umri wangu wanakumbuka hii ya pili ya mwaka 1980 ndiyo mapinduzi yaliyomtoa Shah, kwa hiyo, Iran haikutoa mafuta vilivyo. Kwa hiyo, mwaka 1973/1974 tulikuwa na hali ngumu, mwaka 1979/1980 tulikuwa na hali ngumu, lakini Mheshimiwa Rais wa wakati huo, Baba wa Taifa aliweza kutuvusha. Nami nina imani kwa hali tuliyonayo sasa hivi, Rais wetu Mheshimiwa atatuvusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampa pongezi nyingi sana kwa bidii anayoifanya. Uchumi wa sasa hivi wana neno la Kiingereza linaitwa *Stagflation*. *Stagflation* ni uchumi ambao uwekezaji unapungua, *investments* hazipo. Ndiyo hali tuliyonayo sasa hivi duniani na Watanzania tuko hapo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndugu zangu tutatokaje hapo kwenda mbele? Mimi nachukua mambo

tuliyokuwa tumekubalina kwenye Dira yetu ya Maendeleo na Mipango ya Miaka Mitano. *GDP per capital* yetu kwa sasa ni Dola 1,260, tunataka tufike *GDP per capital* Dola 3,000 mwaka 2025. Mwaka 2025 tutakuwa Watanzania karibu asilimia 70.1. Kwa hiyo, tunachokifanya ni kwamba *GDP* yetu sasa hivi ambayo ni ya Dola za Marekani *62 billion,* tukichukua *GDP per capital* ya Dola 3,000 kwa kila mmoja, kwa hiyo, mwaka 2025 tunapaswa kuwa na *GDP* ya Dola bilioni 210. Angalieni kazi hiyo, kutoka Dola bilioni 62 kwenda Dola bilioni 210.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hapa nakuja kutoa ushauri. Umasikini kwa mwaka 2020, *poverty rate* ilikuwa asilimia 27.1 na mwaka jana 2021 imepungua ikafika asilimia 27. Kwa hiyo, *speed* ya kupunguza umasikini bado iko chini na inaendana na uchumi. *(Makofi)*

Mheshimia Mwenyekiti, matumizi ya umeme nadhani niliwahi kuwaeleza kwamba kipimo kizuri kinachotumika Kimataifa siyo kwamba umeme umefika kijijini, umeme umefika kwenye Kata, umeme umefika sijui wapi? Swali watu wanalotaka kujibiwa, ni watu wangapi kwenye eneo hilo wanatumia umeme; na ni umeme kiasi gani? Sasa *records* ambazo ziko huko duniani zinaonesha hivi, sisi *electricity energy consumption per capital* Tanzania ni *Kilowatt* 95. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jirani yetu Kenya ni *Kilowatt* 170. Sasa *Kilowatt 95* yaani ni umeme ambao unaweza ukautumia ndani ya saa moja, ndiyo kipimo cha *Kilowatt hour*. Kwa hiyo, sisi ni *Kilowatt 95*, Kenya ni *Kilowatt* 170. Ndiyo maana wakati ule nilijadili mambo ya *energy mix* na leo nimesikia Wabunge wengine wamesema wanataka umeme wa upepo na umeme wa jua.

Mheshimiwa Mwenyekiti na ndugu zangu, tukitaka kufanikiwa kwenye mambo ya umeme, lazima twende kwenye umeme wa jua na umeme wa upepo. Kwa mfano, kwa umeme wa jua, China wana *Gigawatt* 252. Yaani *Megawatts* 2,250; kwenye upepo wana *Megawatt* 281,000. Kwa hiyo, kuendana na uchumi wetu ili tuongeze *power per capital,* lazima tuzalishe umeme mwingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kazi tuliyonayo na Mheshimiwa Waziri aliieleza vizuri, uchumi ulishuka ukaja *4.9 percent,* mwakani unataka kwenda *5.3 percent*, lakini kupunguza umasikini lazima uchumi uende kati ya *percent* nane na kumi. Tutafikaje huko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la kwanza, kwa ajili ya muda sitaingia ndani, na ndiyo maana nataka mje mwangalie *percent* ninazoziweka mimi. *Growth*; kilimo, uvuvi na ufugaji, tuwekeze pale na itatoa ajira mpya na tuseme *growth* yake iwe kati ya *percent* moja na mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili, tuwekeze kwenye utalii ambayo tunaheshimu mama amefanya *film* ambayo *ina-promote* utalii, iwe *percent* moja. Tatu, ni madini. Twende kwenye *gold* na msisahau *gold reserve,* nilishaiongelea *gold reserve*; tuweke kwenye *gemstones*, tuweke kwenye *critical technical metals*, *technology metals;* hili nalo nilishawaeleza na tutumie gesi yetu ya *Helium*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, madini yachangie *growth* ya *3.4 percent* halafu tuuze umeme. Cha muhimu sasa ambacho nataka nikiongee, leo nilitoa ahadi, ni

uchumi wa gesi. Uchumi wa gesi unaweza ukachangia *growth* ya *five to six percent*. Nini maana ya uchumi wa gesi? Gesi ina uchumi mzuri kwa sababu mbili; kwa sababu gesi unaweza kuitumia kama malighafi, halafu gesi unaweza ukaitumia kama *source of heat*. Ni vitu viwili vinafanya gesi inakuwa muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa uchumi wa gesi; kwa hiyo, gesi asilia tutatengeneza mbolea, tutazalisha umeme, kutakuwa na *plastics* na *fabrics,* hii *SNG* waliyokuwa wanaongea ya kwenye magari; tutakuwa na kemikali kama *LPG,* gesi mnayotumia kupikia, *ammonia* ambayo iko kwenye mbolea na kwenye ma-*refrigeration; methanol* ambayo inatumika kwenye *plastics, ascetic acid* ambayo inatumika kwenye kutunzia vyakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali linakuja: Je, hiyo gesi tunayo ya kutosha? Kuzalisha umeme unahitaji *thousand cubic feet* kuzalisha *one Kilowatt Hour. U*nahitaji *seven thousand cubic feet* kuzalisha *one megawatt hour*. Je, hiyo gesi tunayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mbolea. Unahitaji *0.57 tons of ammonia* ku-*produce one ton of urea*. Tatu, unahitaji *33 metric million British thermal unit* ya *natural gas* ku-*produce one ton of ammonia*. Nne, tunaenda vizuri Serikali, mkataba wa awali umewekwa, bei ya *LNG* tungekuwanayo sasa hivi, Januari mwaka jana 2021 ilikuwa *US Dollar* sita kwa *1MMBTU (Metric Million British Thermal Unit)*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa kuna simu inalia mpaka huku tunasikia jamani. Naomba mpunguze au mzime.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitunzie muda wangu nami nimesimama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ilikuwa imeshalia na huku simu zinalia.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, naomba basi nimalizie hizo dakika mbili. Kwa hiyo, sasa hii gesi ndiyo maana napendekeza *TPDC* ibaki kwenye kazi hii, kwa sababu sasa hivi tumeshagundua *57.54 TCF*. Jirani yetu *Mozambique* ambaye yuko kwenye *Ruvuma Basin* ameshagundua *a hundred TCF* na huenda ana *two hundred*. Kwa hiyo, *TPDC* isipoweka mkazo huko Ruvuma, tutajua tuna gesi kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni *conventional,* kuna aina nyingine ya gesi inaitwa *shell gas*. Hii *shell gas* ni nyingi sana, ndiyo Marekani inatumia sasa hivi, wala hatujawahi kuanza *exploration*. *Lake Tanganyika* inabidi *TPDC* ieleze kuna mafuta au gesi? Halafu lazima tujadiliane na Kongo na Zambia. *Lake Nyasa* kuna mafuta na gesi, lazima tujadiliane na Malawi. Halafu kwenye *Lake Eyasi* na huku baharini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana mapendekezo yangu nasema kwamba *TPDC* wana kazi kubwa, kubwa, kubwa, tuwaache watutafutie hii gesi kwa ajili ya uchumi wetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Prof. Sospeter Muhongo. *(Makofi)*

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, ahsante. Mengine nitaongea siku nyingine tena. Ahsanteni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unaweza kupeleka kwa maandishi; una mambo mengi mazuri, yapeleke kwa maandishi tu. Tunaendelea na Mheshimiwa Nicholaus Ngassa na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ajiandae.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali jioni hii. Kwanza kabla ya kuchangia nilikuwa nataka nitoe pongezi zangu kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa *statement* ya kusamehe madeni ya wafanyabiashara ya miaka ya nyuma. Jambo hili ni kubwa, limejenga *confidence* kwa wafanyabiashara, limeleta *harmonization* na sasa wafanyabiashara wetu wanafanya biashara zao kwa amani. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni suala la elimu bila malipo. Tunamshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa kutoa dira na sasa tutakuwa na wanafunzi wanasoma kuanzia Darasa la Kwanza mpaka Kidato cha Sita bure. Kwa sisi ambao tumetoka kwenye jamii za wakulima na wafugaji tunajua thamani ya jambo hili, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni nyongeza ya mishahara kwa Watumishi wa Umma. Mheshimiwa Rais

ameongeza mshahara kwa watumishi wa Umma, tunamshukuru pia kwa hili, kwa kuona hii sekta ya muhimu katika uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na jambo la nne ambalo ningependa kutoa pongezi ni suala la udhibiti na usimamizi wa fedha za umma. Tunashukuru sana kwa Serikali kuchukua mawazo mbalimbali ya Bunge toka bajeti ya mwaka 2021 tulipokuwa tukichangia na Mpango wa Maendeleo ya Taifa, tulisema kwamba, Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali zijengewe uwezo; na kwa safari hii wameliona, ofisi zote mbili, kwa maana ya *Internal Auditor General* na Ofisi ya *CAG* kwa maana ya *National Audit Office* wamejengewa uwezo na wametengewa fedha za kutosha kwa ajili ya kuimarisha kazi zao. Tunawashukuru na kuwapongeza Serikali kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mambo takribani sita ningependa niyachangie jioni hii, ambapo nitayachangia kwa ufupi ili niweze kuyamaliza. Jambo la kwanza nitachangia ni mfumo wa kodi na ukusanyaji wa mapato nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1977 ilipovunjika Jumuiya ya Afrika Mashariki tulianza mchakato wa kuirejesha mwaka 1999 na mwaka 2000 Jumuiya ya Afrika Mashariki ikawa imeanza. Tuliporudi kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki nchi zilizokuwa tatu zikiunda Jumuiya ya Afrika Mashariki wakati huo, kila moja ilikuja imeboresha mfumo wake wa ukusanyaji kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uganda walikuja na mamlaka yao ya mapato wanaita *Uganda Revenue Authority* ambayo waliitengeneza mwaka 1991. Kenya

walikuja na mamlaka yao ya mapato wanaita *Kenya Revenue Authority,* (Mamlaka ya ukusanyaji Mapato ya Kenya) ambayo waliitengeneza mwaka 1995, na sisi Tanzania tukaingia na mamlaka yetu ya ukusanyaji wa mapato ambayo tuliitengeneza mwaka 1995 chini ya utawala wa Mheshimiwa Hayati Benjamin Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifuatilia *study* mbalimbali na chambuzi mbalimbali, mpaka sasa tunapoongea Mamlaka yetu ya Mapato Tanzania ni moja ya mamlaka za mapato bora sana katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati na nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Tuna mfumo mzuri wa uendeshaji, lakini tuna mfumo mzuri wa muundo kwa maana ya *institution,* lakini tuna changamoto ambayo tukiweza kui-*address* inaweza ikawa na msaada sana katika ukusanyaji wetu wa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wetu wa mapato, tuna kodi za aina mbili; tuna kodi za moja kwa moja kwa maana ya kusema *direct tax*. Pia tuna kodi ambazo siyo za moja kwa moja kwa maana ya *indirect tax* kwa mfano *VAT*. Changamoto kubwa tuliyonayo ni kwenye kodi za moja kwa moja na hususan hapa tunapokenda kwenye *income tax*. Nitaongea kidogo, niwaombe Serikali mlichukue mliangalie, hata kama siyo bajeti ya mwaka huu, basi bajeti ya mwakani mnaweza mkaliangalia, kwani litapunguza sana usumbufu kwa wafanyabiashara wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi kodi ambazo ni *direct,* (za moja kwa moja), kwa mfano tuna *corporate tax,* tuna *withholding tax,* tuna *income tax,* tuna *service levy,* na kadhalika; ukija katika mfumo wa hizi kodi za moja kwa

moja kwa mfano kodi ambazo zinahusisha vibali na leseni, huwa hazina changamoto sana kwa sababu, zenyewe zina tozo ambazo zimepangwa ziko *fixed*. Kwa hiyo, mtu anajua mimi ninapotaka kuanzisha biashara, leseni yangu ni kiasi fulani. Nataka nisajili kampuni, badaye nitatakiwa kulipa kiasi fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto inakuja kwenye hizi biashara ambazo tunahitaji kufanya *bargaining,* kwa wafanyabiashara wa hizi biashara zetu za kawaida kwenye kodi ya mapato, ndiyo shida kubwa inapoanzia hapo inaleta manung'uniko. Inasababisha mambo makubwa matatu; jambo la kwanza, kunakuwa kuna *inconsistency*. Unakuta mfanyabiashara mmoja ana kiwango sawa na biashara ya mwingine na mtaji sawa, lakini mapato na kodi wanalipa tofauti. Matokeo yake inaleta malalamiko kwa wafanyabiashara wetu. Kwa hiyo, tunaomba Serikali mlichukue hili mchakate vichwa na wataalamu wenu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, muweze kuja na mpango mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbele ya safari mje na *scientific approach* ya kukusanya hizi kodi, tuondokane na huu mfumo wa *bargaining* na ku-*compromise,* unasababisha pia rushwa kwa wananchi, matokeo yake tunajikuta kwamba Maafisa wetu wa *TRA* wengi wana-*compromise* wanaingia katika mitego ya rushwa. Anakwambia ili nikukadirie kodi kiasi fulani, basi hii hela nyingine nipe mimi, weka pembeni au kampatie mtu fulani. Hii ndiyo msingi wa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo, kama Wizara, kama taasisi mliopewa dhamana ya kusimamia masuala ya kodi nchini chakateni vichwa, tumieni wataalamu wenu, shirikisheni wasomi mbalimbali mje na *schedule,* au

*scientific approach* itakayotusaidia kama nchi kutoka hapa tulipo tusiendelee kuwa na mfumo wa kodi wa kufanya *bargaining* na matokeo yake inasababisha rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia madhara ya huu mfumo Serikalini yanaleta *inefficiency,* maana yake ufanisi unakuwa haupo, na ndio maana unakuta tunakadiria kodi, tunasema tutakusanya Shilingi trilioni 31, matokeo yake tunaishia kwenye Shilingi trilioni 27. Hii ni kwa sababu tunajikuta tunaweka viwango ambavyo siyo *realistic.* Kwa hiyo, katika hilo naiomba Serikali ilichukue na ilifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili la msingi ninalopenda kuchangia ni ushirikiano kati ya Serikali na wafanyabiashara katika dhana ya kujenga uchumi jumuishi. Tunasema tunajenga uchumi jumuishi na uchumi wa watu. Sasa Mheshimiwa Waziri naomba hili tuliangalie, kuna wafanyabiashara wa juu, wa kati na wa chini. Wote katika kipindi hiki ambacho tunafanya *transformation,* basi tujitahidi kuwagusa kadiri ya changamoto wanazokabiliananazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi naweza nikatolea mfano kwangu pale Igunga, kuna wafanyabiashara takribani 209 walinyang'anywa vibanda na Serikali kwa maana ya kupitia Halmashauri. Mheshimiwa Jafo alianza kulifanyia kazi hili, akaja Mheshimiwa Ummy na nimemuona Mheshimiwa Bashungwa. Tunaomba hili Serikali mlichukue mlifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara ambao ndio chanzo cha kutoa kodi, na pia ni wadau wa

maendeleo katika maeneo yetu ambao wanatoa ushirikiano kwa Serikali na kwa chama chetu, wanapokuwa wanasumbuliwa na kunyang'anywa vibanda vyao kabla ya mkataba; mkataba umenyang'anywa na Serikali kabla ya miaka miwili, tunaomba Serikali ilimalize hili, wafanyabiashara wetu warudishiwe vibanda vyao. Mkataba wao utakapoisha, watakaa mezani na Serikali, wataweza kujadiliana. Tunafungua nchi. Katika kufungua nchi, ndiyo namna hii ya kuwasaidia wafanyabiashara hata wa ngazi ya chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu napenda kuchangia jioni hii ni suala la mafao ya wastaafu. Katika nchi mpaka sasa tunafanya vizuri na niwapongeze Serikali mnakwenda vizuri; kumekuwa na changamoto moja katika suala la mafao. Unakuta mstaafu anastaafu kwa Daraja F, lakini mafao analipwa kwa Daraja E. Hii nayo imekuwa ni changamoto kubwa na ninadhani maeneo mengi katika nchi hili limekuwa ni tatizo. Mwingine amestaafu kwa kutumia Daraja G, lakini analipwa Daraja F. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaombe Serikali muweke *modality* nzuri ya kuhakikisha mtu anapofikia hatua amestaafu, kuna zile tunaita *declaration;* katika zile fomu asaini tamko la mwisho kwamba hiki ndiyo kiwango cha mafao yangu nitakayoyapata, ili tuepushe usumbufu kwa hawa watu wanapostaafu. Kwani hela wanazopewa za *pension* wanaanza tena kutumia katika nauli za kuja Dodoma au kwenda Dar es Salaam katika kufuatilia mafao yao. Ni usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapofikia mwisho mtu anastaafu, akiwa anaondoka kwa Afisa Utumishi wake au

kwa mwajiri wake anajua mimi nitapokea Shilingi milioni 50, hii mwisho na anaweka saini kwenye tamko, maana yake hatakuwa na usumbufu mwingine wowote. Hawa ma-*accounting officers* kwa maana ya waajiri, kama mtu bado ana tatizo kuhusu mafao yake asiruhusiwe kusaini ile *declaration* kwa sababu inakuja kuwa ni usumbufu baadaye. Kwa hiyo, naomba Serikali mlichukue na lenyewe muweze kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ningependa kuchangia jioni hii ni suala la ruzuku ya pembejeo za kilimo. Naishukuru na kuipongeza Serikali, mmeongeza fedha kwenye kilimo, mmeweka fedha za pembejeo. Hapa Serikali naomba mtusaidie maeneo mawili, jambo la kwanza Serikali tunaomba ruzuku iliyotolewa iwahusishe walengwa, iwafikie walengwa ambao ni wakulima wetu wote ambao wapo katika maeneo mbalimbali ya nchi hii. Kumekuwa na tabia au ukiangalia historia, maeneo mengi ambayo fedha za Serikali huwa zinapigwa, ni ama zimetoka kwenye ruzuku kwa maana ya *subsidy* au zile *stimulus package*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba katika hili Serikali, naamini Wizara ya Kilimo kaka yangu Mheshimiwa Hussein Bashe na kaka yangu Mheshimiwa Mavunde mtalisimamia vizuri, ruzuku hii iweze kuwanufaisha wakulima wetu. Jambo la pili mtakalotusaidia hapa, ruzuku hiyo ifike katika kipindi kinachoendana na misimu ya kilimo. Tunaomba kama ni pembejeo tutakapozipata zikitoka ambazo zimeambatanishwa kwa ruzuku hii, basi zifike katika kipindi kinachohusisha misimu ya kilimo tusije tukapishana na msimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano ni suala la nishati. Napenda kuchangia kwenye suala la umeme na

mradi wa bomba la mafuta la kutoka Uganda kwenda Tanga. Sisi Igunga hili bomba linapota pale. Kuna baadhi ya wananchi walipitiwa, wanatakiwa kulipwa fidia. Walishafanyiwa *assessment,* wamefungua *account,* lakini mpaka leo hawajalipwa fidia zao. Naomba wananchi wa Igunga walipwe hii fidia. Wamelipa fidia eneo la Bulyang'ombe tu pale ambapo wanajenga *site camp,* lakini maeneo ambayo bomba linapita bado hawajalipwa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna vitongoji ambapo bomba linapita walisema wakati wanatambulisha mradi kwamba watapeleka umeme.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba pia umeme katika hivi vitongoji uweze kupelekwa ili hata watakapoanza shughuli zao za bomba basi umeme uwepo wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kuchangia jioni hii ni suala la…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ilishalia.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Naam!

**MWENYEKITI:** Kengele yako ilishalia, nimekuachia umalizie hiyo sentensi.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nashukuru. Naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nicholaus Ngassa. Tunaendelea na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami nichangie hotuba ya bajeti hii ya mwaka 2022/2023. Niianze kwa kuunga mkono bajeti hii kwa sababu bajeti hii inakwenda kujibu matatizo, na shida za wananchi wetu. Ni bajeti ambayo mama amekwenda kusikiliza kilio cha Wabunge na kilio cha Wabunge ni kilio cha wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama ilivyo ada, naweza nikasema mengi kusifia bajeti hii, lakini kwa sababu mengi yameshazungumzwa, niende moja kwa moja kwenye mada ambayo imenisimamisha. Nianze na nukuu ya Mwalimu Nyerere, ili Watanzania tuweze kupata maendeleo, Mwalimu Nyerere anasema, tunahitaji watu, ardhi, siasa safi, na uongozi bora. Sasa mimi nitajikita kwenye uongozi bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, namna nzuri ya kwenda kutekeleza hii bajeti ni lazima tuwe na watu wanaokwenda kusimamia kwa uadilifu, wanaokwenda kufuata misingi ya utawala bora. Ili tuweze kuwapata hawa watu, ni lazima Serikali ijikite kuimarisha vyuo vyetu vya utawala bora. Serikali ijikite kuhakikisha wananchi wanapata mafunzo wawapo kazini, lakini kama haitoshi, basi kuwepo na semina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameanza kuwaamini vijana, ni jambo jema sana, lakini vijana hawa walio wengi bado hawajapita kwenye vyuo vya Utumishi wa Umma. Kwa hiyo, ni muhimu sana tuwapeleke

kwenye semina, tuwapeleke kwenye semina elekezi ili waweze kujua mipaka ya majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niongeze na mfano kidogo. Leo hii wako wateule wa Mheshimiwa Rais; wako ma-*DC* na ma-*RC*. Zipo sheria zinazowalinda na zipo sheria ambazo wanazitumia. Labda kwa kutokuzijua au kwa makusudi, iko sheria moja ya saa 24 kwa ma-*DC* na saa 48 kwa Wakuu wa Mikoa. Sheria hii ilikuwa ikiwaumiza sana wananchi. Matumizi ya sheria hii yamekuwa yakiwaumiza sana wananchi kwa sababu wako ma-*DC* na ma-*RC* wanaitumia sheria hii kinyume na utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sijasahau, Mheshimiwa Mkuchika alipokuwa Waziri wa Utawala Bora alituletea somo hapa, alituambia mtu ambaye anapaswa kukaa ndani saa 24, kwanza ni kwa sababu yeye kuwepo kwake nje kutahatarisha usalama wake; au la, kuwepo kwake nje kutahatarisha usalama wa jamii. Leo hii sheria hii inatumika bila mpangilio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo, huyo mtu akishawekwa ndani, kama ni Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya, lazima akaandike kwenye kitabu cha Polisi pale kwamba, amewekwa ndani saa 24 kwa sababu gani? Kesho yake anatakiwa afikishwe Mahakamani; nitoe mfano mmoja. Mimi kwenye Wilaya yangu ya Liwale ninaye *DC* sasa hivi ana mwaka mmoja, tayari watu 20 wameshawekwa ndani. Kati ya hao 20 hakuna hata mmoja aliyefunguliwa mashitaka. Yuko Diwani wa Kata ya Nangano, Abdallah Lilombe kawekwa ndani. Yupo Mtendaji wa Kata, wa Kata hiyo hiyo Erick Mpinga kawekwa ndani; yupo Mtendaji wa Kijiji, Neema Kibasi kawekwa ndani; Kata ya Ngongowele yupo Mganga

Mfawidhi wa Zahanati kawekwa ndani saa 24; kwenye Kata ya Kimambi yuko Afisa Maliasili na Uvuvi kashawekwa ndani; Afisa Mifugo wa Wilaya kashakaa ndani, Afisa Mifugo wa Kata kashawekwa ndani; na Afisa Manunuzi wa Wilaya kashawekwa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni kwenye Kata ya Makata yuko Mwenyekiti wa *AMCOS* kashawekwa ndani; Katibu wa *AMCOS* kashawekwa ndani; dereva kashawekwa ndani; utingo kashawekwa ndani. Orodha ni ndefu, lakini kati ya hawa hakuna aliyefunguliwa mashitaka hata mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake ni nini? Ni kwamba tunakwenda kushusha utendaji kwenye Halmashauri. Leo Halmashauri ime-*paralyze,* hakuna anayefanya kazi kwa kujiamini, watu wanasubiri maelekezo. Unamweka ndani Afisa Mfawidhi, Mganga Mfawidhi unamweka ndani kwa kosa la kwamba jengo limejengwa vibaya. Yeye sio *engineer* wala sio Afisa Manunuzi. Halafu ukishamweka ndani humpeleki Mahakamani, inasaidia nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa Mheshimiwa Waziri tuimarishe kitengo cha utawala bora. Tupeleke hawa wateule wote kwenye vyuo vya utawala bora wakajifunze; na vilevile wapewe *instrument* yao wasome, waambiwe mipaka yao ni ipi? Unamweka ndani saa 24 mtu, kwa lipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nimelizungumza kwa msisitizo mkubwa kwa sababu, Halmashauri ya Wilaya ya Liwale ime-*paralyze* sasa hivi hakuna anayefanya kazi, wote wanasubiri kuwekwa ndani. Kila mtu anajua kwamba hapa akipita Mkuu wa Wilaya mimi ni kuwekwa

ndani bila hata sababu ya msingi. Kwa hiyo, jambo hili linakwenda kuondoa maana ya utawala bora na Halmashauri zetu zinaenda ku-*paralyze*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Diwani ameshawekwa ndani, hata Mbunge naye atawekwa ndani. Kwa hiyo, nashauri sana, naomba kuimarisha utawala bora. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili naomba nilizungumze kuhusiana na barabara. Nilipopitia bajeti ya kisekta tulipoingia kwenye bajeti ya miundombinu, mimi kama Mbunge wa Jimbo la Liwale niliridhika kidogo baada ya kuona barabara ya Masasi – Nachingwea; Nachingwea – Liwale imekwenda kuwekwa kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami. Tena Mheshimiwa Waziri alisema kwamba, barabara hii anakwenda kuijenga kwa *PPP,* ule mpango wa *EPS plus F,* lakini kwa masikitiko makubwa jana Mheshimiwa Waziri wakati anaizungumza, ametaja barabara kadhaa, lakini barabara ya Masasi – Nachingwea; Nachingwea – Liwale sikuiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ombi langu Mheshimiwa Waziri utakaposimama ku-*wind up* hapo mwisho wa hotuba yako, naomba uniambie barabara ya Masasi – Nachingwea; Nachingwea – Liwale, nini hatima yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, siyo kwa umuhimu, naomba niende kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii. Wakati nachangia kwenye sekta ya maliasili nilizungumzia suala la Wizara hii kutupatia Maafisa wa Wanyamapori kwenye Kata zetu, kutupatia vituo kwenye Kata zetu, lakini kwenye bajeti hii kubwa sijaliona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, wakati nachangia pale nilisema kabisa kwamba kwenye bajeti hii mtarajie kutuletea chakula Liwale, kwa sababu sisi kule mazao yanavunwa mwezi wa Sita na wa Saba, lakini wakulima tayari tangu mwezi wa Nne wamesharudi baada ya mazao yao kuliwa na tembo. Nikapendekeza hapa kwamba tuletewe maaskari kwenye kata zetu kama ilivyo mapolisi kata kwenye kata zile zote ambazo ziko pembezoni mwa hifadhi, tunaomba hawa mapolisi waje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nikapendekeza tuwe na vituo. Wilaya ya Liwale asilimia 60 iko *Selous*. Tunacho kituo kimoja. Kituo hiki kiko pale Liwale Mjini. Nikapendekeza awali kituo kile kilitakiwa kijengwe kwenye Kata ya Barikiwa, nikapendekeza kirudishwe kule kwa sababu umbali wa kutoka Barikiwa mpaka Liwale Mjini ni zaidi ya Kilometa 70. Kwa hiyo, hayo ndiyo mapendekezo niliyatoa kwenye bajeti ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kwenye ku-*wind up* hotuba yake naomba kupata majibu ya hayo mapendekezo yangu kama yalipuuzwa au yamechukuliwa hatua gani? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

Waheshimiwa Wabunge muda wetu wa kuchangia kwa siku ya leo ndiyo umefikia mwisho. Nawashukuru wote kwa michango yenu mizuri. Naamini kwamba wengine wana michango mingi kuliko dakika 10, haziwatoshi. Tujitahidi kupeleka kwa maandishi na Mheshimiwa Waziri yuko tayari kupokea hata kwa maandishi ili tuweze kufanyia kazi hayo mambo muhimu ambayo tunaona kwamba tunaweza kuchangia.

Basi, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku, Bunge Liliahirishwa Hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 17 Juni, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*